NAKALA MTANDAO(ONLINE DOCUMENT)

# BUNGE LA TANZANIA

---

## MAJADILIANO YA BUNGE

---

## MKUTANO WA KUMI NA MBILI

## Kikao cha Tano– Tarehe 10 Septemba, 2018

*(Bunge Lilianza Saa Tatu Asubuhi)*

**D U A**

*Spika (Mhe. Job Y. Ndugai) Alisoma Dua*

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge tukae. Tunaendelea na Mkutano wetu wa Kumi na Mbili, leo ni Kikao cha Tano. Katibu.

**NDG. STEPHEN KAGAIGAI – KATIBU WA BUNGE:**

**HATI ZA KUWASILISHA MEZANI**

Hati zifuatazo ziliwasilishwa Mezani na:-

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU, SERA, BUNGE, KAZI, AJIRA, VIJANA NA WENYE ULEMAVU:**

Taarifa ya Mwaka ya Mfuko wa Fidia kwa Wafanyakazi kwa mwaka 2015/2016 *(The Annual Report of Workers Compensation Fund for the Year 2015/2016).*

Taarifa ya Matoleo ya Gazeti la Serikali pamoja na Nyongeza zake zilizochapishwa tangu Mkutano wa Bunge uliopita kama ifuatavyo:-

1. Toleo Na. 13 la Tarehe 30 Machi, 2018;

2. Toleo Na. 14 la Tarehe 06 Aprili, 2018;
3. Toleo Na. 15 la Tarehe 13 Aprili, 2018;
4. Toleo Na. 16 la Tarehe 20 Aprili, 2018;
5. Toleo Na. 17 la Tarehe 27 Aprili, 2018;
6. Toleo Na. 18 la Tarehe 4 Mei, 2018;
7. Toleo Na. 19 la Tarehe 11 Mei, 2018;
8. Toleo Na. 20 la Tarehe 18 Mei, 2018;
9. Toleo Na. 21 la Tarehe 25 Mei, 2018;
10. Toleo Na. 22 la Tarehe 01 Juni, 2018;
11. Toleo Na. 23 la Tarehe 08, Juni, 2018;
12. Toleo Na. 24 la Tarehe 15 Juni, 2018;
13. Toleo Na. 25 la Tarehe 22 Juni, 2018;
14. Toleo Na. 26 la Tarehe 29 Juni, 2018;
15. Toleo Na. 27 la Tarehe 06 Julai, 2018;
16. Toleo Na. 28 la Tarehe 13 Julai, 2018;
17. Toleo Na. 29 la Tarehe 20 Julai, 2018;
18. Toleo Na. 30 la Tarehe 27 Julai, 2018;
19. Toleo Na. 31 la Tarehe 03 Agosti, 2018;
20. Toleo Na. 32 la Tarehe 10 Agosti, 2018;
21. Toleo Na. 33 la Tarehe 17 Agosti, 2018;
22. Toleo Na. 34 la Tarehe 24 Agosti, 2018; na
23. Toleo Na. 35 la Tarehe 31 Agosti, 2018.

**MWANASHERIA MKUU WA SERIKALI:**

Muswada wa Sheria ya Marekebisho ya Sheria Mbalimbali (Na. 3) wa Mwaka 2018 *(The Written Laws (Miscellaneous Amendments) (Na. 3) Bill, 2018).*

**MHE. MOHAMED O. MCHENGERWA - MWENYEKITI WA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA KATIBA NA SHERIA:**

Maoni ya Kamati ya Katiba na Sheria kuhusu Muswada wa Sheria ya Marekebisho ya Sheria Mbalimbali (Na. 3) wa Mwaka 2018 *(The Written Laws (Miscellaneous Amendments) (No. 3), Bill, 2018).*

**MHE. MASOUD ABDALLAH SALIM (K.n.y. MSEMAJI MKUU WA KAMBI RASMI YA UPINZANI KATIKA WIZARA YA KATIBA NA SHERIA):**

Maoni ya Msemaji Mkuu wa Kambi Rasmi ya Upinzani juu ya Wizara ya Katiba na Sheria kuhusu Muswada wa Sheria ya Marekebisho ya Sheria Mbalimbali (Na.3) wa Mwaka 2018 *(The Written Laws (Miscellaneous Amendments) (No. 3), Bill, 2018).*

**SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa. Katibu

**NDG. STEPHEN KAGAIGAI - KATIBU WA BUNGE:**

**MASWALI NA MAJIBU**

Na. 53

**Ukarabati wa Barabara za Mbarali**

**MHE. ORAN M. NJEZA (K.n.y. MHE. HAROON M. PIRMOHAMED)** aliuliza:-

Je, ni lini Serikali itafanyia ukarabati barabara za Mahongole – Kilambo kilometa 20, Igurusi – Utengule kilometa 22, Chimala – Kapunga kilometa 25 na Mlangali – Ukwavila kilometa 23?

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. JOSEPHAT S. KANDEGE)** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais – TAMISEMI, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Haroon Mulla Pirmohamed, Mbunge wa Mbarali, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Halmashauri ya Wilaya ya Mbarali ina mtandao wa barabara wenye urefu wa kilometa 685 zinazohudumiwa na Wakala wa Barabara Vijijini na Mijini *(TARURA),* kilometa 341 ni za kiwango cha changarawe na kilometa 344.5 ni za udongo.

Katika mwaka wa fedha 2017/2018 Serikali ilipeleka jumla ya shilingi bilioni 1.065 sawa na asilimia 91 ya bajeti

iliyopangwa kwa ajili ya matengenezo ya barabara na madaraja katika Halmashauri ya Wilaya ya Mbarali. Kazi zilizofanyika ni pamoja na ukarabati wa Madaraja ya Mporo III, Mporo IV na Manienga. Matengenezo ya barabara zenye urefu wa kilometa 50 kwa kiwango cha changarawe, ukarabati wa sehemu korofi zenye jumla ya kilometa 30 na matengenezo ya kawaida kwenye barabara zenye urefu wa kilometa 67.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa fedha 2018/2019 Halmashauri ya Wilaya ya Mbarali imetengewa kiasi cha shilingi milioni 220 kwa ajili ya matengenezo maalum katika barabara ya Mlangali – Uturo- Ukwavila na Chimala-Kapunga kwa eneo korofi lenye jumla ya kilometa 11. Vilevile Halmashauri imetengewa shilingi milioni 12.18 kwa ajili ya matengenezo ya makalavati 21 katika barabara ya Igalako-Mwatenga - Kilambo.

**SPIKA:** Mheshimiwa Njeza nimekuona swali la nyongeza tafadhali.

**MHE. ORAN M. NJEZA:** Mheshimiwa Spika, nashukuru sana na vilevile nashukuru kwa majibu mazuri ya Serikali lakini ningependa kuuliza maswali mawili ya nyongeza.

Mheshimiwa Spika, kutokana na ajali nyingi zinazotokea katika Wilaya ya Mbeya na hasa katika Milima ya Uyole na Mbalizi. Je, ni lini Serikali itafanya upanuzi wa barabara zinazoelekea kwenye nchi za jirani za Zambia na Malawi?

Mheshimiwa Spika, je, ni lini Serikali itajenga *by pass* ya Inyala – Simambwe na Inyala – Songwe? Nashukuru sana.

**SPIKA:** Majibu ya maswali hayo muhimu sana, Naibu Waziri, Mheshimiwa Elias Kwandikwa tafadhali.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO (MHE. ELIAS J. KWANDIKWA):** Mheshimiwa Spika, ahsante. Kwanza niseme kwamba *study* zilizofanyika

zinaonyesha kuwa ajali nyingi zinazotokea asilimia 78 zinatokana na makosa ya kibinadamu *(human behavior)* na asilimia 12 iliyobaki ndiyo inasababishwa na mambo mengine ikiwepo miundombinu. Kwa ajali ambazo zinatokea katika Mkoa wa Mbeya niseme tu ajali iliyotokea juzi kwa mfano nimepata fursa ya kuwepo Mbeya juzi, eneo ajali ilipotokea ni eneo ambalo barabara ni nzuri na alama za barabarani zipo, inawezekana lilikuwa tatizo la kiufundi lakini tu kwa ujumla wake Serikali imechukua hatua ya kuendelea kuboresha barabara za Mbeya kwa sababu *nature* ya eneo la Mbeya ni milima na miteremko mirefu ili kuweza kupunguza ajali kwa maana kwamba ile barabara sasa anayoitaja Mheshimiwa Mbunge Inyala – Simambwe ni kati ya barabara ambazo tunaendelea kufanya usanifu ili tuweze kupunguza ule msongamano mkubwa wa magari.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, kwa ujumla wake tu ninapende kutoa wito kwa watumiaji wa barabara kwamba maeneo haya ambayo yanakuwa na milima mikali na alama za barabarani zipo, watumiaji wa magari tuzingatie hizo kanuni za barabarani ili tupunguze ajali wakati Serikali inafanya juhudi za kuboresha barabara zake. Kwa hiyo, tatizo la Mbeya niseme kwa ujumla Serikali inalitambua na tunafanya haraka kuhakikisha kwamba tunaboresha miundombinu na kupunguza ajali katika eneo hili.

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, mtaona muda wetu umechukuliwa sana na swali la kwanza, tuendelee na Mheshimiwa Daimu Iddi Mpakate, Mbunge wa Tunduru Kusini, aulize swali TAMISEMI.

Na. 54

**Kuigawa Wilaya ya Tunduru**

**MHE. DAIMU I. MPAKATE** aliuliza:-

Halmashauri ya Wilaya ya Tunduru ina jumla ya kata 39 na vijiji 157. Halmashauri iliomba kuigawa Wilaya hiyo

ambayo ina ukubwa zaidi ya Mkoa wa Mtwara wenye Wilaya sita:-

(a) Je, Serikali ina mpango gani wa kuigawa Wilaya ya Tunduru ili iwe rahisi kutoa huduma karibu zaidi na wananchi?

(b) Je, Serikali ina mpango gani wa kuzigawa Kata za Mchoteka, Mtina, Namasakala, Lukumbule, Mchasi, Tuwemacho na Misechela ambazo zina wakazi zaidi ya 30,000 kila Kata?

(c) Je, Serikali itaidhinisha lini mgao wa vijiji uliopendekezwa na Halmashauri mwaka 2015 ili kurahisisha utoaji wa huduma kwa wananchi?

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. JOSEPH G. KAKUNDA)** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Ofisi ya Rais, TAMISEMI napenda kujibu swali la Mheshimiwa Daimu Iddi Mpakate, Mbunge wa Tunduru Kusini, lenye sehemu (a), (b) na (c) kwa pamoja kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, taratibu za kuanzisha au kugawanya maeneo ya kiutawala zimeainishwa kwenye Sheria ya Serikali za Mitaa Sura ya 287, pamoja na Mwongozo wa Serikali wa mwaka 2014.

Mheshimiwa Spika, maombi ya kugawa Halmashauri ya Wilaya ya Tunduru na kuanzisha Halmashauri ya Wilaya ya Nalasi na kuzigawa Kata za Mchoteka, Mtina, Namasakala, Lukumbule, Mchasi, Tuwemacho na Msecheke yaliwasilishwa Ofisi ya Rais, TAMISEMI yakiwa pamoja na ombi la kuanzisha mkoa mpya wa Selous. Serikali imetafakari maombi haya na kuyaona kuwa ni ya msingi, hata hivyo, kutokana na changamoto ya kuimarisha kwanza miundombinu kama majengo ya ofisi na nyumba za watumishi na mahitaji mengine kama vifaa vya ofisi, watumishi wa kutosha na vyombo vya usafiri kwenye maeneo mapya ya utawala

yaliyoanzishwa tangu mwaka 2010 na 2012, Serikali imesitisha uanzishwaji ya maeneo mapya ya utawala hadi yaliyopo yaimarishwe kikamilifu.

**SPIKA:** Mheshimiwa Mbunge wa Tunduru swali la nyongeza tafadhali.

**MHE. DAIMU I. MPAKATE:** Mheshimiwa Spika, ahsante kwa kunipa nafasi ya kuuliza maswali mawili ya nyongeza. Pamoja na majibu mazuri aliyotoa Naibu Waziri, nina maswali mwili ya nyongeza.

Mheshimiwa Spika, katika jitihada hizo za kuimarisha maeneo yaliyokuwepo sasa kuna tatizo la Watendaji Kata maeneo mengi katika Jimbo la Tunduru Kusini na Tunduru kwa ujumla walio wengi wanakaimu.

Je, Serikali itapeleka lini watendaji wa kudumu ambao wameajiriwa katika nafasi ya Kata, Vijiji na Katibu Tarafa?

Swali la pili, kwa kuwa majukumu mengi yaliyopo kwa sasa Vijijini yanafanywa na Watendaji wa Vijiji wakishirikiana pamoja na Wenyeviti wa Vijiji; na kwa kuwa Halmashauri nyingi zimeshindwa kutoa posho kwa maana ya asilimia 20 kwenye Vijiji husika.

Je, Serikali haioni haja kwa sasa kutoa posho kwa viongozi wa vijiji kwa maana ya Wenyeviti wa Vijiji ili waweze kufanya majukumu yao vizuri? *(Makofi)*

**SPIKA:** Majibu ya maswali hayo Mheshimiwa Naibu Waziri, TAMISEMI, Ndugu Kakunda tafadhali.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. JOSEPH G. KAKUNDA):** Mheshimiwa Spika, ni kweli kwamba katika nchi tunao upungufu mkubwa wa Watendaji wa Kata, kwa kweli siyo Watendaji wa Kata peke yake bali kada nyingi na Serikali ya Awamu ya Tano imedhamiria kuhakikisha kwamba tunamaliza au

tunapunguza kwa kiasi kikubwa upungufu wa watendaji wetu katika kada mbalimbali. Kwa upande wa Watendaji wa Kata, mwaka jana tuliajiri nafasi chache lakini mwaka huu tunao mpango wa kuajiri Watendaji wa Kata 1,000 nchi nzima. Ninaamini watakapoajiriwa hao watapunguza sana upungufu wa uwepo wa Watendaji Kata katika Kata nyingi hapa nchini ikiwemo Kata za Wilaya ya Tunduru.

Mheshimiwa Spika, katika swali lake la pili kwamba Watendaji wa Vijiji na Wenyeviti wa Vijiji ndiyo wanaofanya kazi kubwa huko kwenye vijiji vyetu. Napenda nikubaliane sana na Mheshimiwa Daimu Mpakate kwamba ni kweli Wenyeviti wa Vijiji na Wenyeviti wa Vitongoji wanafanya kazi kubwa kwa kuwaongoza vizuri watendaji wa vijiji walioko huko kufanya kazi za Serikali kwa niaba ya wananchi.

Mheshimiwa Spika, amesema kwamba posho hawapati, natoa hapa agizo ambalo lilishatolewa na Serikali tayari kwamba suala la kushusha asilimia 20 ya mapato ya ndani kupeleka kwenye Kata, Vijiji na Vitongoji kwa ajili ya posho za Waheshimiwa Wenyeviti wa Vijiji na Vitongoji, hilo ni suala la kikanuni na kisheria.

Kwa hiyo Wakurugenzi wa Halmashauri ni lazima watekeleze agizo hilo kikamilifu. Pale ambapo tutagundua kwamba mtu hatekelezi kwa sababu tu ya ujeuri au ukaidi itabidi tuchukue hatua za kiutawala na kiutumishi. Kuna wale ambao ni Wakurugenzi wanapata shida kidogo kutokana na makusanyo hafifu, tunawaomba sana Mabaraza ya Madiwani waridhie mapendekezo ya wataalam kuhusu kupanua wigo wa vyanzo vya mapato ya ndani ambavyo vitasaidia kuweza kupatikana fedha ambazo hatimaye zitapelekwa kwa viongozi hawa kwa ajili ya posho.

**SPIKA:** Mheshimiwa Lubeleje, nilikuona, swali la nyongeza.

**MHE. GEORGE M. LUBELEJE:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi niweze kuuliza swali moja la nyongeza.

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa Serikali imesitisha ugawaji wa maeneo makubwa yakiwemo Majimbo pamoja na Wilaya, lakini kuna Kata moja iko mlimani inaitwa Kata ya Mkanana, hata Mheshimiwa Spika unaifahamu ni milimani hasa. Makao Makuu ya Kata yako kilometa 50 wanateremka kusikiliza mikutano. Je, Serikali inasemaje kuhusu Kata hii ya Mkanana na Chibwegere ili wazigawe? Wananchi wanapata shida sana kusafiri.

**SPIKA:** Majibu ya swali hilo Mheshimiwa Naibu Waziri, TAMISEMI. Mkanana na Chibwegere.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. JOSEPH G. KAKUNDA):** Mheshimiwa Spika, ni kweli kama alivyosema, tumesitisha, lakini kulingana na umuhimu na mahitaji ya muda maalum, kama ambavyo tumepitisha uanzishwaji wa Halmashauri ya Jiji la Dodoma na kuutangaza Mji wa Dodoma kuwa Makao Makuu ya nchi kwa sababu ni mahitaji maalum kwa muda maalum, kwa suala hili la Kata ya Mtanana kama ambavyo Mheshimiwa Mbunge amelieleza vizuri sana hapa Bungeni na kwa sababu anawawakilisha wananchi wake ambao anaamini wanapata shida kwenda kwenye Makao Makuu ya Kata kilometa 50, namuagiza Mkurugenzi wa Serikali za Mitaa kesho aende Mtanana na timu yake ya wataalam ili watuletee mapendekezo yao.

**T A A R I F A**

**MHE. GEORGE M. LUBELEJE:** Mheshimiwa Spika, ni Mkanana siyo Mtanana. Mtanana ipo Kongwa, Mkanana ni ya kwangu Mpwapwa. *(Kicheko)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Mbunge, haikubaliki.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. JOSEPH G. KAKUNDA):** Mheshimiwa Spika, kama alivyorekebisha ni hivyo hivyo.

**SPIKA:** Seneta ameleta kanuni mpya hapa leo. Alikuwa anaweka sawa kwamba kule Kongwa Kata inaitwa Mtanana, na hii anayoiongelea katika Wilaya ya Mpwawa inaitwa Mkanana, sasa inawezekana Mkurugenzi wake akaelekea Kongwa Mtanana, alikuwa anarekebisha hilo tu. *(Kicheko)*

Waheshimiwa Wabunge, tunaendelea na Ofisi ya Rais, Utumishi na Utawala Bora, swali la Mheshimiwa Aida Joseph Khenani. Mheshimiwa Aida, tafadhali.

Na. 55

**Nafasi Zilizoachwa Wazi na Wenye Vyeti *Fake***

**MHE. AIDA J. KHENANI** aliuliza:-

Je, Serikali ina mkakati gani wa kuziba nafasi zilizoachwa wazi na watumishi waliokumbwa na sakata la vyeti *fake?*

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, MENEJIMENTI YA UTUMISHI WA UMMA NA UTAWALA BORA** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Aida Joseph Khenani, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, napenda kuliarifu Bunge lako kuwa Serikali imeshatoa vibali vya kuajiri watumishi 15,000 ili kuziba pengo lililosababishwa na kuondolewa kwenye orodha ya malipo ya mishahara watumishi wa umma waliobainika kughushi vyeti. Vibali kwa ajili ya watumishi hao vimetolewa katika ngazi ya Wizara, Idara zinazojitegemea, Sekretarieti za Mikoa na Mamlaka za Serikali za Mitaa na waajiri wote wameendelea kujaza nafasi hizo.

Mheshimiwa Spika, Serikali pia imetoa vibali vya ajira kwa mamlaka zote za Serikali za Mitaa Kumb. Na. CFC.26/205/01/PF/91 cha tarehe 22 Agosti, 2017 na kibali kingine cha

tarehe 12, Machi, 2018 kuziba nafasi zote za Watendaji wa Vijiji na Mtaa zilizoachwa wazi kutokana na zoezi la kuhakiki vyeti kwa kuajiri watumishi wapya.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa fedha 2017/2018 kwa kutambua umuhimu wa kuajiri watumishi wa kada mbalimbali, Serikali imetoa vibali vya kuajiri watumishi 22,150 wakiwemo watumishi wa kada za ualimu 6,840, fundi sanifu wa maabara za shule 160, kada za afya 8,000, wahadhiri wa vyuo vikuu 624 na watumishi 6,526 wa kada nyingine.

**SPIKA:** Mheshimiwa Aida, nimekuona, swali la nyongeza.

**MHE. AIDA J. KHENANI:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru.

Mheshimiwa Spika, kulingana na majibu ya Waziri nafikiri anajua kwamba kabla ya mchakato wa kuondoa watu waliokuwa wanajulikana kama wenye vyeti feki au vya kugushi, kulikuwa na upungufu mkubwa wa watumishi kwenye sekta mbalimbali zikiwemo sekta za elimu, kilimo na afya. Sasa kwa kuwa amejibu kwa *data* nina imani anajua upungufu mkubwa, tungependa alieleze Bunge lako; kwa kuwa kulikuwa na upungufu na wakaongoza tena upungufu ukawa mkubwa zaidi na mmeajiri kiasi hiki alichokisema, tunaomba kujua, mpaka sasa kuna upungufu wa watumishi kiasi gani?

Swali la pili, Rais wa kwanza wa Zanzibar aliwahi kusema tumesoma hatukujua, tumejifunza tumetambua. Serikali ya Tanzania inathamini zaidi vyeti kuliko kuangalia taaluma na kazi ambazo watu wamefanya. Baada ya kutumbua kuna watu walikuwa wamebakiza mwaka mmoja kustaafu. Ninapenda kujua Serikali imejipangaje kwa kuangalia mchango ambao waliutoa, kwa sababu wamefundisha watu wengine ni Wabunge, wengine ni Mawaziri... *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Aida, unahutubia, uliza swali.

**MHE. AIDA J. KHENANI:** Mheshimiwa Spika, ninapenda kujua kwamba mna utaratibu gani wa kuweza kuwalipa watumishi wale ambao walitumikia Taifa hili kwa uaminifu mkubwa? *(Makofi)*

**SPIKA:** Swali lako la kwanza ni la takwimu za papo kwa papo, sidhani kama Mheshimiwa Waziri atakuwa tayari, lakini kama lipo basi karibu Mheshimiwa Waziri kwa majibu. Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Utumishi na Utawala Bora, Mheshimiwa Kapteni Mkuchika.

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, MENEJIMENTI YA UTUMISHI WA UMMA NA UTAWALA BORA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru. Niwakumbushe tu Waheshimiwa Wabunge wenzangu, tunapowauliza maswali Mawaziri hatutakiwi kuwataka takwimu maana hatutembei na takwimu kichwani.

Mheshimiwa Spika, kuhusu swali lake la pili, nadhani hili swali humu ndani limeulizwa tena na tena na wanasheria wakafafanua. Maelezo yako hivi, mwajiri alikuajiri wewe akiamini kwamba vyeti ulivyompa ni vyeti sahihi ndiyo maana ukaingia naye mkataba. Kile kitendo tu cha mwajiri kubaini kwamba ulimdanganya umepeleka cheti feki, Waingereza wanasema ina-*nullify* mkataba wako, mkataba wako unakuwa *null and void,* unakuwa umejifuta kwa sababu upande mmoja umewasilisha taarifa ambazo sizo.

Kwa hiyo hapa ndani hatujajipanga kumlipa mtu ambaye mkataba wake ni *fake.*

**SPIKA:** Tunaendelea na Wizara ya Fedha na Mipango, swali la Mheshimiwa Mussa Bakari Mbarouk, Mbunge wa Tanga Mjini.

Na. 56

**Bei Halisi ya Mashine za *EFD***

**MHE. MUSSA B. MBAROUK** aliuliza:-

Kumekuwa na sintofahamu kwa baadhi ya wafanyabiashara na *TRA* kuhusu mashine za *EFDs* hususani bei za mashine na aina za mashine.

(a) Je, bei halali ya mashine ya *EFD* kulingana na aina na ubora wake ni shilingi ngapi?

(b) Kwa kuwa mashine za *EFDs* zinafanya kazi kwa niaba ya *TRA,* je, kwa nini Serikali isitoe mashine hizo bure kwa wafanyabiashara?

**SPIKA:** Majibu ya swali hilo Mheshimiwa Naibu Waziri wa Fedha na Mipango, Mheshimiwa Dkt. Ashatu Kijaji, tafadhali.

**NAIBU WAZIRI WA FEDHA NA MIPANGO** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Fedha na Mipango, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Mussa Bakari Mbarouk, Mbunge wa Tanga Mjini, lenye sehemu (a) na (b), kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Spika, kuna aina tano za mashine za *EFD* kwa ajili ya kutunza kumbukumbu na kutoa risiti za mauzo. Mfanyabiashara anaweza kununua aina mojawapo ya mashine hizo kulingana na mahitaji yake. Aidha, ubora wa mashine zote ni lazima uthibitishwe na Mamlaka ya Mapato Tanzania kabla mashine hizo hazijaingia sokoni na kuanza kutumika. Bei ya kila mashine ni kama ifuatavyo:-

(i) Rejista za Kielekroniki za Kodi - mashine hizi hutumiwa na wafanyabiashara wasiotumia mifumo ya kompyuta au mifumo ya kihasibu na bei yake kwa sasa ni shilingi 590,000.

(ii) Mashine za kielektroniki zinazoweka alama au saini *(Electronic Signature Devices)* - mashine hizi hutumiwa na walipakodi wanaotumia mifumo ya kompyuta na mifumo maalum ya kihasibu na bei zake ni kati ya shilingi 1,000,000 na 1,200,000.

(iii) Printa za Kielektroniki za Kodi *(Electronic Fiscal Printers)* - mashine hizi hutumia mfumo maalum wa kompyuta kufanya mauzo na bei zake ni kati ya shilingi 1,500,000 na 1,700,000.

(iv) Printa za Pampu za Mafuta ya Petroli na Dizeli - mashine hizi hutumiwa na wafanyabiashara wanaouza mafuta ya petroli na dizeli kwa kutumia pampu na bei zake ni shilingi 6,000,000 ikijumuisha gharama za ufungaji na uunganishaji kwenye pampu za mafuta.

(v) Printa za Maduka ya Kubadilisha Fedha za Kigeni - bei za mashine hizi ni shilingi 2,150,000 ikiwa ni pamoja na programu ya mfumo *(software).*

(b) Mheshimiwa Spika, wafanyabiashara wanaponunua mashine za *EFD* hulipa gharama za ununuzi wa mashine hizo na baadaye Serikali hurejesha gharama hizo kama ifuatavyo:-

(i) Wafanyabiashara waliosajiliwa kwenye *VAT;* kwa mujibu wa jedwali la saba chini ya Kanuni ya 54(2) za Sheria ya Usimamizi wa Kodi za mwaka 2016, mashine zilizonunuliwa kwa mara ya kwanza zinagharamiwa na Serikali kwa kumruhusu mfanyabiashara kujirejeshea fedha zake kwa utaratibu wa *input – output tax* kwenye *return* yake ya mauzo ya mwezi husika.

(ii) Kwa wafanyabiashara ambao hawajasajiliwa kutoza Kodi ya Ongezeko la Thamani hurejeshewa gharama za mashine kama ifuatavyo:-

Mosi, wanaoandaa hesabu za mizania; kundi hili linaruhusiwa kujirejeshea gharama za ununuzi wa mashine

kwa kuziingiza gharama husika kama gharama za kuendesha biashara kama ilivyoainishwa kwenye kifungu cha 11(2) cha Sheria ya Kodi ya Mapato.

Pili, wafanyabiashara wasioandaa hesabu za mizania *(presumptive cases)* kwa mujibu wa Kanuni ya 54(2) ya Kanuni za Sheria ya Usimamizi wa Kodi za mwaka 2016 kundi hili la wafanyabiashara wanajirejeshea gharama za mashine kwenye kiasi cha kodi walichokadiriwa kwa mwaka husika. Kama hawatakuwa wamejirejeshea kwa asilimia 100 basi kiasi kilichobakia kitasogezwa mwaka unaofuata.

**SPIKA:** Mheshimiwa Mbarouk ameridhika. Nakuona bado una swali la nyongeza?

**MHE. MUSSA B. MBAROUK:** Mheshimiwa Spika, ndiyo, maswali mawili ya nyongeza.

**SPIKA:** Haya tuyasikie.

**MHE. MUSSA B. MBAROUK:** Mheshimiwa Spika, risiti ni *supporting document* katika masuala ya mahesabu. Sasa risiti zetu za *EFD machines* zina tabia ya kufutika maandishi baada ya muda mfupi, *TRA* tulipokutana nao katika Kamati yetu ya *PAC* walikiri kwanza kwamba karatasi wanazotumia ni dhaifu lakini wakasema kwamba watafanya marekebisho ya karatasi hizo ili zisifutike maandishi kwa muda mfupi. Mpaka leo, tarehe 10 Septemba, bado marekebisho hayo hayajafanyika.

Mheshimiwa Spika, nataka kujua sasa *TRA* tuipe muda gani ili iweze kufanya marekebisho ya karatasi hizi za risiti?

Pili, mwaka 2017 mwanzoni wafanyabiashara wa Mkoa wa Mbeya waligoma baada ya baadhi yao kwenda China na kubaini kwamba mashine zile gharama yake ni sawasawa na shilingi 90,000 ya Kitanzania kwa mujibu wa vyombo vya habari vilivyoripoti wakati ule. Sasa nataka kujua, je, hizi mashine bei yake halisi hasa na taarifa hizi zina ukweli kiasi gani?*(Makofi)*

**SPIKA:** Sasa Mheshimiwa Mbarouk bei yake si amekutajia Mheshimiwa Naibu Waziri. Mheshimiwa Naibu Waziri majibu tafadhali.

**NAIBU WAZIRI WA FEDHA NA MIPANGO:** Mheshimiwa Spika, swali lake la kwanza kuhusu karatasi zinazofutika, napenda kuliambia Bunge lako tukufu kwamba Serikali ilishatoa taarifa kwa wafanyabiashara wote kuhusu wapi pa kununua karatasi hizi kwa ajili ya kutoa risiti za mashine za *EFD.* Zipo karatasi *fake,* hatukatai, zipo sokoni, lakini tumewaelekeza wafanyabiashara wote waende kununua karatasi hizi kutoka kwa mawakala waliothibitishwa na kuidhinishwa na Mamlaka ya Mapato Tanzania ili kuepuka tatizo hili la karatasi kufutika.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, anasema wawape muda mpaka lini, hatuhitaji kupewa muda kwa sababu tatizo hili tulishalishughulikia tayari kama Serikali.

Mheshimiwa Spika, kuhusu swali la pili; nashukuru umenisaidia kumjibu kwamba gharama za mashine ndizo nilizozitaja hapa kulingana na aina ya mashine na aina ya biashara mfanyabiashara anayoifanya. Kwa hiyo, hizo nyingine za kwenye vyombo vya habari, hizo kama Serikali hatuzijui, tunazojua ni hizi nilizozisema, ndiyo kauli na taarifa sahihi kutoka Serikalini. *(Makofi)*

**SPIKA:** Tunaendelea na Wizara ya Habari, Utamaduni, Sanaa na Michezo. Swali la Mheshimiwa Rashid Abdallah Shangazi, Mbunge wa Mlalo.

**MHE. RASHID A. SHANGAZI:** Mheshimiwa Spika, nashukuru sana. Kwanza naomba nitoe pongezi kwa Mtanzania mwenzangu Hassan Mwakinyo kwa kuipeperusha vema bendera ya Tanzania huko Uingereza.*(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Shangazi, huyo bwana kafanya nini huko Uingereza? Siyo watu wote wanajua, lakini basi Mheshimiwa Waziri atatuambia.

Na. 57

**Kupitia Upya Sera ya Michezo**

**MHE. RASHID A. SHANGAZI** aliuliza:-

Je, ni lini Serikali itapitia upya Sera ya Michezo nchini?

**WAZIRI WA HABARI, UTAMADUNI, SANAA NA MICHEZO** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa ruhusa yako naomba kabla ya kujibu swali la Mheshimiwa Rashid Abdallah Shangazi, Mbunge wa Mlalo, nitoe pole kwa ndugu, jamaa na marafiki wa Watanzania wenzetu 11 waliopoteza maisha na wengine 15 waliojeruhiwa katika ajali nyingine mbaya ya Mlima Igawilo, Mkoani Mbeya, Mungu aziweke roho zao pema peponi.

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa kufa ni wajibu na maisha lazima yaendelee, niruhusu vilevile nielezee kidogo yaliyotokea Uingereza usiku wa kuamkia jana kwa Mtanzania mwenzetu Hassan Mwakinyo wa Tanga kwa ushindi mnono alioupata huko Birmingham, Uingereza, baada ya kumchakaza mwanamasumbwi nyota wa Uingereza Sam Eggington katika raundi ya pili tu kati ya raundi 10. *(Makofi)*

Kabla ya pambano hili kufanyika bondia wa Uingereza alikuwa bondia namba nane kwa ubora duniani kati ya Mabondia 1,852 wakati Hassan Mwakinya alikuwa ni Bondia wa 174 na sasa hivi kutokana na matokeo haya Hassan ni wa 16 duniani, ni bondia bora wa kwanza Barani Afrika na bondia wa kwanza Tanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, baada ya haya, naomba sasa kujibu swali la Mheshimiwa Rashid Abdallah Shangazi, Mbunge wa Mlalo kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Sera ya Maendeleo ya Michezo inayotumika sasa hivi ni ya mwaka 1995, ni dhahiri kuwa

katika miaka 23 ya sera tuliyonayo sasa tasnia ya michezo imepitia mabadiliko mengi yanayoleta hitaji la mabadiliko kisera kama vile michezo kuwa chanzo kikubwa cha ajira ya uhakika duniani, kuibuka kwa michezo ya kulipwa, ongezeko la mahitaji ya shule na vyuo mahsusi vya michezo mbalimbali kwa lengo la kulea vipaji toka udogoni kwa wavulana na wasichana, ongezeko la hitaji la viwanja vizuri na vya kutosha ngazi za shule za msingi, sekondari, vyuo, sehemu za kazi na makazi kwa lengo la kuibua viipaji na kupunguza gharama za matibabu kwa magonjwa yanayotokana na mwili kukosa mazoezi, ongezeko kubwa la mahitaji ya vifaa mbalimbali vya michezo na umuhimu wa kujenga uwezo wa ndani kuzalisha vifaa hivyo.

Mheshimiwa Spika, ni kutokana na hali hii halisi Wizara ilianzisha mwaka jana zoezi la kuipitia upya Sera ya Maendeleo ya Michezo ya mwaka 1995, zoezi ambalo limehusisha ukusanyaji wa maoni kutoka kwa wadau mbalimbali ndani na nje ya nchi. Uandaaji wa rasimu kamili ya Sera mpya ya Maendeleo ya Michezo umefikia hatua za mwisho na ni matarajio ya Wizara kukamilisha zoezi hili ndani ya muda mfupi ujao.

Mheshimiwa Spika, kupatikana kwa sera mpya kutaleta tija na kutuwezesha kuleta mabadiliko chanya katika tasnia ya michezo nchini ikiwa ni pamoja na kutuwezesha kubadili sheria iliyoanzisha Baraza la Michezo la Taifa (BMT) ili iweze kuleta ufanisi katika uendeshaji wa michezo nchini, ikiwa ni pamoja na kuainisha vyanzo rasmi na endelevu vya mapato katika maendeleo ya michezo nchini.

**SPIKA:** Mheshimiwa Mbunge wa Mlalo swali la nyongeza tafadhali.

**MHE. RASHID A. SHANGAZI:** Mheshimiwa Spika, ahsante kwa nafasi hii.

Pamoja na majibu ya Mheshimiwa Waziri, lakini hapo utaona amesema kwamba muda mfupi ujao watakuwa wamekamilisha ukusanyaji wa maoni ya wadau.

Swali langu la kwanza, je, wadau ambao ni Waheshimiwa Wabunge na ambao ni wawakilishi wa wananchi mpaka sasa naona bado hatujashirikishwa, haoni kwamba kuliacha kundi kubwa kama hili kunaweza kukaweka matobo tena kwenye sera ambayo inarekebishwa?

Swali la pili, je, ni kwa kiasi Serikali itachukua wajibu hasa kuhakikisha kwamba michezo ya kubahatisha inakuwa sehemu katika sera hii mpya ili kutanua mfuko wa michezo na kuweza kutoa udhamini wa kutosha katika michezo ili hata hawa wanamichezo wasiwe wanajiandaa wenyewe na wakati wakileta sifa za Taifa tunazipokea kama nchi? Ahsante sana. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Rashid Shangazi kwa maswali mazuri, majibu ya maswali haya Mheshimiwa Waziri Dkt. Harrison Mwakyembe, tafadhali.

**WAZIRI WA HABARI, UTAMADUNI, SANAA NA MICHEZO:** Mheshimiwa Spika, ni kweli kwamba rasimu ya sera imejadiliwa na wadau mbalimbali, lakini hatujaleta Bungeni na siyo kawaida. Kutokana na umuhimu wa Bunge hili na vilevile mchango ambao kwa kweli mara nyingi unakuwa umefanyiwa kazi na Waheshimiwa Wabunge tutaangalia uwezekano wa kabla ya kufikia mwisho tuweze kupata mawazo ya Waheshimiwa Wabunge.

Mheshimiwa Spika, pili kuhusu michezo ya kubahatisha ni kweli kabisa katika sera tuliyonayo sasa hivi ya mwaka 1995, michezo ya kubahatisha siyo sehemu ya michezo na tumechukua hatua ya kuingia katika mabadiliko ya sheria mbalimbali ambayo yatawasilishwa leo Bungeni hapa tunafanya mabadiliko ya sheria hiyo ili michezo ya kubahatisha nayo iwe sehemu ya michezo na iweze kuchangia katika maendeleo ya michezo nchini.

**SPIKA:** Nilikuona Mheshimiwa Ally Saleh, swali la nyongeza.

**MHE. ALLY SALEH ALLY:** Mheshimiwa Spika, pamoja na sifa nyingi Mheshimiwa Waziri alizozimimina kwa bondia Hassani Mwakinyo, kama ulivyosema ni kwamba hajulikani, hata nchi ilikuwa haijui kama anapigana mpaka jana usiku baada ya kutoka matokeo. *(Makofi)*

**SPIKA:** Hata Mbunge wa Tanga alikuwa hana habari!

**MHE. ALLY SALEH ALLY:** Naam Mheshimiwa Spika.

**SPIKA:** Nakubali na neno lako hata Mbunge wa Tanga hakujua maana yake hakupongeza.*(Kicheko)*

**MHE. ALLY SALEH ALLY:** Mheshimiwa Spika, sawa.

**SPIKA:** Endelea Mheshimiwa.

**MHE. ALLY SALEH ALLY:** Mheshimiwa Spika, pia katika Kombe la Dunia mchezaji mwingine kutoka Tanga alijitokeza akichezea timu ya Denmark tukabaki tunauma vidole tu, hatukujua kwamba mchezaji yule yupo na anaweza kuisaidia Tanzania.

Mheshimiwa Spika, je, Mheshimiwa Waziri haoni sasa kuna haja ya kuwa na kanzi data endelevu ili kufuatilia vipaji vya watoto wetu wanaozaliwa nje, kuwashawishi kuja kuchezea Tanzania katika timu mbalimbali? kanzi data endelevu? *(Makofi)*

**SPIKA:** Majibu ya swali hilo Mheshimiwa Waziri wa Habari, Utamaduni Sanaa na Michezo, Mheshimiwa Dkt. Harrison Mwakyembe, tafadhali.

**WAZIRI WA HABARI, UTAMADUNI, SANAA NA MICHEZO:** Mheshimiwa Spika, naomba tu nimtaarifu Mheshimiwa Ally Saleh kwamba mwanamasumbwi Mwakinyo katika tasnia ya michezo tulikuwa tunamfahamu kabla ya ushindi wake mkubwa, alikuwa Bingwa wa *WBA* Bara la Afrika sasa huyu mtu Bingwa wa Afrika, usipomjua sasa na wewe lakini tulikuwa tunamtambua.

Mheshimiwa Spika, lingine nimeeleza kwamba katika Wanamasumbwi 1,854 wa *Welterweight* katika dunia alikuwa wa 174, hapo pia siyo padogo ni pakubwa. Kwa hiyo, tumpongeze tu huyu kijana na tunachukua hatua kweli sasa hivi kuhakikisha kwamba vijana wetu wengi wanaofanya vizuri katika michezo duniani tunawatambua na tunaendeleza vipaji vyao.

Mheshimiwa Spika, naomba nimhakikishie tu Mheshimiwa Ally Saleh kwamba hatua hizo tumeshachukua na utaona baada ya muda siyo mrefu kwamba tunawakusanya wote kuweza kuchangia maendeleo ya michezo hapa nchini.

**SPIKA:** Ahsante sana swali namba 58 la Mheshimiwa Devotha Mathew Minja, sasa linaweza kuulizwa, tafadhali.

Na. 58

**Kuchakaa Kwa Viwanda vya Michezo Vinavyomilikiwa na CCM**

**MHE. TUNZA I. MALAPO (K.n.y MHE. DEVOTHA M. MINJA)** aliuliza:-

Viwanja vingi vya michezo vinavyomilikiwa na Chama cha Mapinduzi vimechakaa kutokana na kutoendelezwa kwa muda mrefu. Mfano, Kiwanja cha SabaSaba Mkoani Morogoro.

Je, Serikali haioni kuna haja ya kubinafsisha viwanja hivyo ili viendelee kutumika katika michezo?

**SPIKA:** Hivyo swali hilo mnauliza kwa sababu gani mbona haliwahusu? Kitanda usichokilalia...; Mheshimiwa Waziri wa Habari, Utamaduni, Sanaa na Michezo, Dkt. Mwakyembe majibu ya swali hili chokozi. *(Kicheko)*

**WAZIRI WA HABARI, UTAMADUNI, SANAA NA MICHEZO** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Devotha Mathew Minja, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Sera ya Maendeleo ya Michezo ya mwaka 1995 inaelekeza kuwa utunzaji wa viwanja utafanywa na taasisi zinazomiki viwanja hivyo. Kwa hiyo, viwanja vinavyomilikiwa na Chama cha Mapinduzi mfano kiwanja cha SabaSaba katika Manispaa ya Morogoro ni sawa na viwanja vingine vya michezo vya taasisi binafsi, mashirika ya umma, vilabu na vyama vya michezo. Hivyo, suala la utunzaji na ukarabati vinabakia kuwa jukumu la mmiliki.

Mheshimiwa Spika, viwanja vyote bila kujali mmiliki wake vinatakiwa kutunzwa vizuri ili vitumike kulingana na makusudio yake. Pale ambapo uwezo haupo inashauriwa kutafuta wabia na wafadhili ili wananchi waendelee kunufaika na rasilimali hiyo.

**SPIKA:** Mhesimiwa Tunza Malapo nilikuona endelea na swali la nyongeza.

**MHE. TUNZA I. MALAPO:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru, nina maswali mawili ya nyongeza.

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa Chama cha Mapinduzi kimeshindwa kuendeleza viwanja vingi vya michezo, ikiwemo kiwanja cha Nangwanda Sijaona katika Manispaaa ya Mtwara Mikindani.

Je, Serikali haioni sasa ni wakati mwafaka wa kurudisha viwanja hivyo Halmashauri kama ilivyofanya kwenye mashamba yasiyoendelezwa ya watu binafsi? *(Makofi)*

Swali langu la pili, kwa kuwa michezo ni afya, michezo ni ajira, na michezo ni furaha. Kwa kuwa chama cha Mapinduzi kimeshindwa kuviendeleza viwanja hivi na kuwafanya wanamichezo wetu wacheze katika mazingira duni...

**SPIKA:** Mheshimiwa Tunza napima hapa maswali yako, unaposema Chama cha Mapinduzi kimeshindwa naona kama unavunja Kanuni hapa, malizia swali lako. *(Kicheko)*

**MHE. TUNZA I. MALAPO:** Mheshimiwa Spika, naomba unisikilize. Michezo ni afya, ni furaha na ni ajira. Kwa kuwa, Chama cha Mapinduzi kimeshindwa kuviendeleza viwanja hivi hatuoni kwamba Chama cha Mapinduzi kina nia ya kudunisha wanamichezo wetu kwa sababu wanapata ajali mbalimbali wanapokuwa wanachezea katika viwanja hivyo? Nakushukuru. *(Makofi)*

**SPIKA:** Bado naangalia Kanuni zangu kama swali hili linakubalika. Majibu ya swali hilo Mheshimiwa Waziri wa Habari, Utamaduni, Sanaa na Michezo Mheshimiwa Dkt. Harrison Mwakyembe, tafadhali. *(Kicheko)*

**WAZIRI WA HABARI, UTAMADUNI, SANAA NA MICHEZO:** Mheshimiwa Spika, kwanza naomba nikuhakikishie kupitia Bunge lako tukufu kwamba, siyo kweli kwamba CCM imeshindwa kwa sababu asilimia 99 ya michezo yote nchini inaendeshwa kwenye viwanja hivyo, sasa kushindwa huko kukoje? Sasa hivi tunaanza Ligi Kuu ya Tanzania na sehemu kubwa ya michezo hiyo itachezwa kwenye viwanja hivyo hivyo.

Mheshimiwa Spika, nakubaliana na wewe kwamba vingi haviko kwenye hali nzuri sana na Wizara ilikuwa imeiachia Shirikisho la Soka nchini kufanya majadiliano na wenye viwanja, sasa tumeona maendeleo siyo ya kasi ya kutosha, Wizara imeamua yenyewe sasa siyo tu kwa kushirikisha Shirikisho la Soka nchini, mashirikisho yote ya michezo nchini, kukaa pamoja na wamiliki tuweze kukubaliana namna ya kuboresha hivi viwanja na kuweza kupata misaada ambayo kwa kawaida itakwenda kwa urahisi zaidi kwa taasisi ambazo zina ubia na Serikali. Tunataka watuachie ubia wawe na ubia na Serikali ili tuweze kurabati viwanja, kama ambavo *FIFA* ilivyoweza kukarabati Kiwanja cha Kaitaba na Kiwanja cha Nyamagana.

**SPIKA:** Sasa Mchungaji Msigwa viwanja vya CCM, haya uliza swali tuone, hata kile cha Iringa cha CCM kile. *(Kicheko)*

**MHE. JOSEPH O. MBILINYI:** Kivuli.

**MHE. MCH. PETER S. MSIGWA:** Mheshimiwa Spika, nikushukuru kwa kunipa nafasi. Swali langu kwa Mheshimiwa Waziri pamoja na majibu yake ya swali la msingi, tukumbuke kwamba viwanja hivi vilitengwa wakati mfumo wa chama kimoja na maeneo mengi yalitengwa na wakoloni, kwa maana ya kwamba wananchi wote wafaidike na maeneo hayo. Chama cha Mapinduzi kime-*take advantage* na kwa kweli kimekuwa hakiendelezi hivyo viwanja.

Mheshimiwa Spika, hamuoni kwamba mnapingana na sera yenu ya kutenda haki na usawa katika nchi kwa kuendelea kupora na kunyang'anya hivo viwanja, kuwadhulumu Watanzania wote ambao walishiriki kutengeneza na kuviandaa viwanja hivyo?

**SPIKA:** Majibu ya swali hilo Mheshimiwa Dkt. Mwakyembe, tafadhali.

**WAZIRI WA HABARI, UTAMADUNI, SANAA NA MICHEZO:** Mheshimiwa Spika, viwanja hivi havikuporwa kwa mtu yeyote, hii dhana ya kuporwa inaondoka kabisa kwenye swali la msingi alilouliza Mheshimiwa Devotha Minja.

Mheshimiwa Spika, naomba tu kukuhakikishia tu kwamba kama kuna hoja ya msingi kwamba kuna kuporwa, maana kuporwa *is a criminal act,* basi naomba hili suala lifikishwe Mahakamani ili liweze kuamuliwa inavyostahili. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mbunge wa Mbeya Mjini bado upo tu? Ule uwanja wa Mbeya si ni wa CCM ule?

**MHE. JOSEPH O. MBILINYI:** Mheshimiwa Spika nimerudi leo, ahsante sana.

Mheshimiwa Spika, ukiacha uporwaji wa viwanja *stadiums*. Kwenye mchakato wa kuhakiki mali zake CCM wamepora *properties* nyingi sana za wananchi, ikiwemo majengo ya zahanati, vilabu vya pombe za kienyeji na kadhalika. Itua Mjini Mbeya wamepora vibanda vya maduka na maeneo ya wazi. *(Kicheko)*

Mheshimiwa Spika, kwa nini Bunge kwa niaba ya wananchi lisichukue hatua za kuzuia uporaji huu wa CCM kwa sababu hapa naongea kuna wazee watano Kata ya Tembela, Jijini Mbeya wako polisi kwa sababu walikuwa wanadai haki ya umiliki wa mali zao zilizoporwa na CCM? *(Makofi)*

**SPIKA:** Hilo swali siyo la Mheshimiwa Waziri, Utamaduni Sanaa na Michezo wala haliendani na swali la Mheshimiwa Devotha Minja, na kwa sababu alichosema Mheshimiwa Mbunge siyo kweli hili nafuta.

Waheshimiwa Wabunge, tunaendelea na Wizara ya Nishati swali la Mheshimiwa Issa Ali Mangungu, Mbunge wa Mbagala kwa niaba yake Mheshimiwa Edwin Ngonyani.

Na. 59

**Usambazaji wa Umeme Kwenye Maeneo Yasiyo ya Vijiji**

**MHE. EDWIN A. NGONYANI (K.n.y. MHE. ISSA A. MANGUNGU)** aliuliza:-

(a) Je, Serikali ina mpango gani wa kusambaza umeme kwenye maeneo ambayo hayamo katika miradi ya umeme vijijini, maeneo kama vile Changanyikeni, Ponde, Malela, Vikindu, Goroka A, B katika Kata ya Tuangoma na Majimatitu A, Vigozi, Machinjioni A, Mponda katika Kata ya Mianzini, Mzala, Kwa Mapunda, Kisewe, Dovya, Sai A, B katika Kata ya Chamazi?

(b) Je, ni lini Serikali itamaliza tatizo la *low voltage* katika Jimbo la Mbagala hasa maeneo ya Kiburugwa,

Kilungule, Charambe, Kijichi, Kibondemaji Chemchem na Tuangoma?

**SPIKA:** Majibu ya swali hilo Mheshimiwa Naibu Waziri Nishati, Mheshimiwa Subira tafadhali.

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Nishati napenda kujibu swali la Mheshimiwa Issa Ali Mangungu, Mbunge wa Mbagala, lenye sehemu (a) na (b) kwa pamoja kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, kazi ya ujenzi wa miundombinu ya kusambaza umeme katika maeneo ya Changanyikeni, Ponde, Malela, Vikindu, Goroka 'A' na Goroka 'B', Dovya Kata ya Tuangoma na maeneo ya Mponda, Vigozi, Churuvi Kata ya Mianzini ilianza Oktoba, 2017 na inatarajiwa kukamilika mwezi Oktoba, 2018.

Mheshimiwa Spika, kazi za mradi zinahusiana ujenzi wa njia ya umeme wa msongo wa kilovoti 33 yenye urefu wa kilometa 12.95, njia ya umeme wa msongo wa kilovoti 0.4 yenye urefu wa kilometa 41.34, pamoja na ufungaji wa transfoma 19 za Kv 100 na Kv 200, gharama ya mradi ni shilingi milioni 523.84 na utekelezaji wake umefikia asilimia 90.

Mheshimiwa Spika, Jimbo la Mbagala hususan maeneo ya Kiburugwa, Kitungule, Charambe, Kijichi, Kibondemaji, Chemchem na Tuangoma kulikuwa na tatizo la uwepo wa umeme mdogo, kuanzia mwezi Juni, 2018 Serikali imechukua hatua za makusudi kuondoa tatizo hilo kwa kuboresha nguvu ya umeme kwenye maeneo hayo na hali ya umeme katika maeneo ya Mbagala imeimarika kwa kiasi kikubwa.

Mheshimiwa Spika, kukamilika kwa ujenzi wa kituo kipya cha kupoza umeme cha msongo wa kilovoti 132/33 chenye uwezo wa Mv 50 Mbagala kilichozinduliwa tarehe

22 Februari, 2018 kimeimarisha hali ya umeme katika maeneo hayo. Ahsante. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa *Engineer* Ngonyani swali la nyongeza.

**MHE. ENG. EDWIN A. NGONYANI:** Mheshimiwa Spika, pamoja na kusahisha jina la eneo la Kitungule badala ya Kitungule isomeke Kilungule.

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Ali Mangungu anaishukuru sana Serikali ya Chama cha Mapinduzi kwa kazi kubwa iliyoifanya katika kipindi hiki cha mwaka mmoja na kwa kweli wanaomba yale maeneo yaliyobakia yakamilishwe, kwa hiyo, eneo la kwanza ni ombi.

Mheshimiwa Spika, pili, ndugu zao wa Namtumbo wanaomba kuna vijiji 70 na miji midogo miwili. Katika miji midogo miwili mji mdogo mmoja tu mitaa yake ina umeme, vinginevyo vijiji vyote 70 pamoja na mitaa ya Mji Mdogo wa Lusewa havina umeme. Pamoja na kwamba dalili zinaonekana lakini muda unapita na hakuna dalili ya umeme kupatikana katika Wilaya hiyo nzima ya Namtumbo.

Ni lini Serikali itawasha umeme katika Wilaya ya Namtumbo?

**SPIKA:** Majibu ya maswali hayo mawili Mheshimiwa Naibu Waziri wa Nishati, Mheshimiwa Subira Khamis Mgalu. *(Makofi)*

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI:** Mheshimiwa Spika, swali la kwanza tumepokea pongezi za Mheshimiwa Mbunge Mheshimiwa Issa Ali Mangungu na Serikali tunampongeza sana Mheshimiwa Mbunge kwa kufuatilia maendeleo ya nishati katika Jimbo lake la Mbagala na ombi lake tumelipokea katika maeneo yaliyosalia kama nilivyosema mradi umekamilika kwa asilimia 90 basi asilimia 10 ndani ya muda mfupi itakamilika.

Swali lake la pili la ndugu wa kutoka Jimbo la Namtumbo. Kama ambavyo Mheshimiwa Mbunge amesema naomba nilitaarifu Bunge lako tukufu na niwapongeze Wabunge wote wa Mkoa wa Ruvuma na Mkoa wa Njombe kwa kuiunga mkono Serikali katika utekelezaji wa mradi mkubwa wa ujenzi wa *line* ya kusafirisha umeme Makambako - Songea yenye urefu kilometa 250. Napenda nimtaarifu Mheshimiwa Mbunge tarehe 01 na tarehe 02 tulifanya ziara kukagua mradi huo na kimsingi mradi umekamilika.

Mheshimiwa Spika, ujenzi wa *substation* tatu Madaba, Songea - Makambako umekamilika, ujenzi wa *line* umekamilika, kinachoendelea sasa hivi ni usambazaji umeme katika maeneo ya vijiji 122, vijiji 60 ni Mkoa wa Ruvuma, na vilivyosalia ni Mkoa wa Njombe. Katika Jimbo lake la Namtumbo takribani vijiji 35 vitapata umeme kupitia mradi huu mkubwa wa ujenzi wa *line* ya Makambako - Songea.

Mheshimiwa Spika, naomba nilitaarifu Bunge lako mwezi huu Septemba tarehe 25 au 26 mradi huu utazindua rasmi na sasa hivi kinachoendelea ni *test* mbalimbali zinazoendelea katika *line* hii. Kuanzia tarehe 15 Septemba tutasafirisha umeme kwa mara ya kwanza kwenye Gridi ya Taifa kuelekea Songea Mkoa wa Ruvuma. Nawashukuru sana wananchi wa Mkoa wa Ruvuma kwa kutuunga mkono na kwa kweli mambo mazuri. Ahsante sana.*(Makofi)*

**SPIKA:** Tunaendelea na swali la Wizara hiyo hiyo linaulizwa na Mheshimiwa Innocent Bilakwate, Mbunge wa Kyerwa.

Na 60

### Kufungua Ofisi za *TANESCO*- Kyerwa

**MHE. INNOCENT S. BILAKWATE** aliuliza:-

Je, ni lini Serikali itafungua Ofisi za *TANESCO* Wilayani Kyerwa ili kuwafikishia karibu wananchi huduma zitolewazo

na *TANESCO,* kama vile kununua umeme, kubadilisha mita na huduma nyingine?

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Nishati napenda kujibu swali la Mheshimiwa Innocent Sebba Bilakwate, Mbunge wa Kyerwa kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, katika hatua ya kuboresha huduma kwa wateja Shirika la Umeme nchini *(TANESCO)* kupitia bajeti ya mwaka 2018/2019 inajenga Ofisi ya *TANESCO* Wilaya ya Kyerwa katika Kiwanja Na. 210 C, kilichopo eneo la Rwenkorongo. Kazi ya ujenzi wa ofisi hiyo inaendelea vizuri na inatarajia kukamika mwezi Januari, 2019.

Mheshimiwa Spika, katika hatua za muda mfupi *TANESCO* imefungua ofisi katika Mji wa Nkwenda, kwa ajili ya kuwahudumia wateja wakati kazi ya ujenzi wa ofisi mpya inaendelea. Kwa sasa Meneja wa *TANESCO* Wilaya ya Misenyi pamoja watumishi wengine watatu, wanaendelea kutoa huduma kwa wateja wa maeneo mbalimbali ya Wilaya ya Kyerwa kupitia ofisi hiyo. Ahsante.

**SPIKA:** Mheshimiwa Bilakwate.

**MHE. INNOCENT S. BILAKWATE:** Mheshimiwa Spika, ahsante kunipa nafasi kuuliza maswali mawili ya nyongeza.

Mheshimiwa Spika, mahitaji ya umeme kwa Kyerwa ni makubwa sana, yako maeneo mengi ambayo hayafikiwa kabisa kama Kata ya Bugomola, Kibale, Businde na Bugara na maeneo mengine mengi hayajafikiwa. Ni kwa nini Wizara isiruhusu *TANESCO, REA* wanapomaliza kupitisha *line* kuu, Wizara isiruhusu *TANESCO* wakaanza kuwafungia umeme wananchi ambao wanahitaji umeme?

Swali la pili, *REA* Awamu ya Pili ambayo kwetu Kyerwa ni *REA* Awamu ya Kwanza kwa sababu ndipo umeme ulipopelekwa huyu Mkandarasi amesuasua sana mpaka sasa

ameshindwa maeneo mengi, wako wananchi wengi ambao wamelipia mpaka sasa hawajafungiwa miaka miwili.

Je, ni hatua zipi zinachukuliwa kwa Mkandarasi huyu ambaye inaonekana ameshindwa kufanya kazi? *(Makofi)*

**SPIKA:** Majibu ya swali hilo Mheshimiwa Naibu Waziri Nishati, tafadhali.

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI:** Mheshimiwa Spika, napenda kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Bilakwate naye pia nimpongeze kwa namna ambavyo amefuatilia masuala la nishati katika Jimbo lake.

Mheshimiwa Spika, swali lake la kwanza lilijielekeza kwenye mahitaji ya umeme, kwa nini *TANESCO* isiendelee kuwaunganisha wananchi wa maeneo hayo wanaopenda umeme. Napenda nimtaarifu Mheshimiwa Mbunge kwamba ni kweli katika Mkoa wa Kagera, Mkoa ambao pia ulikuwa haujaunganishwa kwenye gridi ya Taifa tumeunganisha Wilaya za Ngara mpaka Muleba na tunatarajia kukamilisha mpaka Bukoba Mjini.

Mheshimiwa Spika, kutokana na uunganishwaji wa gridi ya Taifa katika maeneo hayo kumejitokeza mahitaji na tumeendelea kuwapa maelekezo *TANESCO* kwamba inapotokea fursa siyo lazima kusubiri miradi ya *REA* Awamu ya Tatu. Kwa hiyo, kama kweli wapo wananchi wa Wilaya ya Kyerwa wanahitaji umeme na wao hoja siyo kusubiri umeme wa *REA* ambapo una bei nafuu wako tayari kulipia hata gharama za kuunganishwa umeme na *TANESCO,* naielekeza *TANESCO* ifanye upembuzi yakinifu na iwapelekee umeme wananchi hao kwasababu wao kwao umeme hawaangalii hoja kwamba ni wa *REA* au ni umeme kupitia *TANESCO.*

Mheshimiwa Spika, swali lake la pili, natambua Kata alizozitaja Mheshimiwa na ni kweli mpaka sasa hivi hazijasambaziwa umeme. Natambua uwepo wa Mkandarasi Makuroi katika Mkoa wa Kagera, lakini ni ukweli

nakiri kwamba katika Wilaya zingine mkandarasi yule hajafanya vizuri, naomba nimthibitishie Mheshimiwa Mbunge kwamba tulimuita Makuroi kwa sababu anafanya pia na Mkoa wa Rukwa, na mimi nilipata fursa ya kutembelea Mkoa wa Rukwa nikaona ni namna gani anavyolegalega lakini kwa sasa ameshaagiza magari na nimeyathibitisha ana magari mengi tu ya kusambaza nguzo na tulithibisha *order* ambazo amezitoa katika viwanda mbalimbali vya nguzo vya Mkoa wa Iringa, kwa sasa hivi kwa kweli tumemuelekeza na wakandarasi wote wa miradi hii kwamba lazima kila Wilaya kuwe na genge lake na wasijielekeze sehemu moja.

Kwa hiyo, naomba nimthibitishe Mheshimiwa Mbunge baada ya jibu au baada ya kikao hiki tukutane ili tuendelee na mikakati yakuwasimamia wakandarasi wote. Ahsante.

**SPIKA:** Nilikuona Mheshimiwa Mbunge wa Tarime Mjini uliza swali.

**MHE. ESTHER N. MATIKO:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru.

Mheshimiwa Spika, Jimbo la Tarime Mjini, Kata za Nkende, Kenyemanyori, Kitare, Nyamisangura na Turwa pamoja na Nyandoto hazina umeme kabisa, Bunge lililopita niliuliza swali kama hili na Naibu Waziri akaahidi atatembelea Tarime ili kuweza kuona wakandarasi wa *REA* ambao tangu mwaka 2016 walitakiwa watekeleze huu mradi, lakini mpaka leo ni Kata ya Nyandoto ndiyo tumeona sasa wameanza kufanyakazi.

Je, ni kwa nini Naibu Waziri hukuweza kutekeleza ile ahadi ambayo uliahidi kwa wana Tarime ili waweze kupata huu umeme?

**SPIKA:** Majibu ya swali hilo Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI:** Mheshimiwa Spika, kwanza namshukuru kwa kutambua kwamba kazi imeanza ka Kata ya Nyandoto kama alivyoitaja, naomba

nimthibitishie Mheshimiwa Mbunge kuwa ahadi yangu ya kutembelea Jimbo la Tarime Mjini na Mkoa wa Mara iko pale pale ila kutokana tu muingiliano wa ratiba, lakini kwa kuwa kazi zetu ziko *site* naomba nimthibitishie baada ya Bunge hili nitatembelea Wilaya hiyo ya Tarime na Wilaya zingine za Mkoa wa Mara kuhamasisha na kukagua miradi hii na kuwapa shime wakandarasi wafanyekazi kwa haraka na kama inavyokusudiwa. Ahsante.

**SPIKA:** Ahsante sana. Kasulu Mjini kuna neno?

**MHE. DANIEL N. NSANZUGWANKO:** Mheshimiwa Spika, nami naomba niulize swali dogo la nyongeza.

Mheshimiwa Spika, Mkoa wa Kigoma tuko *off grid*, kuna mradi wetu mkubwa sana wa Malagarasi ambao tuliambiwa ungeanza *quarter* hii ya kwanza ya *financial year* hii. Ningependa kujua kutoka kwa Waziri ni lini mradi sasa wa *Malagarasi mini-hydro* utaanza ili tuanze kuwa na chanzo cha uhakika cha umeme katika Mkoa wa Kigoma?

**SPIKA:** Majibu ya swali hilo Mheshimiwa Naibu Waziri ni lini?

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi. Ameuliza ni lini mradi huu wa Malagarasi utaanza. Kama ambavyo tuliwasilisha kwenye bajeti yetu ya Bunge hili na ikaidhinishwa na Bunge lako tukufu kwamba mradi huu utaanza kwa mwaka huu wa fedha 2018/2019, lakini jambo kubwa hapa amelizungumzia kwamba Mkoa huu upo *off grid,* naomba nilitaarifu Bunge lako tukufu, hivi karibuni Benki ya Dunia imetoa pesa kwa ajili ya ujenzi wa *line* inayotoka Iringa – Mbeya - Sumbawanga lakini pia kipande cha Nyakanazi - Kigoma kimepata ufadhili wa Benki ya Maendeleo ya Afrika, kwa hiyo, kwa vyovyote vile Mkoa huu tunaanza kuingia kwenye gridi kutokana na miradi hiyo, wananchi wa Kigoma niwathibitishie kwamba kwa kweli Serikali ya Awamu ya Tano inafanyakazi kuhakikisha Mkoa huu unaingia kwenye Gridi ya Taifa. Ahsante. *(Makofi)*

**SPIKA:** Tunakwenda Wizara ya Mambo ya Ndani. Mheshimiwa Dalali Kafumu uliza swali lako kwa niaba yake, Mheshimiwa Mchemba.

Na. 61

**Ujenzi wa Gereza Wilaya ya Igunga**

**MHE. MWANNE I. MCHEMBA (K.n.y. MHE. DKT. DALALY P. KAFUMU)** aliuliza:-

Gereza la Wilaya ya Igunga linakabiliwa na changamoto mbalimbali zikiwemo ukosefu wa ngome, hakuna Ofisi za Mkuu wa Gereza na Utawala, hakuna nyumba za askari lakini pia gereza hilo ni dogo na linahudumia wafungwa na mahabusu wa kiume tu, wafungwa na mahabusu wa kike hupelekwa Gereza Wilaya ya Nzega.

Je, ni lini Serikali itajenga Gereza la Wilaya ya Igunga ili liweze kutoa huduma bora kwa wafungwa mahabusu Wilayani Igunga?

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Dalaly Peter Kafumu, Mbunge wa Igunga, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, ujenzi wa gereza la mahabusu Wilaya ya Igunga ulianza mwaka 2003 ili kuwapokea na kuwahifadhi mahabusu na wafungwa kutoka Wilaya ya Igunga ambao walikuwa wakipelekwa na kuhifadhiwa katika Gereza la Nzega ambalo nalo ni dogo na hivyo kusababisha msongamano mkubwa. Ujenzi huo bado haujakamilika kwani unafanyika kwa awamu kulingana na upatikanaji wa fedha.

Mheshimiwa Spika, ujenzi wa gereza hilo utakapokamilika kutakuwa na maeneo yote muhimu yanayotakiwa kwenye gereza kama vile ngome, ofisi,

mabweni ya wafungwa na mahabusu, jiko, bwalo la chakula na litakuwa na uwezo wa kuhifadhi wafungwa na mahabusu wa jinsia zote.

**SPIKA:** Mheshimiwa muuliza swali uliza swali la nyongeza.

**MHE. MWANNE I. MCHEMBA:** Mheshimiwa Spika, ahsante kwa kunipa nafasi na mimi niulize swali dogo la nyongeza.

Kwa kuwa, Serikali imekiri kutokuwa na nyumba ya mahabusu au kutokuwa na mahabusu ya wanawake katika Wilaya ya Igunga na kuwasababishia ndugu kutokuwasalimia na kutokujua afya zao kwa hao mahabusu ambao ni wanawake na kuwanyima haki zote.

Je, Serikali iko tayari kujenga mahabusu maalum ya wanawake kama dharura ili kuwaondolea adhabu wanayoipata wanawake na usumbufu wa kutoka Igunga kwenda Nzega mara kwa mara? Naiomba Serikali iangalie kwa jicho la huruma.

**SPIKA:** Majibu ya swali hilo Mheshimiwa Naibu Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi. Mahabusu wa Kinyamwezi kwa akina mama!

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Spika, nilizungumza wakati najibu swali la msingi kwamba ujenzi wa gereza hili ambao ulianza mwaka 2003 haujakamilika na nilisema kwamba utakapokuwa umekamilika basi changamoto ya mahabusu kwa wanawake itakuwa imepatiwa ufumbuzi. Kwa hiyo, nimuombe Mheshimiwa Mbunge astahamili wakati ambapo tunajiandaa kutafuta fedha kwa ajili ya kujenga gereza hili ili tuweze kupata ufumbuzi.

Mheshimiwa Spika, kuna jitihada ambazo tumeweza kuchukua katika baadhi ya maeneo mengine nchini ambapo tumeweza kutumia rasilimali za maeneo husika pamoja na

wafungwa na nguvu na ushirikiano wa wananchi pamoja na Wabunge wa maeneo husika kuhamasisha katika ujenzi wa mabweni. Naomba nichukue fursa hii kumuahidi Mheshimiwa Mbunge kwamba nitafanya ziara rasmi katika gereza hili ili tushirikiane pamona na Mbunge wa Jimbo hilo kuona jinsi gani tunaweza tukafanya kutafuta njia za hatua za dharura kuweza kukabiliana na changamoto hii wakati tukisubiri fedha za bajeti za ujenzi wa gereza hili.

**SPIKA:** Tunaendelea na swali la Mheshimiwa Bupe Mwakang'ata. Mheshimiwa Kafumu umechelewa bwana! Mheshimiwa Bupe Mwakang'ata kwa niaba yake Dkt. Ishengoma endelea.

Na. 62

**Manyanyaso kwa Waendesha Bodaboda Nchini**

**MHE. DKT. CHRISTINE G. ISHENGOMA (K.n.y. MHE. BUPE N. MWAKANG'ATA)** aliuliza:-

Vijana wengi wamejiajiri katika shughuli mbalimbali ikiwemo waendesha bodaboda, lakini waendesha bodaboda hao wamekuwa wakisumbuliwa sana na askari wa barabarani kwa kutozwa faini ambazo muda mwingine hazina maana na hivyo kuwakatisha tamaa.

Je, Serikali inachukua hatua gani ili kudhibiti vijana hawa wasinyanyaswe?

**SPIKA:** Majibu ya swali hilo Mheshimiwa Naibu Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi, tafadhali.

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Bupe Nelson Mwakang'ata, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Serikali inatambua mchango mkubwa wa biashara ya pikipiki kwa huduma ya usafiri kwa jamii ambapo vijana wengi wamepata ajira hivyo kukuza kipato chao. Umuhimu mkubwa wa usafiri huu hauwaondolei wahusika wa usafiri huu wajibu wa kuzingatia Sheria na Kanuni za Usalama Barabarani ili kuufanya usafiri huu kuwa salama kwa watumiaji.

Mheshimiwa Spika, pamoja na kwamba Jeshi la Polisi litaendelea kuwachukulia hatua wale wote ambao wanakiuka Sheria na Kanuni za usalama barabarani, ni rai yangu kwa wale wote ambao wanahisi kuonewa ama kunyanyaswa wakati wakitumia usafiri huu kutoa taarifa kwa Jeshi la Polisi ama Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi ili hatua stahiki ziweze kuchukuliwa.

**SPIKA:** Nimekuona Mheshimiwa, uliza swali la nyongeza.

**MHE. DKT. CHRISTINE G. ISHENGOMA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipatia nafasi, naomba niulize maswali mawili ya nyongeza.

Swali la kwanza, namshukuru Naibu Waziri amejibu vizuri lakini waendesha bodaboda hawa wengi hawana ujuzi wa Sheria na Kanuni za Barabarani. Je, kuna mkakati gani wa kuwapatia elimu hii ili kusudi waweze kuepukana na usumbufu na faini wanazozipata?

Swali la pili, kwa kuwa usafiri wa bodaboda unatoa usafiri kwa watu wengi lakini waendesha bodaboda hawa hawana leseni na hawana ujuzi wa kuendesha pikipiki hizi, kiasi kwamba wanasababaisha ajali nyingi na vifo.

Je, Serikali ina mpango gani wa kudhibiti tatizo hili? Ahsante sana.

**SPIKA:** Majibu ya swali hilo la Dkt. Christine Ishengoma, tafadhali Mheshimiwa Naibu Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi.

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Spika, kuhusiana na suala la elimu kuna jitihada mbalimbali ambazo zinafanyika katika kutoa elimu kwa waendesha bodaboda. Miongoni mwa jitihada hizo ni kwanza Jeshi la Polisi limekuwa likitumia utaratibu wa kuwafuata kwenye vijiwe vyao hawa ambao wanaendesha bodaboda na kuwapa elimu, pia kupitia vipindi mbalimbali ambavyo vinaandaliwa kwenye *television,* kwenye *radio* na kupitia kwenye wiki ya Nenda kwa Usalama Barabarani ambavyo vinatumika kwa ajili ya kutoa elimu, kwa hiyo jitihada za kutoa elimu zinafanyika kwa kiwango kikubwa sana.

Mheshimiwa Spika, kuhusiana na swali lake la pili kwamba vijana ambao wanaendesha bodaboda bila leseni. Kwanza nichukua fursa hii kuendelea kusisitiza kwamba kuendesha bodaboda ama chombo chochote cha usafiri bila leseni ni kuvunja sheria na hivyo basi Jeshi la Polisi litaendelea kuwachukulia hatua wale wote ambao wanakiuka sheria za nchi katika eneo la usalama barabarani ikiwemo kuendesha bodaboda bila leseni. Kwa hiyo, nitoe wito kwa vijana wetu ambao hawana leseni kufuata taratibu za Kisheria ili waweze kujipatia leseni.

**SPIKA:** Tunaendelea na Wizara ya Afya, Maendleo ya Jamii, JInsia, Wazee na Watoto, swali la Mheshimiwa Fatma Hassan Toufiq.

Na. 63

**Madhara ya Vipodozi kwa Wanawake**

**MHE. FATMA H. TOUFIQ** aliuliza:-

Baadhi ya wanawake wameathirika na vipodozi vikiwemo kucha na kope kubandika.

Je, ni wanawake wangapi wameathirika macho kutokana na matumizi ya kope bandia?

**SPIKA:** Majibu ya swali hilo Mheshimiwa Naibu Waziri wa Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto, Dkt. Ndugulile.

**NAIBU WAZIRI WA AFYA, MAENDELEO YA JAMII, JINSIA, WAZEE NA WATOTO** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto naomba kujibu swali la Mheshimiwa Fatma Hassan Toufiq, Mbunge wa Viti maalum kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, ieleweke kuwa kucha za kubandika na kope za kubadnika siyo vipodozi. Kwa mujibu wa Sheria ya Chakula, Dawa na Vipodozi, Sura ya 219 inayosimamiwa na Mamlaka ya Chakula na Dawa *(TFDA)* kipodozo ni kitu chochote kinachotumika kwenye mwili au sehemu ya mwili kwa njia ya kupaka, kumimina, kufukiza, kunyunyiza au kupuliza kwa ajili ya kusafisha, kuremba, kupamba, kuongeza uzuri, mvuto au kubadili muonekano. Takribani wagonjwa 700 kwa mwaka hupokelewa katika Hospitali ya Taifa ya Muhimbili...

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, tumsikilize Mheshimiwa Naibu Waziri anapojibu, tupunguze sauti hizi na hili swali ni muhimu sana. Mheshimiwa Naibu Waziri endelea.

**NAIBU WAZIRI WA AFYA, MAENDELEO YA JAMII, JINSIA, WAZEE NA WATOTO:** Mheshimiwa Spika, takribani wagonjwa 700 kwa mwaka hupokelewa katika Hospitali ya Taifa Muhimbili wakiwa na matatizo ya ngozi yanayotokana na kumeza vidonge vinavyobadili rangi ya mwili mzima pamoja na vipodozi vyenye kemikali. Imeelezwa kuwa watu hao wapo kwenye hatari ya kupata magonjwa ya saratani na magonjwa ya ngozi.

Mheshimiwa Spika, kwa sasa Wizara kupitia *TFDA* haina utaratibu wa kudhibiti kope wala kucha za kubandika kwa sababu hakuna sheria inayoipa mamlaka ya kudhibiti bidhaa hizo. Hivyo basi, kutokana na hilo, Wizara kwa kupitia

*TFDA* haina takwimu za kuonesha madhara yanayotokana na matumizi ya bidhaa hizo kwa kuwa hakuna mfumo wa kupokea taarifa za matumizi ya bidhaa husika.

**SPIKA:** Mheshimiwa Toufiq swali la nyongeza tafadhali.

**MHE. FATMA H. TOUFIQ:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana kwa kunipa fursa ya kuuliza mswali ya nyongeza, nina maswali mawili ya nyongeza namshukuru Mheshimiwa Naibu Waziri kwa majibu yake.

Mheshimiwa Spika, pamoja na kuwa Wizara haidhibiti kope bandia na kucha bandia lakini bado zina madhara makubwa sana kwa watumiaji hasa wanawake.

Je, Serikali haioni umefikia wakati kupitia Wizara ya Afya na *TFDA* kufanya utafiti ili kubaini ukubwa wa tatizo?*(Makofi)*

Swali la pili, kwa kuwa Mheshimiwa Waziri amekiri kuwa wagonjwa takribani 700 hupelekwa Muhimbili kutokana na athari za kujibadili rangi.

Je, Serikali haioni umefikia wakati kuwa na mpango kabambe wa kuihabarisha jamii na hasa wanawake kubaki na rangi zao za asili na kuepuka kutumia vipodozi vyenye madhara na hasa wanaume wawe ndiyo waelimishaji? Ahsante sana. *(Makofi)*

**SPIKA:** Majibu ya swali hilo muhimu Mheshimiwa Naibu Waziri wa Afya, tafadhali.

**NAIBU WAZIRI WA AFYA, MAENDELEO YA JAMII, JINSIA, WAZEE NA WATOTO:** Mheshimiwa Spika, tunapokea ushauri wa Mheshimiwa Mbunge wa kufanya tafiti na kubaini madhara ya kucha na kope bandia na baada ya hapo sasa tutaanza kuwa na mfumo wa kuwa na takwimu mbalimbali kuhusiana na madhara haya.

Mheshimiwa Spika, swali la pili ameuliza je, Serikali hatuoni umuhimu wa kuhabarisha jamii kuhusiana na vipodozi ambavyo vinabadilisha rangi ya mwili. Naomba nitumie fursa hii kutoa elimu kidogo kwa Bunge lako tukufu.

Mheshimiwa Spika, Mwenyezi Mungu alituumba na hizi ngozi zetu hizi kwa makusudi yake mahsusi. Kwanza ngozi hizi ni moja ya kinga ya mionzi ya *ultraviolets* ambayo ngozi inatukinga dhidi yake, lakini pili, ngozi hii ni sehemu ya kinga za mwili ama kizuizi cha kinga ya mwili pale wadudu ama bakteria ama vijidudu vya aina yoyote vinapotaka kuingia katika miili yetu vinazuiliwa na ngozi zetu. Tunapokuwa tunajichubua ngozi zetu tunaziondoa kinga hizi na tunaondoa kinga hii dhidi ya miale hi ya *ultraviolet,* lakini tunaondoa kinga hii dhidi ya vimelea vya wadudu hatari.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo mtu ambaye anafanya kujichubua ngozi anaingia katika madhara ya magonjwa ya ngozi, madhara ya kupata saratani ambayo inatokana na vimelea vilevile miale ya jua. Kwa hiyo, mimi naomba kutoa rai tu kwa Watanzania wote ambao wanatusikiliza na Waheshimiwa Wabunge ngozi zetu za asili ni urembo uliotosha, kama Wabunge tulizingatie hilo na wanaume tushiriki, rangi ya asili... naishia hapo *(Makofi/Kicheko)*

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, swali hili kwa vile ni muhimu sana na Mheshimiwa Toufiq alikuwa anaitaka Serikali ichukue hatua na Mheshimiwa Waziri akasema Wabunge na sisi tuwe mfano, basi kwa mamlaka mliyonipa napiga marufuku kabisa Wabunge kuingia humu ndani wenye kucha za kubandika na kope za kubandika. *(Makofi/Kicheko)*

**MHE. PAULINE P. GEKUL:** Na nywele.

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, lakini kwa wale wanaojichubua bado naendelea kuchukua maoni. *(Makofi/ Kicheko)*

Mheshimiwa Stanslaus Shing'oma Mabula, Mbunge wa Nyamagana, swali linalofuata.

Na. 64

**Watoto Wanaoishi Kwenye Mazingira Magumu**

**MHE. STANSLAUS S. MABULA** aliuliza:-

Tatizo la watoto wanaoishi kwenye mazingira magumu linaendelea kuwa kubwa.

(a) Je, Serikali ina mpango gani wa kutatua changamoto hii kubwa hasa katika Jiji la Mwanza?

(b) Je, Serikali haioni umuhimu wa kukijengea uwezo Kitengo cha Ustawi wa Jamii kukabiliana na changamoto hii?

**NAIBU WAZIRI WA AFYA, MAENDELEO YA JAMII, JINSIA, WAZEE NA WATOTO** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kabla sijajibu swali hili la msingi kwanza nikushukuru sana na kukupongeza na wewe kwa kushirikiana pamoja na Serikali katika kuhakikisha kwamba tunarudisha ule uzuri wa asili, nakushukuru na kukupongeza sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto naomba kujibu swali la Mheshimiwa Stanslaus Shing'oma Mabula, Mbunge wa Nyamagana kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, kwa mujibu wa Sheria ya Mtoto Na. 21 ya mwaka 2009, kifungu cha 16, msamiati unaotumika katika kubainisha watoto hao ni watoto walio katika mazingira hatarishi na si watoto wanaoishi katika mazingira magumu. Katika kukabiliana na changamoto hii, Serikali inatekeleza Mpango wa Kutokomeza Ukatili Dhidi ya Wanawake na Watoto wa mwaka 2017/2018 ambao utaisha 2021/2022, ambapo umebainisha majukumu mbalimbali ya wadau katika kuondoa changamoto hiyo. Moja ya shabaha ya mpango huo ni kupunguza idadi ya watoto wanaoishi

katika mazingira hatarishi kwa asilimia 50 ifikapo mwaka 2021/2022 ikiwemo katika Jiji la Mwanza.

Mheshimiwa Spika, katika kupambana na ukatili dhidi ya wanawake na watoto, Jiji la Mwanza limeunda kamati 11 za ulinzi na usalama kwa wanawake na watoto katika mitaa 11; makao ya watoto manne yamesajiliwa; jumla ya watoto walio katika mazingira magumu (hatarishi) 5,843 walibainishwa, wakike wakiwa 3,337 na wanaume, 2,506. Kati ya watoto hao, jumla ya watoto 2,381 walitengenezewa kadi za bima ya *TIKA*, watoto 27 walipelekwa katika Vyuo vya *VETA* na watoto 741 wanasomeshwa katika shule za sekondari. Aidha, zoezi la utambuzi wa watoto wanaoishi na kufanya kazi mitaani katika kata zote 18 umefanyika mwaka 2018. Jumla ya watoto 426 wanawake wakiwa ni 21 na wanaume 405 walitambuliwa. Kati yao watoto 135 walipelekwa kwenye makao ya watoto ya muda, watoto 120 waliunganishwa na familia zao, watoto 165 walirejeshwa kuendelea na masomo na watoto 323 walipata huduma za matibabu.

Mheshimiwa Spika, Serikali kwa kuona umuhimu wa huduma za ustawi wa jamii, imeanzisha Kitengo cha Ustawi wa Jamii katika Ofisi ya Rais, TAMISEMI, lengo likiwa ni kuboresha huduma hizi katika Mamlaka za Serikali za Mitaa. Aidha, Serikali imeendelea kuwajengea uwezo Maafisa Ustawi wa Jamii katika nyanja mbalimbali ikiwa ni pamoja na ulinzi na usalama wa mtoto, haki za mtoto na uendeshaji wa mashauri ya watoto. Serikali pia imeimarisha mipango ya bajeti katika Mamlaka za Serikali za Mitaa kwa kuanzisha kifungu cha malipo *(cost center)* na kuingiza huduma za ustawi wa jamii katika mfumo ulioboreshwa wa mipango na bajeti katika Mamlaka ya Serikali za Mitaa *(Improved Plan Rep.). (Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Mabula swali la nyongeza tafadhali.

**MHE. STANSLAUS S. MABULA**: Mheshimiwa Spika, nashukuru na ninamshukuru Naibu Waziri kwa majibu.

Mheshimiwa Spika, Jiji la Mwanza ni moja kati ya majiji yanayokuwa kwa kasi sana hapa nchini na hasa kwa ongezeko la watu na kasi ya ongezeko la watoto wanaoishi kwenye mazingira hatarishi inaendelea kuwa kubwa sana.

Sasa ningependa kumuuliza Mheshimiwa Naibu Waziri, kasi ya idadi ya uundaji wa kamati hizi za ulinzi na usalama; kamati 11 kwenye mitaa11 peke yake kati ya mtaa 175, anadhani kasi hii inatosheleza kukabiliana na changamoto hii ambayo ipo katika Jiji la Mwanza na maeneo mengine?

Mheshimiwa Spika, lakini swali la pili, tunafahamu kwamba pamoja na tafiti nyingi ambazo zimefanywa moja ya jambo kubwa ni hao wazazi kuwatumikisha watoto walioko kwenye mazingira yanayoonekana ni hatarishi. Nini sasa mkakati wa Serikali madhubuti kwa ajili ya wazazi wanaowatumikisha watoto na mifano ipo. Ukienda pale Dar es Salaam ukiwa unapita barabara ya Ali Hassan Mwinyi, barabara ya Nyerere pale Mwanza na Kenyatta wako wazazi wana kaa kando ya barabara wanatuma watoto kwenda kuomba magari yanaposimama na watoto wanapopewa wanapeleka kwa wazazi wao. Nini mkakati wa Serikali kukomesha masuala yote? *(Makofi)*

**SPIKA**: Mheshimiwa Naibu Waziri Afya, ni kweli katika Jiji la Mwanza watoto hawa wa mazingira magumu ni wengi sana. Majibu Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA AFYA, MAENDELEO YA JAMII, JINSIA, WAZEE NA WATOTO:** Mheshimiwa Spika, ni kweli kasi hii ya uanzishaji wa kamati za ulinzi wa wanawake na watoto bado inasuasua.

Naomba nitumie fursa hii kuwahimiza na kuwaagiza Wakuu wa Mikoa na Wakuu wa Wilaya kuhakikisha kwamba wanatekeleza agizo la Serikali la kuanzisha kamati za ulinzi kwa wanawake na watoto ambayo iko katika mpango wa mkakati wetu wa kitaifa wa kutokomeza ukatili wa kijinsia dhidi ya wanawake na watoto. Tungependa kuona kabla

ya mwaka huu kuisha kamati hizi zimeanzishwa katika ngazi zote kuanzia ngazi ya taifa mpaka katika ngazi ya vitongoji.

Mheshimiwa Spika, swali la pili la Mheshimiwa Mabula lilikuwa linauliza kuhusiana na wazazi kuwatumikisha watoto, kwa maana ya omba omba. Watoto wana haki zao za msingi ambazo zimebainishwa kisheria katika sheria hii ya mtoto ya mwaka 2009. Baadhi ya haki hizi za mtoto ni pamoja na haki ya kutunzwa, haki ya kulindwa, na haki ya kutokutumikishwa kazi nzito.

Sasa Mheshimiwa Mbunge ametuuliza nini sisi kama Serikali tunafanya. Nimeeleza kwamba tumetengeneza mpango mkakati wa kutokomeza ukatili dhidi ya wanawake na watoto na moja ya mkakati wetu ni kuhakikisha kwamba ukatili huu na kutumikishwa huku kwa watoto kunadhibitiwa kupitia mpango mkakati huu.

Vilevile kwa kupitia hizi kamati za ulinzi wa wanawake na watoto tunatarajia kwamba zikiweza kufanya kazi vizuri hii ni moja ya changamoto ambayo inaweza ikatatuliwa kwa kupitia kamati hizi.

**SPIKA:** Mheshimiwa Khadija Nassir nilikuona, swali fupi la nyongeza.

**MHE. KHADIJA NASSIR ALI:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kuniona. Kutokana na mazingira halisi ya watoto hawa *chances* za kupata maambukizi ya UKIMWI ni kubwa sana. Serikali sasa haioni umuhimu wa kuangalia afya za watoto hao kabla ya kuwapatia *settlement* ili kuepusha maambukizi mapya katika jamii? Ahsante.

**SPIKA**: Majibu ya swali hilo Mheshimiwa Naibu Waziri tafadhali.

**NAIBU WAZIRI WA AFYA, MAENDELEO YA JAMII, JINSIA, WAZEE NA WATOTO:** Mheshimiwa Spika, tunatambua kwamba watoto ambao wanaishi katika mazingira hatarishi wako katika *risk* kubwa zaidi ya kupata ya kupata

maambukizi ya magojwa mbalimbali za zinaa ikiwa ni pamoja na ugonjwa wa UKIMWI. Sisi kama Serikali mkakati wa kwanza ni kuhakikisha kwamba watoto hawa wanapata malezi mazuri ya familia zao na pale inaposhindikana jamii inahusika kabla ya sisi kama Serikali kuja kuchukua majukumu ya malezi haya.

Mheshimiwa Spika, vilevile mimi niendelee kuwaomba, kwa sababu watoto hawa wengi wako kule mitaani na wako katika jamii zetu, tuombe tu kwamba sisi kama jamii tushirikiane na Serikali katika kuhakikisha watoto hawa wanapata malezi stahiki. Kama Serikali tuna mpango mkakati mbalimbali ya kuzuia maambukizi ya UKIMWI.

Kwa mujibu wa takwimu za hali ya viashiria hali ya UKIMWI ya mwaka 2017 imeonesha kwamba vijana nao wamekuwa katika *risk* kubwa sana ya kupata maambukizi ya UKIMWI. Hilo tumelitambua tumeweka mipango mikakati mbalimbali ya kuwafikia na kufanya upimaji, lakini vile vile tumeweka mkakati wa kuhakikisha kwamba sasa hata ile dawa kinga ya *pre exposure for prophylaxis* tunaweza kuwapatia kwa baadhi ya makundi ikiwa ni pamoja na vijana.

**SPIKA:** Swali linalofuata Wizara hii hii ya Afya Mheshimiwa Amina Nassor Makilagi uliza swali lako.

Na. 65

**Uwepo wa Sheria Kali Kuwabana Wazazi Wanaowatelekeza Watoto**

**MHE. AMINA N. MAKILAGI** aliuliza:-

Je, Serikali ina mkakati gani wa kuweka sheria kali zitakazowabana wazazi ambao wamekuwa wakitelekeza watoto na familia zao?

**NAIBU WAZIRI WA AFYA, MAENDELEO YA JAMII, JINSIA, WAZEE NA WATOTO** alijibu:-

Mheshimiwa Spika kwa niaba ya Waziri wa Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto naomba kujibu swali la Mheshimiwa Amina Nassor Makilagi, Mbunge wa Viti Maalum kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, matunzo, malezi na ulinzi wa mtoto ni haki ya mtoto kwa mujibu wa Sheria Na. 21 ya mwaka 2009. Aidha, kifungu cha 7 mpaka cha 9 kinatoa majukumu kwa mzazi/mlezi na mtu yeyote mwenye jukumu la kumlea mtoto kuhakikisha kwamba anawatunza na kuwalea watoto ikiwemo kuwapatia huduma zote muhimu kama chakula, malazi, mavazi, elimu na kuwalinda na vitendo vya nyanyasaji, ukatili, unyonyaji na utelekezaji. Kifungu cha 14 cha Sheria ya Mtoto kinatoa adhabu kwa mzazi/mlezi yeyote atakayekiuka kifungu hiki atatozwa faini isiyozidi shilingi milioni tano au kifungo kisichozidi miezi sita au vyote viwili kwa pamoja. Katika kipindi cha mwaka 2016/2017 jumla ya mashauri 6,557 yanayohusu matunzo na malezi ya watoto na wanawake yalishughulikiwa katika ngazi mbalimbali za Halmashauri na Serikali za Mitaa.

Mheshimiwa Spika, Serikali inatoa wito kwa wazazi/walezi na wote wenye jukumu la kutoa malezi na matunzo kwa watoto wahakikishe wanatimiza wajibu wao kikamilifu. Vilevile familia zote ambazo zimetelekezwa zitoe taarifa katika Ofisi za Ustawi wa Jamii zilizoko katika Halmashauri wanapoishi ili mashauri yao yaweze kusikilizwa na watoto kupata huduma stahiki kwa ajili ya makuzi yao.

Mheshimiwa Spika, natoa wito kwa Maafisa Ustawi wa Jamii katika ngazi zote za Serikali kuhakikisha kuwa wanashughulikia kwa haraka mashauri yanayowasilishwa kwenye ofisi zao kwa kutumia sheria na taratibu zilizopo.

**SPIKA:** Mheshimiwa Amina Makilagi swali la nyongeza.

**MHE. AMINA N. MAKILAGI:** Mheshimiwa Spika, ahsante. Pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Naibu Waziri, hapa nitoe ombi kwamba ni vizuri akatuletea takwimu hizi kwa maandishi kwa sababu tatizo la kutelekeza watoto

ni kubwa sana katika nchi yetu, na mfano ni pale Mheshimiwa Mkuu wa Mkoa wa Dar es Salaama alipofanya zoezi la kuwatambua watoto waliotelekezwa. Nilikuwa naomba hapa atuletee kwa maandishi.

Mheshimiwa Spika, naomba niulize maswali mawili ya nyongeza kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa viwango vilivyowekwa vya kutunza watoto waliotelekezwa ni vidogo, lakini hata nilipopitia hii sheria haioneshi kwamba mzazi anayeacha watoto wake anatakiwa apeleke kiasi gani kwa mwezi au kiasi gani kwa mwaka badala yake ni busara ya Mabibi Maendeleo ya Jamii, badala yake ni mahakama zinatumia busara wanalipisha kiwango cha shilingi 2,000 kwa mwezi kiwango ambacho hakitoshi kabisa kutunza watoto.

Je, Serikali ina mkakati gani wa kuweka utaratibu wa kisheria utakaowafanya wazazi wanaotelekeza watoto waweze kubanwa kisheria na waweze kutunza watoto?

Mheshimiwa Spika, swali la pili, kwa sababu baadhi ya wazazi walio wengi katika jamii yetu wanatekeleza watoto kwa kisingizio kwamba si watoto wao, na kwa sababu katika vituo vyetu vya afya na katika zahanati zetu hapa nchini hakuna vipimo vya kupima *DNA*.

Mheshimiwa Spika, ningependa kujua sasa Serikali ina mkakati gani ili kupeleka vifaa hivi na kuweza kuwabana wazazi wote wanaokwepa kulea watoto wao kwa visingizio kwamba si watoto wao? Ahsante. *(Makofi)*

**SPIKA**: Majibu ya maswali hayo Mheshimiwa Naibu Waziri tafadhali.

**NAIBU WAZIRI WA AFYA, MAENDELEO YA JAMII, JINSIA, WAZEE NA WATOTO:** Mheshimiwa Spika, mwitikio wa swali hili unaonesha kwamba suala hili la utelekezaji wa watoto ni changamoto kubwa hata ndani ya nyumba yako. *(Kicheko)*

Mheshimiwa Spika, naomba kujibu maswali mawili ya Mheshimiwa Amina Makilagi kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, kwa mujibu wa taratibu tulizonazo ni kwamba, kiwango na gharama za matunzo ambazo zinatolewa yanapatikana baada ya kufanya *assessment* ya yule mhusika kuona hali yake ya kipato na hali ya maisha na umri wa yule mtoto na pale ndipo mahakama inaweka utaratibu wa kiwango ambacho kinatolewa. Mimi niseme tu kwamba katika suala hili sisi kama Wizara tunaendelea kufanya mapitio ya sera zetu na vilevile kuja na sheria ambayo itajaribu sasa kufanya mapitio ya yote haya kuangalia sasa ni utaratibu gani mzuri tunaweza tukaweka kuhakikisha kwamba wale wote wanaotelekeza watoto basi wanabanwa vizuri zaidi na sheria.

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali lake la pili Mheshimiwa Makilagi ameuliza kuhusiana na kupanua huduma za upimaji wa *DNA*. Niseme tu kwamba upimaji wa *DNA* unafanywa na ofisi au taasisi ya Mamlaka ya Mkemia Mkuu wa Serikali. Upimaji huu si upimaji ambao holela mtu anaweza akanyanyuka akaenda na sampuli yake pale anapojisikia kwenda kufanya upimaji. Kuna taratibu ambazo zimewekwa kwamba ni mamlaka ikiwa ni pamoja na Mahakama, Maafisa Ustawi wa Jamii au Polisi ambao wanaweza wakaagiza na si kila mtu ambaye ukiwa na sampuli yako unafikiri kwamba mtoto si wako unaweza ukaenda pale ukafanya, hatufanyi upimaji, *request* zote zinapatikana kupitia mamlaka husika.

**SPIKA:** Mheshimiwa Mwambe nilikuona, swali fupi la nyongeza.

**MHE. CECIL D. MWAMBE:** Mheshimiwa Spika, ahsante kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali la nyongeza.

Mheshimiwa Spika, kadri ya swali namba 65 linaelezea zaidi kuhusu kutelekeza watoto na familia zao, kwa maana ya matunzo na hili jambo linakwenda sambamba kabisa na masuala ya uzazi wa mpango. Jana tulishuhudia

Mheshimiwa Rais kwenye mkutano wake akisema kwamba Watanzania ambao tumeshiba tunaweza tukazaa kadri tunavyotaka bila kuwa na mipaka.

Sasa swali langu ni kwamba je, Serikali imeamua kubadilisha sera yake ya uzazi wa mpango kutokana na kauli iliyotolewa jana na Mheshimiwa Rais? *(Makofi)*

**SPIKA:** Hili swali chonganishi hili, majibu Mheshimiwa Naibu Waziri tafadhali. *(Kicheko)*

**NAIBU WAZIRI WA AFYA, MAENDELEO YA JAMII, JINSIA, WAZEE NA WATOTO:** Mheshimiwa Spika, Serikali ina Sera ya Uzazi wa Mpango na Sera yetu inasema kwamba hatujaweka kikomo cha idadi ya watoto ambayo familia inapaswa kuzaa. Sera yetu inasema mtu apate idadi ya watoto ambao anamudu kuwatunza na kuwapa nafasi kati ya mtoto mmoja mpaka mwingine. Huo ndio mwelekeo wetu wa sera na Mheshimiwa Rais hajatoka sana katika nje ya sera. *(Makofi)*

**SPIKA:** Kama CHADEMA mna sera watu wasizae semeni, halafu muone mwaka 2020 itakuwaje?

Tunaenda Wizara ya Kilimo swali la Mheshimiwa Jasson Rweikiza.

Na. 66

**Kutokupanda kwa Bei ya Kahawa**

**MHE. JASSON S. RWEIKIZA** aliuliza:-

Serikali ilifuta tozo na kodi kadhaa katika kilimo na biashara ya kahawa, lakini bado bei anayopata mkulima ni ndogo.

Je, ni kwa nini tangu kufutwa kwa tozo na kodi hizo bei kwa mkulima haijapanda?

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO (MHE. OMARY T. MGUMBA)** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa nafasi hii kujibu swali la Mheshimiwa Mheshimiwa Rweikiza. Kwa niaba ya Waziri wa Kilimo napenda kujibu swali la Mheshimiwa Jasson Samson Rweikiza, Mbunge wa Jimbo la Bukoba Vijijini kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, bei ya kahawa duniani inapangwa kwa kuzingatia masoko mawili makuu ya rejea duniani ambayo ni Soko la Bidhaa la New York, Marekani (*New York Commodity Market*) kwa kahawa za arabika na Soko la London, Uingereza *(LIFE)* kahawa ya aina ya Robusta. Mwenendo wa bei katika masoko hayo una athari za moja kwa moja kwenye soko la kahawa na bei anayopata mkulima. Aidha, bei ya kahawa katika masoko hayo pia huathiriwa na ugavi na mahitaji *(demand and supply)* ya kiasi cha kahawa kinachozalishwa duniani kwa wakati husika ambapo uzalishaji wa kahawa nchini ni wastani wa tani 50,000 za kahawa safi sawa na asilimia 0.6 ya kahawa yote duniani na hivyo kutokuwa na ushawishi katika bei ya kahawa.

Mheshimiwa Spika, pamoja na Serikali kufuta tozo na kodi katika zao la kahawa, bei ya mkulima imeshuka kutokana na sababu mbalimbali ikiwemo mzalishaji mkuu wa kahawa duniani, nchi ya Brazil kushusha thamani ya fedha yake *(devaluation of currecy)* na hivyo kahawa yao kuuzwa kwa bei ndogo ili kuvutia wanununuzi wengi. Pia kuongezeka kwa uzalishaji ambapo msimu wa 2018/2019 nchi ya Brazil na nchi nyingine duniani zimeongeza uzalishaji na kua na ziada ya tani 420,000 na kutoeleweka vizuri kwa maelekezo ya Serikali kuhusu uuzaji wa kahawa kwenye soko la moja kwa moja (*direct exports*), kwa kahawa hai *(organic coffee)* na kahawa haki *(tair trade coffee)* miongoni mwa wanunuzi na viongozi wa ushirika.

Mheshimiwa Spika, pamoja na bei ya kahawa katika soko la dunia kushuka kutoka USD 87.4/50kg za kahawa

mwaka 2016/2017 hadi dola 79.8 kwa gunia la kilo 50 la kahawa safi mwaka 2017/2018 bei ya kahawa ya mkulima wa kahawa imeimarika kwa kahawa ya robusta kutoka shilingi 1,400 kwa kilo mwaka 2016/2017 hadi shilingi 1,600 kwa kilo mwaka 2017/2018; na bei ya arabika kupungua kwa kiasi kidogo kutoka shilingi 4,000 kwa kilo mwaka 2016/2017 hadi shilingi 3,800 kwa kilo mwaka 2017/2018. Aidha, bei ya arabika kwa mkulima ingeweza kupungua zaidi kama Serikali isingeondoa tozo katika tasnia ya kahawa.

Mheshimiwa Spika, katika mwa 2017/2018 Serikali ilifuta jumla ya tozo 17 na tozo mbili mwaka 2018/2019 katika tasnia ya kahawa ambazo zimesaidia kuimarisha bei ya mkulima. Aidha, kupungua kwa kodi na tozo hizo kumesaidia bei ya kahawa kuwa nzuri ambapo kwa mara ya kwanza katika msimu wa 2017/2018 kahawa ilitoka nchi ya Uganda na kuletwa Tanzania kutokana na wakulima wa Uganda kuvutiwa na bei iliyokuwa inapatikana Tanzania. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Rweikiza.

**MHE. JASSON S. RWEIKIZA:** Mheshimiwa Spika, kwanza niishukuru Serikali kwa kutoa tozo karibu 20 kwenye tasnia ya kahawa. Hata hivyo, pamoja na shukrani hizo sehemu ya jibu inasema kwamba bei ya kahawa inakuwa ndogo kwa sababu ya kutoeleweka vizuri kwa maelekezo ya Serikali kuhusu uuzaji wa kahawa kwenye soko la moja kwa moja *(direct exports)* kahawa hai *organic coffee* na kahawa haki *(fair trade coffee)* miongoni mwa wanunuzi na viongozi wa ushirika, kutoeleweka vizuri kwa maelezo ya Serikali.

Je, Serikali imechukua hatua gani ili hii ieleweke vizuri na wakulima wapate bei nzuri?

Mheshimiwa Spika, swali la pili, bei ya kahawa ni ndogo kama anavyojua Mheshimiwa Naibu Waziri, lakini pia Serikali imeuzia wanunuzi binafsi wote, walikuwepo wengi Olam, Kagira na wengine imewazuia sasa hivi hawaruhusiwi kununua kahawa kwa wakulima. Hawa walikuwa na bei nzuri kidogo na msimu ulikuwa unawahi hauchelewi kama ilivyo

sasa na mkulima alikuwa anapata nafuu. Kwa nini Serikali imezuia wanunuzi binafsi na inawatesa wakulima? *(Makofi)*

**SPIKA:** Majibu ya maswali hayo mawili muhimu sana hasa la pili, kwa nini mnazuia wanunuzi binafsi na wakulima wanateseka?

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO (MHE. OMARY T. MGUMBA):** Mheshimiwa Spika, ni kweli maelekezo ya Serikali yalikuwa kwamba mnunuzi yoyote mwenye soko la moja kwa moja nje ya nchi kwa kahawa hai na kahawa iliyozalishwa kwa kutumia haki anaruhusiwa kuuza kahawa hiyo ili mradi wakulima wale kwa sababu wanatambulika, wapitie kwenye vyama vyetu vya ushirika. Agizo hilo halikueleweka vizuri kwa wanunuzi wala kwa vyama vya ushirika wakadhani kwamba Serikali tumepiga marufuku kwa ajili ya *direct export*.

Mheshimiwa Spika, hatua gani Serikali imechukua, kwanza tuliwaita wanunuzi wote walifika pale Wizarani wiki moja iliyopita na wadau wengine kwa ajili ya kuwapa ufafanuzi huo na kwa sasa wanunuzi wote wamelielewa hilo na wameshachukua maelekezo ya Serikali. Mnunuzi yoyote mwenye soko la moja kwa moja ambaye anawafahamu wakulima wake anaruhusiwa kukusanya kahawa hiyo na kutuonesha hicho kibali chake kinachoonesha bei aliyouzia ili kwamba tozo na ushuru mwingine wa Serikali tuupate kama inavyostahili.

Mheshimiwa Spika, swali la pili, kwa nini kama Serikali tumekataza wanunuzi binafsi wasinunue kahawa kwa wakulima. Kama Serikali hatujakataza wanunuzi binafsi kununua kahawa kutoka kwa wakulima. Tulichoelekeza Serikali kwa ajili ya kulinda ubora wa kahawa, lakini pia kupata takwimu sahihi tulizielekeza Halmashauri zetu Serikali za Mikoa na Wilaya pamoja na Vyama vya Ushirika, lakini hasa Vyama vya Msingi vya ushirika ndio wenye jukumu la kukusanya kahawa ile kutoka kwa wakulima na kuipeleka wenyewe Moshi na wale wanunuzi watakuja kununua kahawa pale Moshi. Hili tumelifanya kwa ajili ya kudhibiti ubora na pia kwa ajili ya kupata takwimu sahihi.

Mheshimiwa Spika, nimueleze Mheshimiwa Rweikiza, uzalishaji wa kahawa mwaka jana ulikuwa ni tani 50,000 tu lakini kwa mfumo huu mpaka sasa tulishafikia, kwa kahawa ya maganda, zaidi ya tani 80,000. Mpaka msimu ukiisha tunatumaini tutafikisha zaidi ya tani 100,000.

Mheshimiwa Spika, Kwa hiyo lengo lilikuwa kuwawezesha hawa wakulima wauze wenyewe soko la Moshi; lakini kwenye jibu langu la msingi nimeeleza sababu zilizosababisha bei kushuka. Pia kulikuwa na ukiukaji, maelekezo ya Serikali yalikuwa kwamba vyama vya msingi ndivyo vikusanye kahawa ile, lakini...

**SPIKA:** Ahsante Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO (MHE. OMARY T. MGUMBA):** ... baadae kahawa ile ikachukuliwa na vyama vikuu. Nataka nimuhaidi Mheshimiwa Rweikiza mwakani haitokuwa hivyo hivi vyama vyetu vikuu vya ushirika vyenye madeni ya kutupwa havitoweza kuruhusi wa tena kukusanya kahawa kutoka kwa wakulima bali ni vyama vyao vya msingi wakulima wenyewe ndio watakusanya kahawa na kuiuza katika masoko yetu. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri yaani nikuhakikishie Mheshimiwa Naibu Waziri nikiruhusu maswali hapa ni mengi kweli, kwa sababu maswali aliyouliza Mheshimiwa Rweikiza hamjayajibu mmerudia tu sera zenu zile zile. Kwamba mnahitaji takwimu na kadhalika, sawa mnahitaji takwimu, kwa hiyo, mkulima anendelee kupata bei ndogo kisa nyinyi mnataka takwimu sijui na vitu gani?

Swali ni kwamba mkulima anapataje bei na uluwa kidogo aishi vizuri

Hata hivyo muda mnauona Waheshimiwa Wabunge, mniwie radhi. Najua swali hili ni muhimu sana lakini tupate swali la mwisho kwa siku ya leo kuhusu pamba, Mheshimiwa Joyce Sokombi tafadhali. *(Kicheko/Makofi)*

Na. 67

**Kufufua Zao la Pamba – Mara**

**MHE. JOSEPH M. MKUNDI (K.n.y. MHE. JOYCE B. SOKOMBI)** aliuliza:-

Zao la pamba ambalo lililimwa kwa wingi Mkoani Mara na pia ilisaidia sana kuwainua wananchi kimapato.

Je, Serikali inachukua hatua gani za kimkakati za kulifufua zao hilo?

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO (MHE. OMARY T. MGUMBA)** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa kunipa nafasi ya kujibu swali la Mheshimiwa Mbunge na kwa niaba ya Waziri wa Kilimo napenda kujibu swali la Mheshimiwa Joyce Bitta Sokombi, Mbunge wa Viti Maalum kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Serikali inatambua umuhimu wa zao la pamba kwa uchumi wa taifa na wakulima wa pamba nchini. Kutokana na umuhimu huo Serikali imekuwa ikitekeleza mikakati mbalimbali inayolenga kuongeza uzalishaji, tija, ubora na masoko ya uhakika kwa kuimarisha usimamizi katika mnyororo wa thamani wa zao hilo ili kukidhi mahitaji ya soko la ndani na nje ya nchi. Aidha, huduma za ugani, upatikanaji wa pembejeo na mifumo ya masoko imeendelea kuboreshwa ili kuwanufaisha wakulima wa pamba nchini.

Mheshimiwa Spika, mikakati hiyo ni pamoja na kurahisisha upatikanaji wa pembejeo ambapo katika msimu wa 2018/2019 wakulima watapatiwa pembejeo kupitia Vyama vya Ushirika vya Msingi *(AMCOS)*, kuimarisha huduma za ugani ambapo wakuli wawezeshi *(leader farmers)* wapatao 4,532 wawili kutoka kila kijiji kinacholima pamba katika Kanda ya Magharibi wameainishwa na kupewa

mafunzo ya kanuni za kilimo bora cha pamba ili wafikishe huduma za ugani kwa wakulima wenzao kikamilifu.

Mheshimiwa Spika, mikakati mingine kuongeza matumizi ya dhana za kilimo ambapo takribani vyama vya ushirika zaidi ya 300 vitapatiwa mikopo ya matrekta kutoka Benki ya Maendeleo ya Kilimo. Kueneza teknolojia ya kilimo, hifadhi ardhi katika maeneo yanalima pamba nchini na kuboresha mfumo wa masoko ya pamba kwa kuimarisha Vyama vya Ushirika vya Msingi *(AMCOS)* ili viweze kunua pamba inayozalishwa na wakulima na hivyo kuimarisha ubora na usafi wa pamba.

Mheshimiwa Spika, Serikali pia imeanza kurekebisha mfumo wa uzalishaji wa mbegu bora za pamba kwa kufuata vigezo vyote vya ubora kwa mujibu wa Sheria ya Mbegu Na. 18 ya mwaka 2003. Aidha, juhudi zinazofanyika sasa ni kuzalisha kwa wingi mbegu ya aina ya UKM08 chini ya uratibu wa Kituo cha Utafiti cha Ukiriguru Mwanza kwa kushirikiana na sekta binafsi na Bodi ya Pamba. Vilevile aina mbili za mbegu mpya za UK171 na UK173 zitaanza kupatikana kwa wakulima kuanzia msimu wa 2018/2019.

**SPIKA:** Mheshmiwa Mkundi swali la nyongeza.

**MHE. JOSEPH M. MKUNDI:** Mheshimiwa Spika, nashukuru kunipa fursa ya kuulizwa maswali mawili ya nyongeza.

Mheshimiwa Spika, swali la kwanza, pamoja na umuhimu wa huduma za ugani na upatikanaji wa pembejeo lakini bado huduma hizi haziwafikii wananchi kwenye maeneo ya chini kule ambako ndiko kwenye uzalishaji. Nini sasa mkakati wa Serikali ili kuondoa tatizo hili?

Mheshimiwa Spika, swali la pili, kama ilivyo kwa zao la pamba, zao la muhogo ambalo limekuwa muhimu sana kwa wananchi wa Visiwa vya Ukerewe kiuchumi, lakini hata kwa chakula limekuwa linakabiliwa na matatizo mengi sana ya magonjwa, lakini hata tatizo la ardhi kwenye eneo la

Visiwa vya Ukerewe. Je, Serikali ina mkakati wowote wa kutuma timu ya wataalam kufanya utafiti ili basi Visiwa vya Ukerewe vitumie ardhi yake hii ndogo kwa tija zaidi katika kuzalisha zao hili la muhogo? Nashukuru.

**SPIKA:** Sasa Mheshimiwa Mkundi umetoka kwenye pamba tena umeenda kwenye muhogo. Majibu Mheshimiwa Naibu Waziri kwa kifupi tafadhali.

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO (MHE. OMARY T. MGUMBA):** Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa kunipa nafasi kujibu maswali la Mheshimiwa Mbunge.

Mheshimiwa Spika, swali la kwanza, kuhusu mikakati ya Serikali tuliyo nayo kwa ajili ya pembejeo na Maafisa Ugani. Kwanza tumezielekeza Halmashauri zote nchi ni kutenga asilimia 20 ya mapato yao ya ndani kwa maagizo ya Serikali kupitia Waziri Mkuu kwa ajili ya kupeleka kwenye sekta ya kilimo ili Maafisa Ugani hawa waweze kuwezeshwa kwa ajili ya kuwafikia wakulia kwa wakati.

Mheshimiwa Spika, lakini pili, viongozi wote wa Serikali katika ngazi mbalimbali, hasa wale wanaosimamia sekta ya kilimo tumewaambia lazima washiriki katika kilimo ili mashamba yao pia yaweze kuwa mfano kwa wakulima wale ambao wapo wanazunguka. Tunafahamu pia kwamba tuna upungufu mkubwa wa Maafisa Ugani nchini, mahitaji ni zaidi ya 20,000 lakini tulio nao ni 6,800. Tunaendelea kuongea na wenzetu wa Wizara ya Utumishi kwa ajili ya kuongeza Maafisa Ugani nchi nzima ili wawafikie wakulima wetu kwa ajili ya kanuni bora za kilimo.

Mheshimiwa Spika, swali la pili kuhusu zao la muhogo kukubali kule Ukerewe pamoja na vituo vyetu vya utafiti, tuko tayari kama Serikali na tunawaagiza kituo chetu cha utafiti cha pale Ukiruguru, Mwanza pamoja na Ilonga kufika maeneo hayo ya Ukerewe kwa ajili ya kufanya utafiti wa udongo kuona namna gani zao hili linaweza kulimwa katika Visiwa Vya Ukerewe.

**SPIKA:** Kwa sababu ya muda Waheshimiwa, kama mnavyoona tumevuka muda leo kuliko kawaida, maswali yalikuwa mengi lakini tulianza na kuweka hati mezani ilichukua muda kidogo baadhi ya *document* zilikuwa nyingi.

Sasa nianze kwa kuwatambua wageni walioko katika Jukwaa la Spika. Kwanza nimtambue Naibu Mkurugenzi Mkuu wa TAKUKURU *Brigadier General* John Mbungo, ahsante sana. *(Makofi)*

Balozi wa Uswisi nchini ndugu Florence Tinguely Mattil *Ambassador*, Mkuu wa Ushirikiano wa Kimataifa Ubalozi wa Uswiss Romana Tedesschi, Mkuu wa Ushirikiani, haya kama hamjui Kiswahili kazi kwenu. *(Kicheko/Makofi)*

Mkurugenzi wa Elimu kwa Umma TAKUKURU Ekwabi Mujungu, karibu sana; Mkurugenzi wa Utawala na Rasilimali Watu TAKUKURU Alex Mfungo ahsante; Mkurugenzi wa Utafiti na Udhibiti TAKUKURU Sabina Seja; Mkurugenzi wa Uchunguzi TAKUKURU Mbengwa Kasumambuto na Kaimu Mkurugenzi wa Mipango Ndugu Joyce Shirima, karibu. *(Makofi)*

Mmiliki na Mwanzilishi Mkuu wa Taasisi ya *Media for Development International* Ndugu John Riber, *Producer Media for Development International* Louise Riber, Meneja Uzalishaji *Media for Development International* Ndugu Louise Kamin wameambatana na Wakuu wa Idara na Vitengo mbalimbali kutoka TAKUKURU ambao wamekaa jukwaa la kawaida. Nitawatangazia baadae tutakuwa na shughuli maalum inayohusiana na masuala ya TAKUKURU leo. *(Makofi)*

Wageni 24 wa Mheshimiwa Joseph Kakunda, Naibu Waziri Ofisi ya Rais, TAMISEMI ambayo ni kwaya ya Upendo ya Kanisa la Moravian Sikonge wakiongozwa na Ndugu Erasto Kapela, karibuni sana Wanyamwezi wote toka kule Sikonge, lakini sasa mmekuja hapa mtembelee muone kwaya za Dodoma zinavyoimba, mjifunze, karibuni sana Wana Sikonge na Mbunge wenu yupo amejaa tele hapa anaendelea vizuri. *(Makofi)*

Wageni watano wa Mheshimiwa Dkt. Harrison MWakyembe Waziri wa Habari, Utamaduni, Sanaa na Michezo wakiongozwa na ndugu Addo Komba, Kaimu Mkurugenzi Maendeleo ya Michezo Nchini, karibuni wale wageni wale pale. *(Makofi)*

Wageni wawili wa Mheshimiwa Stansalaus Mabula ambao ni rafiki zake kutoka Jijini Dar es Salaam, Ndugu Florence Mambea na Ndugu Neema Kiluvia, karibuni sana, wale pale. *(Makofi)*

Matangazo mengine niwatangazieni Waheshimiwa Wabunge kuwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora, Kepteni Mstaafu George Mkuchika anawatangazieni kuhusu uzinduzi wa filamu kuhusu rushwa na maadili.

Kwa hiyo, leo kutakuwa na uzinduzi wa filamu hiyo baada ya kusitisha Bunge saa saba mchana pale Msekwa kuhusu masuala la rushwa inayoitwa Bahasha iliyotengenezwa kwa ufadhili wa Ubalozi wa Uswisi na Ubalozi wa Uholanzi hapa nchini Tanzania. Uzinduzi huo utafanyika leo saa saba na robo na kufuatiwa na chakula cha mchana kwa washiriki wote watakaoshiriki katika uzinduzi huo. Tunaomba sana Waheshimiwa Wabunge wote tuwe hapo na mimi ni takuwepo pia pamoja nanyi katika zoezi hilo la uzinduzi, ahsante sana. *(Makofi)*

Pia tunaye Balozi wa Uholanzi hapa nchini Tanzania Ndugu Jeroen Verguely na ameambatana na Bi. Neema Matafi, Afisa Ubalozi katika Ubalozi wa Uholanzi nchini, Mheshimiwa Balozi karibu sana hapa Bungeni karibu Dodoma, tutaonana baadae saa saba mchana. *(Makofi)*

Katibu wa Bunge anaomba niwakumbushie Waheshimiwa Wabunge kwamba leo Jumatatu kutakuwa na semina kwa Wabunge wote kama nilivyosema, ambayo inahusu masuala ya rushwa, itafanyika pale Msekwa anawakumbusheni tu. Pia Katibu wa Bunge anaomba niwatangazieni Waheshimiwa Wabunge kuwa katika jitihada

za kuunga mkono Serikali katika kutekeleza Sera ya Taifa ya Masuala ya Jinsia ya mwaka 2000; Bunge kwa kushirikiana na *UNDP* kupitia awamu ya pili ya mradi wa kulijengea Bunge uwezo *(Legislative Support Project)* tumefanikiwa kuandaa mkakati wa Bunge wa masuala la jinsia pamoja na mkakati wa kampeni ya *heforshe* inayotoa fursa kwa Wabunge wanaume kuwa mstari wa mbele katika kuleta mabadiliko ya usawa wa kijinsia ndani na nje ya Bunge kwenye maeneo yeo ya uwakilishi. *(Makofi)*

Mkakati huu ni muhimu na utazinduliwa siku ya alhamisi tarehe 13 Septemba kuanzia saa saba mchana katika ukumbi wa Msekwa na mgeni rasmi atakuwa Mheshimiwa Waziri Mkuu Kassim Majaliwa Majaliwa (Mbunge). Waheshimiwa Wabunge tunaarifiwa tujiandaae siku hiyo ya tarehe 11 Septemba. Tutaarifiana mapema na tatakumbushana kuhusu suala hilo. Itakuwa siku ya Alhamisi tarehe 13 saa saba mchana.

Ndugu Oscar Mukasa na wenzake wameanzisha *caucus* yao ya masuala la kifua kikuu na wangependa kuwataarifu Waheshimiwa Wabunge wote kwamba kuna umoja huo, na wale ambao mtakuwa na *interest* mnaombwa mjiunge.

Aidha, Mheshimiwa Oscar Mukasa mwenye ndiye Mwenyekiti, Makamu Mwenyekiti Omary Badule, Katibu Mkuu Kunti Majala, Naibu Katibu Mkuu Kemilembe Lwota, Mweka Hazina Ndugu Lathifah Chande, na Mweka Hazina Msaidizi Oliver Daniel Semuguruka, tunaombwa tujiunge na umoja huo pia. Ahsante sana, sasa Katibu tuendelee.

**MHE. JAKU HASHIM AYOUB:** Mheshimiwa Spika, Kuhusu Utaratibu.

**MHE. PAULINE P. GEKUL:** Mheshimiwa Spika, mwongozo wa Spika.

**MHE. JAKU HASHIM AYOUB:** Ndio huo huo Mwongozo.

**MWONGOZO WA SPIKA**

**SPIKA:** Haya Katibu nitajieni majina.

**NDG. JOSHUA CHAMWELA – KATIBU MEZANI:** Mheshimiwa Esther Matiko, Mheshimiwa Cecil Mwambe, Mheshimiwa Pauline Gekul, Mheshimiwa Jaku, Mheshimiwa Innocent Bashungwa na Mheshimiwa George Lubeleje.

**SPIKA:** Tutaanza na Seneta Lubeleje.

**MHE. GEORGE M. LUBELEJE:** Mheshimiwa Spika, juzi hapa niliomba Mwongozo nikaahidiwa na Serikali kwamba nitajibiwa na Mwongozo wenyewe ulikuwa hivi, sasa hivi bei ya sukari ni shilingi 2,600 mpaka shilingi 3,000; lakini sukari imejaa kwenye ma-*godown* ya viwanda vyote.

Mheshimiwa Spika, nilikuwa naangalia kwenye *tv* jana Kiwanda cha Sukari cha Kagera magunia yamejaa kabisa, lakini Waziri alitamka kwamba kuna kosa la jinai. Sasa kama kuna kesi, kuna mtu aliingiza sukari hivi wananchi wa Tanzania waendelee kusumbuka kusubiri mpaka kesi iishe, waendelee kununua sukari kwa shilingi 3,000 badala ya shilingi 2,000 kwa kilo?

Mheshimiwa Spika, swali hilo halikujibiwa mpaka leo, hoja yangu ni hiyo.

**SPIKA:** Tutapata ufafanuzi Mheshimiwa Naibu Waziri wa Viwanda, Biashara na Uwekezaji, natumaini baadaye nitakupa nafasi kidogo utupatie ufafanuzi kwa kifupi. Mheshimiwa Esther Matiko kwa kifupi.

**MHE. ESTHER N. MATIKO:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru muongozo wangu ni kwa Kanuni ya 68 (7) kabla Mheshimiwa Waziri wa Habari, Utamaduni, Sanaa na Michezo hajajibu swali la Mheshimiwa Shangazi alitoa pongezi akionesha ni jinsi gani ndugu yetu Hassan Mwakinyo ameweza kuiwakilisha nchi yetu.

Mheshimiwa Spika, naomba Mwongozo wangu kwa sababu imekuwa ni kawaida kwa Serikali kuja kutoa pongezi lakini hawawezi kuandaa Watanzania ambao unakuta wana vipaji mbalimbali, wanakuwa wanafanya juhudi binafsi. Kwa mfano Hasssan Mwakinyo tumemshuhudia akifanya mazoezi kwa kutumia matairi ya gari yaliyozeeka yale mpaka anakuja kufanikisha hapa.

Mheshimiwa Spika, lakini kingine nikataka nijue ni kwa nini Serikali hasa, ukiangalia huyo Hassan Mwakinyo wakati ameshashinda jana wengine tunapenda michezo tulikuwa tunaangalia, akatakiwa afanywe *interview.* Ukiangalia alivyokuwa akiulizwa swali na yule mwandishi wa habari mkalimani wake alichokuwa akimueleza Hassani Mwakinyo na alichokuwa akijibu ni vitu vitatu tofauti.

Mheshimiwa Spika, sasa unaona kwamba Taifa tunashinda taji hili vizuri, lakini kama taifa tunaaibishwa kwa nyanja mbalimbali ambazo kama Wizara husika ingeweza ku-*concentrate* na kuweza kuwasaidia hawa Watanzania ambao wana vipaji hivi tungekuwa tunafika mbali sana. Ni kwanini sasa Wizara hii ipo lakini haiwekezi katika Watanzania wenye vipaji kwenye nyanja mbalimbali za michezo? Nilikuwa nataka kupata muongozo katika eneo hilo wanabaki kuja kutoa sifa tuu Bungeni.

**SPIKA:** Ahsante sana mimi nachukulia kama ni ushauri, ushauri muhimu ambao umeipatia Wizara, Wizara ime-*take note.* Tunaendelea Mheshimiwa Cecil Mwambe.

**MHE. CECIL D. MWAMBE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nimesimama nikiomba muongozo kwa kanuni ya 46 juu ya suala ambalo niliuliza hapa ndani kuhusiana na masula la uzazi wa mpango.

Tunafahamu na hata tunapokwenda kwenye bima ya afya tunaambiwa kwamba watoto watakaogharamiwa na bima ya afya ni wanne. Hii kwa hali fulani tafsiri yake kuna muunganiko kati ya huduma inayotakiwa kutolewa na idadi ya watoto mtu anaotakiwa kuwazaa kwenye familia.

Mheshimiwa Spika, sasa niombe Mwongozo wako kama Serikali inatambua watoto wanne ambao wanaweza kusaidiwa kwa masuala mbalimbali ikiwemo masuala ya bima, na jana tumemsikia Mheshimiwa Rais akisema kwamba tuendelee kuzaa kadri tunavyoweza *as long as* tunaweza kuwalisha na kufanya mambo mengine.

Mheshimiwa Spika, sasa nataka kupata Mwongozo wako, kwa nini tuna UMATI kwanza ambayo inasaidia masuala ya *birth control,* lakini pia tuongezee idadi ya watoto ambao wanaweza kusaidiwa na kutambulika rasmi kisheria kwa sababu hao ndio tunaoweza kuwazaa na kuwatunza. Ikiwezekana bima ya afya turuhusiwe hata kuingiza watoto kumi ili tuweze kuwasaidia vizuri badala ya kuwa *limited* na watoto wanne. *(Makofi)*

**SPIKA:** Huo ni ushauri pia, Mheshimiwa Pauline Gekul.

**MHE. PAULINE P. GEKUL:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru na mimi naomba Mwongozo wako kwa kanuni ya 68(7) juu ya jambo ambalo limejitokeza asubuhi kwenye swali namba 55 juu ya suala la mkakati wa Serikali kuziba nafasi zilizoachwa wazi na watumishi ambao huwenda walipatwa na tatizo la vyeti *fake* na vinginevyo. Hata hivyo sikupata ufafanuzi wa kina na miongoni mwa mkakati ambao Serikali ili *adopt* ilikuwa ni kuhamisha walimu wa *secondary* na kuwapeleka *primary,* jambo ambalo lilikuwa ni jema. Kwa mfano katika shule zetu za *primary* tuna upungufu mkubwa sana wa walimu wa kiume lakini wale ambao wamezidi *secondary* wakawahamishia *primary*.

Mheshimiwa Spika, lakini hivi karibuni Serikali imesitisha zoezi hilo na wale walimu wamerudishwa *secondary* kwa sababu hawajalipwa *allowance* zao pamoja na *disturbance allowance* na Halmashauri wameshindwa kuwalipa kwa sababu hawana vyanzo.

Sasa naomba ikupendeze, Serikali ije itujibu humu ndani, wana mkakati gani sasa wa kuziba zile nafasi za shule za msingi wakati hao wa *secondary* wameshindwa kwa

sababu Serikali imeshindwa kuwalipa na wamekataa wameona kama ni *demotion* kwao. Watuletee mkakati mwingine bado kuna upungufu naomba ikupendeze Serikali ituletee kauli.

**SPIKA:** Sasa Pauline kauli ya nini tena, maana hata hapa juzi tu hapa walimu wameajiriwa sijiu elfu ngapi hata wiki mbili hazijapita. Upungufu wa nchi nzima ni mkubwa, ni mkubwa kweli kweli Wilaya yangu ya Kongwa peke yake ina upungufu wa walimu wa shule za msingi 1,000, Wilaya moja walimu 1,000, sasa na hamuwezi kuilaumu Serikali peke yake tunaofyatua hao watoto si ni sisi? Eee! Kwa hiyo, twende taratibu, Serikali inajitahidi mno. *(Kicheko)*

Mheshimiwa Jaku.

**MHE. JAKU HASHIM AYOUB:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana. Nimesimama kwa Kanuni ya 68 (7) na mbele nitahitaji msaada wako na busara zako, na hekima zako na kiti chako, kanuni ya 153.

Mheshimiwa Spika, kuna jambo ambalo lilitokea siku ya Ijumaa, kukosekana *quorum* katika kupitisha maaamuzi na wengi waislamu tulikwenda msikitini, hatukuwepo. Kwa hiyo nitahitaji msaada wako.

Mheshimiwa Spika, Tanzania hii ina dini mbili kubwa, dini ya kiislam na dini ya kikristu. Jumamosi wasabato wanapata *time* yao kwenda kuabudu, siingilii dini ya mtu, msije mkanihukumu. Jumapili wakristu wanakwenda kuabudu, siku ya Ijumaa ni siku kubwa katika wiki katika waislam, ni siku kubwa hata kuna sura inaitwa *Surat Jumaa* iliteremshwa katika juzuu ya 28 aya ya sita.

Mheshimiwa Spika, lakini mimi nimeshuhudia tarehe 4 Februari, 2018 kuna Askofu alisimikwa anaitwa Jackson Ayois Assostanance katika Dayosisi ya Dar es salaam. Mheshimiwa Rais wa Jamhuri wa Muungano alihudhuria hadhara hiyo, Mheshimiwa Rais Mstaafu Mkapa. Hata hivyo cha kusikitisha kuna Wabunge humu ndani waliacha shughuli za Bunge, na

itakuwa si vizuri kuwataja, walikuwepo takriban siku nne, kwa kuheshimu dini. Katika kutafuta usawa wa kujenga jamii inayojali dini zote kwa usawa siku ya Ijumaa tukafanyiwa angalau saa sita shughuli za Bunge zikaahirishwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nimalizie hoja yangu kwa kusema aya hii; *"Idhaa nuliyyat swallata mina yaumil Ijumaa, fassahau ila dhikrillah wadhulbahi dhaalikum khailulakum in kuntumtaamalun* (endapo inaponadiwa swala siku ya Jumaa basi kimbilieni, na mfanye haraka na achene biashara kufanya huko ni kheri kwa ajili yenu, ikiwa mnalijua hilo)."

Hii mara ya tatu kusimama kwa suala hili, na historia itanikumbuka au itaandika, na niliwaambia wakubwa zangu, sitaki kuwataja; kwa hili hata saa tisa za usiku nikaamshwa, ni usingizi mkali wakati huo nikawaambia hili naam!

Mheshimiwa Spika, kheri tufanyiwe haki, hili Bunge linaitwa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, si Bunge la Tanzania. Asilimia 99 ni waislamu kutoka Zanzibar, Mheshimiwa Spika busara na jicho la rehma naomba uingalie kanuni ya 153 hili ili suala ulipatie ufumbuzi, mamlaka ni ya kwako na ya Kiti chako.

Mheshmiwa Spika, lakini vilevile ningeomba lingewekwa katika kanuni za kudumu leo tupo kesho hatupo lingeingizwa humo. Nikuombe sana kwa unyenyekevu wa hali ya juu. Linatuathiri na maamuzi yanayopitishwa humu ndani wakati mwengine sisi yanatugusa hayatufanyii haki naomba hii Ijumaa... *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante Mheshimiwa Jaku.

**MHE. JAKU HASHIM AYOUB:** Mheshimiwa Spika, ahsante, nimemalizia hoja yangu. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Jaku hajawahi kutoa hoja humu ndani ikashangiliwa kama hii. Mheshimiwa Innocent Bashungwa, ndiye wa mwisho.

**MHE. INNOCENT L. BASHUNGWA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa fursa hii. Nimesimama kwa Kanuni ya 68(7) ikisomwa pamoja na Kanuni ya 46(1) nikiomba Mwongozo wako kuhusu swali namba 66 lililoulizwa na Mheshimiwa Jasson Rweikiza kuhusu kahawa.

Hali ya mkulima wa kahawa msimu huu ni mbaya sana na majibu ya Serikali kusema ukweli hayaridhirishi yanakatisha tamaa kwa mkulima wa kahawa. Ni mwezi wa pili tangu wakulima wa kahawa hususan Mkoa wa Kagera wamepeleka kahawa yao kwenye vyama vya msingi, lakini hawajapata malipo ya awali ya shilingi 1,000.

Mheshimiwa Spika, fedha inayopelekwa kwenye vyama vya msingi kwa mfano Karagwe na Kyerwa tuna vyama vya msingi zaidi ya sabini na saba, haitoshi ukilinganisha na fedha ambazo wakulima wa kahawa wanadai. Matokeo yake kile kidogo kinachoenda kwenye vyama vya msingi kimeleta kaharuki, wale wajanja wachache ndio wanapata na wakulima wanyonge wa Kahawa hawapati fedha zao.

Mheshimiwa Spika, ningependa nikuombe kwa ridhaa yako uruhusu Serikali ilete kauli ya kina inayoelezea changamoto hizi ili mkulima wa kahawa asikate tama. Ninajua nia ya Serikali ni njema, tumelenga kupitia vyama vya ushirika kumsaidia mkulima wa kahawa apate bei nzuri. Hata hivyo maelezo ya Serikali hayaridhishi, nakuomba sana uielekeze Serikali ilete kauli mahususi juu ya changamoto hizi.

Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana. *(Makofi)*

**SPIKA:** Waziri wa Nchi Offisi ya Waziri Mkuu kuhusu hilo la Mheshimiwa Bashungwa.

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU, SERA, BUNGE, KAZI, VIJANA, AJIRA NA WENYE ULEMAVU:** Mheshimiwa Spika, tumesikia hoja ya kimwongozo iliyotolewa na Mheshimiwa Bashungwa. Kwa sababu suala hili linashughulikiwa na Wizara si moja tu peke yake, kwa hiyo, tutaomba tupate

nafasi kama Serikali ili Wizara zote linazohusiana na jambo hili ziweze kukutana kwa pamoja na kile kitakachoweza kuja kusemwa Bungeni iwe ni kauli hasa ya Serikali ambayo imepata ridhaa ya sekta zote ambazo zingeweza kuwa na majibu ya kutatua jambo hili.

**SPIKA:** Ahsante sana, sisi tungeomba tu kwa muda huu mjaribu kuliangalia kwa karibu. Najua mtakuwa mnajua undani ambao sisi hatuna, kwa hiyo, unapotoa maoni wakati huna ukweli wowote unakuwa nje ya mstari kabisa.

Hata hivyo cha muhimu ni kwamba tumeona katika nchi hii bei ya kahawa iliharibika na watu waling'oa kahawa nchi nzima, wakapanda mahindi, nyanya na kadhalika. Kwa mwendo huu tunataka kurudi kule kule, watu waliacha pamba hivi hivi. Mkulima anachohitaji ni bei nzuri, kapata kwenye ushirika, kapata kwa mtu binafsi, ili mradi asomeshe watoto wake, ajitibie na kadhalika. Sasa hili na sisi ndilo liwe lengo letu kubwa, mkulima kupata bei nzuri, habari ya soko la Moshi na lingine hayo ni yatokanayo, lakini mkulima apate bei nzuri; hiyo itafanya zao liendelee kuwa na maana na kuendelea kuwepo. Kama mkulima hapati bei nzuri hata tufanyeje haitusaidii na vyama vyenyewe vya ushirika vitakufa, si zao halipo bwana? Basi muendelee kuliangalia halafu tutashauriana pia.

Kuhusu suala la Mheshimiwa Jaku ni suala muhimu sana, lakini ni jambo pana. Nilipoenda Tanga siku za hivi karibuni kwenye mazishi ya ndugu yetu Maji Marefu, nilienda Tanga Mjini baada ya kumaliza mazishi na ilikuwa ni siku ya Ijumaa. Nikashangaa kule Tanga saa tano watoto wa shule zote wanarudi nyumbani, nikauliza vipi hii? Hii namna gani? Wakasema Tanga ndiyo hivi. Nikasema Tanga sio sehemu ya Tanzania? Watoto wote wanarudi nyumbani? Halafu jumla mpaka Jumatatu. Kwa hiyo, wanakosa Ijumaa, Jumamosi na Jumapili, ya Tanga tuyaache Tanga huko huko. *(Makofi)*

Kwa hiyo, hili ni jambo kubwa hatuwezi sisi Bunge peke yetu tukaliamulia tukabadili utaratibu wa Ijumaa, tujue kabisa kwa namna moja au nyingine na Bunge sisi ni viongozi,

maana yake tutaifanya Mahakama nayo ianze kufikiri kuto kufanya kazi masaa fulani Ijumaa. Vile vile kwa ujumla wote tutaifanya na Serikali nayo ianze kufikiri hivyo. Kwa hiyo, ni jambo linalohitaji uamuzi kidogo mpana wa pamoja, tukiamua tu sisi peke yetu hapa tunaweza tukawapa shida wenzetu. Hata hivyo kama nilivyosema ni wazo muhimu, na tuendelee kulifanyia kazi, tutakuja kufika mahala fulani tutaelewana katika ujumla wake.

Kwa hatua ndogo ndogo ambazo tutachukua sisi kama Bunge hapa ni kwamba kwa siku hiyo ya Ijumaa kwa saa zile za ibada tutaepusha kuwa na kura ya maamuzi wakati ule. Kama ni michango watu wataendelea tu kuchangia wale waliobaki na kadhalika, lakini kufanya maamuzi wakati wenzetu wapo kwenye ibada na tunajua wako kwenye ibada itakuwa kidogo hatutendi inavyotakiwa. *(Makofi)*

Kwa hiyo maamuzi tutayafanya wakati mwengine na sio saa zile za kati ya saa tano na saa saba au na saa nane hivi kwa siku ya Ijumaa. Kwa sasa hivi tulipokee hivyo na tuendelee kuwasiliana na wenzetu sisi kama viongozi mwisho wa siku tutapata namna gani ya kwenda kwa pamoja katika jambo hili. *(Makofi)*

Sasa kwa kumalizia swali la Mheshimiwa Lubeleje nimpe nafasi Mheshimiwa Naibu Waziri Viwanda na Biashara kwa kifupi na pia Dkt. Mwakyembe ntakupa dakika chake pia u-*comment* kuhusu swali la Mheshimiwa Mbunge wa Tarime Mjini na Mheshimiwa Mkuchika atafuata vilevile kwa muda mfupi mfupi. Mheshimiwa Naibu Waziri Viwanda.

**NAIBU WAZIRI WA VIWANDA, BIASHARA NA UWEKEZAJI:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana. Kwanza kabisa nikubaliane na Mheshimiwa Lubeleje kwamba kumekuwa na *trend* ya kuongezeka kwa bei ya sukari katika baadhi ya mikoa.

Mheshimiwa Spika, kimsingi wastani wa bei ya sukari katika mikoa imekuwa ikitofautiana kati ya mkoa na mkoa.

Kuna mikoa ambayo imekuwa ikionesha kushuka kwa bei ya sukari lakini kuna mikoa imekuwa ikionesha kupanda kwa bei ya sukari na kwa bahati nzuri ni kwamba sisi Wizara yetu tunarekodi kila mwezi wastani wa bei ya sukari. Kwa misingi hiyo niseme tu kwamba katika mikoa ambayo imekuwa ikionesha kupanda kwa bei ya sukari mmojawapo ni mkoa wa Dodoma.

Mheshimiwa Spika, niseme tu kwamba hakujawa na bei maalum ya sukari isipokuwa tunatarajia kwamba bei elekezi au bei tunayoitarajia ni ile ambayo itakuwa imetoa gharama za uzalishaji. Hata hivyo nafahamu kuna tabia ya baadhi ya wazalishaji au baadhi ya wadau kutumia mbinu zisizo sahihi za kuingiza sukari nchini. Mheshimiwa Waziri wangu wa Viwanda, Biashara na Uwekezaji juzi tarehe 7 Septemba wakati anajibu swali humu Bungeni alisema pia kuna masuala ambayo mengine ni ya kijinai, lakini kuna masuala ambayo mengine ni ya kiutendaji.

Mheshimiwa Spika, Wizara kwa kuangalia *trend* hiyo imechukua na inayafanyia kazi na tunaamini kabisa kwamba taarifa mtafahamishwa. Ni lengo la Serikali kuona kwamba bidhaa yoyote inayouzwa nchini inauzwa kwa bei ambayo ni nafuu kadiri iwezekanavyo. Tumefanya hivyo katika maeneo mengine na sukari ni eneo ambalo tunalifanyia kazi na tutaleta mrejesho mapema iwezekanavyo kwa kuwashirikisha wadau wote wanaohusika. Ahsante sana.

**SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Naibu Waziri. Nina uhakika Mheshimiwa Lubeleje hajaridhika, lakini itoshe kwa hapo. Mheshimiwa Lubeleje, inatosha. Mheshimiwa Mwakyembe. *(Kicheko)*

**WAZIRI WA HABARI, UTAMADUNI, SANAA NA MICHEZO:** Mheshimiwa Spika, nashukuru sana kunipa fursa niweze kutoa ufafanuzi kidogo.

Mheshimiwa Spika, kuna msemo wa Kiswahili, ukiona vinaelea vimeundwa. *Professional boxing* nchi hii ilikuwa haina uratibu kwa miaka yote kwa sababu sera ilikuwa

haitambui kama kuna ngumi za kulipwa na hata sheria zetu. Tumechukua hatua sisi kwanza kwa kuvunja vyombo vyote vya *professional boxing* hapa nchini ambapo kila kimoja kilikuwa kinapeleka wanamasumbwi nje na ndiyo maana matokeo yalikuwa mabaya sana. Tume-*centralize,* mimi mwenyewe nimefanya zaidi ya mikutano 20 na wanamasumbwi nchi hii. Tumetunga Katiba mpya, nimeunda chombo kimoja ambacho huwezi kwenda kupigana nje bila kupitia chombo hicho wakakuona ulivyokaa, miguu inachezacheza, lishe ndogo, kama hivyo huendi.

Mheshimiwa Spika, ndiyo maana hapo katikati vijana wetu walikuwa wanatumika kupeleka dawa za kulevya, sio leo! Huyu kijana bondia, Hassan amepitia kwenye Kamati yangu, tumemchuja ndiyo maana amekwenda Uingereza. Tarehe 14 Septemba (wiki ijayo), kuna binti anaitwa Feriche anaenda kupigania *commonwealth female lightweight championship,* kule, mkanda huo. Alishapita hapa Bungeni jamani tumchangie kidogo huyu binti wengine mnaojua kusema hapa hajaandaliwa hamkutoa hata senti tano.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo mimi ninachosema tu, hawa vijana wanaandaliwa na ndiyo maana tunaleta hapa Bungeni tuwatukuze. Ahsante sana. *(Makofi)*

**SPIKA:** Nakushukuru sana Mheshimiwa Waziri, Mheshimiwa Kepteni Mstaafu Mkuchika.

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, MENEJIMENTI UTUMISHI WA UMMA NA UTAWALA BORA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba nifafanue hoja ya Mheshimiwa Gekul.

Mheshimiwa Gekul analalamika kwamba swali halijajibiwa vizuri. Mimi ni mwalimu wa *literature,* kabla sijajibu, nalielewa swali. Swali la msingi, muuliza swali alitaka kujua Serikali imechukua hatua gani kuziba mapengo? Sasa Mheshimiwa aliyezungumza habari ya walimu waliohamishwa, kama walimu wamehama kutoka sekondari kwenda msingi hujaongeza ajira Serikalini ila

umewapangia kazi upya. Kwa hiyo mimi nimejibu swali kama alivyotaka muuliza swali. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, la pili amezungumza juu ya walimu kurudishwa. Bunge hili, jumba lako tukufu tunaliheshimu sana. Hapa hapafai kusema mambo ambayo hayana uhakika. Mtoa hoja ameeleza kwamba walihamishiwa shule ya msingi na wamerudishwa, ukiiacha kama hivyo ni kwamba wote wamerudi, si kweli. Wote waliopelekwa wameenda isipokuwa halmashauri tano, na hizo Halmashauri tano Wakurugenzi walisema kuna matatizo ya fedha linashughulikiwa, likishamalizika hilo wale wote waliokuwa wamehamishiwa shule za msingi watakuwa wameenda shule za msingi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, sio vizuri kulidanganya Bunge hili hapa kwamba watu wote ambao walihamishiwa shule za msingi hawajaenda. Si kweli, wamekwenda *over 95 percent.* Nasema swali nimelijibu kama lilivyotaka kuzibwa mapengo Mheshimiwa anazungumza habari ya kuwapangia watu kazi upya. Ukiwapangia watu kazi ambao wamo ndani ya Serikali bila kujali kama ni Wizara gani bado hujaongeza ajira Serikalini. *(Makofi)*

**SPIKA:** Nashukuru sana. Waheshimiwa Wabunge, tunaendelea. Naomba muwepo ili tusikose *quorum* tena. Katibu!

**NDG. STEPHEN KAGAIGAI – KATIBU WA BUNGE:**

**MISWADA YA SHERIA YA SERIKALI**

**Muswada wa Sheria ya Marekebisho ya Sheria Mbalimbali (N a. 2) wa mwaka 2018 *(The Written Laws (Miscellaneous Amendments) (No. 2), Bill, 2018)***

*(Majadiliano Yanaendelea)*

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, mtakumbuka kwamba kazi hii ilipokuwa ikiendelea siku ya Ijumaa ya

Muswada huu Na. 2 siku ya Ijumaa ulikwenda katika hatua ya Bunge Zima na Bunge Zima likamaliza hatua zake zote na Mheshimiwa Mwenyekiti aliyekuwa hapa, Mheshimiwa Najma alimuomba Mheshimiwa Waziri atoe Taarifa ya kazi ya Kamati ya Bunge Zima na Taarifa hiyo ikatolewa. Ilipofikia ni mahali pa Spika kuhoji kuhusu upitishwaji wa Muswada huu na ndipo suala la *quorum* likaja.

Sasa kwa vile *quorum* imekamilika haina wasiwasi sasa naomba nichukue nafasi hii kuwahoji Waheshimiwa Wabunge kuhusiana na Muswada wa Sheria ya Marekebisho ya Sheria mbalimbali (Na. 2) wa Mwaka 2018 *(The Written Laws (Miscellaneous Amendments) (No. 2), 2018).*

*(Hoja Ilitolewa Iamuliwe)*
*(Hoja Iliamuliwa na Kuafikiwa)*

**SPIKA:** Natoa sana pongezi kwa Serikali mlioleta Muswada huu Bungeni. Hata hivyo kabla ya kukamilisha kazi yetu Katibu hebu usomwe tena kwa mara ya tatu.

**NDG. ASIA MINJA – KATIBU MEZANI:**

Muswada wa sheria kwa ajili ya kufanya marekebisho katika sheria mbalimbali zipatazo 13 kwa lengo la kuondoa mapungufu ambayo yamejitokeza katika sheria hizo wakati wa utekelezaji wa baadhi ya masharti katika sheria hizo *(A Bill for an Act to Amend Certain Written Laws).*

*(Kusomwa Mara ya Tatu)*

**SPIKA:** Ahsante sana, kama nilivyokuwa nimesema, sasa hatua zetu zote zimekamilika. Kilichobakia ni Muswada huu kupelekwa mbele ya meza ya Mheshimiwa Rais, akiweka baraka zake basi mabadiliko hayo mbalimbali yatakuwa ni sehemu ya sheria za nchi.

Wale mliokuwa na wasiwasi na akidi, akidi yetu hapa inatakiwa kuwa 195 na hivi sasa mlivyokaa hapa mko 207. Kwa hiyo, hapa nina kila kitu. Anayetoka ina-*deduct*

anayeingia, inakaa sawa sawa, kwa hiyo msiwe na wasi wasi. Nimekaa kisayansi zaidi hapa. Ahsante. *(Kicheko)*

Katibu!

**NDG. ASIA MINJA – KATIBU MEZANI:**

**MISWADA YA SHERIA YA SERIKALI**

**Muswada wa Sheria ya Marekebisho ya Sheria Mbalimbali (Na. 3) wa Mwaka 2018 *(The Written Laws (Miscellaneous Amendments) (No. 3), Bill, 2018)***

**SPIKA:** Haya tunaendelea na Muswada huu ambao tunauanza sasa ambao naomba nimuite Mwanasheria Mkuu wa Serikali ili auwasilishe Muswada huu wa Sheria ya Marekebisho ya Sheria Mbalimbali (Na. 3) wa mwaka 2018. Mheshimiwa Mwanasheria Mkuu wa Serikali, karibu tafadhali.

**MWANASHERIA MKUU WA SERIKALI:** Mheshimiwa Spika, naomba nikushukuru kwa kunipa nafasi ya kuwasilisha maelezo ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali katika Muswada wa Sheria ya Marekebisho ya Sheria mbalimbali (Na.3) wa mwaka 2018 *(The Written Laws (Miscellaneous Amendments) (No. 3) Bill, 2018)* katika Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania tarehe 10 Septemba, 2018.

Mheshimiwa Spika, kwa unyenyekevu mkubwa na kwa kuzingatia masharti ya Kanuni ya 86 ya Kanuni za Kudumu za Bunge Toleo la Januari mwaka 2016 naomba kutoa hoja kwamba Muswada wa Sheria ya Marekebisho ya Sheria Mbalimbali (Na.3) wa mwaka 2018 *(The Written Laws (Miscellaneous Amendments) (No. 3) Act, 2018)* kama ulivyorekebishwa kwa mujibu wa jedwali la marekebisho sasa usomwe mara ya pili na Bunge lako tukufu lijadili na hatimaye lipitishe muswada huu kuwa sehemu ya sheria ya nchi.

Mheshimiwa Spika, naomba kabla ya kutoa maelezo kuhusu muswada huu nianze kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu mwingi wa rehema kwa kutujaalia sisi waja wake

afya njema na kutuwezesha kuendelea kutekeleza majukumu yetu katika Bunge hili. Aidha, ninakupongeza wewe Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Naibu Spika na Waheshimiwa Wenyeviti wa Bunge kwa kuongoza na kusimamia vikao vya mijadala ndani ya Bunge letu kwa umahiri na kuzingatia sheria na kanuni zinazoliongoza Bunge hili. Pia ninawapongeza Waheshimiwa Wabunge wote kwa kuendelea na kutekeleza ipasavyo wajibu wao wa Kikatiba wa kutunga sheria pamoja na kuishauri na kuisimamia Serikali.

Mheshimiwa Spika ninawapongeza watumishi wote wa Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali chini ya Dkt. Evaristo Emmanuel Longopa, Naibu Mwanasheria Mkuu wa Serikali kwa kuendelea na kutekeleza vyema majukumu na kazi za Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali ikiwemo kuandaa muswada huu ambao ulisimamiwa kwa karibu na Bi. Sarah Barahomoka, Mwandishi Mkuu wa Sheria. Tunatambua na tutaendelea kuhakikisha kuwa tunatekeleza majukumu yetu kwa weledi, ufanisi na kwa kuweka mbele maslahi ya nchi yetu chini ya usimamizi mzuri na mahiri wa Mheshimiwa Profesa Palamagamba John Aidan Mwaluko Kabudi, Waziri wa Katiba na Sheria.

Mheshimiwa Spika, ninapenda kuishukuru pia Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Katiba na Sheria chini ya Mwenyekiti wake Mheshimiwa Mohamed Omary Mchengerwa, Mbunge wa Rufiji kwa ushirikiano na ushauri waliotupatia wakati wa kupitia muswada huu mbele ya Kamati hiyo. Kamati hii ilifanya kazi kubwa ikiwemo kusikiliza na kuchambua maoni yaliyowasilishwa na wadau na kutoa mapendekezo yake kwa Serikali kwa nia ya kuboresha muswada huu. Ushauri, maoni na mapendekezo ya Kamati hiyo yametusaidia kuuboresha Muswada huu kama inavyoonekana katika jedwali la marekebisho.

Mheshimiwa Spika, Muswada wa Sheria ya Marekebisho ya Sheria Mbalimbali (Na.3) wa mwaka 2018 *(The Written Laws (Miscellaneous Amendments) (No.3) Bill, 2018)* unapendekeza kufanya marekebisho katika sheria sita zifuatazo:-

Kwanza Sheria ya Mamlaka ya Rufaa Sura ya 141 *(The appellate Jurisdiction Act Cap. 141),* Sheria ya Uendeshaji wa Mashauri ya Madai Sura ya 33 *(The Civil Procedure Code Cap. 33),* Sheria ya Mahakama za Utatuzi wa Migogoro ya Ardhi, Sura ya 216 *(The Land Disputes Courts Act Cap. 216),* Sheria ya Mahakama za Mahakimu Sura ya 11 *(The Magistrates Courts Act Cap. 11),* Sheria ya Baraza la Taifa la Michezo Tanzania Sura ya 49 *(The National Sports Council, Tanzania Cap. 49)* na Sheria ya Takwimu Sura ya 351 *(The Statistics Act, Cap 351).*

Mheshimiwa Spika, marekebisho yanayopendekezwa katika muswada huu yanalenga kuboresha na kuimarisha na utekelezaji wa sheria hizo kwa kuondoa upungufu ulioonekana wakati wa kuzitumia na kuweka masharti mengine ili kuleta uwiano kati ya sheria zinazorekebishwa na sheria zilizopo. Masuala muhimu yanayozingatiwa katika Muswada huu yanahusisha kubadilisha vifungu vya sheria kwa kufuta baadhi ya vifungu vya sheria hizo na kuviandika upya, kuongeza vifungo vipya vya sheria, kufuta baadhi ya maneno kwenye vifungu vya sheria na kuingiza maneno mapya.

Mheshimiwa Spika, Muswada huu umegawanyika katika sehemu kuu saba; sehemu ya kwanza inahusu masharti ya utangulizi ambayo yanajumuisha jina la muswada na tamko kuhusu marekebisho ya sheria mbalimbali zinazopendekezwa kurekebishwa kupitia muswada huu; sehemu ya pili ya Muswada inapendekeza marekebishao katika Sheria ya Mamlaka ya Rufaa, Sura ya 141 *(The Appellate Jurisdiction Act Cap. 141),* sheria hiyo inaainisha masharti kuhusu rufaa katika Mahakama ya Rufani. Marekebisho yanayopendekezwa kupitia muswada huu ni kuongeza vifungu vipya vya 3(a) na 3(b) katika sheria hiyo kwa lengo la kuainisha dhumuni kuu la sheria hiyo na wajibu wa kutenda haki; masharti hayo hayamo katika sheria ya sasa. Kifungu kipya cha 3(a) kinaainisha kuwa dhumuni kuu la sheria ya mamlaka ya rufaa ni kuwezesha maamuzi yanayosimamiwa na sheria hiyo kutolewa kwa haki haraka, usawa na kwa gharama nafuu. Aidha, dhumuni hilo litakuwa msingi utakaozingatiwa na Mahakama na Rufani wakati ikitekeleza mamlaka yake chini ya sheria hiyo.

Mheshimiwa Spika, muswada unapendekeza pia kifungu kipya cha 3(b) ambacho kinaitaka Mahakama ya Rufani kushughulikia jambo linaloletwa mbele yake kwa lengo la kuhakikisha kuwa haki inapatikana na kuna ufanisi *(efficiency)* na kutumia rasilimali zilizopo Mahakamani ikiwemo teknolojia na kwamba mashauri yanamalizika mapema kwa gharama ambayo *panel* husika wanaweza kuimudu. Kama inavyoonekana kwenye jedwali la mrekebisho, Jaji Mkuu amepewa mamlaka ya kutunga kanuni kwa ajili ya utekelezaji bora wa vifungu hivyo vipya.

Mheshimiwa Spika, sehemu ya tatu inapendekeza marekebisho katika Sheria ya Uendeshaji wa Mahakama ya Mashauri ya Madai, Sura ya 33 *(The Civil Procedure Code Cap. 33).* Sheria hiyo inaweka masharti kuhusu utaratibu na masuala muhimu katika uendeshaji wa mashauri ya madai katika Mahakama Kuu, Mahakama ya Hakimu Mkazi na Mahakama ya Wilaya. Marekebisho yanayopendekezwa katika Sheria ya Uendeshaji wa Mashauri ya Madai hayatofautiani na marekebisho ambayo yamependekezwa katika Sheria ya Mamlaka ya Rufaa.

Mheshimiwa Spika, kwa ujumla marekebisho katika sehemu ya pili na sehemu ya tatu ya muswada yanalenga kutekeleza ipasavyo Ibara ya 107(a)(2) ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya mwaka 1977 ambayo inaainisha kanuni za kuzingatiwa na Mahakama nchini katika kutoa uamuzi wa mashauri. Katika kutekeleza masharti hayo ya Katiba, Muswada huu katika sehemu ya pili na sehemu ya tatu unaweka mwongozo ambao uatapaswa kuzingatiwa na majaji na Mahakimu katika kushughulikia mashauri ya madai yaliyopo katika Mahakama ya Rufani, Mahakama Kuu, Mahakama ya Hakimu Mkazi na Mahakama ya Wilaya.

Mheshimiwa Spika, sehemu ya nne ya Muswada inapendekeza marekebisho katika sheria ya Mahama za Utatuzi wa Migogoro ya Ardhi Sura ya 216 *(The Land Disputes Courts Act. Cap. 216).* Marekebisho yanayopendekeza ni kuongeza kifungu kipya cha 41(a) kuhusu mamlaka ya nyongeza *(extended jurisdiction).* Kifungu cha 41(a)

kinachopendekezwa kinaweka masharti kwamba Jaji Mkuu baada ya kushauriana na Waziri mwenye dhama ya masuala ya sheria pamoja na Mwanasheria Mkuu wa Serikali anaweza kutoa amri itakayochapishwa katika Gazeti la Serikali ambayo inampatia Hakimu Mkazi mamlaka ya kusikiliza rufaa au marejeo *(appellate or revisional jurisdiction),* kutoka Baraza la Ardhi na Nyumba la Wilaya au kutoka Baraza la Kata ambayo kwa kawaida husikilizwa na Mahakama Kuu chini ya sheria hiyo. Lengo la marekebisho haya ni kupunguza mrundikano wa rufaa za mashauri ya ardhi katika Mahakama Kuu kutokana na uhaba wa majaji na hivyo kutatua migogoro ya ardhi mapema.

Mheshimiwa Spika, sehemu ya muswada inapendekeza pia kurekebisha kifungu cha 47 cha Sheria ya Utatuzi wa Migogoro ya Ardhi kuhusu rufaa za migogoro ya ardhi kutoka Mahakama Kuu. Kwa sasa kifungu hicho kinaeleza kuwa mtu ambaye hajaridhishwa na uamuzi wa Mahakama Kuu kwa shauri lililoanzia Mahakama Kuu au lililoanzia Mabaraza ya Ardhi akate Rufaa kwenda Mahakama ya Rufani baada ya kupata kibali cha Mahakama Kuu. Katika marekebisho haya, sharti la kuomba kibali kwanza litahusika na mashauri yaliyoanzia katika Mabaraza ya Ardhi pekee na sharti hilo la kuomba kwanza kibali halitahusika kwa shauri lililoanzia katika Mahakama Kuu.

Sehemu ya tano ya muswada inapendekeza marekebisho katika Sheria ya Mahakama za Mahakimu, Sura ya 11 *(The Magistrates Courts Act Cap. 11).* Kama inavyoonekana katika jedwali la marekebisho, mapendekezo kuhusu kuanzisha mahakama inayohamishika *(mobile court)* na mahakama maalum *(special court)* pamoja na masuala kuhusu madai madogo *(small claims)* yameondolewa na Serikali. Marekebisho pekee yaliyoko katika sehemu hii yanahusu kifungu cha 45, kifungu kidogo cha sheria hiyo. Kifungu hicho kwa sasa kinampatia Hakimu mwenye mamlaka ya nyongeza *(extended jurisdiction)* uwezo wa kusikiliza rufaa na shauri ambalo kwa kawaida linasikilizwa na Mahakama Kuu kama shauri hilo litakuwa limeanzia Mahakama ya Wilaya au Mahakama ya Hakimu Mkazi.

Mheshimiwa Spika, marekebisho pekee yaliyoko katika sehemu hii yanahusu Kifungu cha 45, Kifungu kidogo cha sheria hiyo. Kifungu hicho kwa sasa kinampatia Hakimu mwenye mamlaka ya nyongeza *(Extended Jurisdiction)* uwezo wa kusikiliza rufaa na shauri ambalo kwa kawaida linasikilizwa na Mahakama Kuu, kama shauri hilo litakuwa limeanzia Mahakama ya Wilaya au Mahakama ya Hakimu Mkazi.

Mheshimiwa Spika, Muswada unapendekeza kifungu hicho kirekebishwe kwa kuongeza masharti yatakayowezesha Hakimu mwenye mamlaka ya nyongeza kusikiliza na kuamua rufaa katika mashauri yatakayokuwa yameanzia Mahakama ya Mwanzo pia. Marekebisho haya yanalenga kuharakisha utoaji wa uamuzi wa rufaa kuhusu mashauri yaliyoanzia Mahakama ya Mwanzo ambayo yako Mahakama Kuu.

Mheshimiwa Spika, Sehemu ya Sita ya Muswada inapendekeza marekebisho katika Sheria ya Baraza la Taifa la Michezo Tanzania, Sura ya 49 *(The National Sports Council of Tanzania Act, Cap. 49);* Kifungu cha pili (2) cha sheria hiyo kinatoa tafsiri ya maneno Chama cha Mchezo *(Sport Association)* kuwa ni chama ambacho kinasimamia michezo ya ridhaa.

Mheshimiwa Spika, Vyama vinavyosimamia michezo ya kulipwa vimeachwa katika tafsiri hiyo. Hatua hiyo imesababisha watu wanaojihusisha na michezo ya kulipwa *(Professionals)* kuendesha shughuli zao bila kusajili vyama vyao kwa Msajili wa Vyama vya Michezo kwa madai kuwa tafsiri iliyoko kwenye sheria haiwagusi. Marekebisho haya yatawezesha kila chama cha michezo, vikiwemo vyama vya michezo ya kulipwa kusimamiwa ipasavyo na Baraza la Michezo la Taifa na hivyo kutekeleza majukumu yake kwa mwongozo utakaotolewa na Serikali kupitia Baraza la Michezo la Taifa.

Mheshimiwa Spika, Kifungu cha pili (2) cha Sheria hiyo kinarekebishwa pia, kwa kuongeza tafsiri mpya ya neno *Sports*

ambalo linatoa tafsiri zaidi kiasi cha kugusa bahati nasibu za kimichezo *(Sports Betting).* Kukosekana kwa tafsiri hiyo katika sheria ya sasa kumesababisha mamlaka ya kusimamia michezo kutosimamia ipasavyo na kunufaika na baadhi ya michezo, ikiwemo bahati nasibu za kimichezo *(Sports Betting).*

Mheshimiwa Spika, baada ya marekebisho haya Baraza la Michezo la Taifa litaweza kuweka utaratibu wa kuwatambua na kuwasimamia watu wanaoendesha michezo ya kubahatisha katika sekta ya michezo.

Mheshimiwa Spika, Kifungu cha tatu (3) cha Sheria hiyo kinaanzisha Baraza la Michezo la Taifa na kuianisha, pamoja na mengineyo kuwa, baraza hilo linaweza kushtaki au kushtakiwa Mahakamani.

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa, baraza hilo ni Taasisi ya Serikali na kwa kuwa, Mwanasheria Mkuu wa Serikali ndiye Mshauri Mkuu wa Serikali na Taasisi zake kwa masuala yote ya kisheria na anayo haki ya kuhudhuria na kusikilizwa katika Mahakama zote katika Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kupitia Wakili Mkuu wa Serikali. Muswada unapendekeza Kifungu hicho cha tatu (3) kirekebishwe, ili kuongeza masharti yatakayompatia Mwanasheria Mkuu wa Serikali haki ya kuingilia kati shauri lililofunguliwa na/au dhidi ya baraza kwa kuliwakilisha baraza hiloMahakamani katika shauri husika pale inapoonekana kuna umuhimu wa kufanya hivyo. Aidha, baraza limepewa wajibu wa kumfahamisha Mwanasheria Mkuu wa Serikali pale linaposhtakiwa au kushtaki Mahakamani.

Mheshimiwa Spika, Kifungu cha nne (4)) cha sheria hiyo, kinaainisha masharti kuhusu majukumu ya Baraza la Michezo la Taifa; moja ya majukumu hayo ni kukuza na kuendeleza michezo ya ridhaa kwa kushirikiana na vyama vya michezo na ridhaa nchini. Muswada katika sehemu hii unapendekeza kifungu hicho kirekebishwe kwa kuweka masharti ambayo yataliwezesha Baraza la Michezo la Taifa kusimamia vyema vyama vyote vya michezo yote kama ilivyofafanuliwa awali.

Mheshimiwa Spika, Sehemu hii inapendekeza pia, kurekebisha Vifungu vya 6(b), 10 na 21(1) vya Sheria ya Baraza la Michezo la Taifa kwa kusahihisha makosa ya kiuandishi kwa lengo la kuwezesha utekelezaji bora wa sheria hiyo.

Mheshimiwa Spika, Kifungu cha 8(2) cha sheria hiyo kinaelekeza kuwa hesabu za Baraza la Michezo la Taifa zitakaguliwa na Shirika la Ukaguzi Tanzania *(Tanzania Audit Corporation.* Kwa kuwa, Baraza la Michezo la Taifa ni chombo cha Serikali na linapokea fedha kutoka Serikalini, hesabu zake zinatakiwa kukaguliwa na Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali. Hivyo, Muswada unapendekeza kurekebisha Kifungu cha 8(2)(3) na (4) kwa kuweka masharti kwamba, hesabu za baraza hilo zitakaguliwa na Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali na sio Shirika la Ukaguzi la Taifa au Wakaguzi wa shirika hilo, kama inavyotajwa katika sheria sasa.

Mheshimiwa Spika, kwa upande mwingine Kifungu cha 8(3) kinaweka masharti kuwa, ripoti ya ukaguzi ni miongoni mwa taarifa za kifedha zitakazowasilishwa kwa Waziri mwenye dhamana ya michezo, huku Kifungu cha 8(4) kikieleza kuwa Taarifa ya Ukaguzi iwasilishwe katika Bunge.

Mheshimiwa Spika, Sehemu ya Saba ya Muswada inapendekeza marekebisho katika Sheria ya Takwimu, Sura ya 351 *(The Statistic Act, Cap 351);* kama inavyoonekana katika Jedwali la Marekebisho, marekebisho ya jumla yanayopendekezwa katika sheria hiyo ni kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, kwanza kufuta maneno Mkurugenzi Mkuu popote yanapoonekana katika sheria hiyo na badala yake kuweka maneno Mtakwimu Mkuu *(Statistician General).* Lengo la marekebisho haya ni kutumia maneno ambayo yanaakisi majukumu ya Ofisi ya Taifa ya Takwimu katika kusimamia ukusanyaji, uandaaji na utoaji wa takwimu nchini.

Mheshimiwa Spika, pili kufuta maneno *statistical information* na *official statistical information* yaliyoko katika

Vifungu vya 6(2)(c) na (f). Kifungu cha 19, Kifungu cha 22(2), Kifungu cha 28 na Kifungu cha 37(2) na kuweka badala yake maneno *Official Statistics* ambayo ndio maneno sahihi yanayopaswa kutumika.

Mheshimiwa Spika, sehemu hii inapendekeza pia kurekebisha Kifungu cha tatu (3) cha Sheria ya Takwimu kwa kuandika upya tafsiri ya maneno *Official Statistics* ambayo itamaanisha takwimu zilizopatikana kuhakikiwa, kuunganishwa au kusambazwa na/au kwa mamlaka ya Ofisi ya Taifa ya Takwimu.

Mheshimiwa Spika, lengo la marekebisho haya ni kutofautisha takwimu rasmi na takwimu nyingine zinazotolewa na taasisi au watu wengine. Aidha, tafsiri ya maneno *statistical information* ambayo yametumika katika sheria hiyo yameongezwa, ili kurahisisha utekelezaji bora wa sheria hiyo wakati wa kuitumia.

Mheshimiwa Spika, Kifungu cha 17(3)(a) na (b) cha sheria hiyo kinaelekeza kuwa Ofisi ya Takwimu ya Taifa katika kutekeleza jukumu la uratibu wa takwimu chini ya sheria hiyo, itatoa kanuni za utendaji ambazo zitazingatiwa na wakala zinazotoa takwimu rasmi. Pia, ofisi hiyo itaandaa benki ya takwimu za Taifa kwa kutumia benki ya takwimu iliyoanzishwa na wakala husika.

Mheshimiwa Spika, Muswada katika sehemu hii unapendekeza kifungu hicho kirekebishwe kwa kuweka masharti yatakayowezesha kanuni za utendaji kazi kuzingatiwa pia na taasisi nyingine za Serikali na pia Ofisi ya Taifa ya Takwimu kutumia Benki ya Takwimu ya Taasisi za Serikali.

Mheshimiwa Spika, marekebisho mengine katika sehemu hii ni kufuta na kuandika upya vifungu vya 18 na 19 vya Sheria ya Takwimu kwa lengo la kuainisha kwa ufasaha zaidi majukumu ya Mtakwimu Mkuu. Kifungu Kipya cha 18 kinapendekeza kuwa, Mtakwimu Mkuu atakuwa na mamlaka ya kuanzisha, kurekebisha au kufuta takwimu rasmi

zilizokusanywa kwa njia ya tafiti *(Survey)* au sensa. Na kwamba, mtu, taasisi ya Serikali au wakala hautaruhusu ukusanyaji wa takwimu rasmi kufanyika pasipo kupata kwanza kibali cha Mtakwimu Mkuu. Lengo la marekebisho haya ni kumwezesha Mtakwimu Mkuu kusimamia ipasavyo ukusanyaji wa takwimu.

Mheshimiwa Spika, Kifungu Kipya cha 19 kinaweka masharti kuwa mamlaka ya kukusanya takwimu rasmi ambayo Wakuu wa Taasisi za Serikali wanayo kwa mujibu wa sheria zao, yatachukuliwa kuwa yamekasimiwa kwao na Mtakwimu Mkuu. Masharti hayo yapo katika sheria ya sasa, lakini katika Muswada huu yameandikwa kwa namna ambayo inaeleweka zaidi ili kurahisisha utekelezaji bora wa sheria hiyo. Aidha, marekebisho haya yanalenga kutambua takwimu rasmi zinazokusanywa kisheria na taasisi za Serikali kwa ajili ya utekelezaji wa majukumu ya taasisi husika.

Mheshimiwa Spika, Kifungu cha 20 cha Sheria ya Takwimu kinarekebishwa kwa kufuta maneno ya pembeni *(Marginal Notes),* ili yasomeke *"producers of official statistics"* badala ya *"official statistics".* Pia, Kifungu kidogo cha (1) kinarekebishwa kwa kuweka masharti yatakayowezesha kifungu hicho kutumika kwa wazalishaji wa takwimu rasmi.

Mheshimiwa Spika, lengo la marekebisho haya ni kurahisisha utekelezaji bora wa sheria hiyo katika kusimamia upatikanaji wa takwimu rasmi.

Mheshimiwa Spika, Muswada katika Sehemu hii unapendekeza pia, kufuta na kuandika upya Kifungu cha 22(2) cha Sheria ya Takwimu ambacho kinaweka masharti kuhusu ukusanyaji wa takwimu nyingine kwa lengo la kuwezesha kifungu hicho kusomeka na kueleweka vyema na hivyo kurahisisha utekelezaji mzuri wa sheria hiyo.

Mheshimiwa Spika, makerebisho mengine yanayopendekezwa katika sehemu hii ni kuongeza Kifungu kipya cha 24(a) ambacho kinaweka masharti kuwa, mtu

aliyepata kibali cha kutumia takwimu rasmi za Ofisi ya Taifa ya Takwimu hatachapisha au kutoa taarifa husika kwa umma bila kupata kibali cha ofisi hiyo.

Mheshimiwa Spika, Muswada huu unapendekeza pia kufuta Kifungu cha 37(4) cha Sheria ya Takwimu na kukiandika upya kwa kuweka masharti kuwa, mtu yeyote ya atakayechapisha au kusambaza takwimu, rasimu au taarifa ya kitakwimu kinyume na sheria hiyo, atakuwa ametenda kosa la jinai. Marekebisho haya yanalenga kuhakikisha kuwa, masharti kuhusu uchapishaji au usambazaji wa takwimu, rasimu au taarifa za kitakwimu yanatekelezwa ipasavyo.

Mheshimiwa Spika, mwisho, Muswada katika sehemu hii unapendekeza Vifungu Vidogo vya (5) na (6) vya Kifungu cha 37 vifutwe kwa kuwa, masharti yake yameingizwa katika vifungu vilivyorekebishwa kupitia Muswada huu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, baada ya maelezo hayo na kwa mara nyingine tena, nashukuru sana kwa kunipatia nafasi ya kuwasilisha maelezo ya hoja kuhusu Muswada wa Sheria ya Marekebisho ya Sheria Mbalimbali Na.3 wa Mwaka 2018 *(The Written Laws Miscellaneous Amendments, No.3 Bill, 2018).* Naomba sasa Bunge lako Tukufu liujadili na kuupitisha katika hatua ya Kusomwa kwa Mara ya Pili na Mara ya Tatu, ili hatimaye marekebisho yanayopendekezwa yawe sehemu ya sheria za nchi.

Mheshimiwa Spika, naomba kutoa hoja. *(Makofi)*

**WAZIRI WA HABARI, UTAMADUNI, SANAA NA MICHEZO:** Mheshimiwa Spika, naafiki.

*(Hoja ilitolewa iamuliwe)*

**SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Mwanasheria Mkuu wa Serikali. Tunakushukuru sana kwa kuitoa hoja yako na hoja imeungwa mkono. Asante sana kwa kuipitia vizuri namna hiyo, tumekuelewa.

NAKALA MTANDAO(ONLINE DOCUMENT)

**ISSN 0856 - 034X**

THE UNITED REPUBLIC OF TANZANIA

***BILL SUPPLEMENT***

***No.2*** ***8th June, 2018***

*to the Gazette of the United Republic of Tanzania No.23. Vol.99 dated 8th June, 2018*
Printed by the Government Printer, Dodoma by Order of Government

# THE WRITTEN LAWS (MISCELLANEOUS AMENDMENTS)(NO.3) ACT, 2018

## ARRANGEMENT OF SECTIONS

*Section* *Title*

PART I
PRELIMINARY PROVISIONS

1. Short title.
2. Amendment of certain written laws.

PART II
AMENDMENT OF THE APPELLATE JURISDICTION ACT,
(CAP. 141)

3. Construction.
4. Addition of sections 3A and 3B.

PART III
AMENDMENT OF THE CIVIL PROCEDURE CODE,
(CAP.33

5. Construction.
6. Addition of sections 3A and 3B.

PART IV
AMENDMENT OF THE LAND DISPUTES COURTS ACT,
(CAP 216)

7. Construction.
8. Addition of section 41A.
9. Amendment of section 47.

PART V
AMENDMENT OF THE MAGISTRATES' COURTS ACT,
(CAP.11)

10. Construction.
11. Amendment of section 2.
12. Addition of sections 17A, 17B and 17C.
13. Addition of section 42A.
14. Amendment of section 45.

PART VI
AMENDMENT OF THE NATIONAL SPORTS COUNCIL OF TANZANIA ACT,
(CAP.49)

15. Construction.
16. Amendment of section 2.
17. Amendment of section 3.
18. Amendment of section 4.
19. Amendment of section 6.
20. Amendment of section 8
21. Amendment of section 10.
22. Amendment of section 21.

PART VII
AMENDMENT OF THE STATISTICS ACT,
(CAP.351)

23. Construction.

24. General amendment.
25. Amendment of section 3.
26. Amendment of section 17.
27. Repeal and replacement of section 18.
28. Repeal and replacement of section 19.
29. Amendment of section 20.
30. Amendment of section 22.
31. Addition of section 24A.
32. Amendment of section 37.

## NOTICE

**This Bill to be submitted to the National Assembly is published for general information to the general public together with a statement of its objects and reasons.**

Dodoma,
7 June, 2018

**JOHN W. H. KIJAZI**
*Secretary to the Cabinet*

**A BILL**
*for*

An Act to amend certain written laws.

**ENACTED** by Parliament of the United Republic of Tanzania.

PART I
PRELIMINARY PROVISIONS

Short title

**1**. This Act may be cited as the Written Laws (Miscellaneous Amendments)(No.3) Act, 2018.

Amendment of certain written laws

**2**. The written laws specified in various Parts of this Act are amended in the manner specified in their respective Parts.

PART II
AMENDMENT OF THE APPELLATE JURISDICTION ACT,
(CAP. 141)

Construction
Cap. 141

**3**. This Part shall be read as one with the Appellate Jurisdiction Act, hereinafter referred to as the "principal Act".

Addition of sections 3A and 3B

**4**. The principal Act is amended by adding immediately after section 3 the following -

"Overriding objective of

**3A**.-(1) The overriding objective of this Act shall be to facilitate the just, expeditious, proportionate and affordable

Act

resolution of all matters governed by this Act.

(2) The Court shall, in the exercise of its powers under this Act or the interpretation of any of its provisions, seek to give effect to the overriding objective specified in subsection (1).

Duty to uphold objective

**3B**.-(1) For the purpose of furthering the overriding objective specified in section 3A, the Court shall handle all matters presented before it with a view to attaining the following-

(a) just determination of the proceedings;

(b) efficient use of the available judicial and administrative resources including the use of suitable technology; and

(c) timely disposal of the proceedings in the Court at a cost affordable by the respective parties.

(2) A party to proceedings before the court or an advocate for such a party shall have the duty to assist the Court to further the overriding objective and to that effect, participate in the processes of the Court and comply with directions and orders of the Court."

## PART III
## AMENDMENT OF THE CIVIL PROCEDURE CODE, (CAP.33)

Construction Cap. 33

**5**. This Part shall be read as one with the Civil Procedure Code, hereinafter referred to as the "principal Act".

Addition of sections 3A and 3B

**6**. The principal Act is amended by adding immediately after section 3 the following-

"Overriding objective of Act

**3A**.-(1) The overriding objective of this Act shall be to facilitate the just, expeditious, proportionate and affordable resolution of civil disputes governed by this Act.

(2) The Court shall, in the exercise of its powers under this Act or the interpretation of any of its provisions, seek to give effect to the overriding objective specified in subsection (1).

Duty to uphold objective

**3B**.-(1). For the purpose of furthering the overriding objective specified in section 3A, the Court shall handle all matters presented before it with a view to attaining the

following-

(a) just determination of the proceedings;

(b) efficient use of the available judicial and administrative resources including the use of suitable technology; and

(c) timely disposal of the proceedings at a cost affordable by the respective parties.

(2) A party to civil proceedings or an advocate for such a party shall have a duty to assist the Court to further overriding the objective of this Act and, to that effect, to participate in the processes of the Court and to comply with the directions and orders of the Court."

## PART IV
## AMENDMENT OF THE LAND DISPUTES COURTS ACT, (CAP 216)

Construction Cap. 216

**7**. This Part shall be read as one with the Land Disputes Courts Act, hereinafter referred to as the "principal Act".

Addition of section 41A

**8**. The principal Act is amended by adding immediately after section 41 the following new section-

"Extended jurisdiction

41A-(1) Notwithstanding section 41, the Chief Justice may, after consultation with the Minister responsible for legal affairs and the Attorney General, by order published in the Gazette, vest any resident magistrate with the appellate or revisional jurisdiction ordinarily exercisable by the High Court under this Act.

(2) For the purpose of any appeal from or revision in the exercise of jurisdiction referred to under subsection (1), the resident magistrate with extended jurisdiction shall be deemed to be the judge of the High Court, and court presided over by him while exercising such jurisdiction shall be deemed to be the High Court.

(3) The High Court may direct that an appeal or revision instituted in the High Court be transferred to and be heard by a resident magistrate upon whom extended jurisdiction has been conferred by this section."

Amendment

**9**. The principal Act is amended in section 47, by-

of section 47

(a) deleting subsection (1) and substituting for it the following:

"(1) A person who is aggrieved by the decision of the High Court in the exercise of its original jurisdiction may appeal to the Court of Appeal in accordance with the provisions of the Appellate Jurisdiction Act."

(b) adding immediately after subsection (1) the following:

"(2) A person who is aggrieved by the decision of the High Court in the exercise of its revisional or appellate jurisdiction may, with leave of the High Court or Court of Appeal, appeal to the Court of Appeal."

(c) renumbering subsections (2) and (3) as subsections (3) and (4) respectively.

PART V

AMENDMENT OF THE MAGISTRATES' COURTS ACT, (CAP.11)

Construction
Cap. 11

**10**. This Part shall be read as one with the Magistrates' Courts Act, hereinafter referred to as the "principal Act".

Amendment of section 2

**11**. The principal Act is amended in section 2 by adding in the appropriate alphabetical order the following definitions:

""mobile court" means a court established pursuant to section 17A having a pecuniary jurisdiction to cater for small claims or criminal matters of such nature as may be specified by the Chief Justice;

"small claim" means a claim of civil nature the value of which does not exceed one hundred million shillings;

"special court" means a court established pursuant to section 17A for purposes of determination of such matter as may be specified by the Chief Justice;"

Addition of sections 17A, 17B and 17C

**12.** The principal Act is amended by adding immediately after section 17, the following:

"Establishment of mobile courts or special courts

**17A.-**(1) Notwithstanding the provisions of this Act and any other written laws on the jurisdiction of the magistrate courts, the Chief Justice may, if in his opinion it is in the public interest to do so, by Order published in the *Gazette* establish a mobile court or special court for expeditious determination of specified cases.

(2) The Chief Justice shall, in the Order under subsection (1), specify-

(a) matters relating to the jurisdiction of the mobile

court or special court;

(b) the type of cases to be determined by the mobile court or special court; or

(c) such other matters as the Chief Justice may deem appropriate for the purpose of operations of the mobile court or special court.

Rules of procedure for mobile courts or special courts

**17B**. The Chief Justice may make rules prescribing matters relating to practice and procedure of mobile courts or special court.

Appeals from mobile courts or special courts

**17C.-**(1) No appeal shall lie or be made against a decision or order of a mobile courts or special court in respect of small claims except on a point of law, in which case an appeal shall lie before the High Court.

(2) Appeals from mobile court or special court regarding other matters shall be governed in a manner provided for under Part III and IV of this Act."

Addition of section 42A

**13.** The principal Act is amended by adding immediately after section 42 the following new section:

"Representation in mobile courts

**42A.-**(1) An advocate, other than an advocate who is a party acting solely on his own behalf, shall not appear on behalf of any party in small claim proceedings before a mobile court, except that, the court may permit any relative or any member of the household of any party to any proceedings, upon the request of such party, to appear and act for that party.

(2) In any proceedings before a mobile court or special court to which a body corporate is a party, a person in the employment of the body corporate and duly authorized in that behalf, other than an advocate, may appear and act on behalf of that party."

Amendment of section 45

**14**. The principal Act is amended in section 45(1), by adding immediately after the words "High Court" appearing at the end of paragraphs (a) and (b) the words, "under this Part and subpart (c) of Part III to this Act."

## PART VI
## AMENDMENT OF THE NATIONAL SPORTS COUNCIL OF TANZANIA ACT, (CAP 49)

Construction
Cap. 49

**15**. This part shall be read as one with the National Sports Council of Tanzania Act, hereinafter referred to as the "principal Act".

Amendment of section 2

**16**. The principal Act is amended in section 2, by-

(a) deleting the word "amateur" in the definition of the term "sports association" and substituting for it the words "all forms of";

(b) adding in the appropriate alphabetical order the following:

""sports" means an activity involving physical exertion and skill in which an individual or team competes against another for entertainment, and includes sports betting;".

Amendment of section 3

**17**. The principal Act is amended in section 3, by-

(a) adding immediately after subsection (1) the following provisions:

"(2) Notwithstanding the provisions of subsection (1), the Attorney General shall have the right to intervene in any suit or matter instituted by or against the Council.

Cap.5

(3) Where the Attorney General intervenes in any matter pursuant to subsection (2), the provisions of the Government Proceedings Act shall apply in relation to the proceedings of that suit or matter as if it had been instituted by or against the Government.

(4) The Council or such other person on its behalf shall have the duty of notifying the Attorney General of any impending suit or intention to institute a suit or matter for or against the Council.";

(b) renaming subsection (2) as subsection (5).

Amendment of section 4

**18**. The principal Act is amended in section 4, by-

(a) deleting the word "amateur" appearing in subsection (1) (a);

(b) deleting the word "amateur" appearing in subsection (2) (g) and substituting for it the words "all forms of".

Amendment of section 6

**19**. The principal Act is amended in section 6(b), by deleting the word "or" appearing immediately after the word "approval" and substituting for it the word "of".

Amendment of section 8

**20**. The principal Act is amended in section 8, by-

(a) deleting the words "Tanzania Audit Corporation" appearing in subsection (2) and substituting for it the words "Controller and Auditor General";
(b) deleting the word "auditors" appearing in subsection (3), and substituting for it the words "Controller and Auditor General";
(c) deleting the word "auditor's" appearing in subsection (4) and substituting for it the words " Controller and Auditor General".

Amendment of section 10

**21**. The principal Act is amended in section 10, by deleting the words "as many" and substituting for them the words "such number of".

Amendment of section 21

**22**. The principal Act is amended in section 21(1), by deleting the word "up" appearing immediately after the word "binding" and substituting for it the word "upon".

PART VII
AMENDMENT OF THE STATISTICS ACT,
(CAP.351)

Construction Cap.351

**23.** This Part shall be read as one with the Statistics Act, hereinafter referred to as the "principal Act."

General amendment

**24.** The principal Act is amended generally by-

(a) deleting the title "Director General" wherever it appears throughout the Act and substituting for it the title "Chief Government Statistician";
(b) deleting the words "statistical information" and "official statistical information" wherever they appear in sections 5, 6(2)(c) and (f), 19, 22(2), 23(1), 28 and 37(2), (4), (5), (6) and substituting for them the words "official statistics".

Amendment of section 3

**25.** The principal Act is amended in section 3, by -

(a) deleting the definition of the term "official statistics" and substituting for it the following:
""official statistics" means statistics produced, validated, compiled or disseminated by or under the authority of the Bureau;"; and
(b) adding in the appropriate alphabetical order the following new

definition:

““statistical information” means any organized quantitative or qualitative information obtained from different sources through censuses, surveys or administrative data.”

Amendment of section 17

**26.** The principal Act is amended in section 17(3), by -

(a) deleting the word “all” appearing in paragraph (a) and substituting for it the words “Government institutions and”; and

(b) inserting the word “Government institution and” between the words “by” and “agencies” appearing in paragraph (b).

Repeal and replacement of section 18

**27.** The principal Act is amended by repealing section 18 and replacing it with the following:

“Mandate to collect official statistics

**18**.-(1) Without prejudice to section 20, the Chief Government Statistician shall have powers to commence, vary or discontinue the collection of official statistics conducted through surveys or censuses.

(2) A person, Government institution or agency shall not authorise the commencement of the collection of official statistics through surveys or censuses except with the approval of the Chief Government Statistician.”

Repeal and replacement of section 19

**28.** The principal Act is amended by repealing section 19 and replacing it with the following:

“Delegation of powers to collect official statistics

**19.** Notwithstanding the generality of section 18(2) and subject to guidelines issued by the Bureau, powers to collect official statistics afforded to heads of Government institutions pursuant to any written laws shall be deemed to be powers delegated to those institutions by the Chief Government Statistician.”

Amendment of section 20

**29.** The principal Act is amended in section 20, by-

(a) deleting the marginal note and substituting for it the following:

“Producers of official statistics”;

(b) deleting the opening words of subsection (1) and substituting for them the following:

“(1) Official statistics may be produced by-”;

(c) deleting subsection (3).

Amendment of section 22

**30.** The principal Act is amended in section 22, by-

(a) deleting the word "other" appearing in the marginal note;
(b) deleting subsection (2) and substituting for it the following:

"(2) The Bureau may cause to be published statistics collected pursuant to subsection (1).".

Addition of section 24A

**31.** The principal Act is amended by adding immediately after section 24 the following:

"Dissemination of official statistics

**24A.**-(1) Any person who is authorised by the Bureau to process any official statistics, shall before publishing or communicating such information to the public, obtain an authorisation from the Bureau.

(2) A person shall not disseminate or otherwise communicate to the public any statistical information which is intended to invalidate, distort or discredit official statistics.".

Amendment of section 37

**32.** The principal Act is amended in section 37, by -

(a) inserting the words ", being an employee of the Bureau," between the words "person" and "who" appearing in the opening phrase of subsection (1);
(b) deleting subsection (4) and substituting for it the following:

"(4) Any person who publishes or causes to be published or communicates any official statistics or statistical information contrary to the provisions of this Act, commits an offence and is liable, on conviction to a fine of not less than ten million shillings or to imprisonment for a term of not less than three years or to both.";

(c) deleting subsections (5) and (6).

## OBJECTS AND REASONS

This Bill proposes to amend Six laws namely, the Appellate Jurisdiction Act, Cap 141, the Civil Procedure Code, Cap.33, the land Disputes Courts Act, Cap.216 the Magistrates'

Courts Act, Cap.11, the National Sports Council of Tanzania Act, Cap.49, and the Statistics Act, Cap. 351.

This Bill is divided into Seven Parts. Part I deals with preliminary provisions which includes the title of the Bill and the manner in which the laws proposed to be amended are amended in their respective Parts.

Part II proposes amendment to the Appellate Jurisdiction Act, Cap.141. Appeals to the Court of Appeal from decisions of the High Court or Tribunals whose appeals lie to the Court of Appeal are guided by procedural laws contained in the Appellate Jurisdiction Act, written laws creating right of appeal to the Court of Appeal and also, the Court of Appeal Rules, 2009 and other specific Rules and Regulations. Procedural laws are expected to expedite the process of adjudicating disputes, by removing obstacles and must cut down delays in the Court of Appeal.

Despite the provisions of Article 107A (2)(e) of the Constitution directing the courts in Tanzania to dispense justice. So many appeals, revisions, reviews and other applications have been struck out on grounds of procedural irregularities making the jurisprudence of the Court of Appeal overly reliant on procedural technicalities instead of substantive justice expected by the Constitution. Apart from delaying or even eliminating the possibility of attaining substantive justice, the striking out of matters on procedural technicalities, increase the costs of litigation, the parties are invariably forced to initiate the matter afresh, by going back to the High Court to seek an extension of time before much later for the matter to be filed and determined on merit by the Court of Appeal.

Sections 3A and 3B of the proposed amendments which introduce the principle of objectives of attaining substantive justice are intended to give statutory effect to Article 107A (2) (e) of the Constitution which requires the courts, when applying rules of procedure that are couched in mandatory terms to actively take into account the wider interests of substantive justice to facilitate the just, expeditious, proportionate and affordable resolution of the civil disputes. The proposed amendments are not designed to blindly disregard the rules of procedure that are couched in mandatory terms, but are meant to task the Court of Appeal before striking out a matter on ground of procedural irregularity, to weigh the wider interests of substantive justice and decide whether there is an alternative available instead of striking out the matter before the Court of Appeal.

The proposed amendments will deal away with unnecessary objections and insist on the disposal of cases on merit.

Part III proposed amendment to the Civil Procedure Code, Cap.33. In order to expedite disposition of cases the proposed amendments are intended to reduce procedural hurdles for the purposes of expediting both trials and appeals. Powers which will deal with unnecessary objections and insist on the disposal of cases on merit. The proposed addition of new sections

3A and 3B which introduce the principle of objectives of attaining substantive justice are intended to give statutory effect to Article 107A (2) (e) of the Constitution. The said Article requires the courts to determine cases without undue regard to technicalities.

Part IV proposed amendment to the Land Disputes Courts Act, Cap.216. At the moment, there are substantial number of appeals on land disputes pending at the High Court from decisions of the Ward Tribunals and District Land and Housing Tribunals. The backlog of cases in the High Court pending for determination is far beyond the current number of Judges of the High Court. The proposed addition of section 41A are intended to give powers to resident magistrate with extended jurisdiction, to hear and determine appeals originating from the Ward Tribunals and the District Land and Housing Tribunal. By off-loading of some of the pending appeals for determination by resident magistrates with extended jurisdiction, the intended amendments will assist the High Court to timely dispose of land disputes.

Part V proposes amendment of the Magistrate's Courts Act Cap.11 whereby section 2 is amended by adding new definitions appropriate to give meaning to the provisions of the Act. New section 17A is introduced with a view to empower the Chief Justice to establish, by Order published in the *Gazette*, mobile courts and special courts. A new section 17B is introduced to further empower the Chief Justice to make rules of practice and procedure for the mobile courts and special courts. Section 17C is introduced to limit appeals against decisions of a mobile court and special court, in which case, no appeal shall be tenable except on a point of law before the High Court. Section 42A is introduced to make provisions for the restriction of representation by Advocates, the rights of representation by a next of keen and the representation by body corporate. The objectives of the new provisions are to provide for an informal, inexpensive and expeditious form of determination of cases.

This Part further proposes amendment to section 45 to empower a resident magistrate who has been vested by the Minister responsible for Justice with extended jurisdiction, to hear and determine appeals which are ordinarily supposed to be heard and determined by the High Court. The High Court may transfer any such appeal to a resident magistrate for purpose of hearing and determination on extended jurisdiction. This provision is ordinarily resorted for purposes of helping the High Court to clear its backlog of cases.

Part VI proposes amendment to the National Sports Council of Tanzania Act, Cap. 49 whereby sections 2 is amended in the definition of the term "sports association" by deleting the word "amateur" and adding the definite of the term "sports". Section 4 which relates to functions of the Council is amended by removing the use of the term "amateur". Currently those sections empower Council to regulate amateur sports thereby living no organ to regulate professional sports. The amendments are aimed at broadening regulatory mandate of the Council

in all forms sports including professional. Section 3 is amended by introducing provisions which allow the Attorney General to intervene in suits or matters instituted by or against the Council. The amendments are aimed at engaging the Attorney General, who is the head legal adviser of Government, to partake in any dispute against any entity of Government.

Furthermore, amendments are done in sections 6(b) and 21 (1) with a view of rectifying errors. Section 8 is amended so as to name the Controller and Auditor General as the auditor of the Council's accounts instead of auditors from the Tanzania Audit Corporation. Section 10 which relates to Registrar of Sport Association is amended for clarity and appropriateness of provision.

Part VII proposes amendment of the Statistics Act, Cap.351 whereby the Act is amended generally by substituting the title Director General with the title Chief Government Statistician. The objective of the amendment is to provide for an appropriate title that depicts both the head of the National Bureau Statistics and the chief Government advisor in matters relating statistics. Section 3 is amended by making appropriate definition of the terms used in the Act. The Act is further generally amended in sections 6(2)(c), 19, 22(2), 28, and 37(2) by substituting the phrase "statistical information" with the phrase "official statistics". The amendments are intended to make consistent and appropriate usage of the term "official statistics" in the amended sections.

Other amendments include the repeal and replacement of sections 18 and 19 for clarity and appropriateness of provisions relating powers and functions of the Chief Government Statistician. Lastly the Act is amended by adding a new section 24A which relates to dissemination of official statistics. Currently the Act does not make provide for requirement to seek for the approval of the Bureau before disseminating official statistics. These amendments are aimed at restricting the dissemination of statistical information that will invalidate or discredit official statistics. Therefore any person who processes statistical information shall obtain approval of the Bureau before dissemination of information to the public.

## MADHUMUNI NA SABABU

Muswada huu unapendekeza kufanya Marekebisho katika Sheria Sita ambazo ni Sheria ya Mamlaka ya Rufaa Sura ya 141, Sheria ya Mwenendo wa Mshauri ya Madai, Sura ya 33, Sheria ya Mahakama ya Migogoro ya Ardhi, Sura ya 216; Sheria ya Mahakama za Mahakimu, Sura ya 11; Sheria ya Baraza la Michezo la Taifa Sura ya 49 na Sheria ya Takwimu, Sura ya 351.

Muswada huu umegawanyika katika Sehemu Saba. Sehemu ya Kwanza inahusu masharti ya utangulizi ambayo yanajumuisha Jina la Muswada na namna ambavyo Sheria zinazopendekezwa kurekebishwa zitakavyorekebishwa ndani ya Muswada huu.

Madhumuni ya Marekebisho ya Sheria hizi ni kuondoa upungufu ambao umebainika katika utekelezaji wa baadhi ya masharti yaliyomo katika Sheria hizo na pia kuongeza ufanisi kwa taasisi zinazosimamia utekelezaji wa Sheria hizo. Marekebisho yanayopendekezwa yanalenga kuziwezesha Sheria husika kuendana na mabadiliko mbalimbali ya Kiteknolojia, Kisiasa na Kiuchumi ambayo yamejitokeza katika miaka ya hivi karibuni na yanaleta athari katika utekelezaji wake.

Sehemu ya Pili inapendekeza kuifanyia Marekebisho Sheria Mamlaka ya Rufaa, Sura ya 141, kwa kuongeza vifungu vipya vya 3A na 3B kwa lengo la kuweka kwenye sheria msingi unaoitaka Mahakama inapotoa uamuzi katika mashaururi ya madai na jinai itende haki bila kufungwa kupita kiasi na mashauri ya kiufundi yanayoweza kukwamisha haki kutendeka. Msingi huu umeainishwa kwenye Ibara 107(2)(e) ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano. Madhumuni ya mapendekezo haya ni kuitaka Mahakama ya Rufaa itumie njia mbadala ili haki itendeke kabla ya kukataa shauri kwa kuzingatia masharti ya kiufundi.

Mapendekezo haya ya marekebisho yatasaidia kesi za msingi kumalizika pasipokutumia muda mrefu kusikiliza mapigamizi ya awali yasiyo na msingi.

Sehemu ya Tatu inapendekeza kuifanyia Marekebisho Sheria ya Mwenendo wa Makosa ya Madai, Sura ya 33 kwa kuongeza vifungu vipya vya 3A na 3B. Kama ilivyo kwenye mapendekezo ya Sheria ya Mamlaka ya Rufaa Mapendekezo haya ya marekebisho yanalenga kuziwezesha Mahakama kuu, Makahama za Hakimu Mkazi na Mahakama za Wilaya kutenda haki bila kufungwa kupitia kiasi na masharti ya kiufundi yanayoweza kuchelewesha au kukwamisha haki kutendeka.

Sehemu ya Nne inapendekeza kuifanyia marekebisho Sheria ya Mahakama ya Migogoro ya Ardhi, Sura ya 216. Mapendekezo haya ya marekebisho yanalenga kuongeza kifungu kipya cha 41A kinachompa mamlaka Hakimu Mkazi mwenye mamlaka ya zaida kusikiliza na kuamua rufaa kutoka mabaraza ya kata na mabaraza ya ardhi na nyumba ya wilaya. Marekebisho haya

yanalenga kupunguza mlundikano wa rufaa za mashauri ya ardhi katika Mahakama kuu. Aidha, mapendekezo haya ya marekebisho yataiwezesha Mahakama Kuu kumaliza mashauri ya ardhi mapema kutokana na kupungua kwa mlundikano wa mashauri.

Sehemu ya Tano inapendekeza marekebisho katika Sheria ya Mahakama ya Mahakimu, Sura ya 11 ambapo kifungu cha 2 kinarekebishwa kwa kuongeza tafsiri ya maneno ili kuleta maana iliyokusudiwa katika Sheria. Kifungu kipya cha 17A kimeongezwa ili kumpa Jaji Mkuu mamlaka ya kuanzisha Mahakama za kuhamishika na Mahakama Maalum. Kifugu kipya cha 17B kinaongezwa ili kumuwezesha Jaji Mkuu kutunga kanuni na taratibu za uendeshaji wa Mahakama za kuhamishika na Mahakama Maalum. Kifungu kipya cha 17C kinaongezwa ili kuzuia rufaa dhidi ya maamuzi ya Mahakama hizi isipokuwa kwa hoja za kisheria ambazo rufaa hizo zitapelekwa Mahakama Kuu. Kifungu kipya cha 42A kinaongezwa ili kuweka masharti ya uwakilishi wa ndugu au jamaa wa karibu na uwakilishi wa makampuni. Aidha uwakilishi kupitia wakili umezuiliwa. Madhumuni ya marekebisho haya ni kupunguza gharama, kuharakisha utatuzi wa migogoro na kuweka mfumo rahisi wa uendeshaji wa mashauri yenye thamani ndogo. Sehemu hii pia inapendekeza kufanya marekebisho kwenye kifungu cha 45. Mapendekezo haya ya marekebisho yanalenga kumfanya Hakimu mwenye mamlaka ya ziada (*Extended Jurisdiction*) mamlaka ya kusikiliza rufaa ambazo kwa kawaida husikilizwa na Mahakama Kuu awe na mamlaka ya kusikiliza na kuamua rufaa zinazoanzia Mahakama ya Mwanzo. Kwa utaratibu wa sasa, hakimu mwenye mamlaka ya ziada anaweza kusikiliza na kuamua mashauri yaliyoanzia Mahakama ya Wilaya au Mahakama ya Hakimu Mkazi.

Sehemu ya Sita inapendekeza marekebisho katika Sheria ya Baraza la Michezo la Taifa, Sura ya 49, ambapo vifungu vya 2 na 4 vinarekebishwa ili kuliwezesha Baraza kusimamia michezo ya kulipwa. Sheria ilivyo sasa inalipa mamlaka Baraza la Michezo la Taifa kusimamia michezo ya ridhaa pekee, hivyo kupelekea kukosekana kwa chombo mahsusi cha kusimamia michezo ya kulipwa. Marekebisho haya yanalenga kuliongezea Baraza wigo wa usimamizi katika michezo na kuliwezesha kusimamia michezo yote nchini, ikiwemo michezo ya kulipwa. Kifungu cha 3 kinarekebishwa ili kumuwezesha Mwanasheria Mkuu wa Serikali kuingilia shauri lolote lilofunguliwa na au dhidi ya Baraza. Marekebisho haya yanalenga kumshirikisha Mwanasheria Mkuu wa Serikali, ambae ni mshauri wa Serikali katika masuala ya Sheria, katika kuingilia shauri lolote linalohusu chombo chochote cha Serikali.

Aidha, marekebisho mengine yanafanywa katika vifungu vya 6 (b) na 12(1) kwa lengo la kurekebisha makosa ya kiuandishi. Vile vile, kifungu cha 8 kinarekebishwa kwa kumtaja Msimamizi na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali kuwa mkaguzi wa hesabu za Baraza badala ya wakaguzi wa shirika la Tanzania Audit Corporation ambalo halipo kwa sasa. Kifungu cha 10 kinarekebishwa ili kuweka maneno sahihi yanayomuwezesha Waziri kuwateua Wasajili Wasaidizi wa Vyama vya Michezo kwa idadi iliyo kadri ya mahitaji.

Sehemu ya Saba inapendekeza marekebisho katika Sheria ya Takwimu, Sura ya 351 ambapo Sheria inapendekeza marekebisho ya jumla kwa kufuta cheo cha Mkurugenzi Mkuu na badala yake kuweka cheo cha Mtakwimu Mkuu. Lengo la marekebisho haya ni kuongeza matumizi ya cheo sahihi kitakachoonesha kuwa kiongozi huyu ni mkuu wa ofisi ya Taifa ya Takwimu na mshauri mkuu wa Serikali katika masuala ya Takwimu. Sheria inapendekeza marekebisho katika vifungu vya 6(2)(c) na (f), 19, 22(2), 28 na 37(2) kwa kuondoa matumizi ya maneno "statistical information" na badala yake kuweka maneno "official statistics". Marekebisho haya yamelenga kuweka matumizi sahihi ya maneno "official statistics" katika vifungu vilivyoainishwa. Kifungu cha 3 kinarekebishwa kwa kuongeza tafsiri ya misamiati inayotumika katika masharti mbali mbali ya Sheria hii.

Aidha, marekebisho mengine ni pamoja na kufuta vifungu vya 18 na 19 na kuviandika upya kwa lengo la kuongeza ufasaha zaidi katika majukumu ya Mtakwimu Mkuu kama yalivyoainishwa katika vifungu hivyo. Mwisho, Sheria pia inarekebishwa kwa kuongeza kifungu kipya cha 24A kinachohusu usambazaji wa taarifa rasmi za takwimu. Sheria ilivyo sasa haina masharti yanayomtaka mtu kupata idhini ya Ofisi ya Taifa ya Takwimu kabla ya kusambaza taarifa rasmi za takwimu. Marekebisho haya yamelenga kumzuia mtu yeyote kusambaza kwa umma taarifa za takwimu kwa lengo la kupotosha au kuonesha kuwa taarifa rasmi za takwimu zilizotolewa na Ofisi ya Taifa ya Takwimu sio sahihi. Hivyo kwa mujibu wa marekebisho haya, mtu yeyote aliyechakata taarifa za takwimu atalazimika kuomba idhini ya Ofisi ya Taifa ya Takwimu kabla ya kusambaza kwa umma takwimu hizo.

| | |
|---|---|
| Dodoma, | **ADELARDUS L. KILANGI** |
| 23 Mei, 2018 | *Mwanasheria Mkuu wa Serikali* |

**SCHEDULE OF AMENDMENT TO BE MOVED BY THE HON. ADELARDUS L. KILANGI THE ATTORNEY GENERAL AT THE SECOND READING OF THE BILL ENTITLED "THE WRITTEN LAWS (MISCELLANEOUS AMENDMENTS)(NO.3) ACT, 2018"**

*Made under S.O. 86(10)(b)*

The Bill entitled "The Written Laws (Miscellaneous Amendments)(No.3) Act, 2018" is amended as follows:

**A:** In Clause 4, in the proposed section 3B by adding immediately after subsection (2) the following:

"(3) The Chief Justice may make rules for better carrying out the provisions of sections 3A and 3B."

**B:** In Clause 6, in the proposed section 3B by adding immediately after subsection (2) the following:

"(3) The Chief Justice may make rules for better carrying out the provisions of sections 3A and 3B."

**C:** By repealing Clauses 11, 12 and 13.

**D:** In Clause 17(a)-

(a) in the proposed subsection (2) by inserting immediately after the word "right" appearing in the second line the words' "through the Solicitor General".

(a) in the proposed subsection (3) by inserting immediately after the word "any" the words "suit or".

(b) in the proposed subsection (3) by adding a proviso as follows:

"Provided that, the requirement of ninety days notice of intention to sue the Government as stipulated under the Government Proceedings Act shall not apply where the Attorney General intervenes under this section."

**E:** In Clause 24(a) by deleting the proposed title "Chief Government Statistician" and substituting for it the title "Statistician General":

**F:** In Clause 25(a) in the proposed definition of the term "Official Statistic" by deleting the word "or" appearing between the word "compiled" and "dissemination" and substituting for it the word "and".

**G:** In Clause 31, by -

(a) deleting the proposed subsection 24A(2) and substituting for it the following:

"(2) A person who has different findings from statistics disseminated by the Bureau shall, prior to communicating such findings to the public, consult the Bureau."

(b) by adding immediately after the proposed section 24A the following:

"Prohibition on dissemination of statistical information

**24B**.-(1) A person shall not disseminate or otherwise communicate to the public any statistical information which is intended to invalidate, distort or discredit official statistics.

(2) A person shall not disseminate or communicate to the public any statistical information without the approval of the Statistician General."

**H:** By renumbering Clauses 14 to 32 as Clauses 11 to 29 respectively.

Dodoma,
…………………, 2018

**A.L.K**
*AG*

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, sasa nimwite Mwenyekiti wa Kamati ya Katiba na Sheria. Anakuja Mwenyekiti mwenyewe, ili aweze kupitia Maoni ya Kamati ya Katiba na Sheria kuhusu Muswada wa Sheria ambao umetolewa hoja na Mwanasheria Mkuu wa Serikali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, karibu sana.

**MHE. MOHAMED O. MCHENGERWA – MWENYEKITI WA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA KATIBA NA SHERIA:** Mheshimiwa Spika, awali ya yote nichukue fursa hii kumshukuru sana Mwenyezi Mungu mwingi wa rehema, aliyeniwezesha kusimama mbele ya Bunge hili Tukufu nikiwa na afya njema.

Mheshimiwa Spika, lakini Muswada wa Sheria ya Marekebisho ya Sheria Mbalimbali (Na.3) wa Mwaka 2018 uliotangazwa katika Gazeti la Serikali, Namba 23, Juzuu ya 99 la tarehe 8 Juni, 2018 ulisomwa Bungeni mara ya kwanza tarehe 26 Juni, 2018. Baada ya hapo Masharti ya Kanuni ya 84(1) kwa pamoja na Kifungu cha 7(1)(b) cha Nyongeza ya Nane ya Kanuni ya Kudumu za Bunge, Toleo la Januari 2016, yalizingatiwa na Muswada huo ukauleta kwenye Kamati ya Kudumu ya Katiba na Sheria. Kamati iliujadili Muswada huo kwa kuzingatia matakwa ya Kanuni za Kudumu za Bunge.

Mheshimiwa Spika, kwa mujibu wa Kanuni ya 86(1) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Januari, 2016, naomba kuwasilisha Maoni na Ushauri wa Kamati ya Bunge ya Katiba na Sheria kuhusu Muswada wa Sheria ya Marekebisho ya Sheria Mbalimbali (Na.3) wa Mwaka 2018 *(The Written Laws (Miscellaneous Amendments) (No.3) Bill, 2018.* Katika Muswada huu wa Serikali inapendekeza kufanya marekebisho katika Sheria sita. Sheria hizo ni pamoja na:-

(a) Sheria ya Mamlaka ya Rufaa, Sura ya 141.

(b) Sheria ya Mwenendo wa Mashauri ya Madai, Sura ya 33.

(c) Sheria ya Mahakama ya Migogoro ya Ardhi, Sura ya 216.

(d) Sheria ya Mahakama za Mahakimu, Sura ya 11.

(e) Sheria ya Baraza la Michezo la Taifa, Sura ya 49.

(f) Sheria ya Takwimu, Sura ya 351.

Mheshimiwa Spika, mbili, ni Utekelezaji wa Majukumu ya Kamati. Katika kutekeleza masharti ya Kanuni ya 84(1) ya Kanuni ya Kudumu ya Bunge, Kamati ilikutana kwa muda wa wiki mbili katika Ukumbi Na.9 uliopo Jengo la Utawala la Ofisi ya Bunge Dodoma na kufanya yafuatayo:-

(a) Tarehe 20 Agosti, 2018, Kamati iliweka utaratibu wa uchambuzi wa kibunge wa Muswada wa Sheria kwa kuzingatia ruhusa inayotolewa na Kanuni ya 117(8) na kujipanga ipasavyo ili kuwezesha utekelezaji bora wa shughuli za Kamati.

(b) Tarehe 21 Agosti, 2018, Kamati ilidurusu Ibara za Muswada wa Sheria ya Marekebisho ya Sheria Mbalimbali Na. 3, wa mwaka 2018 na kuzingatia Masharti ya Kanuni ya 21(1)(b) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Januari, 2018 inayohusu majukumu ya Mshauri Mkuu wa Bunge wa Mambo ya Sheria katika uchambuzi wa Miswada ya Sheria.

(c) Tarehe 23 Agosti, 2018 Kamati ilipokea maelezo ya Serikali kuhusu madhumuni na sababu za Muswada ambayo yaliwasilishwa na Waziri wa Katiba na Sheria, Mheshimiwa Profesa Palamagamba John Aidan Kabudi.

(d) Tarehe 24 Agosti, 2018 Kamati ilipokea maoni ya Wadau mbalimbali kwa lengo la kuisaidia Kamati katika uchambuzi wa Muswada. Maoni hayo ya Wadau yalitokana na barua za mialiko ambazo zilitolewa na Ofisi ya Bunge

pamoja na matangazo kwa umma ambayo yalitolewa kwa mujibu wa Kanuni ya 84(2) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Januari, 2016. Jumla ya Wadau 12 kutoka kwenye Taasisi mbalimbali waliwasilisha maoni yao kwa kufika mbele ya Kamati au kwa njia ya maandishi kupitia Ofisi ya Katibu wa Bunge. Orodha ya Taasisi hizo ni pamoja na:-

(i) Chama cha Wanasheria Tanganyika (*Tanganyika Law Society – TLS*).

(ii) Kituo cha Sheria na Haki za Binadamu (*Legal and Human Rights Centre – LHRC*).

(iii) TWAWEZA.

(iv) SIKIKA.

(v) Hakielimu.

(vi) *Stallion Attorneys.*

Mheshimiwa Spika, napenda nichukue fursa hii kuwashukuru wadau wote ambao kwa nyakati tofauti waliwasilisha maoni yao mbele ya Kamati na waliowasilisha kwa maandishi. Kwa hakika maoni yaliyowasilishwa yaliisaidia Kamati katika kutekeleza jukumu lake la kuuchambua Muswada huu.

Mheshimiwa Spika, tarehe 25 Agosti, 2018 Kamati ilitathmini hatua iliyofikiwa katika utekelezaji wa majukumu yake. Lengo lilikuwa ni kujiridhisha iwapo uelewa unapatikana kuhusu maudhui na masharti ya Muswada huu miongoni mwa wajumbe wanawezesha Kamati kulishauri Bunge ipasavyo. Katika hatua hiyo, Kamati ilihakiki taarifa ilizokusanya kuhusu Muswada huu na kufanya upembuzi wa taarifa hizo kwa kulinganisha na matarajio katika uchambuzi wa Muswada huu.

Mheshimiwa Spika, tarehe 27 na 28 Agosti, 2018 Kamati ilifanya uchambuzi wa kina wa Muswada kwa

kuzingatia maelezo ya Serikali, maoni ya wadau pamoja na rejea mbalimbali kuhusiana na Muswada huu. Hatua hii iliiwezesha Kamati kuandaa Jedwali la mapendekezo ya Marekebisho ambalo liliwasilishwa rasmi Serikalini ili kutekeleza Masharti ya Kanuni ya 84(3) ya Kanuni za Kudumu za Bunge.

Mheshimiwa Spika, tarehe 29 na 30 Agosti, 2018 Kamati ilifanya mashauriano na Serikali kuhusu marekebisho yaliyopendekezwa na Kamati na kuyawasilisha Serikalini. Mashauriano hayo yalifanyika kwa mafanikio makubwa sana ambapo Serikali ilipokea ushauri wa Kamati na kuufanyia kazi kwa kukubali kuandaa Jedwali la Marekebisho ya Muswada. Jedwali hilo lina marekebisho mbalimbali kuhusu:-

(i) Maudhui katika baadhi ya Ibara za Muswada.

(ii) Dosari za kiuandishi zilizobainika katika baadhi ya Ibara za Miswada.

(iii) Kufutwa au kuandikwa upya au kurekebishwa kwa baadhi ya Ibara za Miswada.

(iv) Kuongeza maneno yaliyosahaulika katika baadhi ya Ibara ili kuleta mantiki iliyokusudiwa katika Ibara husika.

Mheshimiwa Spika, aidha, maelezo ya ziada ya maboresho yalihitajika kuhusu mantiki ya jumla ya dhana ya *Official Statistics* na *Statistical Information* katika Sheria ya Takwimu *(The Statistics Act)* inayofanyiwa marekebisho katika Muswada huu.

Mheshimiwa Spika, kutokana na hoja hizo zilizohitaji mashauriano ya ziada ya Serikali, Kamati ilikuomba muda wa ziada na ukatoa kibali cha kushughulikia Muswada huu kuanzia tarehe 3 hadi 6 Agosti, 2018. Matokeo ya mashauriano hayo, Serikali iliafiki mapendekezo ya Kamati na kukubali kuandaa na kuboresha mambo ya msingi kabisa katika Muswada huu kama inavyoonekana katika Jedwali la Marekebisho (*Schedule of Amendments*).

Mheshimiwa Spika, Uchambuzi wa Maoni ya Kamati, niruhusu niendelee kwa kuelezea uchambuzi na maoni ya Kamati mbele ya Bunge lako hili Tukufu. Naomba kutanguliza maelezo kuwa Muswada huu ulichambuliwa ukiwa na jumla ya Ibara 32 zilizo kwenye sehemu saba ambazo zinapendekeza kufanya marekebisho katika sheria sita kama zilivyoorodheshwa awali.

Mheshimiwa Spika, ili kuliwezesha Bunge lako Tukufu kujadili na kuamua ipasavyo, Kamati ilichambua kwa kina maudhui ya kila ibara kama yanavyoainishwa katika sehemu hii. Katika hatua hiyo, Kamati ilibaini maeneo mbalimbali yaliyo hitaji maboresho na hivyo kushauriana na Serikali.

Mheshimiwa Spika, Uchambuzi na Maoni ya Jumla, Sehemu ya Kwanza. Sehemu hii inayohusu Masharti ya Utangulizi ina jumla ya ibara mbili zinazohusu jina la Muswada na namna ambavyo sheria zinazopendekezwa kurekebishwa zitakavyorekebishwa ndani ya Muswada huu. Kamati ilipitia ibara zote na kukubaliana na Serikali na hivyo kulishauri Bunge liafiki Mapendekezo hayo.

Mheshimiwa Spika, Sehemu ya Pili; sehemu hii yenye jumla ya ibara mbili inahusu mapendekezo ya Serikali kufanya marekebisho kwenye Sheria ya Mamlaka ya Rufaa, Sura ya 141, hizo ni Ibara ya tatu (3) na ya nne (4) zinaongeza Vifungu vipya vya 3A na 3B kwenye Sheria ya Mamlaka ya Rufaa kwa lengo la kuweka msingi unaoitaka Mahakama ya Rufaa inapotoa uamuzi katika mashauri ya madai na jinai itende haki bila kufungwa na masharti ya kiufundi (*technicalities*) yanayoweza kukwamisha haki kutendeka.

Mheshimiwa Spika, Kamati inaridhia mapendekezo ya Serikali kwa kuwa madhumuni yake ni kuitaka Mahakama ya Rufaa ipime uzito wa hoja kwa kila shauri ili haki itendeke kabla ya kukataa shauri kwa msingi wa masharti ya kiufundi *(technicalities).* Hatua hiyo ikitekelezwa kwa umakini na uangalifu itarahisisha utoaji haki katika Mahakama ya Rufaa

nchini na hivyo kuendana na msingi uliowekwa kwenye Ibara ya 107(2)(e) ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya mwaka 1977.

Mheshimiwa Spika, sehemu ya tatu; sehemu hii yenye jumla ya Ibara mbili, Ibara ya tano (5) na sita (6), inapendekeza kufanya marekebisho kwenye Sheria ya Mwenendo wa Makosa ya Madai, Sura ya 33. Ibara hizo zinaongeza vifungu vipya vya 3A na 3B kwenye Sheria ya Mwenendo wa Makosa ya Madai kwa lengo la kuziwezesha Mahakama Kuu, Mahakama za Hakimu Mkazi na Mahakama za Wilaya kutenda haki bila kufungwa na masharti ya kiufundi (*technicalities*) kupita kiasi au kukwamisha haki kutendeka.

Mheshimiwa Spika, Kamati inaafiki mapendekezo haya na kuipongeza Serikali kuona umuhimu wa kupunguza masharti ya kiufundi kupita kiasi ambayo yamekuwa yakichelewesha utoaji haki.

Mheshimiwa Spika, Sehemu ya Nne yenye jumla ya Ibara tatu, Ibara ya saba (7), nane (8) na tisa (9) inapendekeza kufanya marekebisho katika Sheria ya Mahakama ya Migogoro ya Ardhi. Marekebisho haya yanahusu kuongeza Mamlaka ya ziada *(extended jurisdiction)* kwa Hakimu Mkazi ili aweze kusikiliza na kuamua rufaa kutoka Mabaraza ya Ardhi ya Kata na Mabaraza ya Ardhi na Nyumba ya Wilaya. Marekebisho hayo ni kwa kuongeza kifungu kipya cha 41(a) kwenye Sheria ya Mahakama ya Migogoro ya Ardhi.

Mheshimiwa Spika, ni maoni ya Kamati kuwa mapendekezo hayo yanatatua changamoto ya muda mrefu kuhusu mlundikano wa mashauri ya ardhi katika Mahakama Kuu yanayotoka katika Mabaraza ya Kata na Wilaya. Hali hiyo, imekuwa ikiwakatisha tamaa wananchi kuhusu upatikanaji wa haki Ardhi jambo lililoisukuma Kamati na Wabunge wengi kulalamikia jambo hilo kwa muda mrefu sasa. Kwa bahati nzuri, Serikali inakusudia kutatua kero hii kwa mapendekezo hayo. Kamati inaridhia mapendekezo haya na kulishauri Bunge kuafiki ibara hizo.

Mheshimiwa Spika, Sehemu ya Tano; sehemu hii yenye jumla ya ibara tano inapendekeza marekebisho katika Sheria ya Mahakama za Mahakimu, Sura ya 11. Marekebisho hayo yanahusu kuanzishwa kwa Mahakama zinazohamishika (*Mobile Courts*) na Mahakama Maalum (*Special Courts*) pamoja na Mahakama za Madai madogo (*Small Claims Courts*). Maelezo ya Serikali yalionesha kuwa madhumuni ya marekebisho hayo ni kupunguza gharama, kuharakisha utatuzi wa migogoro na kuweka mfumo rahisi wa uendeshaji wa mashauri yenye thamani ndogo.

Mheshimiwa Spika, katika sehemu hii, awali Serikali na Kamati zilitofautiana kiuelewa na kufanya majadiliano na mashauriano ya kina kuhusu masuala matano ya msingi yaliyokuwa yakipendekezwa kubainika kuwa na dosari mbalimbali. Masuala hayo yaliyobainishwa na Kamati kwa ufupi ni:-

Mheshimiwa Spika*,* kwanza, Ibara husika kutoainisha bayana Muundo na Mfumo wa usimamizi wa utekelezaji wa majukumu ya Mahakama zinazo hamishika *(Mobile Courts) na* Mahakama Maalum *(Special Courts)*

Mheshimiwa Spika, pili, ibara husika kutotoa haki ya uwakilishi iliyowekwa kwa mujibu wa Katiba ya nchi na sheria nyingine za nchi.

Mheshimiwa Spika, tatu, ibara husika kutotoa haki ya Rufaa iliyotajwa katika katiba ya nchi katika ibara ya 13 kuwa rufaa ni haki ya kikatiba; na kwa kuwa dhamira ya *Mobile Court* kama ilivyokuwa imeainishwa na Muswada pamoja na maelezo ya mtoa hoja kuwa ni usikilizwaji wa haraka wa maamuzi, kamati iliamini kwamba kukosekana kwa haki ya kukata rufaa kungepelekea wananchi wengi kukosa haki zao za msingi.

Mheshimiwa Spika, nne, mkanganyiko wa dhana mpya ya madai madogo *(Small Claims)* kwa kulinganisha na kiwango cha ukomo wa juu wa madai hayo kilichopendekezwa cha shilingi milioni mia moja na;

Mheshimiwa Spika, tano, kukosekana kwa maelezo ya ziada kuhusu uhalisia wa gharama za manunuzi na uendeshwaji wa gari moja la Mahakama inayohamishika *(Mobile Court Van)* ikilinganishwa na gharama za ujenzi wa Mahakama endelevu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, hata hivyo, kutokana na mashauriano hayo, Serikali iliamua kuondoa Sehemu yote ya tano ya Muswada huu kama inavyoonekana katika jedwali la marekebisho lililoorodheshwa na mtoa hoja. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Sehemu ya Sita; sehemu hii yenye jumla ya ibara nane inapendekeza kufanya marekebisho katika Sheria ya Baraza la Michezo la Taifa, Sura ya 49. ili kuliwezesha Baraza la michezo kusimamia michezo ya kulipwa. Kwa sasa Sheria ya Baraza la Michezo inalipa Mamlaka Baraza hilo kusimamia michezo ya ridhaa pekee jambo linalosababisha kukosekana kwa chombo mahsusi cha kusimamia michezo ya kulipwa. Dosari hii inakusudiwa kurekebishwa kwa mapendekezo haya.

Mheshimiwa Spika, vilevile vifungu vya 6(b) na 12(1) vya Sheria ya Baraza la Michezo la Taifa vinapendekezwa kurekebishwa. Kamati inaridhia mapendekezo hayo na kuipongeza sana Serikali kwa kuongeza mamlaka ya kisheria kwa Baraza la Michezo. Uamuzi huu utaliwezesha baraza kusimamia michezo ya hiari na ya kulipwa hatua hiyo itaongeza udhibiti wa michezo hiyo na mapato ya Serikali yaliyokuwa yakipotea kutokana na udhaifu wa kisheria.

Mheshimiwa Spika, aidha, Kamati imebaini kuwa, marekebisho hayo yanalenga kumwezesha Mwanasheria Mkuu wa Serikali kuingilia shauri lolote linalofunguliwa na baraza au dhidi ya baraza kwa ajili ya kumshirikisha kwa kuwa ndiye Mshauri wa Serikali katika masuala ya sheria.

Mheshimiwa Spika, Kamati inaridhia mapendekezo ya Serikali kwani uwepo wa Mwanasheria Mkuu wa Serikali utahakikisha kulinda na kutetea haki za Serikali kwa kuwa Baraza la Michezo ni Taasisi ya Serikali kama taasisi nyingine

na hivyo Mwanasheria Mkuu wa Serikali ana wajibika kulisimamia katika Mabaraza na Mahakama yoyote kwa niaba ya Serikali.

Mheshimiwa Spika, kamati inatambua kuwa, kuna umuhimu wa kuwepo kwa ukaguzi na udhibiti wa Mapato yatokanayo na shughuli za Baraza la Michezo nchini kwa lengo la kuimarisha nidhamu ya matumizi na kudhibiti upotevu wa fedha za Serikali. Hivyo, mapendekezo haya ni muhimu ili Msimamizi na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali awe na mamlaka kisheria ya kutekeleza majukumu yake kwa manufaa ya Taifa.

Mheshimiwa Spika, aidha, kamati inaridhia marekebisho yenye kumwezesha Waziri kuwateua Wasajili Wasaidizi wa Vyama vya Michezo kwa idadi iliyo kadri ya mahitaji, kwa lengo la kuongeza ufanisi katika utekelezaji wa majukumu ya Baraza la Michezo la Taifa.

Mheshimiwa Spika, hata hivyo, Kamati ina maoni kuwa kwa siku zijazo kuna umuhimu wa kufanya marekebisho katika sheria hii ili kuunda chombo cha kitaifa cha utatuzi wa migogoro ya michezo nchini.

Mheshimiwa Spika, Sehemu ya Saba, sehemu hii yenye jumla ya Ibara kumi (Ibara ya 23 mpaka ibara ya 32) inapendekeza kufanya marekebisho katika Sheria ya Takwimu, Sura ya 351. Marekebisho hayo ni kufuta cheo cha Mkurugenzi Mkuu popote pale kinaposomeka kwenye Sheria ya Takwimu na badala yake kuingiza neno Mtakwimu Mkuu. Lengo ni kutumia cheo sahihi kinachoonesha kuwa kiongozi huyu ni Mkuu wa Ofisi ya Taifa ya Takwimu na Mshauri Mkuu wa Serikali katika masuala ya takwimu. Aidha, inapendekezwa kumpa Mtakwimu Mkuu Mamlaka ya kusimamia na kudhibiti usambazaji wa takwimu nchini.

Mheshimiwa Spika, Kamati imezingatia ongezeko la usambazaji wa takwimu mbalimbali na matumizi yake chini ya usimamizi usioridhisha. Hali hiyo, kwa maoni ya Kamati,

wakati mwingine imesababisha mkanganyiko mkubwa miongoni mwa jamii jambo ambalo linaweza kuathiri ustawi wa Jamii.

Mheshimiwa Spika, hivyo basi, Kamati inalishauri Bunge lako Tukufu kuridhia mapendekezo haya kwa kuwa, yataimarisha usimamizi, udhibiti wa upatikanaji na matumizi ya takwimu nchini kwa mujibu wa sheria. Aidha, hatua hii itaiwezesha Serikali kupata takwimu nyingi zaidi ambazo itazitumia katika kupanga mipango ya maendeleo ya sekta mbalimbali nchini na kustawisha Jamii.

Mheshimiwa Spika, uchambuzi wa maeneo mahsusi na maoni. Zaidi ya uchambuzi wa jumla na maoni niliyoeleza, yapo maeneo matatu mahsusi ambayo kwa maoni ya Kamati ni vema yakabainishwa kwa Bunge lako Tukufu. Maeneo hayo yanahusu utaratibu wa kikanuni wa Mahakama kutenda haki bila kufungwa na masharti ya kiufundi ya sheria, muundo wa Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali na matumizi ya notisi ya siku 90 pamoja na utaratibu wa kisera na kisheria wa utatuzi wa migogoro ya ardhi. Katika maeneo hayo, Kamati ina maoni na mapendekezo mahsusi kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, pendekezo la kwanza, ni utaratibu wa kikanuni wa Mahakama kutenda haki bila kufungwa na masharti ya kiufundi ya sheria. Ibara ya nne (4) na Ibara ya sita (6) ya Muswada zinapendekeza kuwekwa msingi wa kisheria unaoitaka Mahakama kutenda haki bila kufungwa kupita kiasi na masharti ya kiufundi.

Mheshimiwa Spika, Kamati inaunga mkono mapendekezo haya na imeshauriana na kukubaliana na Serikali kuboresha zaidi uandishi wa ibara hizi. Lengo ni kuweka bayana masharti yake na kuwezesha uzingatiaji wa mahitaji ya haki kuonekana na watu wote kwamba inatendeka.

Mheshimiwa Spika, pili, ni maboresho katika muundo wa Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali pamoja na matumizi ya notisi ya siku 90. Ibara ya 17 inapendekeza kumpa

Mwanasheria Mkuu wa Serikali mamlaka ya kuingilia mashauri yoyote yanayohusiana na Baraza la Michezo la Taifa kwa kuwa ni chombo cha Serikali. Katika uchambuzi zilijitokeza hoja mbalimbali kuhusu uandishi wa ibara hiyo. Kwa mfano matumizi ya maneno Mwanasheria Mkuu wa Serikali badala ya Wakili Mkuu wa Serikali yalijadiliwa kwa kina. Serikali ilikubaliana na Kamati kuboresha uandishi wa ibara hii ili kutambua majukumu ya Wakili Mkuu wa Serikali kwa kuzingatia muundo mpya wa Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali.

Mheshimiwa Spika, aidha, Serikali ilikubali ushauri wa Kamati kwamba, masharti ya Sheria ya Mashauri ya Serikali kuhusu utoaji wa notisi ya siku 90 kwa Mwanasheria Mkuu wa Serikali yasihusike inapotokea Mwanasheria Mkuu wa Serikali ameingilia shauri ambalo tayari lipo Mahakamani. Kwa sababu hiyo Serikali imeboresha Ibara ya 17(4) ili isomeke kama ifuatavyo:

*"Provided that, the requirement of ninety days notice of intention to sue the government as stipulated under the Government Proceedings Act shall not apply where the Attorney General intervenes under this section.*

Mheshimiwa Spika, tatu, ni maboresho ya uandishi wa ibara ya 24, 25 na 31. Matumizi ya maneno katika utungaji wa Sheria ni jambo muhimu linaloweza kuepusha mkanganyiko wa masharti ya sheria. Kwa sababu hiyo, Kamati ilijielekeza kwenye usahihi wa matumizi ya maneno na kuepuka utata. Katika kufanya hivyo, ilibainika kuwa neno "*chief*" limetumika katika sehemu inayopaswa kutumia neno "*general*" katika Ibara ya 24(a).

Mheshimiwa Spika, katika Ibara ya 25(a) neno *"or"* lilipendekezwa kutumika katikati ya maneno *"compiled"* na *"dissemination"* ambapo kwa maoni ya Kamati matumizi yake hayaendani na mantiki iliyokusudiwa.

Mheshimiwa Spika, aidha, uandishi wa Ibara ya 31 uliibua hoja kuhusu udhibiti wa usambazaji wa takwimu.

Namna ilivyoandikwa katika Ibara ya 31 kwenye mapendekezo la kifungu cha 24(a)(2) haiendani na kusudio na mantiki ya mapendekezo.

Mheshimiwa Spika, Serikali ilikubaliana na kamati na hivyo kufanya maboresho mbalimbali ya kiuandishi katika Ibara za 24, 25 na 31 kwa lengo la kuondoa utata wa kisheria uliobainika na kuweka msingi mzuri wa utekelezaji na tafsiri ya sheria husika.

Mheshimiwa Spika, utaratibu wa kisera na kisheria wa utatuzi wa migogoro ya ardhi. Sehemu ya Nne ya Muswada inapendekeza marekebisho katika Sheria ya Mahakama ya Migogoro ya Ardhi, Sura ya 216 kwa kuongeza kifungu kinachompa Hakimu Mkazi mamlaka ya ziada ya kusikiliza na kuamua Rufaa kutoka kwenye Mabaraza ya Kata na Mabaraza ya Ardhi na Nyumba ya Wilaya.

Mheshimiwa Spika, Kamati inaunga mkono mapendekezo haya kwa kuwa yanalenga kupunguza mlundikano wa rufaa za mashauri ya ardhi katika Mahakama Kuu.

Mheshimiwa Spika, hata hivyo, pamoja na manufaa ya marekebisho hayo, Kamati ina maoni kuwa marekebisho yanayopendekezwa hayatoshelezi kutatua changamoto nyingi nchini zinazohusiana na utatuzi wa migogoro ya ardhi. Miongoni mwa changamoto hizo ni pamoja na:-

(i) Uwepo wa udhibiti na usimamizi usioridhisha wa kinidhamu na kimaadili katika Mabaraza ya Ardhi;

(ii) Uchache wa Mabaraza ya Adhi nchini, mathalan, mikoa mingi nchini ina Baraza la Nyumba na Ardhi la Wilaya moja tu linalohudumia mkoa mzima badala kila wilaya kuwa na Baraza;

(iii) Vyombo vya utatuzi wa migogoro ya ardhi kusimamiwa na mamlaka tatu (Ofisi ya TAMISEMI, Wizara ya

Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi pamoja na Mahakama); na

(iv) Ukosefu wa ajira za kudumu kwa Wenyeviti wa Mabaraza ya Nyumba na Ardhi ya Wilaya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa msingi huu, Kamati inaishauri Serikali ifanye utaratibu wa kisera na kisheria ili kurudisha mfumo wa utatuzi wa migogoro ya ardhi katika mfumo wa Mahakama kwa kuwa mfumo wa Mahakama nchini umeimarishwa na kuboreshwa zaidi ya mfumo wa Mabaraza ya Ardhi.

Mheshimiwa Spika, hitimisho; kwa mara nyingine tena naomba nikushukuru sana wewe kwa kutoa kibali ili Kamati ya Katiba na Sheria iweze kuufanyia kazi Muswada huu. Aidha, naomba kuwatambua na kuwashukuru Wadau mbalimbali waliofika na kutoa maoni na ushauri wao kwa Kamati.

Mheshimiwa Spika, kwa namna ya pekee kabisa naomba niwashukuru Wajumbe wa Kamati ya Katiba na Sheria kwa weledi na umahiri wao waliouonesha wakati wa uchambuzi wa Muswada huu na hatimaye kutoa maoni na mapendekezo ya msingi ya kuuboresha. Naomba majina yao yote yaingie kwenye Kumbukumbu Rasmi za Bunge *(Hansard).*

Mheshimiwa Spika, nawashukuru Watumishi wote wa Ofisi ya Bunge hususan Katibu wa Bunge Ndugu Stephen Kagaigai kwa Uongozi thabiti ambao umerahisisha utendaji kazi wa Kamati. Aidha, namshukuru Mkurugenzi wa Idara ya Kamati za Bunge Ndugu Athuman Hussein; Mkurugenzi Msaidizi Nduhu Angelina Sanga; Washauri wa Bunge wa Mambo ya Sheria, Ndugu Stephano Seba Mbutu, Ndugu Maria Mdulugu, Ndugu Nesta Kawamala, Ndugu Evelyne R. Shibandiko, Ndugu Thomas Shawa.

Mheshimiwa Spika, pia napenda kuwashukuru Makatibu wa Kamati Ndugu Stanslaus Kagisa, Ndugu

Dunford P. Mpelumbe pamoja na Msaidizi wa Kamati Ndugu Rahel Masima waliofanikisha kazi ya uchambuzi na uratibu wa shughuli za Kamati kwa kuiwezesha Kamati yangu kutekeleza majukumu yake ipasavyo na kuhakikisha taarifa hii inakamilika kwa wakati.

Mheshimiwa Spika, naomba kuwasilisha. (*Makofi*)

**SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Mchengerwa, Mwenyekiti wa Kamati ambayo imechambua Muswada huu, Kamati ya Katiba na Sheria, tunawashukuruni sana kwa maoni yenu muhimu.

**MAONI NA USHAURI WA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA KATIBA NA SHERIA KUHUSU MUSWADA WA SHERIA YA MAREKEBISHO YA SHERIA MBALIMBALI (NA.3) WA MWAKA 2018*(THE WRITTEN LAWS (MISCELLANEOUS AMENDMENTS) (NO.3) BILL, 2018* KAMA YALIVYOWASILISHWA MEZANI**

---

## 1.0 UTANGULIZI

**Mheshimiwa Spika,** Muswada wa Sheria ya Marekebisho ya Sheria Mbalimbali Na. 3 wa Mwaka 2018 [*The Written Laws (Miscellaneous Amendments) (No.3) Bill, 2018]* uliotangazwa katika Gazazeti la Serikali Na. 23 Juzuu ya 99 la tarehe 8 Juni, 2018, ulisomwa Bungeni mara ya kwanza tarehe 26 Juni, 2018. Baada ya hapo, Masharti ya Kanuni ya 84(1) kwa pamoja na Kifungu cha 7(1)(b) cha Nyongeza ya Nane ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Januari, 2016, yalizingatiwa na Muswada huo ukapelekwa kwenye Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Katiba na Sheria. Kamati iliujadili Muswada huo kwa kuzingatia matakwa ya Kanuni za Kudumu za Bunge.

**Mheshimiwa Spika**, kwa mujibu wa Kanuni ya 86 (5) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la 2016, naomba kuwasilisha Maoni na Ushauri wa Kamati ya Bunge ya Katiba na Sheria kuhusu Muswada wa Sheria ya Marekebisho ya Sheria Mbalimbali (Na.3) wa Mwaka 2018*(The Written Laws (Miscellaneous Amendments) (No.3) Bill, 2018.* Katika

Muswada huu Serikali inapendekeza kufanya marekebisho katika Sheria 6 zifuatazo:

a) *Sheria ya Mamlaka ya Rufaa*, Sura ya 141;
b) *Sheria ya Mwenendo wa Mashauri ya Madai*, Sura ya 33;
c) *Sheria ya Mahakama ya Migogoro ya Ardhi*, Sura ya 216;
d) *Sheria ya Mahakama za Mahakimu*, Sura ya 11;
e) *Sheria ya Baraza la Michezo la Taifa*, Sura ya 49; na
f) *Sheria ya Takwimu*, Sura ya 351.

## 2.0 UTEKELEZAJI WA MAJUKUMU YA KAMATI

**Mheshimiwa Spika**, katika kutekeleza masharti ya Kanuni ya 84(1) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Kamati ilikutana kwa muda wa wiki mbili katika **Ukumbi Na.9** uliopo Jengo la Utawala la Ofisi za Bunge Dodoma na kufanya yafuatayo:

**a)** **Tarehe 20 Agosti, 2018,** Kamati iliweka utaratibu wa uchambuzi wa kibunge wa Miswada ya Sheria kwa kuzingatia ruhusa inayotolewa na Kanuni ya 117 (8) na kujipanga ipasavyo ili kuwezesha utekelezaji bora wa shughuli za Kamati;

**b)** **Tarehe 21 Agosti, 2018,** Kamati ilipitia (ilidurusu) Ibara za Muswada wa Sheria ya Marekebisho ya Sheria Mbalimbali Na. 3, wa mwaka 2018 na kuzingatia Masharti ya Kanuni ya 21 (1) (b) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Januari, 2018 inayohusu majukumu ya Mshauri Mkuu wa Bunge wa Mambo ya Sheria katika uchambuzi wa Miswada ya Sheria;

**c)** **Tarehe 23 Agosti, 2018** Kamati ilipokea maelezo ya Serikali kuhusu madhumuni na sababu za Muswada ambayo yaliwasilishwa na Waziri wa Katiba na Sheria, Mhe. Prof. Palamagamba John Kabudi (Mb);

**d)** **Tarehe 24 Agosti, 2018** Kamati ilipokea maoni ya Wadau mbalimbali kwa lengo la kuisaidia Kamati katika uchambuzi wa Muswada. Maoni hayo ya

Wadau yalitokana na barua za mialiko ambazo zilitolewa na Ofisi ya Bunge pamoja na matangazo kwa Umma ambayo yalitolewa kwa mujibu wa Kanuni ya 84(2) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Januari, 2016. Jumla ya **Wadau 12** kutoka kwenye Taasisi mbalimbali waliwasilisha maoni yao kwa kufika mbele ya Kamati na au kwa njia ya maandishi kupitia Ofisi ya Katibu wa Bunge. Orodha ya Taasisi hizo ni:-

(i) Chama cha Wanasheria Tanganyika (*Tanganyika Law Society – TLS*)
(ii) Kituo cha Sheria na Haki za Binadamu (*Legal and Human Rights Centre – LHRC*),
(iii) TWAWEZA
(iv) SIKIKA,
(v) Hakielimu, na
(vi) *Stallion Attorneys.*

Napenda kuchukua fursa hii kuwashukuru Wadau wote ambao kwa nyakati tofauti, waliwasilisha maoni yao mbele ya Kamati na waliowasilisha kwa maandishi. Kwa hakika Maoni yaliyowasilishwa yaliisaidia Kamati katika kutekeleza jukumu lake la kuuchambua Muswada huu.

e) **Tarehe 25 Agosti, 2018** Kamati ilitathmini hatua iliyofikiwa katika utekelezaji wa majukumu yake. Lengo lilikuwa ni kujiridhisha iwapo uelewa unaopatikana kuhusu maudhui na masharti ya Muswada huu miongoni mwa Wajumbe unaiwezesha Kamati kulishauri Bunge ipasavyo. Katika hatua hiyo, Kamati ilihakiki taarifa ilizokusanya kuhusu Muswada huu na kufanya upembuzi wa taarifa hizo kwa kulinganisha na matarajio katika uchambuzi wa Muswada huu;

f) **Tarehe 27 na 28 Agosti, 2018** Kamati ilifanya uchambuzi wa kina wa Muswada kwa kuzingatia maelezo ya Serikali, maoni ya Wadau pamoja na rejea mbalimbali kuhusiana na Muswada huu. Hatua

hii iliiwezesha Kamati kuandaa Jedwali la mapendekezo ya Marekebisho ambalo liliwasilishwa rasmi Serikalini ili kutekeleza Masharti ya Kanuni ya 84(3) ya Kanuni za Kudumu za Bunge;

**g)** **Tarehe 29 na 30 Agosti, 2018** Kamati ilifanya mashauriano na Serikali kuhusu marekebisho yaliyopendekezwa na Kamati na kuyawasilisha Serikalini. Mashauriano hayo yalifanyika kwa mafanikio makubwa ambapo Serikali ilipokea ushauri wa Kamati na kuufanyia kazi kwa kukubali kuandaa Jedwali la Marekebisho ya Muswada. Jedwali hilo lina marekebisho mbalimbali kuhusu:

i) Maudhui katika baadhi ya Ibara za Muswada;
ii) Dosari za kiuandishi zilizobainika katika baadhi ya Ibara za Miswada;
iii) Kufutwa, kuandikwa upya au kurekebishwa kwa baadhi ya Ibara za Miswada;na
iv) Kuongeza maneno yaliyosahaulika katika baadhi ya Ibara ili kuleta mantiki iliyokusudiwa katika Ibara husika.

Aidha, maelezo zaidi na maboresho yalihitajika kuhusu mantiki ya jumla ya dhana ya ***Official Statistics*** na ***Statistical Information*** katika Sheria ya Takwimu *(The Statistics Act) inayofanyiwa Marekebisho katika Muswada huu.*

**Mheshimiwa Spika,** kutokana na hoja hizo zilizohitaji mashauriano zaidi na Serikali, Kamati ilikuomba muda wa ziada na ukatoa kibali cha kushughulikia Muswada huu kuanzia tarehe 3 hadi 6 Agosti, 2018. Matokeo ya mashauriano hayo, Serikali iliafiki mapendekezo ya Kamati na kukubali kuandaa na kuboresha mambo ya msingi katika Muswada huu kama inavyoonekana katika Jedwali la Marekebisho (*Schedule of Amendments*).

## 3.0 UCHAMBUZI NA MAONI YA KAMATI

**Mheshimiwa Spika,** niruhusu niendelee kwa kueleza uchambuzi na maoni ya Kamati mbele ya Bunge lako Tukufu. Naomba kutanguliza maelezo kuwa Muswada huu ulichambuliwa ukiwa na **Jumla ya Ibara 32 zilizo kwenye sehemu saba ambazo zinapendekeza kufanya Marekebisho katika Sheria Sita (6)** kama zilivyoorodheshwa awali.

**Mheshimiwa Spika,** ili kuliwezesha Bunge lako Tukufu kujadili na kuamua ipasavyo, Kamati ilichambua kwa kina Maudhui ya kila Ibara kama yanavyobainishwa katika sehemu hii. Katika hatua hiyo, Kamati ilibaini maeneo mbalimbali yaliyo hitaji maboresho na hivyo kushauriana na Serikali.

### 3.1 Uchambuzi na Maoni ya Jumla

#### 3.1.1 Sehemu ya kwanza:

**Mheshimiwa Spika,** sehemu hii inayohusu Masharti ya Utangulizi ina jumla ya Ibara mbili zinazohusu ***Jina la Muswada*** na ***namna ambavyo Sheria zinazopendekezwa kurekebishwa zitakavyorekebishwa*** ndani ya Muswada huu. Kamati ilipitia Ibara zote na kukubaliana na Serikali na hivyo kulishauri Bunge liafiki Mapendekezo hayo.

#### 3.1.2 Sehemu ya Pili

**Mheshimiwa Spika,** sehemu hii yenye jumla ya Ibara mbili inahusu mapendekezo ya Serikali kufanya marekebisho kwenye *Sheria ya Mamlaka ya Rufaa*, Sura ya 141. Ibara hizo ni Ibara ya 3 na ya 4 zinaongeza Vifungu vipya vya **3A** na **3B** kwenye *Sheria ya Mamlaka ya Rufaa* kwa lengo la kuweka msingi unaoitaka Mahakama ya Rufaa inapotoa uamuzi katika mashauri ya Madai na Jinai itende haki bila

kufungwa na masharti ya kiufundi (*technicalities*) yanayoweza kukwamisha haki kutendeka.

**Mheshimiwa Spika, Kamati inaridhia mapendekezo ya Serikali kwa kuwa madhumuni yake ni kuitaka Mahakama ya Rufaa ipime uzito wa hoja kwa kila shauri ili haki itendeke kabla ya kukataa shauri kwa msingi wa masharti ya kiufundi *(technicalities).* Hatua hiyo ikitekelezwa kwa umakini na uangalifu itarahisisha utoaji haki katika Mahakama ya Rufaa nchini na hivyo kuendana na Msingi uliowekwa kwenye Ibara ya 107(2)(e) ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.**

### 3.1.3 Sehemu ya Tatu

**Mheshimiwa Spika,** sehemu hii yenye jumla ya Ibara mbili, Ibara ya 5 na 6, inapendekeza kufanya marekebisho kwenye *Sheria ya Mwenendo wa Makosa ya Madai*, Sura ya 33,. Ibara hizo zinaongeza Vifungu vipya vya **3A** na **3B** kwenye *Sheria ya Mwenendo wa Makosa ya Madai* kwa lengo la kuziwezesha Mahakama Kuu, Mahakama za Hakimu Mkazi na Mahakama za Wilaya kutenda haki bila kufungwa na masharti ya kiufundi (*technicalities*) kupita kiasi au kukwamisha haki kutendeka.

**Mheshimiwa Spika, Kamati inaafiki mapendekezo haya na kuipongeza Serikali kuona umuhimu wa kupunguza masharti ya kiufundi kupita kiasi ambayo yamekuwa yakichelewesha utoaji haki.**

### 3.1.4 Sehemu ya Nne

**Mheshimiwa Spika,** sehemu hii yenye jumla ya Ibara tatu, Ibara ya 7, 8 na 9 inapendekeza kufanya marekebisho katika *Sheria ya Mahakama ya Migogoro ya Ardhi*. Marekebisho hayo yanahusu kuongeza Mamlaka ya ziada *(extended jurisdiction)* kwa Hakimu Mkazi ili aweze kusikiliza na kuamua Rufaa

kutoka Mabaraza ya Ardhi ya Kata na Mabaraza ya Ardhi na Nyumba ya Wilaya. Marekebisho hayo ni kwa kuongeza Kifungu kipya cha **41A** kwenye *Sheria ya Mahakama ya Migogoro ya Ardhi*.

**Mheshimiwa Spika, ni maoni ya Kamati kuwa mapendekezo hayo yanatatua changamoto ya muda mrefu kuhusu mlundikano wa mashauri ya ardhi katika Mahakama Kuu yanayotoka katika Mabaraza ya Kata na Wilaya. Hali hiyo, imekuwa ikiwakatisha tamaa Wananchi kuhusu upatikanaji wa haki Ardhi jambo lililoisukuma Kamati na Wabunge wengi kulalamikia jambo hilo kwa muda mrefu sasa. Kwa bahati nzuri, Serikali inakusudia kutatua kero hii kwa mapendekezo hayo. Kamati inaridhia mapendekezo haya na kulishauri Bunge kuafiki Ibara hizo.**

### 3.1.5 Sehemu ya Tano

**Mhesmimiwa Spika,** sehemu hii yenye jumla ya Ibara tano inapendekeza Marekebisho katika *Sheria ya Mahakama za Mahakimu*, Sura ya 11. Marekebisho hayo yanahusu kuanzishwa kwa Mahakama zinazohamishika (*Mobile Courts*) na Mahakama Maalumu (*Special Courts*) pamoja na Mahakama za Madai madogo (*Small claims Courts*). Maelezo ya Serikali yalionesha kuwa madhumuni ya marekebisho hayo ni kupunguza gharama, kuharakisha utatuzi wa migogoro na kuweka Mfumo rahisi wa uendeshaji wa mashauri yenye thamani ndogo.

**Mheshimiwa Spika,** katika sehemu hii, awali Serikali na Kamati zilitofautiana kiuelewa na kufanya majadiliano na mashauriano ya kina kuhusu Masuala Matano (5) ya msingi yaliyokuwa yakipendekezwa kubainika kuwa na dosari mbalimbali. Masuala hayo yaliyobainishwa na Kamati ni:-

i) **Ibara husika kutoainisha bayana Muundo na Mfumo wa usimamizi wa utekelezaji wa majukumu ya Mahakama zinazo hamishika**

***(Mobile Courts) na* Mahakama Maalum *(Special Courts),***

ii) **Ibara husika kutotoa haki ya uwakilishi iliyowekwa kwa mujibu wa Katiba ya nchi na Sheria nyingine za Nchi,**

iii) **Ibara husika kutotoa haki ya Rufaa iliyotajwa katika Katiba ya Nchi katika Ibara ya 13 kuwa Rufaa ni haki ya Kikatiba. Na kwa kuwa dhamira ya *Mobile Court* kama ilivyokuwa imeainishwa na Muswada pamoja na maelezo ya Mtoa Hoja kuwa ni usikilizwaji wa haraka wa Maamuzi, Kamati iliamini kwamba kukosekana kwa haki ya kukata Rufaa kungepelekea Wananchi kukosa haki zao.**

iv) **Mkanganyiko wa dhana mpya ya madai madogo *(Small Claims)* kwa kulinganisha na kiwango cha ukomo wa juu wa madai hayo kilichopendekezwa cha Shilingi Milioni Mia Moja, na**

v) **Kukosekana kwa maelezo ya ziada kuhusu uhalisia wa Gharama za manunuzi na uendeshaji wa gari moja la Mahakama inayohamishika *(Mobile Court Van)* ikilinganishwa na gharama za ujenzi wa Mahakama endelevu.**

Hata hivyo, kutokana na mashauriano hayo, Serikali iliamua kuondoa sehemu ya tano ya Muswada huu kama inavyoonekana katika Jedwali la Marekebisho lililowasilishwa na Mtoa hoja.

### 3.1.6 Sehemu ya Sita

**Mheshimiwa Spika,** sehemu hii yenye jumla ya Ibara nane inapendekeza kufanya marekebisho katika *Sheria ya Baraza la Michezo la Taifa*, Sura ya 49. ili kuliwezesha Baraza la michezo kusimamia michezo ya kulipwa. Kwa sasa Sheria ya Baraza la Michezo inalipa Mamlaka Baraza hilo kusimamia michezo ya ridhaa pekee jambo linalosababisha kukosekana kwa

chombo mahsusi cha kusimamia michezo ya kulipwa. Dosari hii inakusudiwa kurekebishwa kwa mapendekezo haya. Vilevile Vifungu vya 6(b) na 12(1) vya *Sheria ya Baraza la Michezo la Taifa* vinapendekezwa kurekebishwa.

**Mheshimiwa Spika, Kamati inaridhia mapendekezo hayo na kuipongeza Serikali kwa kuongeza Mamlaka ya kisheria kwa Baraza la Michezo. Uamuzi huu utaliwezesha Baraza kusimamia michezo ya hiari na ya kulipwa hatua ambayo itaongeza udhibiti wa michezo hiyo na mapato ya Serikali yaliyokuwa yakipotea kutokana na udhaifu wa kisheria.**

**Aidha, Kamati imebaini kuwa, marekebisho hayo yanalenga kumwezesha Mwanasheria Mkuu wa Serikali kuingilia shauri lolote linalofunguliwa na Baraza au dhidi ya Baraza kwa ajili ya kumshirikisha kwa kuwa ndiye Mshauri wa Serikali katika masuala ya Sheria.**

**Mheshimiwa Spika, Kamati inaridhia mapendekezo ya Serikali kwani uwepo wa Mwanasheria Mkuu wa Serikali utahakikisha kulinda na kutetea haki za Serikali kwa kuwa Baraza la Michezo ni Taasisi ya Serikali kama Taasisi nyingine na hivyo Mwanasheria Mkuu wa Serikali ana wajibika kulisimamia katika Mabaraza na Mahakama yoyote kwa niaba ya Serikali.**

**Mheshimiwa Spika, Kamati inatambua kuwa, kuna umuhimu wa kuwepo kwa ukaguzi na udhibiti wa Mapato yatokanayo na shughuli za Baraza la Michezo nchini kwa lengo la kuimarisha nidhamu ya matumizi na kudhibiti upotevu wa Fedha za Serikali. Hivyo, mapendekezo haya ni Muhimu ili Msimamizi na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali awe na Mamlaka kisheria ya kutekeleza majukumu yake kwa manufaa ya Taifa.**

**Aidha, Kamati inaridhia marekebisho yenye kumwezesha Waziri kuwateua Wasajili Wasaidizi wa Vyama vya Michezo kwa idadi iliyo kadri ya mahitaji, kwa lengo la kuongeza ufanisi katika utekelezaji wa majukumu ya Baraza la Michezo la Taifa.**

**Hata hivyo, Kamati ina maoni kuwa kwa siku zijazo kuna umuhimu wa kufanya marekebisho katika Sheria hii ili kuunda Chombo cha Kitaifa cha Utatuzi ya Migogoro ya Michezo nchini.**

### 3.1.7 Sehemu ya Saba

**Mheshimiwa Spika,** sehemu hii yenye jumla ya Ibara kumi (Ibara ya 23, 24, 25, 26, 27, 28, 29, 30, 31 na Ibara ya 32) inapendekeza kufanya marekebisho katika *Sheria ya Takwimu*, Sura ya 351. Marekebisho hayo ni kufuta cheo cha Mkurugenzi Mkuu popote pale kinaposomeka kwenye *Sheria ya Takwimu* na badala yake kuingiza neno *Mtakwimu Mkuu*. Lengo ni kutumia cheo sahihi kinachoonesha kuwa kiongozi huyu ni Mkuu wa Ofisi ya Taifa ya Takwimu na Mshauri Mkuu wa Serikali katika masuala ya Takwimu. Aidha, inapendekezwa kumpa Mtakwimu Mkuu Mamlaka ya kusimamia na kudhibiti usambazaji wa takwimu nchini.

**Mheshimiwa Spika, Kamati imezingatia ongezeko la usambazaji wa takwimu mbalimbali na matumizi yake chini ya usimamizi usioridhisha. Hali hiyo, kwa maoni ya Kamati, wakati mwingine imesababisha mkanganyiko mkubwa miongoni mwa jamii jambo ambalo linaweza kuathiri ustawi wa Jamii.**

**Hivyo basi, Kamati inalishauri Bunge kuridhia mapendekezo haya kwa kuwa, yataimarisha usimamizi, udhibiti wa upatikanaji na Matumizi ya takwimu nchini kwa mujibu wa Sheria. Aidha, hatua hii itaiwezesha Serikali kupata takwimu nyingi zaidi ambazo itazitumia katika kupanga Mipango ya**

**Maendeleo ya Sekta mbalimbali nchini na kustawisha Jamii.**

### 3.2 Uchambuzi wa Maeneo Mahsusi na Maoni

**Mheshimiwa Spika,** zaidi ya uchambuzi wa jumla na maoni niliyoeleza, yapo maeneo matatu mahsusi ambayo kwa maoni ya Kamati ni vema yakabainishwa kwa Bunge lako Tukufu. Maeneo hayo yanahusu Utaratibu wa Kikanuni wa Mahakama kutenda Haki bila Kufungwa na Masharti ya Kiufundi ya Sheria, Muundo wa Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali na Matumizi ya Notisi ya Siku 90 pamoja na Utaratibu wa Kisera na Kisheria wa Utatuzi wa Migogoro ya Ardhi. Katika maeneo hayo, Kamati ina maoni na mapendekezo mahsusi kama ifuatavyo:

#### 3.2.1 Utaratibu wa Kikanuni wa Mahakama kutenda Haki bila Kufungwa na Masharti ya Kiufundi ya Sheria

**Mheshimiwa Spika,** Ibara ya 4 na Ibara ya 6 ya Muswada zinapendekeza kuwekwa msingi wa kisheria unaoitaka Mahakama kutenda haki bila kufungwa kupita kiasi na masharti ya kiufundi.

**Kamati inaunga mkono mapendekezo haya na imeshauriana na kukubaliana na Serikali kuboresha zaidi uandishi wa Ibara hizi. Lengo ni kuweka bayana masharti yake na kuwezesha uzingatiaji wa mahitaji ya haki kuonekana na Watu wote kwamba inatendeka.**

#### 3.2.2 Maboresho katika Muundo wa Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali pamoja na Matumizi ya Notisi ya Siku 90

**Mheshimiwa Spika,** Ibara ya 17 inapendekeza kumpa Mwanasheria Mkuu wa Serikali Mamlaka ya kuingilia mashauri yoyote yanayohusiana na Baraza la

Michezo la Taifa kwa kuwa ni chombo cha Serikali. Katika uchambuzi zilijitokeza hoja mbalimbali kuhusu uandishi wa Ibara hiyo. Kwa mfano matumizi ya maneno Mwanasheria Mkuu wa Serikali badala ya Wakili Mkuu wa Serikali yalijadiliwa kwa kina.

**Mheshimiwa Spika, Serikali ilikubaliana na Kamati kuboresha uandishi wa Ibara hii ili kutambua majukumu ya Wakili Mkuu wa Serikali kwa kuzingatia Muundo Mpya wa Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali.**

**Aidha, Serikali ilikubali ushauri wa Kamati kwamba, masharti ya *Sheria ya Mashauri ya Serikali* kuhusu utoaji wa notisi ya siku 90 kwa Mwanasheria Mkuu wa Serikali yasihusike inapotokea Mwanasheria Mkuu wa Serikali ameingilia shauri ambalo tayari lipo Mahakamani. Kwa sababu hiyo Serikali imeboresha** Ibara ya 17(4) ili isomeke kama ifuatavyo:

> ***Provided that, the requirement of ninety days notice of intention to sue the government as stipulated under the Government Proceedings Act shall not apply where the Attorney General intervenes under this section.***

### 3.2.3 Maboresho ya Uandishi wa Ibara ya 24, 25 na 31

**Mheshimiwa Spika,** matumizi ya maneno katika utungaji wa Sheria ni jambo muhimu linaloweza kuepusha mkanganyiko wa masharti ya Sheria. Kwa sababu hiyo, Kamati ilijielekeza kwenye usahihi wa matumizi ya maneno na kuepuka utata. Katika kufanya hivyo, ilibainika kuwa neno "***chief***" limetumika katika sehemu inayopaswa kutumia neno "***general***" katika Ibara ya 24 (a).

**Mheshimiwa Spika**, katika Ibara ya 25 (a) neno "**or**" lilipendekezwa kutumika katikati ya maneno "compiled" na "dissemination" ambapo kwa maoni ya Kamati matumizi yake hayaendani na mantiki iliyokusudiwa. Aidha, uandishi wa Ibara ya 31 uliibua hoja kuhusu udhibiti wa usambazaji wa takwimu. Namna ilivyoandikwa katika Ibara ya 31 kwenye pendekezo la Kifungu cha 24 A- (2) haiendani na kusudio na mantiki ya mapendekezo.

**Mheshimiwa Spika**, Serikali ilikubaliana na Kamati na hivyo kufanya maboresho mbalimbali ya kiuandishi katika Ibara za 24, 25 na 31 kwa lengo la kuondoa utata wa kisheria uliobainika na kuweka msingi mzuri wa utekelezaji na tafsiri ya Sheria husika.

### 3.3 Utaratibu wa Kisera na Kisheria wa Utatuzi wa Migogoro ya Ardhi

**Mheshimiwa Spika,** sehemu ya Nne ya Muswada inapendekeza marekebisho katika Sheria ya Mahakama ya Migogoro ya Ardhi, Sura ya 216 kwa kuongeza Kifungu kinachompa Hakimu Mkazi Mamlaka ya ziada ya kusikiliza na kuamua Rufaa kutoka kwenye Mabaraza ya Kata na Mabaraza ya Ardhi na Nyumba ya Wilaya.

**Mheshimiwa Spika, Kamati inaunga mkono mapendekezo haya kwa kuwa yanalenga kupunguza mlundikano wa Rufaa za mashauri ya Ardhi katika Mahakama Kuu.**

Hata hivyo, pamoja na manufaa ya marekebisho hayo, Kamati ina maoni kuwa marekebisho yanayopendekezwa hayatoshelezi kutatua changamoto nyingi nchini zinazohusiana na utatuzi wa migogoro ya Ardhi. Miongoni mwa changamoto hizo ni pamoja na:-

i) Uwepo wa udhibiti na usimamizi usioridhisha wa nidhamu na Maadili katika Mabaraza ya Ardhi;
ii) Uchache wa Mabaraza ya Adhi nchini. Mathalan, Mikoa mingi nchini ina Baraza la Nyumba na Ardhi la Wilaya moja tu linalohudumia Mkoa mzima badala kila Wilaya kuwa na Baraza;
iii) Vyombo vya utatuzi wa Migogoro ya ardhi kusimamiwa na Mamlaka tatu (Ofisi ya TAMISEMI, Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi pamoja na Mahakama); na
iv) Ukosefu wa ajira za kudumu kwa Wenyeviti wa Mabaraza ya Nyumba na Ardhi ya Wilaya.

**Mheshimiwa Spika, kwa msingi huu, Kamati inaishauri Serikali ifanye utaratibu wa Kisera na Kisheria ili kurudisha Mfumo wa utatuzi wa migogoro ya Ardhi katika Mfumo wa Mahakama kwa kuwa Mfumo wa Mahakama nchini umeimarishwa na kuboreshwa zaidi ya Mfumo wa Mabaraza ya Ardhi.**

## 4.0 HITIMISHO

**Mheshimiwa Spika**, kwa mara nyingine tena naomba nikushukuru sana wewe kwa kutoa kibali ili kamati ya Katiba na Sheria iweze kuufanyia kazi Muswada huu. Aidha, naomba kuwatambua na kuwashukuru Wadau mbalimbali waliofika na kutoa maoni na ushauri wao kwa Kamati.

**Mheshimiwa Spika,** kwa namna ya pekee kabisa naomba niwashukuru Wajumbe wa Kamati ya Katiba na Sheria kwa weledi na umahiri wao waliouonyesha wakati wa kuchambua Muswada huu na hatimaye kutoa mapendekezo ya msingi ya kuuboresha. **Naomba Majina yao yaingizwe kwenye Kumbukumbu Rasmi za Bunge (HANSARD).**

1. Mhe. Mohamed Omary Mchengerwa,Mb-**Mwenyekiti**
2. Mhe. Najma Murtaza Giga, Mb–M**akamu /Mwenyekiti**

3. Mhe.Joseph Kizito Mhagama, Mb-Mjumbe;
4. Mhe. Makame Mashaka Foum, Mb - Mjumbe;
5. Mhe. Asha Abdallah Juma, Mb - Mjumbe;
6. Mhe. Amina Saleh Mollel, Mb - Mjumbe;
7. Mhe. Wanu Hafidh Amer, Mb - Mjumbe;
8. Mhe. Prof. Jumanne Abdallah Maghembe,Mb-Mjumbe;
9. Mhe. Dkt. Mathayo David Mathayo, Mb - Mjumbe;
10. Mhe. Nimrod Elirehemah Mkono, Mb - Mjumbe;
11. Mhe. Susan Peter Maselle, MB - Mjumbe;-
12. Mhe. Alfredina Apolinary Kahigi, Mb - Mjumbe;
13. Mhe. Latifah Hassan Chande,Mb - Mjumbe;
14. Mhe. Saed Ahmed Kubenea, Mb - Mjumbe;
15. Mhe. Ally Abdulla Saleh, Mb - Mjumbe;
16. Mhe. Jacqueline Kandidus Ngonyani Msongozi,Mb - Mjumbe;
17. Mhe. Bupe Nelson Mwakang'ata, Mb - Mjumbe;
18. Mhe. Sixtus Raphael Mapunda, Mb - Mjumbe;
19. Mhe. Hassan Seleman Kaunje, Mb - Mjumbe;
20. Mhe. Yahaya Omary Massare, Mb - Mjumbe;
21. Mhe. Upendo Furaha Peneza, Mb - Mjumbe;
22. Mhe. Tundu Antiphas Mughwai Lissu, Mb - Mjumbe
23. Mhe. Emmanuel A.Mwakasaka, Mb - Mjumbe
24. Mhe. Dkt.Damas Daniel Ndumbaro, Mb - Mjumbe

**Mheshimiwa Spika**, nawashukuu Watumishi wote wa Ofisi ya Bunge hususan Katibu wa Bunge **Ndg. Stephen Kagaigai** kwa Uongozi thabiti ambao umerahisisha utendaji kazi wa Kamati. Aidha, namshukuru Mkurugenzi wa Idara ya Kamati za Bunge Ndg. Athuman Hussein, Mkurugenzi Msaidizi Ndg. Angelina L. Sanga, Washauri wa Bunge wa Mambo ya Sheria, Ndg. Stephano Seba Mbutu, Ndg. Maria Ndulugu, Ndg. Nesta Kawamala, Ndg. Evelyne R.Shibandiko, Ndg. Thomas A. Shawa na Makatibu wa Kamati Ndg. Stanslaus Kagisa, Ndg. Dunford P. Mpelumbe pamoja na Msaidizi wa Kamati Ndg. Rahel Masima waliofanikisha kazi ya uchambuzi na uratibu wa shughuli za Kamati kwa kuiwezesha Kamati yangu kutekeleza majukumu yake ipasavyo na kuhakikisha taarifa hii inakamlika kwa wakati.

**Mheshimiwa Spika,** naomba kuwasilisha.

Mohamed Omary Mchengerwa, Mb
**MWENYEKITI**
**KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA KATIBA NA SHERIA**
10 Septemba, 2018

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, sasa nimwite Msemaji Mkuu wa Kambi Rasmi ya Upinzani juu ya masuala ya Katiba na Sheria. (*Makofi*)

Sasa Mheshimiwa Ally Saleh kama ilivyo ada kuna shida kidogo, mnatuweka katika wakati mgumu wakati mwingine; shida yangu ipo kwenye utangulizi tu lakini kwenye haya mambo yako yanayohusu sheria na nini na maoni yako yote yako vizuri lakini utangulizi haulengi chochote katika haya yaliyoko mezani. Kwa hiyo, ni ushauri wangu kwamba ungeendelea na kuanzia namba mbili kwenda mbele.

**MHE. ALLY SALEH ALLY – (K.n.y MSEMAJI MKUU WA KAMBI RASMI YA UPINZANI BUNGENI KWA WIZARA YA KATIBA NA SHERIA):** Mheshimiwa Spika, hewala!

Mheshimiwa Spika, napenda kuwasilisha maoni ya Kambi ya Upinzani kwa mujibu wa kifungu 76 cha Kanuni za Bunge na kama ulivyoniagiza nitaanza kwenye sehemu ya pili ambacho kinaanza hivi, sheria zinazofanyiwa marekebisho katika Muswada huu. Muswada ulio mbele ya Bunge lako unapendekeza kuzifanyia marekebisho sheria sita, ambazo ni kama hizo zilizotajwa katika orodha hiyo.

Mheshimiwa Spika, kuhusu mabadiliko ya marekebisho yanayopendekezwa katika Sheria ya Mamlaka ya Rufaa, Sura ya 141 na Sheria ya Uendeshaji wa Makosa ya Madai Sura ya 633, kwa mujibu wa Muswada kwenye madhumuni na sababu, lengo ni kwamba Mahakama inapofanya kazi yake kwenye mashauri ya madai na jinai

isifungwe na sababu za kiufundi ambayo kwa kiwango kikubwa yanaweza kukwamisha haki kutendeka. Mapingamizi mengi ya awali yanatokea kutokana na sababu za kiutaratibu na kiufundi katika uwasilishwaji wa kesi. Hivyo mambo hayo ya kiufundi kwa njia moja au nyingine yanapelekea mhusika wa kesi kucheleweshewa haki ya msingi.

Mheshimiwa Spika, Kambi Rasmi ya Upinzani, haikuwa na tatizo na jambo hilo ambalo limeelezwa vizuri kama ndio lengo kuu la kuleta marekebisho kwenye kifungu cha nne (4) cha Muswada kinachorekebisha kifungu cha tatu (3) cha sheria kwa kuongeza vifungu vipya vya 3A na 3B, lakini katika vifungu hivyo dhana au lengo lililoongelewa halionekani.

Mheshimiwa Spika, Kambi Rasmi ya Upinzani inaungana na maoni yaliyotolewa na wadau ya kuongeza kifungu kipya cha 3C ambacho kitabeba maudhui kama lengo la marekebisho ya Muswada linavyohitaji. Naomba kunukuu mapendekezo ya mmoja wa wadau waliowasilisha maoni yao katika Kamati ya Bunge,

*"No appeal, revision, review, or application in the Court of Appeal shall be struck out on grounds of Procedural irregularity. In such an event the Court shall on its own motion rectify the irregularity or grant a party concerned time to rectify the irregularity."*

Mheshimiwa Spika, Kambi Rasmi ya Upinzani inaamini kifungu hiki ndio hasa kilikuwa lengo kuu la kuletwa kwa marekebisho ya sheria husika ili kuokoa muda wa usikilizwaji wa mashauri ya msingi, kama yanavyopelekwa kwenye Mahakama ya Rufaa.

Mheshimiwa Spika, Sheria ya Mahakama za Utatuzi wa Migogoro ya Ardhi, Sehemu ya Nne. Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni kwa mara kadhaa tumeeleza ndani ya Bunge lako Tukufu changamoto mbalimbali katika mfumo wa kutatua migogoro ya ardhi ikiwemo namna ambavyo

Mabaraza ya Ardhi yanavyoingiliwa na Wakuu wa Wilaya na kushindwa kutoa haki bila upendeleo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, itakumbukwa kuwa Mkuu wa Mkoa wa Dar es Salaam alitangaza kufuta Mabaraza ya Kata huku akijua kuwa Mabaraza hayo yameanzishwa kwa mujibu wa sheria za nchi yetu. Sio Waziri wala Rais ambaye alimkemea mkuu huyo wa mkoa ambaye kwa muda mrefu amekuwa *notorious* wa kuvunja taratibu za kisheria bila kuchukuliwa hatua. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, hata aliyekuwa Mkuu wa Wilaya ya Kinondoni Ally Salum Hapi alinukuliwa akipinga hukumu iliyokuwa imetolewa na Mwenyekiti wa Baraza la Ardhi la Wilaya huku akijua kuwa zipo taratibu za rufaa ambazo zinatakiwa kufuatwa na upande ambao haujaridhika na maamuzi ya baraza kama hilo.

Mheshimiwa Spika, ukiacha Mabaraza ya Ardhi kuingiliwa katika maamuzi na wateule wa Rais, zipo changamoto za thamani ya ardhi za kata na vijiji kuwa chini kisheria huku ikiwa tofauti na uhalisia wa soko. Katika moja ya Muswada wa Marekebisho ya Sheria Mbalimbali uliowasilishwa Novemba, mwaka uliopita, Kambi Rasmi ya Upinzani ilieleza na kufafanua kuhusu athari za kuongeza thamani ya ardhi kwa upande wa Baraza la Ardhi la Wilaya na Mahakama Kuu katika mashauri ya madai na kuacha kuongeza thamani ya ardhi katika ngazi ya kata na vijiji kwa sababu itasababisha ongezeko la mashauri ya ardhi Mahakama Kuu, jambo ambalo lingefanyiwa kazi katika ngazi za chini.

Mheshimiwa Spika, Kambi Rasmi ya Upinzani inatambua kuwa ngazi za Halmashauri ya Kijiji ina mamlaka ya usuluhishi pekee na masuala ya uamuzi wa kisheria yanaanzia katika Baraza la Kata. Jambo la msingi na kuangalia mbele ni Serikali kuleta mkakati wa namna ya kuboresha ngazi hizi za chini ili ziwe na uwezo wa kukabiliana na migogoro ya kiardhi. Hata kabla mwaka haujaisha, Serikali imeona athari za marekebisho yake ya

mwaka uliopita ambazo zimesababisha kuongezeka kwa mashauri ya ardhi katika Mahakama Kuu na Mahakama ya Rufaa.

Mheshimiwa Spika, pendekezo la Serikali katika Muswada huu ni kumpa Jaji Mkuu mamlaka ya kuwapa mamlaka Mahakimu wakazi ya kushughulika na rufani zinazotokana na maamuzi ya Mabaraza ya Ardhi ya Wilaya.

Mheshimiwa Spika, Serikali bila kuzingatia kuwa hata hao Mahakimu Wakazi wamezidiwa na mashauri mengine imeamua kuwapa mzigo mwingine wa kushughulika na mashauri yanayohusu mambo ya ardhi. Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inapendekeza kuwa kuwe na mjadala mpana kuhusu utatuzi wa migogoro ya ardhi kwa maana ya kuyaboresha Mabaraza ya Ardhi kuanzia ngazi za chini mpaka Mahakama ya Rufaa ikiwa ni pamoja na kuwa na mkakati wa kuhakikisha ardhi inapangwa na kupimwa ili kupunguza migogoro ya ardhi nchini.

Mheshimiwa Spika, ni wakati muafaka pia kuangalia uwezekano wa kuyaondoa Mabaraza ya Ardhi kuwa chini ya Wizara ya Ardhi na Makazi na kuyapeleka kwenye Wizara ya Katiba na Sheria kwa sababu ukiangalia kwa makini utatuzi wa migogoro ya ardhi ni lazima uzingatie sheria na taratibu na pia kuyaondoa kupokea maelekezo ya Wakuu wa Mikoa na Wilaya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Sheria ya Mahakama za Mahakimu Sura ya 11; Kambi Rasmi ya Upinzani haikushangaa kukutana na marekebisho ya Sheria ya Mahakama za Mahakimu. Kama tulivyoeleza kwenye hoja ya Muswada namba tatu katika Mkutano huu wa Bunge, tulieleza kuwa imeibuka tabia ya Serikali ya Awamu ya Tano kutamka na kuelekeza mambo ambayo baadaye huyahalalisha kisheria.

Mheshimiwa Spika, mahakama zinazotembea tayari zimeshaanza kufanya kazi na magari ya mahakama hizo

yanaonekana mitaani huku wananchi wakijiuliza yameanzishwa kwa mujibu wa sheria gani. Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inapenda kupata maelezo ya Waziri juu ya uwepo wa magari ya mahakama ambayo tayari yamekuwa *branded* kuwa ni mahakama inayotembea na wakati huohuo Bunge halijapitisha utaratibu huo kisheria. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kifungu cha 11 cha Muswada kinachorekebisha kifungu cha 2 cha Sheria ya Mahakama za Mahakimu, Sura 11 kinatoa tafsiri ya maneno *mobile court*, *small claim* na *special court* ili kuleta maana iliyokusudiwa katika sheria. Kambi Rasmi ya Upinzani, imestuka kidogo na tafisiri ya *small claim.*

Mheshimiwa Spika, kifungu cha 11 cha Muswada kinachoongeza kifungu cha 17A, katika sheria mama kwa kuanzisha hizo mahakama zinazohamishika na Mahakama maalum. Kifungu cha 17B kinampa mamlaka...

Mheshimiwa Spika, nitaendelea mbele, katika maelezo ya sababu na madhumuni Mwanasheria Mkuu anasema kuwa rufaa zitakatwa Mahakama Kuu kwa hoja za kisheria tu.

Mheshimiwa Spika, nitakwenda kwenye kifungu cha sita, Sheria ya Takwimu, Sura ya 351; marekebisho yanayopendekezwa kufanyika kwenye Sheria ya Takwimu ukiyasoma kwa tafakuri na kwa dhana pana utaona kuwa yamejikita katika kudhitibi tafiti ambazo zitakuwa zinafanyika na kuwaeleza wananchi matokeo ya tafiti hizo.

Mheshimiwa Spika, kwa dhana nyingine ni kwamba mapendekezo haya yanapoteza kabisa dhana ya kufanya utafiti, *Social Science Research* na matokeo yake kuwafikia wananchi husika wa tafiti hiyo. Kwani kabla ya kuanza inatakiwa uombe kibali kwa Mtakwimu Mkuu, kwa mujibu wa kifungu cha 18(2).

Mheshimiwa Spika, kifungu cha 24 cha Muswada kinaongeza kifungu kipya cha 24A kwenye Sheria ya Takwimu Sura 351 na kifungu hiki kinahusu usambazaji wa takwimu rasmi. Kifungu cha 24A(1) kinasema:

*"Any person who is authorised by the Bureau to process any official statistics, shall before publishing or communicating such information to the public, obtain an authorisation from the Bureau."*

Mheshimiwa Spika, kifungu cha 24A kama kilivyorekebishwa kinasema kwamba;

*"(2) A person who has different findings from statistics disseminated by the Bureau shall, prior to communicating such findings to the public, consult the Bureau."*

Mheshimiwa Spika, kifungu hiki kinamlazimisha mtafiti yeyote kabla ya kutoa matokeo ya utafiti wake ni lazima afanye mashauriano na Ofisi ya Takwimu. Kambi Rasmi ya Upinzani, katika hili la mashauriano inaona kuna uwezekano mkubwa kuwa ikawa ni kumwambia mtafiti kurekebisha matokeo ya utafiti uendane na matakwa ya Ofisi ya Takwimu au kufutwa kwa utafiti husika. Kwa ujumla kifungu hiki kina nia ovu na utafiti utakaokuwa unafanywa hapa nchini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, lengo la utafiti ni kutafuta suluhisho la tatizo na siyo kushindana na Serikali, hivyo wasiwasi wa Serikali unatoka wapi? Hii inazidi kutupa mashaka kwamba kuna uwezekano mkubwa kwamba takwimu zinazotolewa na Ofisi ya Takwimu zina upungufu ambao hawataki Watanzania waufahamu.

Mheshimiwa Spika, kifungu cha 24B (a)(1) ambacho kina utata sana na kimepingwa sana na wadau wengi, lakini kwa kuangalia au kusoma vifungu vyote viwili *harmoniously* utagundua kwamba kifungu cha pili kinasochomeka kuwa;

*"A person shall not disseminate or otherwise communicate to the public any statistical information which is intended to invalidate, distort or discredit official statistics"*

Mheshimiwa Spika, kifungu hiki hakina maana na hakitakiwi kuwepo kwani tayari kimo ndani ya kifungu cha 24A(1) kwenye maneno, *"...shall before..., obtain an authorization from the Bureau."*

Mheshimiwa Spika, na kama Mwanasheria Mkuu wa Serikali anaona ni muhimu kifungu hicho kiwepo, kinazusha hoja kubwa, ambayo ni, je, kuna utafiti unaofanyika kwa lengo maalum la kupingana na tafiti za Serikali au kuzifanya takwimu za Serikali zionekane hazifai?

Mheshimiwa Spika, Kambi Rasmi ya Upinzani inaona kuwa mawanda *(scope)* ya kifungu yana malengo mabaya na siyo maendeleo chanya katika mustakabali wa nchi yetu.

Mheshimiwa Spika, kifungu hiki kinaikinga Serikali na kuwafanya watendaji wake mara zote wawe katika *comfort zone* yaani wasiweze kuwajibika. Takwimu zozote zitakazotolewa ziwe ni zile ambazo ni sahihi tu, tukumbuke kwamba wanaofanya kazi hiyo ni binadamu na makosa kwa binadamu ni jambo la kawaida. Hoja nyingine ni je, makosa katika takwimu yanaonekana vipi bila kufanya utafiti? Ili nchi iweze kwenda mbele ni lazima kuwe na *check and balance* kwa upande wa Serikali na taasisi huru.

Mheshimiwa Spika, sambamba na kifungu hicho, kifungu kipya cha 24B(2) kinachosomeka kama ifuatavyo:

*"A person shall not disseminate or communicate to the public any statistical information without the approval of the Statistician General."*

Mheshimiwa Spika, kama ambavyo kifungu cha 24B(1) tulivyoshauri kuwa kifutwe na hiki cha (2) tunashauri kifutwe

pia, kwani dhana nzima ni kupata kibali au ruhusa kabla ya kutangaza matokeo ya utafiti. Kwani watendaji wote katika Ofisi ya Takwimu wanafanya kazi kwa niaba ya Mtafiti Mkuu.

Mheshimiwa Spika, ni rai ya Kambi Rasmi ya Upinzani kwamba kifungu hiki kipya cha 24A na 24B vifutwe kwani msingi wake ni wa kudhibiti watafiti wetu katika kututafutia suluhisho la matatizo yaliyopo katika jamii zetu. Sisi tunaamini kuwa maendeleo ya nchi yanategemea sana tafiti zitakazofanyika ziwe, *scientific au social science researches.(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, hitimisho; Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni kwa ujumla inaona kuwa dhana ambayo ilikusudiwa katika marekebisho yaliyoletwa katika sheria mbalimbali haionekani katika vifungu vya sheria ambavyo vinapendekezwa kutungwa ili kuwa sheria. Jambo hilo linatia wasiwasi sana juu ya nia iliyojificha ya Serikali.

Mheshimiwa Spika, tukumbuke kwamba sheria hizi zinatungwa na Bunge letu, na pale ambapo zinaonekana kuwa ni sheria mbaya, kwa maana ya kuwa zina nia/ lengo ovu basi lawama hizo zinarudi kwa watunga sheria ambao ni sisi Wabunge. Katika hilo Kambi Rasmi ya Upinzani imetoa mtazamo wake hapo awali wakati tukipitia marekebisho yanayoombwa na Serikali kupitishwa na Bunge.

Mheshimiwa Spika, baada ya hayo, pamoja na kuomba hotuba hii yote, isipokuwa sehemu ambayo umetaka tuitoe iingie katika *Hansard,* naomba kuwasilisha. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Ally Saleh, Msemaji Mkuu wa Kambi Rasmi ya Upinzani kwa Wizara ya Katiba na Sheria, tunakushukuru sana.

# MAONI YA MSEMAJI MKUU WA KAMBI RASMI YA UPINZANI-WIZARA YA KATIBA NA SHERIA KUHUSU MUSWADA WA MAREKEBISHO YA SHERIA MBALIMBALI MWAKA 2018(The Written Laws (Miscellaneous) (NO.3) Act, 2018

*Yanatolewa chini ya Kanuni ya 86(6) ya Kanuni za Bunge, toleo la mwaka 2016*

## 1. UTANGULIZI

**Mheshimiwa Spika**, awali ya yote napenda kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kunijaalia afya njema pamoja na ulinzi anaotupatia kila siku katika kutekeleza wajibu wetu wa kibunge wa kuishauri na kuisimamia serikali kwa mujibu wa Ibara ya 63 ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya mwaka 1977.

Sambamba na hilo niendelee kumtakia afya njema na awahi kurudi nyumbani Mhe. Tundu Antiphas Lissu, Msemaji Mkuu wa Kambi Rasmi ya Upinzani- Wizara ya Katiba na Sheria na pia Mnadhimu Mkuu wa Kambi Rasmi ya Upinzani ili kwa pamoja tuzidi kutimiza wajibu wetu wa kikatiba kama nilivyoeleza hapo awali.

**Mheshimiwa Spika,** Kwa kuwa Wizara hii ndiyo inayosimamia masuala ya utoaji haki na kuhakikisha kwamba haki inatolewa kwa watu wote bila ubaguzi wa aina yoyote,

**[MANENO YAMEONDOLEWA KWA MAELEKEZO YA KITI]**

**Mheshimiwa Spika,** kwa heshima kubwa naomba kutoa pongezi kwa waheshimiwa wabunge toka Kambi Rasmi ya Upinzani kwa utulivu mkubwa wanaouonyesha katika kipindi hiki cha mkakati wa kuwafanya bidhaa, na pia nawapa pole wale wote ambao wamejiweka sokoni na kupokea *price tag* kutoka Chama cha Mapinduzi. Jambo la kufurahisha na la msingi ni kwamba Watanzania wafahamu vema kinachoendeleakatika biashara hiyo ya viongozi waliochaguliwa na wananchi kugeuka kuwa

bidhaa kwa kauli mbiu ambayo imeshachuja ya "kuunga mkono juhudi". Kama dhana ni kuunga mkono juhudi kwa nini na Wabunge wa CCM wasijiuzulu ili wazidi kumuunga mkono Rais wao nje ya Bunge? Dhana hii ya kuviona Vyama vya Upinzani kama wapinga maendeleo itakoma siku CCM watakapokuwa Chama cha Upinzani na ndipo mtakapojua kuwa demokrasia ni msingi wa maendeleo wa Taifa lolote lile pale ambapo raia wote wanashirikishwa bila kujali itikadi zao za kidini, kisiasa au za kikabila.

**[MANENO YAMEONDOLEWA KWA MAELEKEZO YA KITI]**

**Mheshimiwa Spika,** baada ya kutoa utangulizi huo, naomba kutoa maoni ya Kambi Rasmi ya Upinzani kwenye baadhi ya sehemu na vifungu vya muswada ambavyo tunaona kunahitajika marekebisho.

## 2. SHERIA ZINAZOFANYIWA MAREKEBISHO KATIKA MUSWADA HUU

**Mheshimiwa Spika,** muswada ulio mbele ya Bunge lako unapendekeza kuzifanyia marekebisho sheria 6, ambazo ni;

- **i.** Sheria ya Mamlaka ya Rufaa Sura 141 (The Appellate Jurisdiction Act, Cap 141);
- **ii.** Sheria ya Uendeshaji wa Mashauri ya Madai, Sura 33 (The Civil Procedure Code, Cap 33)
- **iii.** Sheria ya Mahakama za Utatuzi wa Migogoro ya Ardhi, Sura 216(The Land Disputes Courts Act, Cap 216)
- **iv.** Sheria ya Mahakama za Mahakimu, Sura 11(The Magistrates' Courts Act,Cap.11);
- **v.** Sheria ya Baraza la Michezo la Taifa Sura 49(The National Sports Council of Tanzania Act, Cap. 49);
- **vi.** Sheria ya Takwimu, Sura 351(The Statistics Act, cap 351).

## 3. MAREKEBISHO YA SHERIA YA MAMLAKA YA RUFAA SURA YA 141 NA SHERIA YA UENDESHAJI WA MAKOSA YA MADAI SURA YA 33

Mheshimiwa Spika, kuhusu mabadiliko/marekebisho yanayopendekezwa katika sheria ya Mamlaka ya Rufaa, Sura ya 141 na sheria ya uendeshaji wa makosa ya madai sura ya 33, kwa mujibu wa muswada kwenye Madhumuni na Sababu,lengo ni kwamba Mahakama inapofanyakazi yake kwenye mashauri ya madai na jinai isifungwe na sababu za kiufundi ambayo kwa kiwango kikubwa yanaweza kukwamisha haki kutendeka. Mapingamizi mengi ya awali yanatokea kutokana na sababu za kiutaratibu na kiufundi katika uwasilishwaji wa kesi. Hivyo mambo hayo ya kiufundi kwa njia moja au nyingine yanapelekea mhusika wa kesi kucheleweshewa haki ya msingi.
Kambi Rasmi ya Upinzani, haikuwa na tatizo na jambo hilo ambalo limeelezwa vizuri kama ndio lengo kuu la kuleta marekebisho kwenye kifungu cha 4 cha muswada kinacho rekebisha kifungu cha 3 cha sheria kwa kuongeza vifungu vipya vya 3A na 3B. Lakini katika vifungu hivyo dhana au lengo lililoongelewa halionekani.

**Mheshimiwa Spika,** Kambi Rasmi ya Upinzani inaungana na maoni yaliyotolewa na wadau ya kuongeza kifungu kipya cha 3C ambacho kitabeba maudhui kama lengo la marekebisho ya muswada linavyohitaji. Naomba kunukuu mapendekezo ya mmoja wa wadau waliowasilisha maoni yao katika Kamati ya Bunge,

*“No appeal, revision, review, or application in the Court of Appeal shall be struck out on grounds of Procedural irregularity. In such an event the Court of Appeal shall on its own motion rectify the irregularity or grant a party concerned time to rectify the irregularity.”*

Kambi Rasmi ya Upinzani inaamini kifungu hiki ndio hasa kilikuwa lengo kuu la kuletwa kwa marekebisho ya sheria husika ili kuokoa muda wa usikilizwaji wa mashauri ya msingi, kama yanavyopelekwa kwenye mahakama ya rufaa.

## 4. SHERIA YA MAHAKAMA ZA UTATUZI WA MIGOGORO YA ARDHI, SURA 216

**Mheshimiwa Spika,** Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni kwa mara kadhaa tumeeleza ndani ya Bunge lako tukufu changamoto mbalimbali katika mfumo wa kutatua migogoro ya ardhi ikiwemo namna ambavyo Mabaraza ya Ardhi yanavyoingiliwa na Wakuu wa Wilaya na kushindwa kutoa haki bila upendeleo.

**Mheshimiwa Spika**, Itakumbukwa kuwa Mkuu wa Mkoa wa Dar es Salaam alitangaza kufuta Mabaraza ya Kata huku akijua kuwa Mabaraza hayo yameanzishwa kwa mujibu wa Sheria za nchi yetu. Sio Waziri wala Rais ambaye alimkemea Mkuu huyo wa Mkoa ambaye kwa muda mrefu amekuwa *notorious* wa kuvunja taratibu za kisheria bila kuchukuliwa hatua.

**Mheshimiwa Spika**, hata aliyekuwa Mkuu wa Wilaya ya Kinondoni Ally Salum Hapi alinukuliwa akipinga hukumu iliyokuwa imetolewa na Mwenyekiti wa Baraza la Ardhi la Wilaya huku akijua kuwa zipo taratibu za rufaa ambazo zinatakiwa kufuatwa na upande ambao haujaridhika na maamuzi ya Baraza.

**Mheshimiwa Spika**, ukiacha Mabaraza ya Ardhi kuingiliwa katika maamuzi na wateule wa Rais, zipo changamoto za thamani ya ardhi ya Kata na Vijiji kuwa ya chini kisheria huku ikiwa tofauti na uhalisia wa soko. Katika moja ya muswada wa Marekebisho ya Sheria mbalimbali yaliyowasilishwa Novemba mwaka uliopita, Kambi Rasmi ya Upinzani ilieleza na kufafanua kuhusu athari za kuongeza thamani ya ardhi kwa upande wa Baraza la Ardhi la Wilaya na Mahakama Kuu katika mashauri ya

madai na kuacha kuongeza thamani ya ardhi katika ngazi ya Kata na Vijiji kwa sababu itasababisha ongezeko la mashauri ya ardhi Mahakama Kuu jambo ambalo lingefanyiwa kazi katika ngazi za chini.

**Mheshimiwa Spika**, Kambi Rasmi ya Upinzani inatambua kuwa ngazi ya Halmashauri ya Kijiji ina mamlaka ya usuluhishi pekee na masuala ya uamuzi ya kisheria yaanzia katika Baraza la Kata. Jambo la msingi na kuangalia mbeleni ni Serikali kuleta mkakati wa namna ya kuboresha ngazi hizi za chini ili ziwe na uwezo wa kukabiliana na migogoro ya ardhi.

**Mheshimiwa Spika**, Hata kabla mwaka haujaisha Serikali imeona athari za marekebisho yake ya mwaka uliopita ambazo zimesababisha kuongezeka kwa mashauri ya ardhi katika Mahakama Kuu na Mahakama ya Rufaa. Pendekezo la Serikali katika muswada huu ni kumpa Jaji Mkuu mamlaka ya kuwapa Mamlaka Mahakimu Wakazi ya kushughulikia rufaa zinazotokana na maamuzi ya Mabaraza ya Ardhi ya Wilaya.

**Mheshimiwa Spika**, Serikali bila kuzingatia kuwa hata hao Mahakimu wakazi wamezidiwa na mashauri mengine imeamua kuwapa mzigo mwingine wa kushughulikia mashauri ya ardhi.

**Mheshimiwa Spika**, Kambi Rasmi ya Upinzani ya Bunge lako tukufu inapendekeza kuwe na mjadala mpana kuhusu utatuzi wa migogoro ya ardhi kwa maana ya kuyaboresha mabaraza ya ardhi kuanzia ngazi za chini mpaka Mahakama ya Rufaa ikiwa ni pamoja na kuwa na mkakati wa kuhakikisha ardhi inapangwa na kupimwa ili kupunguza migogoro ya ardhi nchini.

**Mheshimiwa Spika**, ni wakati mwafaka pia kuangalia uwezekano ya kuyaondoa Mabaraza ya ardhi kuwa chini ya Wizara ya Ardhi na Makazi na kuyapeleka kwenye Wizara ya Katiba na Sheria kwa sababu ukiangalia kwa makini utatuzi wa migogoro ya ardhi ni lazima uzingatie

sheria na taratibu na pia kuyaondoa kupokea maelekezo ya Wakuu wa Mikoa na Wilaya.

**5. SHERIA YA MAHAKAMA ZA MAHAKIMU SURA YA 11**

**Mheshimiwa Spika,** Kambi Rasmi ya Upinzani haikushangaa kukutana na marekebisho ya sheria ya Mahakama za Mahakimu. Kama tulivyoeleza kwenye hoja ya muswada namba tatu katika mkutano huu wa Bunge, tulieleza kuwa imeibuka tabia ya serikali ya awamu ya tano kutamka na kuelekeza mambo ambayo baadaye huyahalalisha kisheria.

**Mheshimiwa Spika,** Mahakama zinazotembea tayari zimeshaanza kufanya kazi na magari ya Mahakama hizo yanaonekana mitaani huku wananchi wakijiuliza yameanzishwa kwa mujibu wa sheria gani. Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inapenda kupata maelezo ya Waziri juu ya uwepo wa Magari ya Mahakama ambayo tayari yamekuwa *branded* kuwa ni Mahakama inayotembea na wakati huohuo Bunge halijapitisha utaratibu huo kisheria.

**Mheshimiwa Spika,** kifungu cha 11 cha muswada kinachorekebisha kifungu cha 2 cha sheria ya Sheria ya Mahakama za Mahakimu, Sura 11 kinatoa tafsiri ya maneno "mobile court" , "small claim" na "special court" ili kuleta maana ya iliyokusudiwa katika sheria.

**Kambi Rasmi ya Upinzani**, imestuka kidogo na tafisiri na "small claim" au madai madogo, kuwa na madai ambayo thamani yake haizidi shilingi milioni mia moja. Tunaamini hizi ni fedha nyingi na uwakilishi mahakama katika kesi ya madai ya kuanzia milioni ishirini ni muhimu awepo wakili wa kumsaidia mlalamikaji. Kiasi hicho kwa uchumi na mazingira ya Tanzania ni fedha nyingi sana, hivyo basi tunashauri, pindi sheria hizi zinapotungwa tujaribu kuangalia mazingira na hali halisi kesi hizo zitakapokuwa zinaendeshewa. Vinginevyo tunaweza kusema hii ni mbinu nyingine ya kupoka haki badala ya kutoa haki kwa wahusika.

**Mheshimiwa Spika,** tunaamini kabisa kuwa dhana nzima ya uanzishwaji wa mahakama hizi ni nzuri ya kuharakisha mashauri, lakini utaratibu wake bado utakuwa na kasoro

**Mheshimiwa Spika,** kifungu cha 12 cha muswada kinachoongeza kifungu kipya cha 17A, katika sheria mama kwa kuanzisha hizo mahakama zinazohamishika na Mahakama maalum. Kifungu kipya cha 17B kinampa mamlaka Jaji Mkuu kutunga kanuni na utaratibu wa uendeshaji wa hizo mahakama. Kifungu kipya cha 17C kinaongelea kuhusu rufaa za uamuzi utakaofanywa na mahakama tajwa hapo awali

**Mheshimiwa Spika,** kifungu kipya cha 17C(1) kinaeleza kuwa, nanukuu;

> *" No appeal shall lie or be made against a decision or order of a mobile courts or special court in respect of small claims except on a point of law,........"*

Kifungu hiki Kambi Rasmi ya Upinzani inakiona ni kifungu kinachomwondolea mhusika haki yake ya msingi ya kukata rufaa, na ikitiliwa maana kuwa katika mahakama hizi mashauri yanaingizwa katika hatua za mwanzo. Aidha, kifungu hiki pia wadau waliowasilisha maoni yao wametaka kifanyiwe marekebisho kutokana na kasoro kama hizo ambazo tumezibainisha.

**Mheshimiwa Spika,** katika kifungu Katika maelezo ya sababu na madhumuni AG anasema kuwa rufaa zitakatwa mahakama kuu kwa hoja za kisheria tu. Sasa mahakama hizo, kwa mujibu wa kifungu 42A kimezuia uwakilishi kupitia mawakili, sasa nani atabaini hizo hoja za mapungufu ya kisheria ambazo zitakatiwa rufaa kwenda mahakama kuu?

**Mheshimiwa Spika,** Kambi Rasmi ya Upinzani inarudia tena kwamba, lengo la uanzishwaji wa hizi mahakama ni zuri

na hatupingani nalo, ila sheria zinazotoa mwongozo wa utaratibu wa uanzishwaji na utekelezaji wake ndio bado una kasoro kubwa. Kwa kuwa mapungufu yamekwisha bainika wazi kupitia mawasilisho ya wadau kama ambavyo na Kambi imeonesha, hivyo basi ni muhimu marekebisho yakafanyika ili kutoa mwafaka wa pamoja kati na wadau wa hiyo sheria. Tunaamini sheria ikishirikisha wadau wote inapelekea utekelezaji wake kuwa rahisi, na hili litaondoa migogoro ambayo inaweza kutokea kutokana na kunyimwa kwa haki ya rufaa na haki ya uwakilishi wa mawakili.

**Mheshimiwa Spika,** mbali na hilo, marekebisho haya yanamtia matatani mtunga kanuni, ambaye ni Jaji Mkuu, kwani inamlazimisha kutunga kanuni ambazo zinaendana na sheria na vifungu hivi vilivyotungwa na AG kwa utendaji mzuri havitekelezeki. Hivyo Jaji Mkuu analazimika kutunga kanuni kandamizi ili ziendane na sheria inayotungwa kwa mfumo lazimishi wa Serikali na Bunge la CCM.

## 6. SHERIA YA TAKWIMU SURA YA 351

Mheshimiwa Spika, marekebisho yanayopendekezwa kufanyika kwenye sheria ya takwimu ukiyasoma kwa tafakuri, na kwa dhana pana utaona kuwa yamejikita katika kudhitibi tafiti zitakazokuwa zinafanyika na kuwaeleza wananchi matokeo ya tafiti hizo.

**Mheshimiwa Spika,** kwa dhana nyingine ni kwamba mapendekezo haya yanapoteza kabisa dhana ya kufanya utafiti "Social Science Research" na matokeo yake kuwafikia wananchi husika wa tafiti hiyo. Kwani kabla ya kuanza inatakiwa uombe kibali kwa Mtakwimu Mkuu, rejea kifungu kipya katika muswada cha 18(2).

**Mheshimiwa Spika**, kifungu cha 24 cha muswada kinaongeza kifungu kipya cha 24A kwenye sheria ya Takwimu Sura 351 na kifungu hiki kinahusu usambazaji wa takwimu rasmi.

Kifungu cha 24A (1) kinasema kwamba; ***"Any person who is authorized by the Bureau to process any official statistics, shall before publishing or communicating such information to the public, obtain an authorization from the Bureau."***

**Mheshimiwa Spika**, kifungu cha 24A(2) kama kilivyorekebishwa na kusomeka kwamba;

> ***"(2) A person who has different findings from statistics disseminated by the Bureau shall, prior to communicating such findings to the public, consult the Bureau."***

Kifungu hiki kinamlazimisha mtafiti yeyote kabla ya kutoa matokeo ya utafiti wake ni lazima afanye mashauriano na Ofisi ya Takwimu. Kambi Rasmi ya Upinzani, katika hili la mashauriano inaona kuna uwezekano mkubwa kuwa ikawa ni kumwambia mtafiti kurekebisha matokeo ya utafiti uendane na matakwa ya Ofisi ya Takwimu au kufutwa kwa utafiti husika. Kwa ujumla kifungu hiki kina nia ovu na utafiti utakaokuwa unafanywa hapa nchini.

**Mheshimiwa Spika,** lengo la utafiti ni kutafuta suluhisho la tatizo na sio kushindana na Serikali, hivyo wasiwasi wa Serikali unatoka wapi? Hii inazidi kutupa mashaka kwamba kuna uwezekano mkubwa kwamba takwimu zinazotolewa na Ofisi ya Takwimu zina mapungufu ambayo hawataki watanzania wayafahamu.

**Mheshimiwa Spika,** kifungu cha 24B (1) ambacho kina utata sana na kimepingwa sana na wadau wengi, lakini kwa kuangalia au kusoma vifungu vyote viwili **"harmoniously"** utagundua kuwa kifungu cha pili kinasochomeka kuwa;
***"A person shall not disseminate or otherwise communicate to the public any statistical information which is intended to invalidate, distort or discredit official statistics"***

Kifungu hiki hakina maana na hakitakiwi kuwepo kwani tayari kimo ndani ya kifungu cha 24A(1) kwenye maneno,

*"......shall before........, obtain an authorization from the Bureau."*

**Mheshimiwa Spika,** na kama Mwanasheria Mkuu wa Serikali anaona ni muhimu kifungu hicho kiwepo, kinazusha hoja kubwa, ambayo ni, je kuna utafiti unaofanyika kwa lengo maalum la kupingana na tafiti za Serikali au kuzifanya takwimu za Serikali zionekane hazifai? Kambi Rasmi ya Upinzani inaona kuwa mawanda (scope) ya kifungu yanalengo baya maendeleo chanya katika mustakabali wa nchi yetu.

Kifungu hiki kinaikinga Serikali na kuwafanya watendaji wake mara zote wawe kwenye ***"comfort zone"*** yaani wasiweze kuwajibika. Takwimu zozote zitakazotolewa ziwe ni sahihi tu, tukumbuke kwamba wanaofanya kazi hiyo ni binadamu na makosa kwa binadamu ni jambo la kawaida, hoja nyingine ni je, makosa katika takwimu yanaonekana vipi bila kufanya utafiti? Ili nchi iweze kwenda mbele ni lazima kuwe na ***"check and balance"*** kwa upande wa Serikali na taasisi huru.

**Mheshimiwa Spika,** sambamba na kifungu hicho, kifungu kipya cha 24B(2) kinachosomeka kwamba;

> *"A person shall not disseminate or communicate to the public any statistical information without the approval of the Statistician General."*

**Mheshimiwa Spika,** kama ambavyo kifungu cha 24B(1) tulivyoshauri kuwa kifutwe na hiki cha (2) tunashauri kifutwe pia, kwani dhana nzima ni kupata kibali au ruhusa kabla ya kutangaza matokeo ya utafiti. Kwani Watendaji wote katika Ofisi ya Takwimu wanafanyakazi kwa niaba ya Mtafiti Mkuu.

**Mheshimiwa Spika,** ni rai ya Kambi Rasmi ya Upinzani kwamba kifungu hiki kipya cha 24A na 24B vifutwe kwani msingi wake ni wa kudhibiti watafiti wetu katika

kututafutia suluhisho la matatizo yaliyopo katika jamii zetu. Sisi tunaamini kuwa maendeleo ya nchi yanategemea sana tafiti zitakazofanyika ziwe***, "Scientific au Social Science Research".***

## 7. HITIMISHO

**Mheshimiwa Spika,** Kambi Rasmi ya Upinzani kwa ujumla inaona kuwa dhana ambayo ilikusudiwa katika marekebisho yaliyoletwa katika sheria mbalimbali haionekani katika vifungu vya sheria ambavyo vinapendekezwa kutungwa ili kuwa sheria. Jambo hilo linatia wasiwasi sana juu ya nia iliyojificha ya Serikali.

**Mheshimiwa Spika,** tukumbuke kwamba sheria hizi zinatungwa na Bunge letu, na pale ambapo zinaonekana kuwa ni sheria mbaya, kwa maana ya kuwa zina nia/ lengo ovu basi lawama hizo zinarudi kwa watunga sheria ambao ni wabunge. Katika hilo Kambi Rasmi ya Upinzani imetoa mtazamo wake hapo awali wakati tukipitia marekebisho yanayoombwa na Serikali kupitishwa na Bunge.

**Mheshimiwa Spika,** baada ya kusema hayo, naomba kuwasilisha.

..............................
**Ally Salehe(Mb)**
**K.n.y Msemaji Mkuu wa Kambi Rasmi ya Upinzani-**
**Wizara ya Katiba na Sheria.**
**10.09.2018**

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, sasa tunaingia eneo la uchangiaji. Kama ilivyo ada Waheshimiwa Wabunge, mkitumia dakika kumi itakuwa vizuri ili tuwapate wengi kidogo iwezekanavyo. Tuanze na Mheshimiwa Saada Mkuya, atafuatiwa na Mheshimiwa Pauline Gekul. Mheshimiwa Saada!

**MHE. SAADA MKUYA SALUM:** Mheshimiwa Spika, nashukuru sana kwa kupata nafasi hii ingawa sijategemea kama nitakuwa mtu wa mwanzo. Hata hivyo kwa sababu leo ndiyo tunakamilisha marekebisho ya sheria mbalimbali kama ilivyo taratibu.

Mheshimiwa Spika, kwanza nichukue fursa hii kuipongeza sana Serikali, kumpongeza Mwanasheria Mkuu wa Serikali pamoja na Waziri kwa uwasilisho wao lakini vilevile kutokana na uchambuzi mzuri ambao umepelekea sasa kurekebishwa sheria hizi mbalimbali ambazo leo zimeletwa. Katika marekebisho haya kuna sheria kama saba ambazo zinataka kurekebishwa lakini marekebisho haya nilitegemea sana yangefuata ahadi ya Serikali ya kuleta ama marekebsiho ya sheria au taarifa kuhusiana na jambo ambalo tulilizungumza tarehe 28, Juni, 2018.

Mheshimiwa Spika, nimepata faraja kwamba leo uko wewe mwenyewe. Nina *Hansard* hapa ambayo iliendana na majadiliano ya Sheria ya *VAT* ya Mwaka 2014 na katika *Hansard* hiyo tuliongea wengi lakini jambo zuri ambalo nimeliona katika *Hansard* hiyo, naomba kwa ruhusa yako nisome. Tulipokuwa tukichangia na katika uchangiaji huo, Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu, Sera, Bunge, Kazi, Ajira, Vijana na Wenye Ulemavu alizungumza haya:-

"Mheshimiwa Mwenyekiti, ndiyo naendelea huko lakini limegusa pia mioyo ya Wabunge kutoka Bara kwa maana halisi uliyoisema ya huo uwiano wa utozaji kodi." Akaendelea; "Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini ukitazama mfumo mzuri wa kufikia maafikiano ambayo yanaweza kuwa ni maafikiano ya amani na yenye mwelekeo sahihi na hasa linapotokea jambo la namna hii na wakati mwingine ikiwa na mtazamo wa upande wa pili wa Muungano kama vile unanyimwa haki kwa namna moja ama nyingine ni suala ambalo kwa heshima sana sana Kikao chako cha leo Serikali tunaomba utupe nafasi haraka sana tukakutane na wenzetu wa upande wa pili." *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, na akaendelea; *"...kwa sababu kwa upande mwingine..."* Alinyamazishwa, lakini baadaye akaendelea; "Mheshimiwa Mwenyekiti, wakati mwingine inabidi twende tukashughulikie hata kama masuala ya kodi si masuala ambayo yanahitaji kuingizwa na tafsiri ya Kimuungano lakini zipo sheria ambazo zitatakiwa zikafanywie kazi ili kuliweka hili jambo kuwa na *harmony*"

Mheshimiwa Spika, lakini aliendelea na akazungumza kwamba; "Mheshimiwa Mwenyekiti, sisi kama Serikali tutoe hapa, na tunatoa *commitment* tutakapokutana kwenye Mkutano unaokuja jambo hili liwe tumelimaliza kabisa na liwe limepata sura nzuri na tuwe tumeondoa hilo wingu ambalo linaonekana kabisa kwa upande wa pili wa wenzetu unanyanyasika ama kuonewa." *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nimesoma hii *Hansard* kwa sababu niliitegemea sana. Siku ya Ijumaa tumefanya marekebisho ya sheria mbalimbali; leo Jumatatu tunamalizia hiki kiporo cha marekebisho mbalimbali, humu ndani hakuna marekebisho ya sheria ama taarifa ambayo ingesabaisha sasa kuona kwamba ile *commitment* ya Serikali inatekelezwa katika kipindi hiki kama ambavyo iliahidiwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, hili halimo katika haya marekebisho, lakini sisi Wabunge tunapaswa kabisa kuona jambo hili linavyokuwa linaendelea. Hapa ninapozungumza kila mwezi Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar inabidi i-*allocate 700 million shillings* kwa ajili ya malipo ya *VAT.* Hata hivyo, hilo tu siyo jambo lenyewe, tulitoa *commitment* sheria italetwa lakini hata hiyo sheria ya marekebisho ya sheria nimeangalia kwa undani kabisa hata hiyo Sheria ya *VAT* ya Mwaka 2014, *the way* ilivyoandikwa haigusi kabisa kwamba Zanzibar iwe inatozwa *VAT* kwenye umeme. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, sasa ama kuletwe sheria turekebishe tuondoe huu mkanganyiko au kuletwe taarifa. Leo ndiyo tuko mwezi wa Septemba na tunakamilisha *Miscellaneous, we don't see anything.* Serikali iliahidi na tulichukua hiyo ahadi, tuliondoka hapa kwa matumaini

kabisa. Mimi nimerudi Zanzibar kila mtu anasema yaani hii *relief* tutaipata mwezi wa Septemba na niliwaambia kwamba kwa sababu Serikali imetoa *commitment,* tutapata *relief* mwezi wa Septemba. *We are finishing this thing off today,* twende wapi, tuseme wapi? Hakuna hata taarifa ya kusema kwamba haya mambo yanaendelea.

Mheshimiwa Spika, sikuwa na hoja *per se* naungana na Serikali na Miswada au Marekebisho ya Sheria Mbalimbali ilizoleta lakini nimekuwa *disappointed* kuona Sheria ya *VAT* au angalau maelezo yake hayamo kama vile ambavyo tumeahidiwa. *At this point what are we going to do?* Tunafanya nini? Jambo dogo ambalo linakwaza na linasababisha maendeleo yazorote kwa upande mwingine wa Muungano. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, *we are doing a very good job* kwa upande wa *The Government of the United Republic of Tanzania,* lakini kuna vikwazo kama hivi ambavyo *they are just unnecessary blocks.* Mimi naweza nikasema *they are unnecessary blocks* ambazo zinasababisha tukwame. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, wakati wa Kamati, kipindi cha Kamati nilipata bahati ya kuhudhuria kwenye Kamati ya Nishati lakini kwa sababu ya agenda hii, wakati tayari kulikuwa kuna ratiba ya hii agenda upande wa Zanzibar aliitwa Meneja wa Shirika la Umeme, alikuja yeye na wenzake wawili, meneja *at that level,* lakini upande wa Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania waliokuwa wakihudhuria kile kikao; Waziri wa Nishati, Naibu Waziri, Katibu Mkuu, Mkurugenzi Mkuu wa *EWURA,* wa *TANESCO* na wengine. Tulijadili jambo hilo.

Mheshimiwa Spika, bahati mbaya kikao kimefanyika *at the Ministerial level* lakini kulikuwa kuna kikao kingine ambacho bahati mbaya nyingine kulikuwa kunazungumzwa kuhusiana na deni la Zanzibar lakini watendaji ambao wametoka Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar hawakupata nafasi ya kuingia katika maeneo ya Bunge lako kwa sababu

za kiutaratibu, sijaelewa, lakini wakawa -*blocked,* hawakuweza kuingia. *Anyway, my point is,* tumepata *commitment* tarehe 28, Juni, mbona mpaka leo hizi sheria zinakamilika hakuna kitu kwenye sheria hizi za marekebisho ya sheria mbalimbali? Hakuna taarifa, hakuna marekebisho kama ndiyo ambayo yalikuwa yakikusudiwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, yangu yalikuwa hayo. *I'm sorry to say this* lakini kidogo nimepata ukakasi. Nakubaliana na hoja ya Serikali 100 kwa 100 lakini nimekuwa *disappointed* kuona kwamba ile *commitment* ambayo ilizungumzwa tarehe 28, Juni, leo haipo; Ijumaa haikuwepo na leo Jumatatu tunakamilisha *Miscellaneous Amendments* hakuna. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ahsante. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante sana kwa mchango wako. Leo jioni wakati wa kuhitimisha kwa hakika tutataka ufafanuzi ambao ni makini kwa sababu hili jambo tulilizungumza sana humu ndani na tulisema vitu vingine... tutaongea jioni. *(Makofi)*

Mheshimiwa Hawa Mchafu yupo? Makamu wa Mwenyekiti wa Nishati, hayupo. Mheshimiwa Mwenyekiti wa Kamati ya Nishati, pia hayupo. Mjumbe yeyote wa Kamati ya Nishati. Hakuna Mjumbe yeyote wa Kamati ya Nishati, wamesafiri wote? Basi nitalifuatilia kivyangu ngoja tuliache kwanza, nilitaka kujua tu kwamba kuna Watendaji walitoka Zanzibar halafu wakawa *blocked* hapa kwetu. Yaani iweje Kamati iwaalike watu maana hawawezi kuwa walikuja bila kualikwa. Halafu wamekuja mpaka hapa Dodoma halafu wakawa *blocked* getini wasiingie na nina hakika basi waliowaalika ni Kamati sasa ni kwa nini waliwa-*block* ndiyo nadhani sina sababu yaani kukupa mzigo huo ueleze *unless* unalifahamu, kama unalifahamu tafadhali.

**MHE. ZUBEDA H. SAKURU:** Mheshimiwa Spika, nikiwa kama Mjumbe wa Kamati ya Nishati; ni kweli tulikuwa tunamjadala ambao ulikuwa unajadili deni la *ZECO,* lakini ilishindikana kutoka na taratibu zinazosemekana ni chini ya utaratibu wa Ofisi yako. Kwamba watu wa upande ule

hawatakiwi kuhojiwa na Kamati ya upande wa Muungano. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ndiyo Mheshimiwa!

**MHE. AJALI R. AKBAR:** Mheshimiwa Spika, kama alivyochangia Mjumbe ambaye amemaliza sasa hivi ni kweli hivi vitu vingine vinasingiziwa Ofisi yako kimsingi kwa sababu sisi Wajumbe tuliwataka wale watu tufanye *reconciliation* kati ya *TANESCO* Bara na *TANESCO* Visiwani. Lakini ilionekana kwamba Ofisi yako, ndiyo ambayo ilikuwa imeweka *restriction* huo ndiyo ambao ndiyo ulikuwa ndiyo ambao ndiyo msimamo halisi. *(Makofi)*

**SPIKA:** Basi na mimi kama unavyoniona ninavyotoa macho yaani sielewi nashangaa mlikosea kutokurudi kwangu kama Kamati ili nilitolee ufafanuzi jambo hilo. Wakati mwingine watendaji wetu hawa wanapenda sana ku-*block* vitu yaani watu wanafikiri humu Serikalini ukiwa unakwamisha jambo wewe ndo mtendaji mzuri, yaani siyo kwamba wewe ni *facilitator*, ukiwa wewe ni bwana kukwamisha basi wewe ni mtumishi wa Bunge au Serikali *class one* hata katika mambo ambayo yanatakiwa kuyaweka vizuri. *(Makofi)*

Nitalifuatilia kwa karibu na wakati mwingine likitokea jambo kama hilo tafadhali tujulishane haraka sana; kwa sababu tunajenga nyumba moja sisi au siyo watu waliotoka Uganda au waliotoka Sudani Kusini au waliotoka Egypt, hapana ni watanzania na Kamati hizi ni Kamati za kitanzania. Hili ni Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania siyo Bunge la Tanzania kama alivyosema rafiki yangu mmoja hapa asubuhi ya leo.

Mheshimiwa nilishakutaja, Mheshimiwa Pauline Gekul.

**MHE. PAULINE P. GEKUL:** Mheshimiwa Spika nakushukuru kunipa nafasi nichangie machache katika hii *Miscellaneous Amendments*. Nitachangia maeneo matatu naomba nijiekeze kwenye eneo la kwanza nalo ni eneo la

*Amendment* ya *Statistics Act* hiyo *Cap* ya 351 kwenye kifungu cha 31 ambacho kinarekebishwa hicho ambacho kinafanya marekebisho ya 24 A(1) na (2), mimi nijielekeze kwenye (2) inasema hivi: *"A person shall not disseminate or otherwise communicate to the public any statistical information which is intended to invalidate, distort or discredit official statistics*." Pia hoja ni kwamba hizi *statistical information* ni zinatokana na *census surveys or administrative data.*

Mheshimiwa Spika, sikuona sababu sana ya Serikali kuleta marekebisho haya, binafsi naona labda Serikali inakuwa iko *feared* kwamba watu mbalimbali wanapotoa takwimu mbalimbali huenda haziwapendezi sana ndiyo maana wanataka kuweka kapini kuzuia haya. Sanasana hofu yangu iko kwenye *administrative data* ambazo zinatolewa mara kwa mara na huenda haziwapendezi sana wenzetu wa Serikalini ndo maana wanayaleta haya.

Mheshimiwa Spika, hizi *statistical data* ambazo zinatoka kwenye *National Bureau of Statistics* siyo kwamba zote wakati wote ni sahihi. Sasa wanapotaka kuleta marekebisho ya sheria kwamba mtu anapokuwa ana *invalidate* au ana *distort* au ana *discredit official statistics* wakati zina makosa Mheshimiwa Waziri sidhani kama ni *solution* sahihi sana kwa Watanzania.

Mheshimiwa Spika, ni vizuri Serikali ikawa na *open minded* kwamba mtu anaweza akakosoa, lakini wakarekebisha kwa *data* zao. Niwape mfano kwenye *National Bureau of Statistics* ya kwenye Tanzania *in figures* ya mwaka 2016, naamini Mheshimiwa Waziri ata-*refer* na ata-*confirm* hili, Mlima Hanang na bahati nzuri ni mzaliwa wa Hanang nafikiri ana *original* huko, Mlima wa Hanang anaufahamu uliko Mheshimiwa Waziri. Kwenye *National Bureau of Statistics* wanasema mlima huu uko Arusha. Hizi ni *data* ambazo wamekusanya ziko kwenye *figure* zenu, lakini wanasema mlima huu upo Arusha. Mlima Hanang Mheshimiwa Waziri anaufahamu mwenyewe, ndugu zake wanakaa huko, uko Manyara, uko Kateshi, uko Hanang. Hata hivyo, kwenye hizi *data* ambazo ni *official* zimeshafanyiwa

*research* na ziko chini ya hii *Bureau* wanasema Mlima Hanang uko Arusha.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, nafikiri ni vizuri Serikali isiwe inaleta marekebisho kama haya kutafuta tu ku-*pin* Watanzania wasiongee na kutoa takwimu zao; ambazo kimsingi wao kama Serikali wanapaswa kuzirekebisha tu hakuna ugomvi wowote pale anapokosea. Siyo mpaka kuweka adhabu na vitu kama hivyo kuwatisha watu. Labda *otherwise* waniambie ni kwa sababu ya TWAWEZA walivyotoa takwimu kwamba umaarufu wa Rais umeshuka kutoka 90 mpaka asilimia 55, sasa hofu inaingia kuweka mazuio tu ambayo hayana maana yoyote. Kwa hiyo, binafsi naona sababu ya hili na sijui kwanini mnaleta.

Mheshimiwa Spika, nijielekeze kwenye jambo la pili ambalo nataka kuchangia kuhusu suala zima la haya Mabaraza ya Ardhi. Haya mabaraza yamesaidia sana kwenye maeneo mengi. Tatizo lililopo ukiachilia mbali hizo rufaa ambazo lazima waende juu zaidi, tatizo ambalo lipo kwenye haya mabaraza tunafahamu kwamba *staffing* yake hairidhishi. Pia Wenyeviti wa Mabaraza haya kwenye Wilaya siyo Wilaya zote, juzi tu wiki iliyopita Mheshimiwa Lukuvi, Waziri wa Ardhi alijibu kwamba, hata kule kwetu Manyara mfano sasa wana mpango wa kuanzisha mabaraza haya Mbulu. Muda wote mkoa mzima ulikuwa unahudumiwa pale Babati.

Mheshimiwa Spika, Mabaraza haya kwenye Kata hayajawa *strengthened,* siyo Kata zote ambazo tuna Mabaraza haya ya Ardhi, lakini hata uendeshaji wao na mafunzo ndo tatizo; nilifikiri kwamba Serikali badala ya kufanya, hili ambalo wamelifanya binafsi sioni kama ni baya kwamba sasa wanataka Mahakimu Wakazi watusaidie katika kushughulika na hizo rufaa, sioni kama ni tatizo. Tatizo langu ni kwamba tunahangaika na vitu vidogo lakini hatu-*address* tatizo lililopo kwenye Mabaraza ya Ardhi.

Mheshimiwa Spika, kwenye mabaraza haya Wenyeviti wao hawana uhakika wa ajira zaidi ya uteuzi ambao unafanyika na Waziri. Hata hivyo, lakini pia tunachukua muda

mrefu sana mfano kwenye Baraza letu la Wilaya ya Babati, Mwenyekiti amestaafu miezi kadhaa iliyopita mkataba umekwisha, lakini katika *renewal* ya mkataba wake kuna kuwa na umbea mwingi, kuna kuwa na fitina nyingi, kunakuwa na figisu nyingi, kuna kuwa na tuhuma nyingi, kuna kuwa kuchomekeana, kwa sababu labda Mkuu wa Wilaya au Mkuu wa Mkoa amesema hii kesi peleka hivi unavyotaka anapowakatalia kwa mujibu wa taratibu na sheria basi sasa katika uteuzi wake *memo* nyingi zinapelekwa kwa Waziri kwamba huyu asiteuliwe na wanachi wanakosa haki zao.

Mheshimiwa Spika, nafikiri niungane na Maoni ya Kambi Rasmi ya Upinzani kwamba ni vizuri hao Wenyeviti ajira zao zikaangaliwa kwa upya wapewe katika *terms* za *permanent* badala ya hiyo mikataba ambayo wakati mwingine inasababisha kesi zinasimama, lakini wakati huohuo uteuzi unakuwa haufanyiki mapema. Ushauri wangu ni kwamba, ni vizuri kwa sasa Serikali itenge fedha nyingi ili ianzishe mabaraza haya katika wilaya zote itasaidia sana kui-*easen* haya matatizo ambayo tunayapata.

Mheshimiwa Spika, ushauri ambao nataka kutoa pia kama tatizo ni hizi kesi za ardhi, hebu Wizara ya Ardhi tuitengee bajeti ya kutosha ili maeneo mengi yapimwe, migogoro hii ni kwa sababu maeneo mengi katika nchi yetu haijapimwa bado. Hatimiliki za kimila zinatolewa kwa uchache sana, lakini hatimiliki za viwanja na maeneo mengine ni tatizo kwa maeneo mengi na upimaji unakuwa haujafika maeneo mengi. Kwa hiyo tatizo la kuwa-*address* pamoja na kwamba sasa *referral* wanazileta kwenye kwa Mahakimu Wakazi ni vizuri pia wakatenga fedha ili haya yakafika mwisho. Nilitamani kushauri mengi sana kwenye eneo hili lakini naona kama muda wangu hautoshi naomba niende kwenye jambo la tatu.

Mheshimiwa Spika, kwenye jambo la tatu, nataka nizungumzie hizi *Mobile Courts au Special Courts* wamechomoa kipengele hiki wamefanya vizuri; lakini ni vizuri watujibu. Zile gharama ambazo zilikuwa zimeshatumika

kununua magari maana tunasikia walishayaandaa. Hayo magari sasa wanayapeleka wapi? Hii ni hofu yangu tu kwamba, ni vizuri wakati mwingine Bunge letu tukajiangalia kwamba Serikali inakuwa imeshafanya mambo yake, wanataka sisi tuwe *rubber stamp,* wanataka sasa walazimishe vitu kama hivi wakati wao walishafanya maamuzi na inasemekana na hizo *van* wameshazinunua na sidhani kama Bunge hili tuliwapitishia hiyo bajeti, sasa watuambie wanazipeleka wapi?

Mheshimiwa Spika, hofu yangu nyingine, kama walikubaliana nasikia huko wanavyojadiliana kwenye Kamati walishakubaliana mpaka kushusha zile *small claims* mpaka milioni 70, lakini mpaka wameshakubaliana hatua ya kuruhusu ma-*advocate* waweze kuhusika, sasa nini kimewafanya wachomoe? Kwa nini waondoe wakati walishakubaliana? Isije ikawa wanataka kutumia uchochoro wa *Chief Justice* kupitia kanuni wakaanza ku-*practice* hiki kitu wakati huo wameshatuambia kwamba sasa wameondoa, wanaangalia mlango mwingine wa ku-*practice* hiki kitu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kama ilifikia hatua ya nia mbaya kiasi hiki kwamba inafikia kwenye nchi hii mtu tu unaweza ukashtakiwa ukanyimwa haki ya kutokuwa na Wakili kukuwakilisha, yaani hata tu kuthubutu kuwa na nia mbaya kiasi hicho…

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa mzungumzaji)*

Mheshimiwa Spika, nakushukuru.

**SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Pauline Gekul kwa mchango wako, dakika zilizobaki hazitoshi kwa mchangiaji mwingine tutaanza jioni.

Nimemwona Mwenyekiti wa Kamati ya Nishati. Hebu tulikuwa tumekwama jambo fulani, sijui kama ulifuatilia kama unaweza ukatupa mwanga jambo linalohusu Kamati yako.

**MHE. DUNSTAN L. KITANDULA:** Mheshimiwa Spika, bahati mbaya sikulipata vizuri na ndiyo nilikuwa nakuandikia hapa kwa sababu tulikuwa na kikao na Wenyeviti wengine na kikao na Balozi wa Uholanzi. Kwa hiyo, kwa ridhaa yako nitaomba nikuone Ofisi ili niweze kupata kwa uhakika jambo hili na kuweza kulitolea maelezo.

**SPIKA:** Mheshimiwa ni kwamba Kamati yako ilikaa pamoja na mambo mengine kujadili lile suala la malipo ya *ZECO* au ya Zanzibar kuhusiana *VAT* ambao wanatozwa na *TANESCO*. Kamati yako ikawa imemwita Waziri wa Nishati na watu wake na upande wa Zanzibar wakawa wamekuja watu wa *ZECO* na Kamati hiyo ilikuwa ikifanyikia hapa Dodoma katika viwanja vya Bunge inavyosemekana.

Halafu wale Watendaji wa kutoka Zanzibar wakazuiliwa kuhudhuria katika Kamati yako yaani walizuiwa getini. Sasa nataka kujua jambo hili lilikuwaje, ilikuwaje ninyi kama Kamati muwaalike watu watoke Zanzibar waje mpaka hapa, halafu wakazuiliwa!

**MHE. DUNSTAN L. KITANDULA:** Mheshimiwa Spika, ni kweli Kamati ilikutana na Wizara ya Nishati wakati tunapanga ratiba ilionekana ni vyema wawakilishi wa *ZECO* waalikwe na Wizara ya Nishati. Hata hivyo, siku ambayo tunafanya kikao tukapata taarifa vilevile kutoka kwenye Ofisi ya Bunge kwamba kulikuwa hakuna kibali cha kufanya mazungumzo na watu wa *ZECO*. Kwa hiyo, tuendelee na watu wa Nishati wakati utaratibu mwingine unaendelea.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, tulifanya mazungumzo na Wizara na wakatueleza maendeleo ya jambo hilo linavyokwenda na kimsingi Kamati hatukuridhishwa na *speed* ya jambo hili linavyoshughulikiwa, tukaipa maagizo Wizara kwamba vyovyote itavyokuwa ikifika mwezi Novemba, basi jambo hili liwe limefika mwisho kwa sababu ni jambo la muda mrefu ambalo linaonekana halishughulikiwi kwa kina. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ni hayo. *(Makofi)*

**SPIKA:** Nakushukuru sana ni *weakness* ya utendaji kwenye Ofisi yangu, nitaifuatilia. Nafikiri Makatibu mnaniangusha ninyi, Kamati walikubaliana kwamba Wizara wawaalike *ZECO* waje kama ni sehemu ya *entourage* ya Wizara, ninyi Bunge mnakataa kama nani? Linawahusu nini? Sasa hebu mambo mengine tusiwe tunaenda hivyo, Bunge lina heshima yake hili, asitokee mjanja mjanja fulani hataki jambo fulani liwe anasingizia huku kwenye Bunge na ninyi mnatumika kwa ajili ya mambo ya kipuuzi. *(Makofi)*

Kwa sababu kama Waziri anakuja na hawa watu anakuja nao yeye mwenyewe unafikiri yeye kwenye kikao hicho ndiyo anaanza kukaa nao hapo? Si maana yake lazima walishakaa huko, wanapokuja kwenu wameelewana, wanaelewa wanachokuja kusema kwenye Kamati, kwani ndio wanakutana hapohapo. Sasa ninyi Bunge kuwazuilia, mnazua kwa faida gani sasa? Haya Makatatibu tuambie sasa mambo ya Zanzibar, jibuni ninyi sasa. Ni matatizo madogo madogo tu, yuko mtu alifanya mambo ya hovyo sasa siwezi kujua kwa sasa hivi ni mapema mno, lakini jambo kama hili nawaaihidi halitajirudia tena, ni jambo la hovyo tu. *(Makofi)*

Waheshimiwa tutaendelea saa 11jioni, nasitisha shughuli mpaka wakati huo na wachangiaji watapata nafasi wala msiwe na wasiwasi, ataanza Mheshimiwa Damas Ndumbaro na wengine mtafuata msiwe na wasiwasi.

*(Saa 7.00 Mchana Bunge lilisitishwa mpaka Saa 11.00 Jioni)*

*(Saa 11.00 Jioni Bunge lilirudia)*

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge tukae. Tunaendelea, Mheshimiwa Dkt. Damas Ndumbaro na atafuatiliwa na Mheshimiwa Abdallah Mtolea. Mheshimiwa Ndumbaro.

**MHE. DKT. DAMAS D. NDUMBARO:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana kwa kunipa nafasi ili niweze kuchangia Muswada huu wa Marekebisho ya Sheria Mbalimbali Na.3

wa mwaka 2018. Muswada huu unafanya marekebisho kwenye sheria tano mbalimbali ambazo zinajumuisha jumla ya vifungu 27. Ningeomba nichangie kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, suala la kwanza, niwapongeze sana Serikali kwa kuja na mapendekezo mazuri sana. Ukisoma Muswada huu katika sehemu yake ya pili, ya tatu na ya nne ambayo inarekebisha Sheria ya Mahakama ya Rufaa, Sheria ya Mwenendo wa Kesi za Madai pamoja na Sheria ya Utatuzi wa Migogoro ya Ardhi, kwa ujumla wake vimeleta kitu kipya katika mfumo wa Sheria, lakini kitu kipya ambacho ni kizuri i.

Mheshimiwa Spika, moja kati ya changamoto kubwa katika uendeshaji wa kesi mbalimbali imekuwa ni mbinu za kisheria ambazo zinatumika Mahakamani na baadaye zinapelekea kunyima haki. Sasa katika sehemu hizi tatu yamekuja mapendekezo kwamba mbinu hizi za kisheria *(legal technicalities)* ziwekwe pembeni sasa ili kuhakikisha kuwa haki inapatikana, tena kwa haraka, kwa uwiano sawia na kwa gharama nafuu. Ni wazi kabisa kwa mtu yeyote ambaye amewahi kujeruhiwa na mbinu za kisheria huko Mahakamani atapokea mapendekezo haya ya Serikali kwa mikono yote miwili. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Sehemu ya Nne pia inaongelea kuwapa Mamlaka Mahakimu wa Mahakama za Hakimu Mkazi ili waweze kusikiliza rufaa zinazotoka kwenye Mabaraza ya Ardhi ya Wilaya kama vile Majaji wa Mahakama Kuu. Tunaongelea hapa Kifungu cha 41A ambacho kinatoa Mamlaka sasa kwa Mheshimiwa Jaji Mkuu kuwateua Mahakimu wa Mahakama za Hakimu Mkazi kuweza kusikiliza rufaa kama Mahakama Kuu yaani kitaalam inaitwa *extended jurisdiction.*

Mheshimiwa Spika, hii ni muhimu sana, inakwenda kutibu ugonjwa mkubwa sana wa ucheleweshaji wa rufaa za ardhi ambao umekuwa ukilalamikiwa na kila mtu. Katika mashauri mbalimbali yanayohusiana na ardhi rufaa zake zimekuwa zikichelewa kutokana na uhaba wa Majaji wa Mahakama Kuu sasa zile rufaa zinazohusiana na ardhi

zitakwenda sasa kwa Mahakimu ili ziweze kushughulikiwa kwa haraka zaidi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, suala lingine ambalo napenda kuliongelea katika Muswada huu ni kwamba sasa Sheria imeweka tahafifu zaidi kwa rufaa katika masuala ya ardhi. Endapo kesi itaanzia Mahakama Kuu kwa hivi sasa, mtu akitaka kukata rufaa kwenda Mahakama ya rufaa hahitaji tena kuomba kibali cha Mahakama Kuu. Hapa tunarudi kule kule, tunaondoa zile *legal techinicalities* ambazo zimekuwa zikiwasumbua watu kwa muda mrefu. Kuomba kibali kutokwenda Mahakama ya Rufaa ni kazi ngumu sana, inachukua muda mwingi sana, inachukua fedha nyingi sana hivyo kupoteza haki. Tunaipongeza Serikali kwa kuamua kufanya mabadiliko haya kwenye Kifungu cha 47(1) ili kupunguza urasimu huo ambao utasaidia kuokoa muda, fedha na hatimaye kuleta haki kwa warufani mbalimbali.

Mheshimiwa Spika, pia ningeomba kuongelea Sheria ya Baraza la Michezo Tanzania, Sura ya 49. Kuna mambo mengi yemeingizwa lakini ningeomba niliongelee kwa ufupi suala moja; kutambua kwamba sasa hivi michezo yetu siyo michezo ya ridhaa pake yake. Tumeshafikia kwenye michezo ya kulipwa katika ngumi, soka na michezo mingine, lakini sasa tulikuwa tumefungwa na sheria. Sasa hivi mabadiliko haya yanakwenda kutambua na inapokuwa ni michezo ya kulipwa maana yake vijana wetu tunawapa ajira zaidi, tunatoa fursa, kwa hiyo, haya ni mabadiliko mazuri sana ambayo Serikali imekuja nayo.

Mheshimiwa Spika, katika Sheria hiyo, tunaiomba Serikali ifikirie katika siku zijazo, tena ikiwezekana za hivi karibuni, kuleta mabadiliko ambayo yataingiza utatuzi wa migogoro katika sekta ya michezo, kwa sababu sekta ya michezo sasa hivi ina migogoro mingi na utatuzi wake umekuwa ukibakia katika sekta husika kwa kutegemea Katiba zao.

Mheshimiwa Spika, hizo Katiba zinaleta matatizo zaidi kuliko kutatua matatizo. Ni wakati sasa Serikali ifikirie kuanzisha

chombo cha usuluhishi wa migogoro ya michezo cha Kitaifa ambapo migogoro yote ya michezo ikishashindikana katika vyama vyake husika ama endapo mgogoro huo unamhusu mwanachama na chama chenyewe, basi uletwe kwenye hicho chombo cha kitaifa cha kusuluhisha migogoro.Mabadiliko haya yanakwenda mbali zaidi, yanaongelea Sheria ya Takwimu. Ningependa kuongelea tafsiri ambayo imeongezwa ya maneno *"official statistics* na *statistical information"* ambayo hayakuwepo hapo awali, lakini kwa sasa hivi maneno haya yameongezwa na kuongeza maneno hayo yameleta tafsiri nzuri zaidi ambayo haikuwepo hapo awali.

Mheshimiwa Spika, kwa ujumla Serikali imekuja na mapendekezo mazuri sana hata sisi tuliokuwa kwenye Kamati tuliyaunga mkono karibu yote na tulifikia kwenye hatua nzuri sana, hivyo naomba kuunga mkono hoja. Ahsante. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Dkt. Damas Ndumbaro, Mbunge wa Songea Mjini. Kama nilivyokwishataja Mheshimiwa Abdalah Mtolea ndiye anayefuata na baadaye atafuatiwa na Mheshimiwa Asha Abdallah Juma.

**MHE. ABDALLAH A. MTOLEA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi nitoe mchango wangu katika Muswada ulio mezani hii leo.Nianze na nyongeza iliyowekwa ya Kifungu cha 41(A) kwenye Sheria ya Mahakama ya migogoro ya ardhi.

Mheshimiwa Spika, nahisi ni *typing error* na siyo kwamba ndivyo walivyokuwa wamekusudia, wanasema kwenye Kifungu hiki kwamba Jaji Mkuu kwa kushauriana na Waziri wa Sheria na Katiba na Mwanasheria Mkuu, wakishashauriana ndiyo wanaweza kuruhusu kutoa tangazo kwenye Gazeti la Serikali juu ya hii *extended jurisdiction.* Kitendo cha kusema Jaji Mkuu kwa kushirikiana na Waziri wa Katiba na Sheria na Mwanasheria Mkuu peke yao maana yake wanamweka nje Waziri wa Ardhi na kwenye Sheria zote za ardhi anatajwa mtu wa kufanya naye *consultation* ni

Waziri. Waziri kwenye Sheria hizi anakuwa ni Waziri mwenye dhamana na masuala ya ardhi.

Mheshimiwa Spika, sasa hapa wamekwenda moja kwa moja kwa kusema kwamba ni Waziri wa Katiba na Sheria ambavyo ukishamtaja Mwanasheria Mkuu yuko mle *it is automatically* kwamba Waziri wa Katiba na Sheria na yeye yumo. Kwa hiyo, walioachwa hapa ni Waziri wa Ardhi na tukikubali ibaki hivi maana yake sasa Waziri wa Ardhi yeye atakuwa anasikia tu tangazo limetolewa gazetini la kufanya marekebisho kwenye mambo ambayo yeye anayasimamia lakini hakushauriwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kipengele hiki nafikiri kimekaa vibaya sasa na kwa bahati mbaya sikufanya *amendments* na hapa ilitakiwa tu ibaki Waziri, isiwe Waziri wa Katiba na Sheria. Kwa hiyo ni vizuri wakaliangalia hili ka tafsiri zao wasomi waone wataiondoa hiyo ya Katiba na Sheria ibaki Waziri tu ili awe anaingia Waziri wa Ardhi. Atakuja kujibu Mheshimiwa Waziri asiwe na midadi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, bado tatizo letu linarudi pale pale; ijumaa nilikuwa nachangia hapa kwamba hizi fursa za kufanya *amendments* kwenye hizi Sheria hatuzifanyi ipasavyo, tunadonyoa donyoa tu. Kwa mfano; unapokuja kugusa sheria inayohusu migogoro ya ardhi, migogoro ya ardhi katika nchi hii ni mingi kweli kweli, kesi za ardhi ni nyingi sana. Wananchi wanaonewa kweli kweli kwa sababu wka sasa kesi za ardhi ni kati ya wenye fedha dhidi ya wasiokuwa na fedha ndiyo migogoro ya ardhi, lakini hii inatakiwa ianzie kwenye Baraza la Ardhi la Kata. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Baraza hilo ukimkuta mtu amesoma sana atakuwa amemaliza darasa la saba, lakini wengi wanaochaguliwa kuunda hayo Mabaraza siyo watu wenye weledi mkubwa wa mambo ya kijamii tu, mambo ya kawaida, wala hayo mambo yenyewe ya ardhi, lakini kesi ndiyo zianzie huko. Pia hata mazingira wanayofanyia kazi siyo rafiki ya kuonesha kwamba haki pale inaweza kutendeka. Anaweza akaja mmoja kati ya wanaogombana, yeye kwa

sababu ana hali nzuri ya kifedha ndiyo atagharamia hicho kikao, ndiyo atawabeba hao wajumbe kwenye gari lake kwenda kwenye *site* kupima hiyo mipaka, wakati huo mlalamikaji au mlalamikiwa mwingine ambaye hali yake ni hohe hahe na yeye ataomba *lift* humo humo. Katika mazingira ya namna hiyo huwezi kutegemea haki itendeke.

Mheshimiwa Spika, sasa tulitegemea wanapokuja na Muswada kwenye ardhi, maana yake mngekuja na Muswada ambao unakwenda sasa kumaliza tatizo la migogoro ya ardhi, lakini badala yake wamekuja kugusa vipengele vichache sana ambavyo bado haviwezi kutatua msongamano wa kesi za ardhi zilizoko kwenye Mabaraza ya Kata, zilizopo kwenye Mabaraza ya Wilaya, kwa sababu hata akimpa mamlaka huyu Hakimu Mkazi bado anataka tu aondoe lile rundo la kesi lililopo kwenye Baraza la Wilaya lihamie kwake. Hii bado haiwezi kumaliza migogoro.

Mheshimiwa Spika, sasa tulitaka kwanza walete Sheria ya kuondoa mfumo uliopo sasa kwamba kesi ziwe ni kesi, zishughulikiwe na Mahakama za kawaida, waziwezeshe mfumo wa Mahakama wa kawaida ndiyo ushughulikie hii migogoro ya ardhi, kwamba watu badala ya kuanza kwenye Mabaraza ya Kata ni afadhali waanze kwenye Mahakama za Mwanzo endapo watazipa nguvu hiyo ili zianze kushughulikiwa kisheria kuanzia hatua ya awali. Leo zinashughulikiwa kienyeji kwenye hatua ya awali, halafu hilo *file* ndiyo linakwenda mpaka Mahakama Kuu mpaka Mahakama ya Rufaa, watu wana-*refer* kwenye vitu ambavyo vilifanywa na watu ambao hawa weledi wa mambo ya ardhi.

Mheshimiwa Spika, sasa hivi kesi za ardhi hazihitaji tu haya mapatano ya kawaida, zinahitaji sana usuluhishi wa kisheria. Sasa lazima tuisaidie nchi hii kwa kuweka sheria ambazo zitamsaidia mwananchi. Juzi wakati Rais yuko Serengeti alikutana na mama mmoja akimlilia kuhusu alivyodhulumiwa haki zake za ardhi. Sasa huyo ni yule ambaye alipata fursa ya kuonana na Mheshimiwa Rais akapeleka kilio chake na Mheshimiwa Rais kwa uchungu

sana akaona kweli hapa pana tatizo. Watu wa namna hii wako wengi sana katika nchi hii ambao haki zao zinapotea, lakini hayo Mabaraza ya Kata yanaingiliwa sana na Wanasiasa na wateule wengine mbalimbali. Ziko kesi zinashughulikiwa kwenye haya Mabaraza anakuja Mkuu wa Wilaya anasema hiyo kesi isimame na kweli inasimama.

Mheshimiwa Spika, kwa mfano, pale Dar es Salaam, Mkuu wa Mkoa aliwahi kuyazuia Mabaraza yote ya Ardhi Dar es Salaam yasifanye kazi na yalikaa kimya karibuni mwaka mzima, yanavyokaa kimya haki za watu zinapotea. Sasa tulitegmea mkwamo huu, matatizo haya yataondolewa na mabadiliko ya kisheria kwenye mfumo ambao tunaishi nao, lakini wasomi wanakuja hapa hawagusi huko bado wanatuachia migogoro ya ardhi iendelee kutatuliwa na Mabaraza ya Kata ambayo watu hawana uwezo huo.

Mheshimiwa Spika, sasa hili ni tatizo na tatizo hili ni kubwa sana kwenye hizi *amendments*. Kila zinapokuja hizi *amendments* hazimalizi matatizo. Kwa hiyo, tusaidie siku nyingine tukatae yakija marekebisho hapa yanadonyoa donyoa tu vitu viwili, vitatu tuseme hapana, hebu waende wakajipange waje hiyo sheria waifanyie marekebisho yote. Kwa mfano, wamegusa hapa suala la kuondoa *techinicaliries* kwenye Mahakama. Ni jambo jema sana kwa sababu kweli kulikuwa na mkwamo mkubwa, ilikuwa sasa hivi ukienda Mahakamani husikilizi tena watu wakibishana kuhusu ku-*prove* tatizo liko wapi, bali wanabishana kwenye *technicalities,* kwa hiyo iliondoa ladha kabisa ya kwenda Mahakamani.Sasa kama hili limeondolewa ni jambo jema, sasa kwa nini na huku wasifanye hivyo?

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo tunayoyategemea kutoka kwa Waziri wa Katiba na Sheria, Mheshimiwa Profesa Kabudi, ni makubwa sana kuliko anayotuletea. Tunayotegemea kutoka kwa Mwanasheria Mkuu ni makubwa sana kuliko ambayo anatuletea hivi sasa. Kwa hiyo, ni vizuri waisaidie nchi hii kwa kuondoa matatizo ambayo yapo kwenye masuala haya ya kisheria.

Mheshimiwa Spika, nakushukuru. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Abdallah Mtolea. nilishakutaja Mheshimiwa Asha Abdallah Juma.

**MHE. ASHA ABDULLAH JUMA:** Mheshimiwa Spika, ahsante kunipa nafasi hii kwa leo ili kuweza kuchangia katika Muswada huu wa marekebisho ya Sheria mbalimbali, Sheria Na.3 ya mwaka 2018.

Mheshimiwa Spika, nianze kwanza kwa dhati kabisa kuipongeza Serikali kwa kupitia kwa *AG* na timu yake kwa kuweza kuleta marekebisho haya. Inaonyesha dhahiri kwamba Serikali imejipanga kuondoa mapengo pengo, mashimo shimo yote yaliyokuwemo kidogo kidogo katika Sheria. Unapoleta marekebisho ina maana kuna upungufu fulani na hii ni nzuri. Kwa hivyo nipongeze hiyo timu ya *AG* pamoja na Kamati yetu ambayo pamoja na wadau wengine wamefanya kazi kubwa sana ya kuchambua Muswada huu na kuweza kuuleta hapa, ambao utakidhi kwa kiasi kikubwa kuondoa zile kasoro ambazo zilikuwepo.

Mheshimiwa Spika, kwanza nianze kwa kutazama marekebisho katika ile Sheria ya Mamlaka ya Rufaa, Sura ya 141 hapa kwa kweli inaonekana Serikali hii imedhamiria kushughulikia tatizo katika usikilizaji wa mashauri na kuweka urahisi…

**SPIKA:** Mheshimiwa Asha sekunde tu.

**MHE. ASHA ABDULLAH JUMA:** Naam!!

**SPIKA:** Simama kidogo kuongea. Nilitaka nichukue fursa hii kuwajulisha Waheshimiwa Wabunge wote kwamba Mheshimiwa Waziri Mkuu tuko naye, amerudi salama safari yake ya kutoka China. Tunatumaini atapata siku hapa atueleze habari za China huko na kama aliweza kula chura na nyoka kidogo ameona wana-*taste* ipi. Mheshimiwa Asha endelea sasa. *(Makofi/Kicheko)*

Mheshimiwa Spika, katika sheria hii, wamefanya marekebisho ili kurahisisha na kuwezesha kuondoa zile *technicalities* ambazo zilikuwa zinazuia au zinaongezea urasimu katika kumalizia kesi. Kwa mfano, mara nyingi ilikuwa mtu anaambiwa kesi yako imetupwa, hujafanya hiki, hujafanya hiki, kitu ambacho kidogo kilikuwa kinapelekea watu kukosa haki zao. Kwa hiyo, marekebisho haya yatawezesha Majaji na Mahakimu bila kukwazwa na vipingamizi hivyo kuendeleza mashauri na kuyamaliza kwa haraka na pia kuwapatia haki zao wale wanaohitaji kwa wakati, bila kuchelewa. Vilevile itaweza kumalizia mashauri hayo kwa haraka zaidi kuliko ilivyokuwa siku za nyuma. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, sheria nyingine ambayo imefanyiwa marekebisho ni hii Sheria ya Ardhi, Sura ya 216. Hii vilevile imeongezea Mahakimu uwezo wa kusikiliza kesi za ardhi zinazotoka kwenye Mabaraza ya Ardhi na kuzipatia maamuzi haraka. Tunambua kwamba huko kwenye suala la ardhi ndiko kwenye migogoro mingi sana; matatizo mengi ambayo yanawakumba wananchi ni migogoro katika kugombea ardhi au kutofautiana katika ardhi. Kwa hiyo, marekebisho haya yanatoa nafasi kwa mashauri haya kumalizwa kwa haraka sana.

Mheshimiwa Spika, sheria nyingine ni hii Sheria ya Takwimu, Sura 351. Tumeiona ni muhimu sana kwamba kuwe na udhibiti, mtu asiweze ku-*publish*; ku-*publish* ni nini?

**MBUNGE FULANI:** Kuchapisha.

**MHE. ASHA ABDULLAH JUMA:** Mheshimiwa Spika, kuchapisha bila kupitisha kwenye Ofisi ya Mtakwimu Mkuu ambaye ndiye mwenye mamlaka ya kuona hizo takwimu ndiyo stahiki, mtu yeyote yule atabidi apitie huko. Hilo ni jambo nzuri kwa ustawi wa nchi, kwa sababu vinginevyo zinaweza kupatikana takwimu ambazo siyo sahihi na mtu akaweza kuzichapisha zikaweza kuitia nchi yetu katika matatizo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, vilevile iko Sheria ya Mahakama za Mahakimu, Sura 11. Hapa Serikali ilipendekeza *mobile courts* ambazo kwa kweli tumeridhika sana, baada ya ushauri, Serikali imeondoa mapendekezo haya ya kutaka kuleta *mobile courts,* kwa sababu kwa kweli kwa sasa hivi zingekuwa mzigo zaidi, kwa sababu hizi Mahakama zilizopo ni nyingi pia. Hizo gharama ambazo tuliona kama zingetumika kutengeneza hayo magari ya *mobile courts* zingekuwa kubwa. Ni bora kujenga majengo ambayo yanaweza yakatumika kwa Mahakama au kama Mahakama kesi zimemalizika, tumeshakuwa watu wazuri, basi zitatumika kwa kazi nyingine kama vituo vya afya au *libraries* kuliko kutumia fedha nyingi hivi kuanzisha *mobile court*. Kwa hilo, Serikali tunaipongeza, ilikubaliana na Kamati ikaliondoa pendekezo hilo. Sasa siku za mbele sijui tena kama itaona kuna haja, itakuja kuirudisha lakini itatuambia hivyo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, sheria nyingine ni hii ya Baraza la Michezo, Sura 49. Kwa kweli kulikuwa hakuna sheria ya kusimamia vyama vya michezo. Serikali imeona hilo na ni kweli kwa sababu michezo siku hizi ni tija na ni kitega uchumi, kwa hiyo, lazima kuwe na watu watakaokuwa wanasimamia.

Mheshimiwa Spika, vilevile hili suala la *sportingbet* siku hizi imeenea sana na inaonekana kupata pesa nyingi sana, lakini hakuna sheria inayoidhibiti. Kwa hiyo, Serikali pale ikiingiza mkono wake, itaweza kuyachunga vizuri mapato na kuchunga haki za wenye sheria hiyo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nafikiri kwa mchango wangu huo, naona kama inatosha, niwaachie wenzangu wengine. Naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Asha Abdallah Juma. Mheshimiwa Halima Mdee.

**MHE. HALIMA J. MDEE:** Mheshimiwa Spika, nashukuru. Kwanza, napongeza taarifa ya Kamati ya Bunge ya Katiba na Sheria kwa kitendo chake cha kuzuia Sehemu ya Tano

ambayo ilikuwa inafanyia marekebisho *The Magistrate Court Act* na kuruhusu Jaji Mkuu kwa mapendekezo yake ama kwa maslahi ya umma kwa kadri atakavyoona inafaa kuanzisha Mahakama Maalum na Mahakama za kuhamishika. Ni imani yangu kwamba hii Sehemu ya Tano iliyoondolewa ambayo kwa bahati mbaya sana ilikuwa inampelekea Jaji Mkuu kuunda Mahakama kupitia *regulations* mbalimbali na kusema kabisa hizi Mahakama zitamsimamia nani kwa utaratibu gani?

Mheshimiwa Spika, kama Bunge litaruhusu kwa njia ya pembeni, kwa sababu tumeambiwa hapa leo asubuhi kwamba tayari magari husika yameshanunuliwa, zimetumika shilingi bilioni 48, kila gari shilingi milioni 350 na fedha hizi ni mkopo kutoka Benki ya Dunia. Swali langu kwa Mheshimiwa Waziri, Kamati ya Bunge imesema hii Sehemu ya Tano isipitishwe, hivyo vifaa vilivyonunuliwa vinaenda kufanya kazi gani? Isije ikawa tumepigwa changa la macho kama Bunge, tunaambiwa hili suala tumelitoa, lakini linaenda kuingilia kwa upande wa nyuma. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, sasa Mheshimiwa Waziri atuambie kwa sababu Mwenyekiti wa Kamati amesema hapa kwamba magari yameshanunuliwa. Mjumbe wa Kamati amesema hapa kwamba magari yameshanunuliwa. Mkopo wa Benki ya Dunia siyo bure, ni mkopo ambao Watanzania tunaenda kuulipa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, wote tunajua tokea Awamu ya Tano imeingia madarakani, kiwango cha kukopa cha nchi hii kimeongezeka katika kiwango ambacho haijawahi kutokea katika historia ya nchi hii. Kwa hiyo, haiingii akilini, wananchi wanaonyeshwa vitu, hivyo vitu vinaonekana kama vina tija tukijiaminisha kwamba tunatumia fedha zetu za ndani, kumbe watoto, wajukuu na vitukuu watalipa mzigo mkubwa sana. Sasa tunataka Mheshimiwa Waziri atuambie kwa *cost benefit analysis,* hii shilingi milioni 350 kwa gari ambalo *life span* yake ni miaka mitano tu au miwili, kwa sababu ni magari tu yanayo-*move*, huu mzigo wa matumizi mabovu ya fedha za umma ataubeba nani? *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nikija kwenye hoja nyingine kuhusiana na hii Sheria ya Takwimu. Kwa mtu yeyote mwenye akili timamu anajua mabadiliko haya ya kuongeza kifungu cha 24A na kufanya mabadiliko ya kifungu cha 37, malengo yake ni udhibiti. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, wanasema kwamba utafiti hauwezi kutolewa kwa umma bila *approval* ya *Bureau.* Wakati *TWAWEZA* walivyokuwa wakimsifia Mheshimiwa Dkt. Magufuli, kwamba anakubalika kwa asilimia 90, anakubalika kwa asilimia 77, hakuna mtu aliyeona kwamba ni shida hizi tafiti. Mara moja tu baada ya *TWAWEZA* kusema Rais ameporomoka kutoka asilimia 90 huko mpaka asilimia 50 imekuwa nogwa. Hivi imefika nchi hii sasa hivi watu inakuwa kutoa maoni kwamba mtazamo wa nchi, Watanzania mmoja, mmoja wanaona ni hivi, imekuwa ni nogwa! *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hili Bunge ni kwa bahati mbaya sana na sisi tumezubaa tunaingiliwa. Juzi Mwenyekiti wa Kamati ya Bajeti amebadilishwa. Yeye atasema kwamba ameamua.

**MHE. JAKU HASHIM AYOUB:** Taarifa, taarifa.

**SPIKA:** Nilisikia taarifa mahali. *(Kicheko)*

**MHE. JAKU HASHIM AYOUB:**Kuingiliwa, aah!

**MHE. HALIMA J. MDEE:** Mheshimiwa Spika...

**SPIKA:** Nilisikia taarifa kidogo. *(Kicheko)*

**MHE. HALIMA J. MDEE:** Mheshimiwa Spika, muda wangu.

*(Hapa Baadhi ya Waheshimiwa Wabunge waliongea bila mpangilio)*

**SPIKA:** Maana kuna Kiswahili cha Bunge kuingiliwa, sijui kama kinakubalika hasa kutoka Zanzibar. Mheshimiwa Jaku, kinakubalika Kiswahili hicho? *(Kicheko)*

**MHE. JAKU HASHIM AYOUB:** Mheshimiwa Spika, kidogo dada yangu Mheshimiwa Halima Mdee, unajua Kiswahili kina maana nyingi hasa sisi watu wa Pwani hebu tutafsiria kuingiliwa wapi? Hilo tu.

**WABUNGE FULANI:** Aaaaa.

**SPIKA:** Mheshimiwa Halima futa hiyo bwana. *(Kicheko)*

**MHE. HALIMA J. MDEE:** Mheshimiwa Spika, hoja yangu nini?

**SPIKA:** Weka sawa hiyo Mheshimiwa Halima.

**MHE. HALIMA J. MDEE:** Mheshimiwa Spika, Bunge ndiyo chombo cha kusimamia Serikali. Hii sheria imeletwa, narudia, lengo ni kudhibiti ili ukiletwa utafiti wowote ambao unaenda kinyume na maslahi mapana ya Serikali ya Awamu ya Tano, utafiti hautatoka kwa umma. Ni kwa bahati mbaya sana wameleta hapa haya mabadiliko hawajasema kama hii *Bureau* isikubali huu uchapishwaji utolewe, *remedy* ni nini kwa huyu mtu au kwa hiki chombo kilichofanya utafiti? *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, sasa hivi narudia, Bunge lako limedhibitiwa, linaingiliwa. Sasa hivi Katiba ya nchi inavunjwa, vyama vya siasa vimedhibitiwa, sasa hivi Mahakama zimedhibitiwa. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Halima hebu *substantiate,* mbona unatoa madai makubwa. Unamwona Shekhe Masoud amekaa hapa, unasema kwamba Bunge limeingiliwa, anashangaa nini unasema. *(Kicheko)*

**MHE. HALIMA J. MDEE:** Mheshimiwa Spika, ngoja niseme hivi, tumeshuhudia juzi Mwenyekiti wa Kamati ya bajeti, Mheshimiwa Hawa Ghasia, yeye najua atasema

kwamba amejiuzulu kwa matamanio yake mwenyewe, lakini sisi wenye akili timamu tunajua ni kwa sababu alivyosimama na korosho. Tunajua akaletwa Mjumbe mwingine kutoka kwenye nje ya Kamati, akawekwa pale. *(Makofi)*

**SPIKA:** Hilo siyo kweli. Huwezi kumsemea mtu. Mheshimiwa Halima...

**MHE. HALIMA J. MDEE:** Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, hizi sheria...

**SPIKA:** Mheshimiwa Halima unaingia kwenye uwanja ambao huna ushahidi nao. Sasa wewe ndiyo unakuwa na maneno ya kuzusha tena. Mimi taarifa nilizonazo tulizisema, kwamba Mheshimiwa ameachia ngazi yeye mwenyewe na siyo kwamba ameingiliwa, hapana, hakuna vitu vya aina hiyo. Kwa hiyo, habari za *speculations* tuziache, hazina maana hata kidogo. Malizia dakika zako, halafu nyoosha Kiswahili, kile Kiswahili kingine kile, naona mashekhe wanapata shida hapa. *(Makofi)*

**MHE. HALIMA J. MDEE:** Mheshimiwa Spika, hoja yangu ni ndogo tu, kwamba sisi kama Bunge tuna jukumu kubwa la kuisimamia Serikali. Tuna jukumu kubwa la kuhakikisha kwamba, sheria zinazoletwa kwenye Bunge hili zina lengo siyo la kulinda mtu ambaye yuko kwenye madaraka, siyo kusaidia chama ambacho kiko kwenye madaraka, ila ni sheria ambazo zitaisaidia nchi. Hiyo ndio hoja yangu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kama Bunge tutashindwa kusaidia nchi, hii nchi ikivurugika, hakuna atakayepona, ndiyo hoja yangu hapa. Hoja yangu hapa ni kwamba huu Muswada wa Takwimu tunaambiwa kwamba, kwa mfano, mtu yeyote ambaye atachapisha bila ruhusa atakuwa amefanya kosa na adhabu yake siyo pungufu ya shilingi milioni kumi au kifungo kisichopungua miaka mitatu au vyote viwili.

**WABUNGE FULANI:** Duuuh.

**MHE. HALIMA J. MDEE:** Hebu firikia tuna taasisi hii, ina vigezo vyake imeenda kuomba kibali, imepata kibali imefanya utafiti, imeenda kusema utafiti huu, mwenye mamlaka amekataa kutoa ruhusa... *(Makofi)*

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa mzungumzaji)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Halima ni kengele ya pili, nashukuru sana. Utapata ufafanuzi tu, wala hamna shida.

Tunaendelea na Mheshimiwa Edwin Ngonyani, atafuatiwa na Mheshimiwa Cecil Mwambe na Mwenyekiti wa Kamati atatufungia Mheshimiwa Mchengerwa.

**MHE. ENG. EDWIN A. NGONYANI:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi hii. Nachukua fursa hii kuwapongeza sana mwenzetu walioko Serikalini na hasa Waziri wa Sheria na Katiba pamoja na Mwanasheria wake Mkuu na timu yote iliyoko katika Wizara ile. Hiki walichotuletea kimekuja kwa wakati muafaka.

Mheshimiwa Spika, nawashukuruni sana katika kuleta marekebisho haya kwenye Sheria ya Michezo. Sasa tunaamini kwamba hakutakuwa tena na vurugu katika michezo na hasa kuchanganya kati ya michezo ya ridhaa na michezo ya biashara, kwa mfano, ngumi za kulipwa. Nashukuru sana, mmeileta kwa wakati na ni siku nzuri sana mmeleta huu Muswada siku ambayo tumeamkia na furaha iliyoletwa na Bondia wetu aliyeshinda kwa kishindo huko London, usiku wa kuamkia jana, nawashukuruni sana. Tunaomba mwendelee kurekebisha hili eneo, lakini tuzingatie vilevile masharti ambayo baadhi ya michezo yanatawaliwa na sheria za Kimataifa. Tusizipuuze, tuziangalie zikae vizuri, tuziingize katika mfumo wetu wa utoaji haki katika maeneo ya michezo.

Mheshimiwa Spika, vile vile ningeusemea huu Muswada wa Marekebisho unaohusu Mtakwimu Mkuu wa nchi yetu. Ni kweli kumekuwa na vurugu nyingi sana katika

utoaji wa taarifa kiasi ambacho watu wengi sana tumekuwa tukishindwa kuamini taarifa ipi ni ya kweli. Serikali inatoa taarifa yake kupitia *National Bureau of Statistics* lakini tunapata taarifa nyingine kutoka vyanzo mbalimbali vinavyopingana na *statistics* hizo, tukimtaka mtu wa *NBS* ajaribu kuangalia au kuhakiki taarifa zinazotoka, kwamba pengine kutokana na kupitwa kwa muda taarifa zake hazikuwa sahihi lakini kumbe tunao watu wengi tu wanaotengeneza taarifa mbalimbali kwa madhumuni mbalimbali na mara nyingi sana wanaishia kuyumbisha watafiti ambao wanapenda sana kutumia taarifa mbalimbali kama *reference* ya kufanya utafiti ambao utaweza kusaidia nchi yetu.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, nampongeza sana Mwanasheria Mkuu na Mwandishi Mkuu wa Sheria, lakini najua hawa wote wanaongozwa na Mheshimiwa Waziri Prof. Palamagamba Kabudi, hongera sana kwa kazi kubwa unayoifanya. Najua kuna changamoto nyingi, watu wamezoea kujitolea takwimu wanavyopenda, tumeona mara nyingi sana taarifa zinatoka zinazopingana, zote zimefanywa kwa wakati mmoja na ukubwa wa sampuli ni ule ule, lakini matokeo yanakuwa tofauti kabisa. Ni kwa sababu tu kila anayefanya utafiti kwa kawaida wengine wanaanza kwanza na majibu halafu wanakwenda kufanya utafiti ku-*justify* majibu wanayotaka kuyatoa. Kwa hiyo, tunashukuru sana kwa sasa Muswada huu kuletwa kuhakikisha kwamba takwimu yoyote kabla haijaenda kwa walaji, lazima kwanza ihakikiwe na ikubaliwe na *National Bureau of Statistics.* Tunakushukuru sana kwa kazi hiyo nzuri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nilikuwa na wasiwasi na *mobile courts* lakini pengine siyo vizuri kuiongelea tena kwa sababu mmekubali ushauri wa Kamati yetu ya Katiba na Sheria, tunashukuru. Hizi *mobile courts* zina uzuri wake, lakini kuna changamoto zake na kwa sababu ni masuala ya haki hata kama changamoto ni kidogo, mimi nashukuru sana kwa Serikali kukubali kuondoa vifungu hivyo ili tukaliangalie upya

kwa undani zaidi kabla hatujarudi tena au tukaliweka vizuri zaidi kwa namna ambayo mtaona inafaa.

Mheshimiwa Spika, nawashukuruni sana kwa kazi hiyo kubwa mliyoifanya na kwa kweli sikupenda sana nichangie baada ya mabadiliko haya yaliyoletwa na Serikali kwa sababu mengi yaliyoletwa yameniondoa katika maeneo yale ambayo nilikuwa na dukuduku nayo na kwa kweli sikujua kama Serikali hii ni sikivu kiasi hiki. Nawashukuruni sana, mwendelee kuwa sikivu katika maeneo mengi ili hatimaye nchi hii iende kwa namna ambayo hakuna ambaye atasikia amenyimwa haki, hakuna ambaye atafika mahali atakata tamaa ya maisha kwa sababu upatikanaji wa haki unakuwa mgumu.

Mheshimiwa Spika, tunashukuru sana kwa namna walivyorahisisha na hasa lile eneo walilogusa la matajiri ambao kila wakati tumekuwa tukipata nao shida kwa kutumia wanasheria waliobobea na badala ya kuzungumzia changamoto au dhuluma iliyopo wanaanza kubishana kwenye utaalamu wa uandishi, hapa koma ilikosewa, mara suala hili halikuanza kwa muda ambao ulitakiwa, siku zimezidi, *technicalities.* Nawashukuru sana kwa kuliondoa hili. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naamini wataondoa hili katika maeneo mengi zaidi, siyo haya machache tu ambayo kwa hapa naona zaidi wameyaingiza kwenye masuala ya ardhi na makosa mengine machache yaliyoyaingizwa katika Muswada huu. Naomba sheria nzima ile ya Mwenendo...

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa mzungumzaji)*

**MHE. ENG. EDWIN A. NGONYANI:** Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja kwa asilimia mia moja. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante sana. Mheshimiwa Cecil Mwembe halafu Mheshimiwa Mchengerwa jiandae kutufungia.

**MHE. CECIL D. MWAMBE:** Mheshimiwa Spika, ahsante kwa kunipa nafasi nami niweze kuchangia hoja iliyopo mbele yetu. Niende moja kwa moja kwenye kitabu cha hotuba ya Kamati, Sehemu ya Tano, kipengele cha 3.1.5.

Mheshimiwa Spika, pamoja na uamuzi wa Serikali wa kuondoa hii Sehemu ya Tano kwenye Muswada wao waliouleta hapa mbele, lakini kule ndani kunaonesha kabisa hakukuwa kuna nia njema. Kwa sababu ukiangalia pale ndani, ndiyo maana wachangiaji wengi waliopita wanasema mhimili wako unapokwa madaraka yake. Kabla Serikali haijaleta huu Muswada au wakati inafanya maandalizi ya kuleta huu Muswada mbele yako, tayari wao walikuwa wameshaanza kufanya manunuzi mbalimbali, pamoja na kuamua kutumia hili jina la *mobile court*. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ukienda kwenye kitabu cha hotuba ya Kambi Rasmi ya Upinzani, kule ndani utakuta kuna sehemu tumesema, tumefanya utafiti na maeneo yameonekana na kuna ushahidi wa kutosha, kuna magari yanazunguka mitaani yameandikwa *mobile court.* Sasa tunajiuliza kwamba ni namna gani *Attorney General* au Mwanasheria Mkuu wa Serikali aliamua kuanzisha kitengo ambacho wanakuja kukiombea ruhusa ndani ya Bunge lako Tukufu? Hii siyo haki. Ndiyo maana hata tunakuja kuambiwa kwamba mpaka magari yatakayotumika kwa ajili ya kuendeshea hizi Mahakama yalishanunuliwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, leo tulikuwa na semina hapa na watu wa TAKUKURU. Wakati Mheshimiwa Rais anachukua nchi, wakati ule anatuhutubia sisi, alisema kati ya mambo atakayopingana nayo makubwa sana ni pamoja na masuala ya rushwa. Ni wazi kabisa kwa kutumia macho ya kawaida, utakuta huu Muswada au utakuta haya marekebisho yanayoletwa hapo walitaka sisi tuwe kama *rubber stamp* ya kuthibitisha uhalifu mkubwa uliofanyika katika maeneo haya. Nakuomba ikiwezekana pamoja na kwamba Serikali wamaeamua kuondoa jambo hili, hebu tengeneza Tume ndogo ikafuatilie mkataba huu ulioingiwa

kati ya Benki ya Dunia na kutusaidia hayo magari, ulikuwa na manufaa gani kwa Watanzania? *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, haya magari yanayotajwa yenye thamani kubwa sana, hayawezi kuingia maeneo mengi ya majimbo yetu kutokana na shida kubwa ya miundombinu iliyoko huko. Kwa mfano, hilo gari wanalosema ni *mobile court,* linatakiwa likafanye kazi kwenye Jimbo la Ndanda, Kijiji cha Namalembo ambapo hakuna barabara na maeneo mengi ni mabovu, hakuna madaraja, gari ni ndefu zaidi ya mita 35 litafikaje kule chini kabisa maporini? Kwa hiyo, haukufanyika utafiti wa kutosha. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ukiingia hapa kwenye hiki kitabu cha hotuba ya Mwenyekiti wa Kamati, ni wazi kule ndani anasema kwamba, tungeamua kutumia busara au Mahakama ingeamua kutumia busara, wangewaeleza wale wafadhili watujengee vyumba vya Mahakama kwenye maeneo yetu, kwa sababu hii ndiyo shida halisi ya nchi yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, haya masuala ya *mobile court* yamefanyika nchi nyingi; utafiti unaonyesha yamefanyika India, Pakistan pamoja na Bangladesh. Haya maeneo yana *population* kubwa, kiasi kwamba kuhamisha watu kwenda eneo lingine, ni suala rahisi. Sisi nchi yetu hatujawa wengi kiasi tunahitaji kupata hizi huduma kule chini kabisa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, pamoja na nia ya kutaka kuharakakisha mashauri mbalimbali, lakini ndani yake kunaonekana kulikuwa na nia ovu ya watu kutaka kupiga dili katika ununuzi wa haya magari kwa sababu gharama hiyo siyo halisi na uchunguzi ufanyike, kwa sababu watu wa TAKUKURU wapo, walilisikia hili, tunaomba walifanyie uchunguzi waje waeleze. Bunge lako lilitaka kutumika kama *rubber stamp* kuona watu wanapiga dili kwenye haya mambo ya magari. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, tukueleze tu, kama ambavyo wengine wametoka hapa kuchangia na umekataa kutumia

neno fulani la kusema Bunge linaingiliwa. Tukijaribu kugeuza maneno tunajenga tafsiri potofu hata kwa watu wetu wanaotusikiliza. Hili ni neno la kawaida kabisa la Kiswahili. Tunachotaka kumaanisha ni kwamba majukumu ya Bunge sasa kwa namna fulani yanatumika na Serikali kupitishia vitu vyao wanavyovitaja wao, hii ndiyo maana ya taarifa iliyotoka. Kiswahili halisi cha hili neno ni kupokwa madaraka kwa Bunge na mhimili mwingine. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Cecil Mwambe, kwa kuwa umeamua kulivaa hilo vizuri, hebu fafanua vizuri. Unalilaumu Bunge kwa jambo gani? Kuna jambo gani ambalo Bunge limefanya likapokwa kutokana na vitendo vyake hili Bunge mpaka unalilaumu wakati na Spika amekaa hapa, ni kitu gani hicho?

**MHE. CECIL D. MWAMBE:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana. Nataka nikupe mifano michache. Kwa mfano, leo asubuhi wewe mwenyewe Mheshimiwa Spika ulimwagiza Mwenyekiti wa Kamati ya Miundombinu wafanye mjadala na watu wa *ZECO* kuhusiana na masuala ya *VAT* ambayo inatozwa kule Zanzibar pamoja na hapa. Umesema kwamba watu wale walizuiliwa nje, sasa aliyewazuia nani? Wewe wenyewe unasema siyo wewe uliyetoa amri ya kuwazuia, lakini walizuiwa wasiingie kwenye mhimili wako. Sasa aliyewazuia wale watu ni nani? Ndiyo ninachojaribu kumaanisha. *(Kicheko/Makofi)*

Mheshimiwa Spika, jambo lingine...

**SPIKA:** Mheshimiwa Cecil bahati mbaya umeamua kuingia kwenye eneo ambalo...

*(Hapa baadhi ya Waheshimiwa Wabunge waliongea bila utaratibu)*

**SPIKA:** Unajua ninyi mara nyingi mnasema Wabunge hamheshimiki na kadhakalika, lakini mnatumia muda wenu mwingi mnapokuwa hapa kuusema mhimili wenu wenyewe, kuupaka matope mnayotaka na rangi mnazozitaka, halafu

mnataka mkitoka mheshimike, kitu ambacho siyo kweli. Kama tungekuwa tunaunga mkono baadhi ya watu kuzuiliwa huko nje tungesema hapa kwamba jambo hilo siyo sahihi? Kwa maana hiyo Bunge limepokwa madaraka au imekuwaje? Hili ni jambo ambalo kidogo halikukaa vizuri kwa jinsi lilivyokuwa, lakini Kamati haikuwa imewaalika *ZECO,* baada ya kufuatilia sasa mambo yalivyo, ilikuwa Mheshimiwa Waziri wa Nishati na Madini katika msafara wake, hawa watu wa *ZECO* ni wamojawapo. Sasa waliachana wapi, walikutana wapi, hilo siyo suala la Kamati wala siyo suala la Bunge hili. Kwa hiyo, tuelewane. Kama kuna nia mbaya ndani ya Bunge napaswa kulaumiwa, tufanye hivyo, mimi sikatai, lakini kulipakapaka matope tu Bunge ambayo wala hayana sababu sidhani kama ni sawasawa sana. *(Makofi)*

Mimi ningependa niwarudishe kwenye misingi tu, najua tunatamani sana tuonyeshe kwamba Bunge hili la Kumi na Moja liko lilivyo. Niliwahi kuwaambia wakati ule, Kikwete hafai, Awamu ya Nne haina maana leo hii, aah afadhali ya Kikwete, hivi hivi. Litakuja Bunge la Kumi na Mbili na la Kumi na Tatu, mtasema la Kumi na Moja la Ndugai lilikuwa afadhali, ndiyo binadamu walivyo. *(Makofi/Kicheko)*

Tusipakazie mahali ambapo hatuna sababu ya kupakazia, sisi tuweke tu hoja yetu. Habari ya hayo magari ya *mobile,* wangapi mnayajua au mmeshayaona hayo magari?

**WABUNGE FULANI:** Hatujayaona.

**SPIKA:** Mimi binafsi yangu sijaliona, ndiyo nasikia, najifunza kutoka kwenu. Tunapojifunza kutoka kwenu ndiyo tumeshapokwa? Kwa hiyo, ndiyo tumeingiliwa? Tupe habari tufanyie kazi. *(Kicheko/Makofi)*

**MHE. CECIL D. MWAMBE:** Mheshimiwa Spika, pamoja muda wangu, nashukuru pia kwa maelezo yako ya kutaka kutuweka sawa, lakini nikuongezee kitu kingine hapa. Hayo magari yalishanunuliwa, sasa tunapata wasiwasi kwamba Bunge hili ndilo linalopitisha bajeti na kwamba hata misaada

ya kifedha na isiyo ya kifedha inayopewa nchi hii, maana yake inapita humu ndani na kujadiliwa, pamoja na hayo masuala ya mikataba lakini mambo haya yamefanyika bila ushiriki wako wala ushiriki Bunge lako.

Mheshimiwa Spika, bado tunaona, kwa mfano, Mheshimiwa Rais sasa hivi amekuwa akifanya ziara. Juzi tu ameenda huko Tarime, ukiangalia jumla ya pesa alizozigawa kwenye ziara yake nzima ni karibia shilingi bilioni moja inafika pale. Tunasema siyo jambo baya kufanya jambo lile, kugawa hizo fedha na kufanya kitu kingine na watu wanasema sasa, Mheshimiwa Rais sasa tuanze kumwita Mzee wa Mapesa, hili jina liondolewe kwa Mheshimiwa Cheyo. Sasa tunajiuliza, haya ndiyo matumizi halisi ya hizi bajeti tunazoziweka? *(Makofi)*

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU (SERA, BUNGE, VIJANA NA WENYE ULEMAVU:** Mheshimiwa Spika...

**SPIKA:** Kwa kuwa umeamua mwenyewe kutoka kwenye mada na inaelekea hukuwa umejiandaa kuchangia, nitafika mahali nitakuwa sina *option* isipokuwa kukusimamisha tu. Kama kuna manunuzi ambayo yamefanyika kinyume na utaratibu, wajibu wako kama Mbunge ni kuleta jambo hilo kupitia swali, kupitia utaratibu mwingine wowote ule.

*(Hapa baadhi ya Waheshimiwa Wabunge walikuwa wakiongea bila mpangilio)*

**SPIKA:** Ndiyo unateuleza hapa hilo jambo lenyewe na hapo hapo unamwaga lawama kibao. Hivi kweli ndiyo tunavyoendesha mambo duniani? Hilo ni sawasawa? Ndiyo unaeleza jambo lenyewe; ukieleza jambo lenyewe na lawama kibao, hata kama ni Upinzani, ndiyo hivyo? Hatuendi hivyo! Tumia nafasi yako kama Mbunge na baadaye Waheshimiwa Mawaziri watajibu hapa. Kwa hiyo, hili siyo sawa hata kidogo, unakosea sana. Nadhani kama huna hoja ya hizi sheria hebu tuendelee, kama huna tumalizie hapo.

**MHE. CECIL D. MWAMBE:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru. Narudi tena kwenye hoja yetu ya msingi, kama ulivyosema tulipe taarifa Bunge ili liweze kufanyia kazi haya masuala. Naiomba meza yako, lakini pia naliomba Bunge hili lipewe taarifa rasmi na Serikali na huu upande wa Mahakama kwamba ilikuwaje wao wakaanza kufanya *purchases* ikiwa ni pamoja na kununua haya magari ya Kitengo cha *Mobile Court* kabla hawajatushirikisha? Kwa sababu tuna shida kubwa sana kwa ajili ya ujenzi wa Mahakama na tunakumbuka mwaka 2017 Mheshimiwa hapa alitangaza kwamba...

**SPIKA:** Sasa hilo unalolieleza ndiyo lugha ya kibunge hiyo, umenielewa? Siyo unavalisha watu lawama tu. Sasa unaongea kama Mbunge sasa. *(Kicheko/Makofi)*

**MHE. CECIL D. MWAMBE:** Mheshimiwa Spika, naendelea kukuomba tu, najua unaulinda muda wangu. Kwa hiyo, tunaomba sasa Bunge lako lipewe taarifa rasmi na Mheshimiwa Waziri atakapokuja hapa na mwisho wa siku atuambie, kwa sababu wameamua kuondoa hii Sehemu ya Tano kilichokuwa kimesababisha magari hayo yanunuliwe, sasa waje watuambie rasmi, baada ya magari haya kufika, wanakwenda kuyafanyia nini? *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ukienda kwenye masuala ya kisheria, siyo mzuri sana lakini tunapata taarifa mbalimbali. Sheria ilirekebishwa mwaka 2010 ambayo inampa *Chief Justice* mamlaka ya kufanya matumizi yoyote ya kitu ambacho kiko kwake. Sasa tunapata hofu, wanaweza wakaingilia upande wa kanuni, haya magari tukaanza kuyaona yakiwa yanafanya kazi. Kwa hiyo, Bunge lako liambiwe moja kwa moja kwamba jambo hili halitatokea tena, magari haya ikiwezekana huo mkataba usitishwe huko kabla magari hayajafika, hizo fedha zikafanyie shughuli nyingine. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, tuna shida ya maji, tuna shida ya vyumba Mahakama, kwa nini walikubali tu kisehemu kidogo cha kununuliwa magari ili kuweza kuwatembeza hao

Mahakimu ambayo hayawezi kufika kokote? Humu ndani hatujawahi kupitisha bajeti hata ya matengenezo ya hayo magari? Kwa hiyo, tafsiri yake ni kwamba watakwenda kutumia tena vibaya fedha iliyotengwa na Bunge lako kwa ajili ya shughuli za Kimahakama ambazo kila mara wamekuwa wakilalamika kwamba hizo pesa haziwatoshi. Mbaya kuliko, pamoja na kukiondoa hiki kifungu, ndiyo maana tunasema kulikuwa na nia ovu nyuma yake labda, walikuwa wanasema kwamba hata hizo *mobile courts* zikienda kufanyika vijijini, yule mshtakiwa haruhusiwi kuwa hata na mwakilishi wa kisheria. Hii ni tofauti na Ibara ya 13 cha Katiba.

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa mzungumzaji)*

**MHE. CECIL D. MWAMBE:** Mwenyekiti Spika, kwa hiyo, tunaomba utusaidie. *(Makofi)*

**SPIKA:** Muda wako umeisha. Nakushukuru sana. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, tunaendelea na Mheshimiwa Mchengerwa.

**WABUNGE FULANI:** Hayupo.

**SPIKA:** Mheshimiwa Mchengerwa hayupo?

**WABUNGE FULANI:** Ndiyo.

**SPIKA:** Basi, sasa Mwenyekiti wa Kamati tena inakuwaje huyu?

Sasa tunaanza upande wa Waheshimiwa Mawaziri. Nawaomba Waheshimiwa msitoketoke ili *quorum* yetu ikae sawasawa ili jambo hili liishe jioni hii ya leo. Mheshimiwa Angeline Mabula, tafadhali una dakika tano, ukitumia chini ya hapo nitashukuru.

**NAIBU WAZIRI WA ARDHI, NYUMBA NA MAENDELEO YA MAKAZI:** Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa kunipa fursa hii. Nianze kwa kuunga mkono hoja na niwapongeze sana Mheshimiwa Waziri pamoja na Mwanasheria Mkuu. Nitajibu baadhi ya hoja chache ambazo zimetolewa kwenye taarifa ya Kambi Rasmi ya Upinzani.

Mheshimiwa Spika, hoja ya kwanza ilikuwa inazungumzia suala la Wakuu wa Mikoa na Wakuu wa Wilaya kuingilia utendaji wa Mabaraza. Naomba niseme kwamba suala hili lilishaongelewa humu ndani na lilipatiwa majibu, lakini mbali na kupatiwa majibu, Waziri mwenye dhamana ya TAMISEMI alilitolea maelekezo kwa maandishi mwezi Februari. Mimi sikutegemea kama lingekuja hapa, kwa sababu baada ya maelekezo hayo, hakuna tena jambo kama lile ambalo lilijitokeza. Kwa hiyo, nawaomba tu Waheshimiwa Wabunge kwamba pale wanapotoa hoja zao na zikafanyiwa kazi wawe wanafuatailia pia kuweza kujua, kuliko kukaa linajirudiarudia suala ambalo tayari lilishapatiwa ufumbuzi na kazi zinaenda vizuri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spiaka, suala la pili walikuwa wanaongelea suala la uboreshaji wa Mabaraza ya Ardhi. Ni kweli Mabaraza ya Ardhi ya Kata mengi hayafanyi kazi vizuri kama yanavyokusudiwa. Tukumbuke tu pia ile Tume ya Shivji wakati inaanza, ni nini kilisababisha mpaka Mabaraza haya yaanzishwe? Lengo pia ilikuwa ni kusogeza huduma kule chini kwa wanavijiji au kwenye mitaa kule ambako wanafahamiana zaidi. Kilichokuwa kinakusudiwa pale ni kutatua migogoro hii katika namna ya ushirikishaji zaidi. Sasa tatizo ambalo limekuwa likijitokeza sana, pengine watu wale wanakuwa wamezoeana sana, wengine wanaoneana aibu na unaweza katika utendaji unakuwa hauendi vizuri.

Mheshimiwa Spika, hili kama Serikali tumeliona, kupitia Ofisi ya Msajili wa Mabaraza tunashirikiana na Halmashauri zote kwa ajili ya kuwapa mafunzo mbalimbali wapate uelewa wa kuweza kusimamia kazi hizi. Kazi hizi pia zinafanywa na Wanasheria wa Halmashauri mbalimbali. Kuna Wilaya au Mikoa ambayo tumeshafanya nayo kazi na

kazi inakwenda vizuri. Kwa hiyo, niseme kwa hili pengine ni uelewa mdogo wa wale watu wanaochaguliwa.

Mheshimiwa Spika, nitoe rai tu pale ambapo zinaundwa hizi Kamati kule, waangalie watu wenye uadilifu wanaoweza kufanya kazi yao vizuri, lakini wajibu pia wa Halmashauri zetu ni kuhakikisha kwamba Mabaraza yale wanaya-*own* ili yaweze kufanya kazi yake kulingana na taratibu. Kwa sababu yako chini ya Mkurugenzi, yanatakiwa kuwa na bajeti zao kwa Mkurugenzi, yanatakiwa pia kuwa na mwongozo, pengine hata kuwa na *By-laws* zinazowaelekeza hata katika utozaji wa tozo wanazotoza pale.

Mheshimiwa Spika, ndiyo maana unakuta wakati mwingine hawako moja kwa moja katika utaratibu unaohusika. Serikali imeliona hili na ndiyo maana tunafanyia kazi kwa karibu sana tukisaidiana na Wanasheria wa Halmashauri. Hii imefanikiwa sana katika maeneo tuliyopita ambapo tumetoa semina hizo kwa kuwaunganisha, kazi inakwenda vizuri. Kwa hiyo, niseme hilo lilishaonekana.

Mheshimiwa Spika, ukiangalia usimamizi wa sekta ya ardhi, unasimamiwa na Wizara tatu tofauti. Mabaraza ya Kata, yako chini ya TAMISEMI, lakini ukija hapa Wilayani unakuta yako chini ya Wizara ya Ardhi, akienda Mahakama Kuu, yuko Sheria na Katiba. Kwa hiyo, tunajaribu ku-*harmonize* namna bora ya utendaji ili kuweza kuona wanafanyaje kazi zao.

Mheshimiwa Spika, pia kwenye suala la namna ya utatuzi wa kesi zao, ukija ngazi ya Wilaya kunakuwa na tatizo. Changamoto kubwa tuliyonayo ni Watendaji hawatoshelezi, ndiyo maana unakuta Mwenyekiti mmoja anakuwa anasimamia Mabaraza matatu au manne. Hiyo tumeshaiona na kama nilivyojibu swali juzi, tayari tunao 20 ambao wataajiriwa kwenda kuziba mapengo yale. Tayari pia tumetoa maelekezo ili waweze kupatikana wengine waweze kufanyiwa *vetting,* kila tunapopata ajira waweze kuingia ku-*solve* tatizo hili. Kwa sababu lengo la kuanzisha

Mabaraza yale ni kurahisisha na kumfanya yule mwananchi wa kawaida aweze kutatuliwa kesi yake mapema na katika mazingira yale yale aliyoyazoea. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, suala lingine ambalo wameliongelea ni haya Mabaraza kuwa na msongamano. Wamesema kwamba Mabaraza ya Wilaya yaondolewe katika Wizara ya Ardhi na kupelekwa Wizara ya Katiba. Bado hali inarudi ile ile, kwa sababu lengo la kuanzisha Mabaraza haya ilikuwa ni kuondokana na msongamano uliokuwepo kwenye Mahakama. Kwa sababu ya *nature* ya migogoro ile, mingi inakwenda kutatuliwa wakati mwingine kwenye *site.* Kwa hiyo, huwezi kukwepa ukasema kwamba Mabaraza haya yarudi huku, utarudisha tena ule mzigo ambao tulikuwa tukiupigia kelele.

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa mzungumzaji)*

**NAIBU WAZIRI WA ARDHI, NYUMBA NA MAENDELEO YA MAKAZI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Waziri. Sijui kwenye Kamati walisemaje, lakini labda tuwe tunanyamaza, haya Mabaraza kweli haya, mahali pengi ni *disaster* tu. Wajanja likishakuwa pale, wanakata rufaa kwenda Wilayani na kwa sababu kwenye Wilaya karibu zote hazina haya Mabaraza, yako Mkoani, kwa hiyo, mtu wa Kongwa, mwanakijiji wa kawaida aanze kupanda mabasi kuja Dodoma yaani ni tatizo. *(Makofi)*

Kwa hiyo, tunaishauri tu Serikali kwa ujumla wake, yaani bora hata mfumo ule wa Kimahakama angalau umekaa vizuri kuliko huu. Ni kuliangalia tu, ni ushauri tu, siyo lazima. Huenda wenzetu mnavyoliona mko sahihi zaidi. *(Makofi)*

Tunaendelea na Mheshimiwa Dkt. Ashatu, tafadhali jitahidi usizidi dakika kumi.

**NAIBU WAZIRI FEDHA NA MIPANGO:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa fursa hii ili nami niweze kuchangia hoja hii iliyoko mezani iliyowekwa na Mwanasheria Mkuu wa Serikali.

Mheshimiwa Spika, nianze kwa kumpongeza sana Mwanasheria Mkuu wa Serikali na wataalam wake pamoja na Mheshimiwa Waziri wa Katiba na Sheria kwa kazi nzuri waliyoifanya katika kutuletea hoja hii iliyoko mezani. Imekuja kwa wakati muafaka kabisa, kwa kweli nawapongeza sana kwa kazi nzuri ambayo wameifanya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, napenda kuchangia machache katika hoja hii. Nianze na hoja ya kwanza ambayo imeongelewa sana hasa kuhusu marekebisho katika Sheria yetu ya Takwimu, Sura 351, ambapo wanasema kwamba sheria inajikita katika kudhibiti tafiti zitakazokuwa zinafanyika hapa nchini.

Mheshimiwa Spika, napenda kuliarifu Bunge lako Tukufu kwamba marekebisho ya sheria hii ni msaada mkubwa sana wa hao tunaowadanganya tunawatetea leo. Kwa nini nasema hivyo? Marekebisho haya yanamtaka kila mtu au taasisi inayofanya utafiti kwa ajili ya matumizi ya kupanga sera au kupanga mipango ya maendeleo, afuate utaratibu ili matokeo ya tafiti yake yatumike katika kufuatilia na kutathimini mipango ya maendeleo iliyowekwa. Hiyo ndiyo dhana halisi ya marekebisho haya tunayoleta.

Mheshimiwa Spika, katika hili ambalo Serikali inapendekeza, Taifa letu limekuwa katika ombwe kubwa la kutokuwa na takwimu ambazo siyo sahihi. Nitoe mfano mmoja, mwaka 2012 nilikuwa nafanya *research* yangu ya *Personnel Economics,* nikiwa natoka Chuo Kikuu cha Agdal, nimekuja Tanzania kufuatilia taarifa rasmi, sikuzipata, nikaenda kuzipata taarifa za Tanzania kutoka South Africa. Kwa nini ilitokea hiyo? Ni kwa sababu hakukuwa na marekebisho haya ya sheria ambayo yangewasaidia watu wenye takwimu zao ambazo sasa zitakuwa ni takwimu sahihi, kwa hiyo, ndicho ambacho sheria hii inapendekeza.

Mheshimiwa Spika, tunachokifanya ni kutoa wigo mpana zaidi kwa watafiti wetu hasa katika kutumia kanuni na taratibu za ukokotoaji wa taarifa za kitakwimu ili kuziba pengo hili ambalo takwimu za Tanzania hazipatikani Tanzania, zinakwenda kupatikana sehemu nyingine. Tuna watafiti wengi, sasa hao watafiti tunataka kuwasaidia tu. Kwa hiyo, *NBS* wanachotaka kukifanya ni kuhakikisha kila tafiti inayofanyika inakuwa *formalized* na inatumika kwa ajili ya kupanga mipango mbalimbali ya maendeleo ndani ya Taifa letu. Hicho ndicho ambalo tunataka kufanya. Kwa hiyo, hiki kinachosemwa kwamba tunaenda kudhibiti, hapana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, hoja hii inachanganywa na kwamba Ofisi yetu ya Taifa ya Takwimu inakwenda kudhibiti hata *research* zinazofanyika kwenye vyuo vyetu vya elimu ya juu. Siyo sahihi hata kidogo. Tafiti zinazofanyika kwenye vyuo vyetu zina taratibu zake, wala Ofisi ya Taifa ya Takwimu haihusiani na tafiti za kwenye vyuo vyetu. Kwa hiyo, hili tusiwadanganye Watanzania, tuwaeleze ukweli dhamira ya Serikali ya Chama cha Mapinduzi ya Awamu ya Tano, nini tunataka kufanya. Tuwaeleze ukweli Watanzania waelewe. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, umetolewa mfano wa TWAWEZA, hivi leo unaweza ukamwambia TWAWEZA akasema ile tafiti yake ni *official statistic,* kwa kuwa amefuata nini? Hata *methodology* aliyotumia haifahamiki. Anawezaje kusema kwamba ile ni takwimu sahihi sasa, kwamba itumike katika kupanga mipango ya maendeleo? Siyo sahihi. Tuwasadie Watanzania, tuwaeleze ukweli na hao TWAWEZA waje tukae pamoja ili tuweze kuwa na takwimu sahihi za kupanga maendeleo sahihi ya Taifa letu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, hoja ya pili ambayo napenda kuisemea ni ile inayosema kwamba mtafiti yeyote kabla ya kutoa matokeo, ni kile kifungu kinachopendekezwa cha 24A(2). Kinachoongelewa hapa, lengo la kifungu hiki ni kuhakikisha kuwa tunatoa nafasi ya majadiliano ya kitaalam baina ya mtafiti na jopo letu la wataalam katika sekta husika.

Mheshimiwa Spika, nimetangulia kusema kwamba tunataka kupata *formalized* takwimu ndani ya Taifa letu. Kwa hiyo, lazima tukae pamoja, wewe mtafiti unayesema umefanya *research* yako kuonyesha kwamba hali ya umaskini ni kiwango fulani tukae pamoja basi utujuze, umetumia *methodology* gani? *Sample* uliyochukua kuja ku-*generalized* matokeo ya takwimu yako umetumia watu wangapi? Huwezi kufanya *research* ya watu watano halafu ukatuambia Watanzania wanasema, Watanzania hawawezi kuwa ni watu watano. *Research* zina taratibu zake na ndicho ambacho tunapendekeza katika kifungu cha 24A. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, lakini yako mapendekezo mengine kwamba kifungu cha 24B kifutwe kwa kuwa maudhui yake yameelezwa katika kifungu cha 24A. Napenda kuliambia Bunge lako Tukufu kwamba kifungu cha 24A(1) kinahusu mtu ambaye amepewa takwimu na hapa ndiyo nataka tuelewane, kifungu hiki kinamwongelea mtu ambaye amepewa takwimu na Ofisi ya Taifa ya Takwimu kwa ajili ya kufanya uchambuzi wa kina, yaani *further analysis.* Kwa hiyo, hapa kwanza amepewa takwimu, ndicho kifungu hiki kinachoongelea, anakwenda kufanya *further analysis.* Sasa wewe umepewa takwimu na mtu aliyekusanya, anajua amejua ametumia *methodology* gani kukusanya takwimu zake, kabla hujatoa matokeo, ukiambiwa urudi tuweze kukubaliana kama kweli ulielewa nini kilikusanywa, unalalamika, hii siyo sawa hata kidogo. Naomba tuweze kuelewana. Kwa hiyo, kifungu hiki kama Serikali tunapendekeza kiendelee kuwepo kwa sababu kinaongelea mtu aliyechukua takwimu kutoka Ofisi ya Takwimu ya Taifa.

Mheshimiwa Spika, kifungu cha 24B(2) nacho kinapendekezwa kifutwe. Nimesema hiki cha kwanza nilichokiongelea, mtafiti huyu kapewa takwimu na Ofisi ya Taifa ya Takwimu. Hiki cha 24B kinaongelea taarifa za kitakwimu ambazo zimekusanywa sasa na mtafiti mwenyewe. Kwa hiyo, ni vifungu viwili tofauti vinavyooongelea maana tofauti, ndiyo maana Serikali yetu imependekeza ili tuweze kuwasaidia. Huyu aliyekuja kuchukua taarifa kutoka Ofisi ya Taifa ya Takwimu afanye

kazi yake, afanye *further analysis* ili turudi mezani tukae kwa pamoja kwa maana tu ya kuelewana nini ameelewa na nini amepata kutoka kwenye takwimu ambazo zimekusanywa na Ofisi ya Taifa ya Takwimu? Hiki cha pili kinamwongelea anayekwenda kukusanya taarifa zake yeye mwenyewe. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia ni vizuri tukaelewana. Nawashukuru Waheshimiwa Wabunge wengi wamesema hapa, kwamba kumekuwa na ombwe la kila mmoja kuja na taarifa zake. Ofisi ya Taifa ya Takwimu inasema mfumuko wa bei wa mwezi Agosti, ni asilimia 3.3, anaibuka mtu mwingine anakwambia mfumuko ni asilimia 2.2 bila kueleza kwa undani amekusanyaje taarifa zake kumfikisha kwenye hayo matokeo anayotueleza. Ndiyo lengo la kifungu hiki, tuelewane kwa pamoja, tutoke kwa pamoja kama Taifa, lengo likiwa ni maendeleo kwa Watanzania. Tusitoe takwimu ambazo kila mmoja akiamua basi atamchanganya tu Mtanzania na tushindwe kukaa chini na kufanya kazi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naomba niseme jambo la mwisho...

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa mzungumzaji)*

**SPIKA:** Ahsante sana. Dakika zako kumi zimeisha.

**NAIBU WAZIRI FEDHA NA MIPANGO:** Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja, ahsante sana. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante sana. Mheshimiwa Dkt. Mpango, usizidi dakika kumi.

**WAZIRI FEDHA NA MIPANGO:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana kwa nafasi hii ili nami nichangie hoja iliyoko mbele yetu. Nianze kwa kuunga mkono hoja na niwapongeze sana Mheshimiwa Waziri wa Katiba na Sheria na timu yake yote na Mheshimiwa Mwanasheria Mkuu Mkuu wa Serikali kwa kazi nzuri sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nami naomba niseme mambo machache. La kwanza kulikuwa na hoja ile ambayo ilitokana na malalamiko yalitokea katika Bunge la Bajeti ya kutoza *VAT* (Kodi ya Ongezeko la Thamani) kwenye umeme ambao unauzwa na *TANESCO* kwa *ZECO*. Suala lilikuwa kwamba kwa nini marekebisho haya hayakuletwa kwenye Muswada wa Sheria mbalimbali wa mwaka 2018 ili kuweza kumaliza…

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, hasa mnaokaa huko nyuma, CCM kule nyuma yaani mmegeuza kuwa ni…Mheshimiwa Waziri endelea.

**WAZIRI FEDHA NA MIPANGO:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru. Nilikuwa nasema, hoja ilikuwa ni kwa nini hatujaleta marekebisho kwenye Muswada wa Sheria Mbalimbali ili kujibu malalamiko ambayo Mheshimiwa Saada Mkuya aliyaeleza Bunge lililopita.

Mheshimiwa Spika, labda niseme tu kwanza Sheria yenyewe ya *VAT* tunajua ilianza kutumika mwaka 1998. Kwa mujibu wa sheria ile, bidhaa zinatozwa *VAT* ikiwa ni pamoja na umeme. Sheria ile ikafanyiwa marekebisho tukapata Sheria mpya ya *VAT* ya mwaka 2014 na kwa bahati nzuri wakati ule Mheshimiwa Saada ndiye alikuwa Waziri wa Fedha.

Mheshimiwa Spika, katika utaratibu ule, *ZECO* ilikuwa inalipa *VAT* wanaponunua umeme, halafu Mamlaka ya Mapato ikawa inarejesha *VAT* kwa Waziri wa Fedha wa Zanzibar. Utaratibu huo ukazusha malalamiko mengi tu ikiwa ni pamoja na matatizo ya marejesho ya *VAT*, masuala ya uhakiki na kadhalika. Pia wauzaji wa *re-exports* nao wakawa wanalalamika ikapelekea turekebishe ile sheria Juni, 2016 kupitia Muswada wa Fedha wa mwaka 2016.

Mheshimiwa Spika, tulichofanya ni nini? Tulichofanya ni kwamba umeme utozwe *VAT* kwa kiwango cha asilimia sifuri kwenye bidhaa ambazo zinatengenezwa Bara na kuuza Zanzibar. Kwa hiyo, bidhaa zote ambazo zinazalishwa Bara, zitozwe *VAT* lakini kwa kiwango cha asilimia sifuri, kadhalika

upande wa pili nao. Ndiyo marekebisho ya msingi tuliyofanya mwaka 2016. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, shida ikaja kwamba *ZECO* wakatafsiri kwamba umeme ni bidhaa lakini sheria inasema bidhaa, *ZECO* wakatafsiri kwamba umeme ni bidhaa na kwa hiyo, unatakiwa uwe *zero-rated.* Sasa ubishani umekuwa hapa, umeme ni bidhaa au siyo, ni huduma. Kwa hiyo, haya ndiyo tumekuwa nayo. Hiyo ni changamoto ya kwanza.

Mheshimiwa Spika, changamoto ya pili, siku za nyuma kidogo mwaka 2008, *EWURA* ilipandisha bei ya umeme kwa asilimia kama 21.7 na ikafanya hivyo kwa makundi yote ya watumiaji wa umeme; wale wanaonunua jumla na wale wa umeme wa majumbani. Sasa lilipofanyika hilo, *ZECO* wakalipinga, wakakataa kabisa kulipa umeme kwa hivyo viwango vipya. Matokeo yake ikawa malimbikizo yanayotokana na hiyo tofauti ya bei, tofauti ya *VAT* yamekuwa yanaendelea hivi, lakini pia hata ile tozo ya *EWURA* yenyewe. Kwa hiyo, deni limekua mpaka kufikia mwishoni mwa mwezi Juni, lile deni ukijumlisha vyote limefikia takribani shilingi bilioni 138.7. Kati ya hizo, za kodi peke yake ni kama shilingi bilioni 20.4.

Mheshimiwa Spika, nachojaribu kueleza ni nini? Ni kwamba jambo hili ni pana. Ni kweli kabisa dhamira yetu ilikuwa tungeweza kuleta marekebisho katika Bunge hili, lakini jambo hili ni pana. Kama nilivyosema, kwanza kuna mgogoro kati ya *ZECO* na *TANESCO* juu ya ulipaji wa hiyo *VAT* baada ya yale marekebisho tuliyofanya katika Sheria ya Fedha ya mwaka 2016. La pili, *ZECO* wakalalamikia viwango vya bei ya umeme ambavyo vilikuwa vimewekwa na *EWURA*.

Mheshimiwa Spika, siyo hivyo tu, bado tuna changamoto. Sisi tunasheria ya *VAT* kama ilivyorekebishwa mwaka 2014, lakini Zanzibar nao wana sheria yao ya *VAT*. Sasa hapa kuna changamoto kidogo. Kwa mfano, sisi Sheria ya *VAT* ya mwaka 2014 inatoza *VAT* kwenye huduma za simu *(interconnection charges)* na tunafanya hivyo kwa kiwango cha asilimia sifuri, lakini Sheria ya *VAT* Zanzibar ya mwaka

1998 inaelekeza kuwa huduma zote kutoka Bara hazistahili kuwa *zero-rated* na hili linalalamikiwa sana na wadau upande huu wa Muungano. Siyo tu hivyo, ukiangalia ile Sheria ya *VAT* ya mwaka 2004, hainipi mamlaka kama Waziri wa Fedha kuweza kusamehe *VAT* kwenye huduma ikiwa ni pamoja na kwenye umeme.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, nachosema ni nini? Nachosema ni hivi, jambo hili ni pana, mawanda yake ni mapana, tusingeweza kuleta...

**MHE. SAADA MKUYA SALUM:** Taarifa.

**WAZIRI FEDHA NA MIPANGO:** Naomba unipe nafasi.

**SPIKA:** Nitakupa nafasi, lakini tulia tu kidogo.

**WAZIRI FEDHA NA MIPANGO:** Mheshimiwa Spika, tusingeweza kufanya marekebisho yale ambayo tulikuwa tumeahidi kufanya kwenye Bunge lililopita.

Mheshimiwa Spika, sasa tumefanya nini? Tumefanya mambo kadhaa, moja, kama Serikali yamekuwepo majadiliano kati ya *TANESCO* na *ZECO* juu ya vile viwango ili waweze kupata kiwango muafaka cha bei ya umeme. Haya ni ya muda mrefu toka 2013 wanazungumza. La pili, Wizara ya Nishati na *EWURA* wametafuta Mtaalam Mwelekezi ambaye anafanya *study* inaitwa *Cost of Service Study* ili sasa kuweza kujua gharama ya kutoa huduma ya umeme kwa wateja mbalimbali, hawa wa jumla na wa majumbani, hivi ni nini hasa? Haya ndiyo yatatuwezesha kufanya maamuzi sahihi.

Mheshimiwa Spika, kwa upande wetu kama Wizara ye Fedha, tumeandaa Waraka tayari, ninayo rasimu ya Waraka na rasimu hii imefikia ngazi ya kupata maoni ya wadau ikiwa ni pamoja na Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar. Wameshapelekewa rasimu ya Waraka na ninayo rasimu hapa ili tuweze sasa kupata uamuzi rasmi wa Serikali juu ya jambo hili. Hii ndiyo itatuwezesha tuseme turekebishe Sheria

ya *VAT* ile Sura ya 148 na kwa hiyo, ni muhimu Serikali iweze kuji-*pronounce* kwa maana ya kwanza kuondoa hizi kero ambazo zimekuwepo muda mrefu lakini pia kuweza kuona madhara yake ya kufanya hivyo ni nini? Kwa mfano, upande wa mapato iko wazi kabisa.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, nilichotaka kueleza ni kwamba Marekebisho ya Sheria Mbalimbali ya mwaka 2018 hatukuweza kufanya hivi ili tuweze ku-*accommodate* haya mawanda mapana ambayo ninajaribu kuyaeleza.

Mheshimiwa Spika...

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa mzungumzaji)*

**SPIKA:** Muda hauko upande wetu, malizia Mheshimiwa Waziri.

**WAZIRI WA FEDHA NA MIPANGO:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana kwa nafasi na naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Saada nilikuahidi kukupa nafasi kwa ajili ya taarifa uliyotaka kutoa.

**TAARIFA**

**MHE. SAADA MKUYA SALUM:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana na namshukuru sana Mheshimiwa Waziri. Laiti kama hili nisingelisema leo, haya maelezo yasingetoka leo, nashukuru.

Mheshimiwa Spika, nilikuwa nataka kumpa taarifa, Mheshimiwa Dkt. Mpango, ni kaka yangu halisi kabisa kwamba Sheria ya *VAT* ya mwaka 2014 wakati huo Saada Mkuya Salum ndiye alikuwa Waziri wa Fedha, tumeweka kifungu cha 48, naomba nikisome. *Marginal notes* inasema *Supply of essential services,* kinasema:-

*"Where water, gas, oil, electricity or thermal energy is supplied through a pipeline cable or other continuous distribution network and delivered to a place in Tanzania Mainland or from a place in Mainland Tanzania to a place outside the United Republic of Tanzania such supply shall be treated as a supply made in Mainland Tanzania." (Makofi)*

Mheshimiwa Spika, *this is the VAT Act* ambayo mimi pamoja na Bunge lako, ni Bunge lako Tukufu lilipitisha. *It doesn't say anywhere* kwamba *supply* ambayo inakuwa *made in Zanzibar,* inatoka *Tanzania Mainland made in Zanzibar, place of taxation* itakuwa ni *Tanzania Mainland, it doesn't say that.* Kwa hiyo, tukienda kwenye *reference* ya marekebisho haya kwanza hata hiki kifungu ambacho nimekisoma hakiipi mamlaka *TANESCO* kuitoza *VAT ZECO. (Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, nilikuwa nataka kumpa taarifa kaka yangu kwamba hii ndiyo sheria ambayo tuliipitisha. *Mandate* ya *TANESCO* kutoa *VAT* kwa sababu tunajua *principle* ya *VAT* ni kwa mlaji wa mwisho, *TANESCO* haina *mandate* ya kutoza *VAT* kwa umeme *raw* unaonunuliwa na *ZECO. (Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante sana. Wala sina haja ya kukunyanyua tena Mheshimiwa Waziri wa Fedha, *unless* una-*opt* hivyo. Siyo nia yangu kufungua mjadala mkubwa katika jambo hili, lakini kama kuna kitu unataka kusema, nisikuzie.

**WAZIRI WA FEDHA NA MIPANGO:** Mheshimiwa Spika, hapa tulipofika ni pazuri. Nimwombe Mheshimiwa Saada na timu yake na Wazanzibar wengine walete hayo maoni kule kwenye *process* ambako tumeshafikia, tunakwenda vizuri. Nisisitize tena, ni muhimu sana, Muungano huu, wote tunaapa kuulinda na kutetea Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, lakini tuifanye kwa busara, kwa faida ya pande zote mbili, tusiende kwa jazba, kabisa. Tuna nia njema ya kuhakikisha kwamba Muungano wetu unaimarika. Niseme hayo tu. *(Makofi)*

**SPIKA:** Nini?

**MHE. ALI SALIM KHAMIS:** Mheshimiwa Spika, ahsante. Kiukweli Mheshimiwa Waziri analidanganya Bunge lako. Anasema anafanya *process,* siyo kweli. Hili jambo tumeshalizungumzia sana katika maeneo mbalimbali, usitudanganye. Huu Muungano ni wetu sote, sasa usitake kuleta tofauti ikaonekana kwamba kuna mvutano baina ya Muungano pande zote mbili, hili jambo ifike mahali liishe. Ahsante. *(Makofi)*

**SPIKA:** Hayo maneno uliyosema 'siyo kweli', nayafuta kabisa kwamba Waziri analidanganya Bunge, siyo kweli hata kidogo, yeye ametoa maoni ambayo ndiyo msimamo wa Serikali.

Sisi wenzenu kwa kweli tungependa jambo hili liishe kama tulivyosema *last time,* yaani liishe tu. Halina afya hata kidogo kwa nchi yetu. Kwa hiyo, hao wataalam wakeshe liishe tu. *(Makofi)*

Sasa kwa sababu ahadi ilikuwa ni Bunge hili, basi tunasongeza ahadi kwa Bunge lijalo. Bunge lijalo haliko mbali sana, kwa hiyo, ni vizuri kwa kweli mtakapotoka hapa, basi mjitahidi Bunge lijalo tusikie lugha nyingine ili tuendelee na mambo mengine. Tunajua ni kubwa na lina mambo mengi lakini ni muhimu liishe kwa sababu ya *interest* kubwa zaidi za Muungano wetu na kwenye uwanja wa kisiasa ndiyo hatutaeleweka kabisa. Nasikia baadhi ya lugha zinazosemwa hapa, watu wana hasira kweli kweli, kwa hiyo, liishe. Itakuwa ni jambo la maana sana, tunawaomba sana wahusika wote mliangalie suala hili. *(Makofi)*

Profesa Kabudi dakika 15, tafadhali. Mheshimiwa Waziri wa Afya hebu mwachie Profesa, ahsante. *(Kicheko)*

**WAZIRI WA KATIBA NA SHERIA:** Mheshimiwa Spika, nianze kwa kukushukuru sana kwa kunipa nafasi hii nami nichangie hoja hii. Nianze moja kwa moja kwa kuunga

mkono hoja iliyowasilishwa na Mwanasheria Mkuu wa Serikali wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

Mheshimiwa Spika, nitazungumzia sehemu mbili tu; Sehemu ya Tano ya Muswada ambayo Serikali imeiondoa na suala la ndugu yangu Mheshimiwa Mtolea kuhusu *extended jurisdiction.* Nasikitika kwamba wengi waliolizungumzia suala hili sasa hivi hawamo ndani ya Bunge na lengo langu lilikuwa nitoe ufanuzi na wenyewe wakiwepo ili wasikie maelezo haya.

Mheshimiwa Spika, Mahakama ni mhimili kama ambavyo Bunge ni mhimili, kama ambavyo *Executive* ni mhimili. Ndiyo maana nchi nyingine za Ulaya kwa kujua Mahakama ni mhimili bajeti yake na mambo yake huwa hayapelekwi Bungeni.

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, sasa nitakuwa nawataja majina ili wapiga kura wenu wasikie, maana nawaona hapa kwenye kioo changu. Hatuwezi kutulia tukasikiliza kinachoendelea? Tuna shida gani Wabunge wa Tanzania? *What is it?* Tusikilizane. Ni aibu kubwa sana kwamba wewe unakaa unapiga *story* tu, halafu kesho wewe huyo huyo unasimama unauliza jambo ambalo limezungumzwa hapa Bungeni, inakuwa haifai. Naomba kila mmoja atulie, asikilize. Sasa nitaanza kuwa nataja majina na tusameheane kwa hilo na unajua ukitajwa hapa itasikika mpaka kule kwa waliokuleta hapa. Mheshimiwa Waziri endelea.

**WAZIRI WA KATIBA NA SHERIA:** Mheshimiwa Spika, Mahakama ni mhimili, Bunge ni mhimili na *Executive* ni mhimili. Hawa wanasheria wameondoka, nilitaka niwakumbushe *lecture* ya *first year, Constitutions and Legal System. The Judiciary enjoys sovereignty and the Parliament enjoys sovereignty.* Katika dhana nzima ya *separation of powers, the Parliament can only check the Executive and not the Judiciary.* Ndiyo maana nimesikitika sana, wanasheria ndani ya Bunge kuanza kuzungumzia mhimili wa Mahakama kwa lugha ya kejeli, dharau na kuibagaza Mahakama. Mkitaka kujua ugumu wa kuwa Jaji, someni Zaburi ya 15.

Ndiyo maana kama kuna kazi nilimwomba Mungu aniepushe nayo ni kuwa mhukumu. Ndiyo maana nchi za wenzetu, bajeti ya Mahakama, masuala ya Mahakama hayaletwi ndani ya Bunge, kama ambavyo Mahakama haiwezi kujadili maamuzi ya Bunge. *The decision of the Speaker or Chair in the Parliament cannot be impeached or questioned in a Court of law and equally the Parliament cannot question the Chief Justice, cannot question the Judiciary. (Makofi)*

Mheshimiwa Spika, sasa bahati mbaya hii lugha imeanzishwa na wanasheria na bahati mbaya hawapo. Nilitaka wawemo humu na namshukuru sana Mheshimiwa Simbachawene, kila siku hunikumbusha nisiwakumbushe *marks* zao darasani. Namheshimu mdogo wangu Simbachawene, sitawakumbusha *marks* zao darasani, ni lazima tujue. *(Kicheko/Makofi)*

Mheshimiwa Spika, maadam huu ni mhimili, mhimili wa Mahakama hauwezi kuja hapa kuleta jambo, unaituma *Executive,* kama ambayo mambo ya Bunge Spika haji kuyaleta hapa, anaituma Ofisi ya Waziri Mkuu. Kwa hiyo, Muswada huu *basically* ulikuwa ni Muswada wa *Judiciary* na mwenye mamlaka ya mwisho ubaki au utoke ni *Chief Justice* ambaye yeye peke yake ndiye anayemwapisha *Head of State* na yeye peke yake Rais akiwa *impeached* ndiye anayetia saini ya kumwondoa baada ya *impeachment,* siyo mtu wa kuja kubagazwa ndani ya ukumbi huu.

Mheshimiwa Spika, ndiyo maana siku *Chief Justice* alipoamua kuja hapa ilibidi Spika aende akae naye kwenye *gallery.* Spika huwa anakaa kwenye *gallery?* Hamkujiuliza? *Why did the Speaker escort the Chief Justice here* na kukaa naye kwenye *gallery?* Ni kwa sababu ni mhimili mwingine. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, suala hili lililetwa na mhimili. Mhimili wa Mahakama baada ya mashauriano ya muda mrefu na kuona jambo hili halieleweki, Jaji Mkuu kwa mamlaka yake aliniarifu kwamba ameshafanya majadiliano na mashauriano huko kunakohusika na kwa mamlaka yake

anauondoa Muswada huu na sasa atatumia mamlaka yake aliyonayo kikatiba na kisheria kuzitangaza hizi mahakama chini ya *Judicature and Application of Laws Act, section 4* na chini ya *section 10* ya *The Magistrate's Court Act.* Akifanya hivyo hapitii uchochoro, anatimiza mamlaka aliyonayo na mamlaka hayo anayo *Chief Justice,* Spika na Rais. Rais ana uwezo wa kutunga sheria peke yake, *decrees, proclamation* na *instruments. (Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ndiyo maana mwaka 1964 Mwalimu kwa kutumia mamlaka yake ya kutunga sheria peke yake alitoa *decree* mbili baada ya Muungano: Moja, kutangaza Katiba ya muda ya Muungano na pili kutangaza Serikali ya Muungano, *by decree.* Mamlaka hayo Rais anayo au *by instrument,* mamlaka hayo Rais anayo au *by proclamation,* mamlaka hayo Rais anayo. Waraka wa Spika, *circular* yake inayohusu taratibu za kuendesha Bunge ni sheria. Hivyo hivyo kwa Jaji Mkuu, Waraka wake, *circular* yake ya kuendesha Mahakama ni sheria. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, lingine nataka kusema kwamba dhana hii ya Mahakama siyo mpya. *The Chief Justice, our current Justice is a person inbuilt with humility.* Hakustahili kuleta jambo hili hapa kwa sababu tayari lilikwishaagizwa na Waraka wa Mahakama Na.2 wa tarehe 14 Machi, 1977 na Jaji Mkuu Francis Nyalali na naomba niwasome, kupeleka Mahakama ya Wilaya na ya Hakimu Mkazi Vijijini. Nitasoma *paragraph* tatu tu. Ya kwanza inasema: -

*"Ingawa kwa mujibu wa Fungu la 9 la Sheria ya Mahakimu (Magistrates Court Act, 1963), Mahakama ya Wilaya inayo mamlaka kimahakama katika wilaya nzima ilipo na kadhalika Mahakama ya Hakimu Mkazi inayo mamlaka ya aina hiyo katika mkoa mzima ilipo. Vikao vya Mahakama hizo kwa desturi na mazoea hufanyika mahali pamoja tu yaani kwenye Makao Makuu ya Wilaya na Mkoa, palipo na makao ya kudumu ya Mahakama hizo. Matokeo yake ni kwamba kesi zote katika kesi hizo husikilizwa siku zote kwenye makao hayo ya kudumu yaliyomo mijini na wanavijiji kuzifuata haki zao huko mijini."*

Mheshimiwa Spika, naruka nakwenda *paragraph* ya nne, inasema:-

*"Kuna jambo lingine muhimu sana. Huu mtindo wa watu vijijini kuzifuata Mahakama hizi mijini hugharimu fedha nyingi sana katika kuwafikisha na kuwalipa posho. Kwa mujibu wa sheria, mashahidi wanaotoka karibu na kikao cha Mahakama haiwagharimu kitu. Hivyo basi, ili kupunguza gharama kubwa za utekelezaji wa haki ya kuongeza hadhi ya Mahakama na sheria kwa watu, iko haja ya kubadilisha mtindo wa watu kuzifuata Mahakama na kuweka mtindo wa Mahakama kufuata watu." (Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nisome ya mwisho kwa umuhimu wa maelezo ya leo, inasema:-

*"Kwa utekelezaji mwema wa agizo hili kila Msajili wa Wilaya wa Mahakama Kuu pamoja na Naibu Msajili Mkuu Mikoa ya Dar es Salaam, Pwani na Morogoro, atayarishe ratiba au mpango utakaowezesha motokaa za Idara ya Mahakama zilizopo Wilayani na Mikoani zitumike kuzipeleka Mahakama kwa watu katika kila wilaya isipokuwa zile motokaa tu zilizotengenezwa kwa watumishi wengine maalum. Nakala ya ratiba hizo zitawasilishwa kwa Msajili wa Mahakama Kuu". (Makofi)*

Mheshimiwa Spika, hili siyo jambo jipya, Waraka huu hapa. Kwa mantiki hii, kwa kweli *the Chief Justice was doing a courtesy to the Parliament, he was not obliged, or compelled. When a person comes with gesture of humility, don't abuse his sense of humility. I am indeed flabbergasted, perturbed with this kind of behavior. We can't continue in this way. If we condone this type of behavior, we are not only demeaning the Parliament, we are demeaning the entire legal fraternity. (Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ni kweli kabisa fedha zilizotumika kununua haya magari na yamenunuliwa na yanakuja, yatazinduliwa na yatatumika, zilipitishwa na Bunge hili hili. Someni *development budget.*

*(Hapa baadhi ya Waheshimiwa Wabunge waliongea bila mpangilio)*

**WAZIRI WA KATIBA NA SHERIA:** Kumbukeni *Vote* 40, nendeni mkaangalie, fedha hiyo ni pamoja na fedha iliyojenga *Law School of Tanzania,* ndiyo fedha ambayo kila siku natangaza Mahakama za kujenga hapa, Mahakama za Mwanzo zinazojengwa kwa mtindo wa Moladi, za Wilaya, Mahakama Kuu, pamoja na *Mobile Courts.* Fedha yote ni *package* hiyo. *(Makofi)*

*(Hapa baadhi ya Waheshimiwa Wabunge waliongea bila mpangilio)*

**WAZIRI WA KATIBA NA SHERIA:** Mheshimiwa Spika, sasa anayesema fedha hiyo haikupita katika Bunge, akasome *Vote 40* na siyo hela ya Serikali. Unajua humu ndani tuko Mawaziri ambao unatakiwa ukiwa Waziri wa Wizara hizo uwe na hekima kubwa: Waziri wa Katiba na Sheria, Waziri wa Mambo ya Ndani na wa Ulinzi na Kujenga Taifa. Mimi nikishaomba hela hapa, ni hela ya Mahakama wala siingilii. Nikishamwombea fedha *Attorney General,* simwingilii matumizi ya fedha yake, kwa sababu tayari Katiba inamlinda *equally* Jeshi la Wananchi, *equally* Polisi. Kwa hiyo, fedha hii…

*(Hapa baadhi ya Waheshimiwa Wabunge waliongea bila mpangilio)*

**SPIKA:** Muwe mnaelewa Kiswahili na msikilize vizuri. Kinachozungumzwa hakina mchanganyiko wowote. Ndiyo ile ambayo tunasema sijui wengine darasani ilikuwaje, tuwe tunasikiliza vizuri kinachozungumzwa.

**WAZIRI WA KATIBA NA SHERIA:** Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, fedha hiyo ni fedha ambayo tumeipa Mahakama. Tukishaipa Mahakama hatuiingilii matumizi yake, wala mimi sihusiki na tenda za huko. Ni mhimili kama ambavyo Bunge likishapewa fedha kupitia kwa Waziri Mkuu, Waziri Mkuu haliingilii Bunge wala matumizi yake. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, nataka nisisitize tena kwa Wabunge, Sehemu hii ya Tano ilikuwa ni sehemu ya mhimili wa Mahakama, mhimili wa Mahakama umeiondoa. Sitaki kudanganya Mahakama hizi Jaji Mkuu ana mamlaka ya kuzianzisha na kabla ya kwenda Australia kwenye Mkutano wa Majaji Wakuu wa *Commonwealth* ameniambia anazianzisha kwa mamlaka yake, zitaanza kufanya kazi kwa mamlaka yake na zitakwenda sehemu mbalimbali kwa mamlaka yake. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, hakuna anayelazimishwa kwenda kwenye hizo Mahakama. Wanasheria mko huku, ni *choice of forum.* Mheshimiwa Mtolea, *is choice of forum.* Ukiamua kwenda kwenye hizo Mahakama ujue mipaka yake ni nini. Hutaki, unataka wakili, nenda Mahakama za kawaida. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kama kwa ndugu zangu wa Zanzibar, ukiona haki yako ya binadamu Zanzibar imevunjwa ukifungua shauri la kudai haki yako ya binadamu chini ya Katiba ya Zanzibar mwisho ni Mahakama Kuu ya Zanzibar. Ndivyo Katiba ya Zanzibar inavyosema. Ukitaka liende kwenye Makahama ya Rufaa, fungua chini ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano. Kwa hiyo, *it is a choise of forum,* hakuna anayelazimishwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, sasa hatuwezi kuendelea kujadili jambo ambalo, nami nilishangaa limekujaje kwenye hotuba, kwa sababu tayari Serikali imeliondoa. Sasa kwa sababu mkamia maji, watu walikuwa wamekamia maji, waliyakamia, sasa hawakunywa. Kwa sababu hawakunywa maji waliyoyakamia, ndiyo zogo hili. *(Kicheko/Makofi)*

Mheshimiwa Spika, tujikumbushe wanasheria, mwenda tezi na omo marejeo ni ngamani. Siku itakapofika ya Farao asiyemjua Yusufu, tukatoka humu, tutarudi Mahakamani, tutarudije huko? *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante sana. Tunakushukuru sana Mheshimiwa Profesa Kabudi kwa maelezo mazuri sana. Ndiyo maana nikawaambia rafiki zangu wanaosema tumeingiliwa, jamani, jamani, hebu muwe na subira.

Tunaendelea na Mheshimiwa Mwanasheria Mkuu wa Serikali, mtoa hoja, karibu hapa mbele umalizie kwa dakika 20. *(Makofi)*

**MWANASHERIA MKUU WA SERIKALI:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana. Naomba nichukue fursa hii kukushukuru kwa kunipatia nafasi ya kuhitimisha hoja kuhusu Muswada wa Marekebisho ya Sheria Mbalimbali Na.3 wa mwaka 2018. Aidha, nakupongeza kwa namna ambavyo umeweza kuongoza mjadala wa Muswada huu vizuri. Hoja hii imechangiwa na jumla ya Waheshimiwa Wabunge nane ambao wamechangia kwa kuzungumza ndani ya Bunge.

Mheshimiwa Spika, nawashukuru sana Waheshimiwa Wabunge kwa michango yao mizuri. Kwa hakika tumepokea maoni mazuri ambayo yamelenga kuboresha siyo Muswada tu, bali hata masharti mengine ya sheria mama na namna bora ya kutekeleza sheria husika.

Mheshimiwa Spika, kwa ujumla maoni na ushauri uliotolewa na Waheshimiwa Wabunge wakati wa kuchangia Muswada huu ni ushahidi kwamba Bunge hili linatambua umuhimu wa marekebisho ya sheria kwa lengo la kuboresha utekelezaji madhubuti wa sheria zilizopo na kwa hakika jambo hilo ni endelevu. Serikali itaendelea kuleta Bungeni marekebisho ya aina hii kila inapoonekana kuna umuhimu huo kwa lengo la kuboresha masharti ya sheria zetu na kuzifanya ziendane na wakati.

Mheshimiwa Spika, napenda kumshukuru kwa dhati Mheshimiwa Omary Mchengerwa, Mbunge ambaye alisoma Maoni ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Katiba na Sheria kwa kutoa maelezo mazuri ya ufafanuzi juu ya maudhui ya Muswada pamoja na mapendekezo ya marekebisho kwenye Muswada. Naamini maelezo yake ambayo yaliainisha maoni

ya wadau waliofika kwenye Kamati hiyo, yamewasaidia Waheshimiwa Wabunge na wananchi kwa ujumla kuelewa vyema maudhui ya Muswada huu. Maoni na ushauri wa Kamati vimezingatiwa kwa kiasi kikubwa na vimeuboresha Muswada huu kama inavyoonekana kwenye Jedwali la Marekebisho ambalo Waheshimiwa Wabunge waligawiwa ndani ya Bunge.

Mheshimiwa Spika, namshukuru pia, Mheshimiwa Ally Saleh, ambaye alitoa maoni kwa niaba ya Msemaji wa Kambi Rasmi ya Upinzani wa Wizara ya Katiba na Sheria kwa hotuba na maoni yake kuhusu Muswada huu.

Mheshimiwa Spika, naomba kuwashukuru pia Mawaziri na Manaibu Waziri ambao pia wamechangia katika Muswada huu. Mheshimiwa Profesa Kabudi, Waziri wa Katiba na Sheria; Mheshimiwa Dkt. Mpango, Waziri wa Fedha na Mipango; Mheshimiwa Angeline Mabula, Naibu Waziri wa Ardhi; na Mheshimiwa Dkt. Ashatu, Naibu Waziri wa Fedha na Mipango.

Mheshimiwa Spika, baada ya utangulizi huo, naomba sasa nijibu hoja kadhaa au kutoa ufafanuzi kwa hoja zilizotolewa na Waheshimiwa Wabunge. Kama nilivyosema, Wabunge nane walichangia.

Mheshimiwa Spika, kabla ya hayo, nami niseme kidogo juu ya sintofahamu iliyotokea kwenye Ibara ya 11, 12 na 13 za Muswada. Kama nilivyoeleza katika hotuba yangu hapo mwanzoni, Serikali iliondoa Ibara hizo tatu. Ibara hizo zinahusu zile *mobile courts, special courts* na *small claims* na tulifuata maelekezo ya Kanuni ya 88(2) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Januari, 2016.

Mheshimiwa Spika, baada ya kuwa tumefuata utaratibu huo, hatukutegemea kwamba suala hili lingeingia tena kwenye hotuba ya Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Katiba na Sheria na hata kwenye hotuba ya Msemaji Mkuu wa Kambi ya Upinzani. Basi, tutaendelea na haya mengine yaliyobaki.

Mheshimiwa Spika, kulikuwa na mchango kutoka kwa Mheshimiwa Gekul aliyesema kwamba marekebisho katika Ibara ya 31 ya Muswada huu yanalenga kuleta vikwazo na ni vyema kuwa na nafasi ya kukosoa takwimu za Serikali. Nataka tu kumfahamisha Mheshimiwa Gekul kwamba, nadhani alikuwa hajaangalia yale marekebisho katika Jedwali la Marekebisho yaliyoletwa na Serikali, Ibara (g) kwa sababu imefanya marekebisho katika sehemu hiyo.

Mheshimiwa Spika, kulikuwa pia na maoni kutoka kwa Mheshimiwa Mtolea, aliyezungumza kwamba katika haya masuala ya Mabaraza ya Ardhi yanahitajika mabadiliko makubwa katika sheria kuliko haya ambayo yanaonekana ni madogo madogo na kwamba ziko changamoto nyingi tungezifanyia kazi zote kwa pamoja. Nakubaliana na Mheshimiwa Mbunge kwamba changamoto ni nyingi katika eneo hili la utatuzi wa migogoro inayohusu ardhi, lakini zinafanyiwa kazi. Hatua hizo ziko za muda mfupi na za muda mrefu.

Mheshimiwa Spika, kuna baadhi ya mambo Mheshimiwa Waziri wa Katiba na Sheria wakati fulani alipata nafasi ya kuyazungumza, huwezi ukayatatua kwa haraka haraka kwa sababu kuna masuala huko ya imani, ya kimila, ya mapokeo na kadhalika ambayo yanahitaji mjadala mrefu na mpana wa Kitaifa. Huwezi ukasema usubiri mpaka hayo yote uwe umeyajadili na kufikia muafaka. Unaweza ukachukua hatua kwa yale ambayo unaweza kuyachukulia hatua wakati huo. Kwa hiyo, mabadiliko haya ni kati ya mambo ambayo yameonekana kwamba yanaweza yakafanyiwa kazi kwa muda huu na hayo mengine yataendelea kufanyiwa kazi.

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Halima alitoa maoni yake kwamba anafikiri lengo la mabadiliko ya Sheria ya Takwimu ni moja tu, ni kudhibiti. Napenda kusema kwamba, kwa kweli karibu nchi zote na hasa zilizoendelea zina sheria na ni sheria madhubuti za kusimamia takwimu. Kwa kweli, kwa nchi zilizoendelea nafikiri sheria zao pengine ni kali zaidi kuliko hata sheria tulizonazo kwa sababu, wanajua takwimu

ni kila kitu. Takwimu ni uchumi, ni siasa, ni mendeleo, ni amani, ni maridhiano na mshikamano. Kwa hiyo, hawafanyi mchezo na takwimu. Ndiyo maana hata katika baadhi ya vyuo vikuu wale wanaoandika zile tasnifu za uzamivu *(Ph.D)* kama ina takwimu za aina fulani Serikali inaweza ikaamua kwamba zisitolewe kwa sababu ya maslahi mapana ya nchi.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, ni kweli kwa upande mmoja kwamba lengo la sheria hii ni kuweka udhibiti lakini ni udhibiti chanya ili kuhakikisha kwamba wote tunakwenda pamoja na hakuna mtu anayetumia nafasi ya takwimu kupotosha, kueleza kitu kisicho cha ukweli, kueleza kitu au kutoa kitu ambacho hakijafanywa kwa njia za kisayansi, kwa njia zinazokubalika kitaalamu na kitaaluma na kwa hiyo, anatupotosha. Tumeshaambiwa, sehemu nyingi sana katika nchi mbalimbali zimepata matatizo kwa sababu ya takwimu. Hata yale mauaji ya kimbari ya Rwanda kulikuwa na masuala ya takwimu humo yaliyohusika na yalichangia.

Mheshimiwa Spika, hitimisho. Baada ya maelezo haya, naomba kukushukuru tena kwa kunipatia fursa hii ya kutoa maelezo ya kuhitimisha hoja iliyo mbele ya Bunge lako Tukufu. Nawaomba Waheshimiwa Wabunge wote waunge mkono marekebisho kama yalivyopendekezwa katika Muswada na Jedwali la Marekebisho.

Mheshimiwa Spika, naomba kutoa hoja.

**WAZIRI WA HABARI, UTAMADUNI, SANAA NA MICHEZO:** Mheshimiwa Spika, naafiki.

*(Hoja ilitolewa iamuliwe)*

**SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Mwanasheria Mkuu wa Serikali. Hoja imetolewa na imeungwa mkono. Tunakushukuru sana Mheshimiwa Mwanasheria Mkuu wa Serikali. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, mtaona kuna tabia ina muda sasa, watu wanachokoza, wanaisema Serikali wee,

inapofika wakati Serikali inatakiwa kujibu, wao wanachimba, wanatoroka humu ndani, lakini mnajua wanachokifanya? Kwa wao kazi tayari kwa sababu watu wao wanakuwa wameshachukua *clip*, wanarusha kwenye *You Tube; You Tube* inapoangaliwa nchi nzima, dunia nzima, wanaona mawazo yale. Utamzuiaje Mtanzania yeyote au mwanadunia yeyote kuwaamini wale kwamba walichosema ndicho chenyewe?

Nanyi upande wa Serikali hakuna *clip* utakayoiona ya *AG,* Profesa Kabudi, Waziri wa Fedha, akielezea mambo, hakuna. Kwa hiyo, sasa twendeni kisasa. Wanavyoenda wao na sisi twende hivyo hivyo, eeh.

**WABUNGE FULANI:** Bunge live.

**SPIKA:** Tuwakute huko huko, eeh, kabisa kabisa. Wanafanikiwa sana katika kuidanganya jamii kwa sababu, habari za upande wa pili zinakuwa hakuna. *(Makofi)*

**WABUNGE FULANI:** Bunge live.

**SPIKA:** Katibu.

**NDG. ASIA MINJA – KATIBU MEZANI:**

**KAMATI YA BUNGE ZIMA**

*(Muswada wa Sheria ya Marekebisho ya Sheria Mbalimbali Na. 3 wa Mwaka 2018 [The Written Laws Miscellaneous Amendments (No. 3) Bill, 2018]*

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, tukae.

Katibu tuendelee.

**NDG. MOSY LUKUVI – KATIBU MEZANI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa naomba tujielekeze katika Muswada wa Sheria ya Marekebisho ya Sheria Mbalimbali Na. 3 wa Mwaka 2018.

Ibara ya 1
Ibara ya 2
Ibara ya 3

*(Ibara zilizotajwa hapo juu zilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima bila Mabadiliko yoyote)*

Ibara ya 4

*(Ibara iliyotajwa hapo juu ilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima pamoja na marekebisho yake)*

Ibara ya 5

*(Ibara iliyotajwa hapo juu ilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima bila mabadiliko yoyote)*

Ibara ya 6

*(Ibara iliyotajwa hapo juu ilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima pamoja na marekebisho yake)*

Ibara ya 7
Ibara ya 8
Ibara ya 9
Ibara ya 10

*(Ibara zilizotajwa hapo juu zilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima bila mabadiliko yoyote)*

Ibara ya 11
Ibara ya 12
Ibara ya 13

*(Ibara zilizotajwa hapo juu zilifutwa na Serikali)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Gekul.

**MHE. PAULINE P. GEKUL:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana. Mimi langu ni dogo tu, naomba nipate ufafanuzi kwa majibu ya Mheshimiwa Waziri wa Katiba na Sheria wakati anajibu. Alisema kwamba, *cases* ambazo zitapelekwa kwenye hizi *mobile courts of which* amesema kwamba tu zitaanzishwa...

**MWENYEKITI:** Sasa unajadili wapi wakati hii imeondolewa?

**MHE. PAULINE P. GEKUL:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba tu ufafanuzi kwenye hitimisho lake, ikikupendeza.

**MWENYEKITI:** Lakini imeondolewa sasa. Atatoaje ufafanuzi kwa kitu ambacho kimeondolewa, hakiko mezani?

**MHE. PAULINE P. GEKUL:** Mheshimiwa Mwenyekiti, amejadili, alicho-*conclude* ndiyo ambacho...

**MWENYEKITI:** Kaa chini Mheshimiwa. Katibu.

Ibara 11
Ibara 12
Ibara 13

*(Ibara zilizotajwa hapo juu zilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima bila mabadiliko yoyote)*

Ibara 14

*(Ibara iliyotajwa hapo juu Ilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima pamoja na marekebisho yake)*

Ibara 15
Ibara 16
Ibara 17
Ibara 18
Ibara 19
Ibara 20

*(Ibara zilizotajwa hapo juu zilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima bila mabadiliko yoyote)*

Ibara 21
Ibara 22

*(Ibara zilizotajwa hapo juu zilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima pamoja na marekebisho yake)*

Ibara 23
Ibara 24
Ibara 25
Ibara 26
Ibara 27

*(Ibara zilizotajwa hapo juu zilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima bila mabadiliko yoyote)*

Ibara 28

*(Ibara iliyotajwa hapo juu ilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima pamoja na marekebisho yake)*

Ibara 29

*(Ibara iliyotajwa hapo juu ilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima bila Mabadiliko yoyote)*

**NDG. MOSY LUKUVI – KATIBU MEZANI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kutoa taarifa kwamba Kamati ya Bunge Zima imemaliza kazi yake.

**SPIKA:** Bunge linarejea.

*(Bunge lilirudia)*

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, tukae. Mheshimiwa Mwanasheria Mkuu wa Serikali, Taarifa.

**T A A R I F A**

**MWANASHERIA MKUU WA SERIKALI:** Mheshimiwa Spika, kwa mujibu wa Kanuni ya 89(1) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Januari, 2016, napenda kutoa Taarifa kwamba Kamati ya Bunge Zima imeupitia Muswada wa Sheria ya Marekebisho ya Sheria Mbalimbali Na. 3 wa Mwaka 2018 *[The Written Laws Miscellaneous Amendments (No. 3) Bill, 2018]* Ibara kwa Ibara na kuukubali pamoja na marekebisho yaliyofanyika.

Mheshimiwa Spika, naomba kutoa hoja kwamba Muswada wa Sheria ya Marekebisho ya Sheria Mbalimbali Na. 3 wa Mwaka 2018 *[The Written Laws Miscellaneous Amendments (No. 3) Bill, 2018),* kama ulivyorekebishwa katika Kamati ya Bunge Zima, sasa ukubaliwe.

Mheshimiwa Spika, naomba kutoa hoja.

**WAZIRI WA HABARI, UTAMADUNI, SANAA NA MICHEZO:** Mheshimiwa Spika, naafiki. *(Makofi)*

**SPIKA:** Asante sana Mheshimiwa Mwanasheria Mkuu wa Serikali. Hoja imetolewa na imeungwa mkono. *(Makofi)*

Ahsante sana. Sasa wajibu wangu hapa ni kuwahoji Waheshimiwa Wabunge kuhusiana na Muswada huu wa Sheria ya Marekebisho ya Sheria Mbalimbali Na. 3 wa Mwaka 2018.

*(Hoja ilitolewa iamuliwe)*
*(Hoja iliamuliwa na Kuafikiwa)*

**SPIKA:** Katibu.

**NDG. ASIA MINJA - KATIBU MEZANI:**

Muswada wa Sheria kwa ajili ya Kufanya Marekebisho katika Sheria Mbalimbali zipatazo sita (6) kwa lengo la kuondoa mapungufu ambayo yamejitokeza katika Sheria hizo wakati wa utekelezaji wa baadhi ya masharti katika Sheria hizo *(A Bill for an Act to amend Certain Written Laws)*

*(Kusomwa Mara ya Tatu)*

(Muswada wa Sheria ya Marekebisho ya Sheria Mbalimbali Na. 3 wa Mwaka 2018 *[The Written Laws Miscellaneous Amendments (No. 3) Bill, 2018) ulipitishwa na Bunge)*

**SPIKA:** Sasa naomba nitangaze rasmi kwamba Muswada huu umepitishwa rasmi na Bunge katika hatua zake zote. Kwa hiyo, utaendelea na safari yake ambapo utahitaji kibali cha Mheshimiwa Rais kuweka saini yake kwa ridhaa yake. Kwa jinsi hiyo, hilo likifanyika kwenye kikao kijacho tutawataarifu.

Nachukua nafasi hii kuwashukuru sana Waheshimiwa Wabunge wote na kipekee Kamati yetu ya Katiba na Sheria iliyoshughulikia Muswada huu na Waheshimiwa Wabunge wengine wote ambao mli-*pick interest* kwenye jambo hili. Hizi ni sheria mbalimbali, nina hakika kabisa Wabunge wengi kutoka Kamati mbalimbali huwa mna-*pick interest* ya kuangalia mabadiliko yanayokuja katika Mabadiliko ya Sheria Mbalimbali, japo yanapitia katika Kamati moja, lakini mnashiriki katika kujaribu kujazia na kuboresha. Kama alivyosema Mwanasheria Mkuu wa Serikali, tutaendelea kuwa na Miswada ya namna hii kwa sababu ni wajibu wetu kama Bunge kurekebisha, kufuta, kuleta jambo jipya na kadhalika, kila tunapoletewa mapendekezo na Serikali.

Nawashukuru sana wataalam wote ambao wamehusika na jambo hili ikiwa ni pamoja na watalaam wetu wa Bunge ambao wanafanya kazi hapa Bungeni chini ya Katibu wa Bunge. Tunawashukuru sana. *By the way,* sijui kama Waheshimiwa Wabunge mnajua kwamba hapa

Bungeni tuna vijana mahiri sana na wasomi wazuri sana. Niwataarifuni hivyo, tuna vijana wazuri sana na ndiyo wanasaidia sana hizi Kamati katika kuchambua Miswada mbalimbali na mambo mengine. Tunayo *cream* kabisa ya watumishi ambao wanatutumikia hapa Bungeni. Ni jambo jema, muwatumie kila mnapoona inafaa. *(Makofi)*

*Otherwise,* Mheshimiwa Waziri wa Katiba na Sheria, Mheshimiwa Mwanasheria Mkuu wa Serikali, *Chief Whip,* Mheshimiwa Waziri Mkuu tunashukuru sana timu yako. Hata ulipokuwa hupo tumefanya kazi kwa ushirikiano mkubwa, mambo yameenda kama yalivyopangwa kwenye ratiba. Nawe tunakukaribisha, karibu tena nyumbani, karibu sana tuweze kuendelea na shughuli kama kawaida. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, mnakumbuka ratiba yetu kesho itakuwa inahusiana na Muswada ule wa *PPP.* Natumaini mtakuwa mmeshaupitia. Kamati husika ninayo Taarifa yenu kwamba mko tayari kwa maoni yenu na ndugu zangu upande wa Upinzani natumaini pia maoni yenu yatakuwa yako tayari. Ushauri wangu ni kujikita katika mada iliyopo Mezani. Mnapoandika maoni yenu mnatumia ile utangulizi kwenda nje ya uwanja kwanza, kuandika mambo ambayo hayapo, kila mtu anashangaa, halafu ndiyo unarudi sasa kwenye swali. Ni sawasawa na wale wanafunzi enzi zile, akina Profesa Kabudi wanajua, unapewa mtihani wa kujadili jambo na labda mtihani wenyewe ni wa saa moja. Sasa *supervisor* anasema haya anza kuandika, wewe unaanza na utangulizi, unapiga utangulizi saa moja, wanaposema *pens down,* wewe ndiyo unaanza *back to the question,* lakini muda wa kujibu umeshaisha. *(Kicheko)*

Kwa mfano kesho ni *PPP,* unaanza kama ni utangulizi wako *PPP, main body* ni *PPP, conclusion* yako *PPP.* Pale inakuwa tunaenda vizuri na hasa siyo tu *PPP* kwa ujumla, lakini zaidi kinachopendekezwa na Serikali ni kitu gani na unadhani ni namna gani kikawa bora zaidi. Kwa sababu, lengo letu kama Bunge kwa kweli, ni kuboresha. Kuishauri Serikali kwa kuboresha kilichokuja ili kiwe kizuri. Ilikuwa ni kilio cha Waheshimiwa Wabunge cha muda mrefu, masuala ya

*PPP* hayajakaa sawa, sasa hii ni fursa. Badala ya kulaumiana, ooh, Bunge hili eeh, tujenge nchi yetu. *Let us play our role* ya kujenga.

Waheshimiwa Wabunge, vinginevyo, nawashukuruni sana na kwa jinsi hiyo, kwa vile shughuli zote katika meza hii zimekamilika na zimeisha, basi naahirisha Shughuli za Bunge hadi kesho, saa tatu asubuhi.

*(Saa 1.06 Jioni Bunge liliahirishwa hadi Siku ya Jumanne, Tarehe 11 Septemba, 2018, Saa Tatu Asubuhi)*